Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 15 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda ) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 212

**Ofisi za Waheshimiwa Wabunge Katika Ngazi za Mikoa/Kanda**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge ni moja kati ya mihimili mikuu mitatu ya nchi ambalo halina Ofisi zake hadi kwenye ngazi ya Mikoa kama ilivyo kwa Mahakama na Serikali ambazo zina Ofisi zake hadi kwenye ngazi ya Mikoa jambo ambalo linazifanya zionekane kuwa na mtandao na hadhi yenye nguvu zaidi kuliko Bunge:-

(a) Je, ni kwa nini Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lisiwe na Ofisi zake hadi kwenye ngazi ya Mikoa au Kanda ili kurahisisha kazi za Wabunge na kuwahudumia Wabunge kwa haraka zaidi pindi wanapohitaji msaada kwenye ofisi yao?

(b) Kwa kuwa baadhi ya ofisi za Wabunge ni hisani za Serikali na watu binafsi jambo linalopunguza hadhi ya Bunge. Je, ni lini Bunge litajiondoa kwenye fedheha hiyo ya upangaji kwa kuwajengea Ofisi Wabunge wote?

(c) Kwa kuwa licha ya kwamba Wabunge wengi kutokuwa na Ofisi zenye hadhi ya Kibunge, na wale walio na Ofisi za kupanga, Ofisi hizo zote zina gharama zake kama ukarabati na matumizi mengine ya kawaida kama vile viburudisho kwa wageni wa Wabunge na kadhalika.

Je, Bajeti ya Ofisi hizo huandaliwa na nani na kwa utaratibu gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Bunge ni chombo cha Uwakilishi wa wananchi na kwa umuhimu wake ni mhimili kati ya mihimili mitatu ya dola yaani Bunge, Serikali na Mahakama. Taasisi hizi tutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara ya 63 (2) na (3) ya Katiba inalipa Bunge Mamlaka ya kuishauri Serikali na kusimamia utekelezaji wa mpango na uendeshaji ulioidhinishiwa fedha katika Vikao vya Bunge la Bajeti. Bunge lina Ofisi tatu ambazo ziko Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

Kwa hivi sasa Ofisi hizi zinatosheleza kuwahudumia Wabunge na kurahisisha kazi zao Mikoani na Majimboni. Kwa msingi huo hakuna umuhimu wa kuanzisha Ofisi za Kanda au za Mikoa isipokuwa za Mikoa zile za Wabunge wa Viti Maalum.

(b)Ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge sio hisani ya Serikali ila ni utekekezaji wa mipango na mikakati iliyowekwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Lengo ni kuimarisha na kurahisisha kazi za Wabunge na kuwahudumia wananchi ili kupata maisha bora kwa kila Mtanzania. Iwapo kuna Waheshimiwa Wabunge wamepanga au wanahisaniwa na watu binafsi katika kutekeleza majukumu yao ya kikatiba, taarifa haijatufikia na ikiwasilishwa itafanyiwa kazi.

(c)Uendeshaji wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge unazingatia makadirio yaliyoidhinishwa na Bunge hili. Lengo ni kuziwezesha Ofisi za Wabunge kuwa zenye hadhi ya kutumiwa na viongozi ambao ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Mahitaji yote muhimu yatawekwa ikiwa ni pamoja na mapendekezo anayoeleza Mheshimiwa Mbunge pale ambapo tutakuwa na uwezo wa kifedha.

Aidha ushauri wa kila mara wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wadau kwenye ubora na hadhi ya Ofisi hizo utazingatiwa na kuingizwa kwenye Bajeti.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo. Pamoja na majibu mazuri ya

Mheshimiwa Waziri kuna huo mpango wa kujenga Ofisi za Wabunge lakini kwa watu wengine kuamini ni mpaka waone. Je, ujenzi huu utaanza lini?

La pili, ili kupata nafasi ya kujenga unahitaji upate kiwanja. Je, ni nani atakayeshughulikia upatikanaji wa viwanja na hati miliki ya viwanja hivi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Ofisi za Wabunge katika nchi yetu ni suala la kihistoria. Pale tulipopata uhuru ofisi zilianza kujengwa mojawapo ikiwa ya Mbunge wangu wa wakati huo. Lakini tulipobadilisha Katiba na nchi ikawa ya Chama kimoja Ofisi za Wabunge zikahamishwa kwenye Ofisi za Chama tawala hadi 1992.

Baada ya hapo Serikali imeanza kutenga fedha na miaka miwili mitatu iliyopita imekuwa ikitengwa shilingi bilioni moja kila mwaka ambazo kwa kweli hazitoshelezi na mimi naamini kabisa jawabu la suala hili ni baadaye wakati wa Bunge hili tutakapopitisha muswada wa uendeshaji wa Bunge yaani *Parliamentary Admnistration Bill* ambayo itachukulia maanani pamoja na mambo mengine Ofisi za Wabunge katika maeneo yao.

Kuhusu swali lake la pili ni kwamba hizi ni Ofisi za Serikali. Kwa hiyo, viwanja na Hati Miliki zitatafutwa na Afisa Tawala wa Wilaya husika.

**NAIBU SPIKA:** Tungoje huo Muswada utakaokuja. Tunaenda sasa Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, endelea.

Na. 213

**Mapato ya Gesi Kuhudumia Shughuli za Muungano**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 16/7/2007 Serikali ilisema Bungeni kuwa mapato ya gesi yanaingia kwenye Muungano na kuhudumia shughuli za Muungano.

(a) Je, ni kiasi gani kimepatikana toka kuanza kupatikana gesi hiyo?

(b) Je, ni kiasi gani cha gawio kilipelekwa Zanzibar?

(c) Je, ni asilimia ngapi ya mapato yanayopatikana Zanzibar inapata?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ilielezwa hapa Bunge tarehe 16 Julai, 2007 katika mkutano wa nane Kikao cha Ishirini na Nne wakati wa kujibu hoja ya Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kuwa maduhuli yatokanayo na gesi yanaingizwa kwenye Mfuko wa Serikali ya Muungano. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2008/2009, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano ziko katika mchakato wa kumaliza tatizo hili kwa kumteua Mshauri Mwelekezi atakayeshauri namna ya kugawana gharama na mapato yatokanayo na shughuli za utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi. Mshauri Mwelekezi ni Kampuni ya *Aberdeb University Petroleum Economics Consultants (AUPEC)* ya Uingereza na imeanza kazi mwezi Juni 2008 na itakamilisha kazi hiyo mwezi Novemba 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya utangulizi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, mapato yaliyotokana na gesi asilia tangu mwezi Julai 2004 hadi nwezi Machi 2008 ni shilingi bilioni 32.29 na fedha hizo zilikusanywa na Serikali ya Muungano wa Tanzania.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kiasi cha gawiwo kilichopelekwa Zanzibar kama nilivyoeleza kwenye maelezo ya utangulizi, Mshauri Mwelekezi atatoa mapendekezo ya jinsi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano zitakavyogawana gharama na mapato yatokanayo na shughuli za utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi.

(c)Mheshimiwa Naibu Spik,napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge avute subira hadi hapo taarifa ya Mshauri Mwelekezi itakapotoa mapendekezo yake kuhusu mgawanyo wa gharama na mapato yatokanayo na shughuli za utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi kati ya Serikali ya Zanzibar na Muungano na kisha kutathiminiwa na Serikali zote mbili kabla ya kuanza kutekelezwa.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika maelezo yake alisema hakuna gawio linalopelekwa Zanzibar na kwa kuwa suala hili ni la Muungano. Je, kutokana na hali hiyo wakati panapitishwa mahesabu na kujulikana kamili hiyo fidia Zanzibar itapatikana?

La pili, kwa kuwa katika Muungano wetu yapo mambo 22 unaweza kunieleza matumizi haya ni Wizara ngapi au sehemu ngapi inatumika katika Muungano wetu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema kwenye maelezo kwenye jibu langu la msingi hakuna gawio lililopelekwa Zanzibar lakini hiyo haina maana ya kwamba hakuna kumbukumbu za mapato na kama tulivyosema mapato yaliyopatikana ni bilioni 32.3. Mshauri Mwelekezi ameshaanza kazi na anatarajiwa kumaliza Novemba 2008 kama nilivyotoa maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba atakapotoa maeleo kumbukumbu zipo na hizo pesa zio kama zimepotea kadri atakavyotuelekeza naamini Serikali zote mbili zitakaa pamoja aidha pia naamini kuna kazi ambayo inafanywa na Tume ya Pamoja na ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi ambayo inasimamiwa na Makamu wa Rais. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na mambo haya yote yatapatiwa ufumbuzi baada ya kupata ripoti ya Mshauri Mwelekezi.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mapato yatokanayo na gesi bado hayajakuwa yameshamiri. Je, Serikali inapoingia Mikataba na Mwekezaji katika kuchimba gesi kipo kipengele cha kusema kwamba gesi yetu inakuwa ni *equite* katika mgao huo wa *shares*?

**NAIBU SPIKA:** Hilo ni suala jingine lakini majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba masuala yote ya gesi yanaongozwa hivi sasa na sera iliyopo.

Tumesema juzi wakati wa kufafanua kwenye masuala ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa Bajeti kwamba masuala yote ya gesi yanahitaji mwongozo ambao tunaupitia upya kwa kutengeneza Sera na Sheria mpya ya matumizi ya gesi asilia ambayo tunatarajia kuyaleta hapa katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya ridhaa ya Wabunge. Isipokuwa naomba niseme kwamba tunatarajia tuangalie tafsiri ya uwekezaji ambao una maslahi kwa taifa tumeshasema.

Lakini pia tafsiri ya mapato inalenga kwenye matumizi ya gesi asilia na ndiyo mapato yanayotokana nayo. Kwa hiyo, ni masuala yote ambayo tunatarajia tuyazingatie wakati wa kuingia kwenye mchakato wa kutafsiri Sheria mpya na mapato yanayotokana na gesi asilia. Pamoja na hili suala la kuzingatia kama gesi hiyo inaweza kuwa ni *equite* na tutaangalia wenzetu wanaozalisha gesi katika mazingira kama yetu wanafanyeje.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongezea majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri kuhusu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Bunge wa Pangani. Kwanza kabisa gesi yote inayochimbwa Tanzania sio tu sehemu ya *equite* lakini ni gesi ya Watanzania na makubaliano yaliyokuwepo kati ya waendelezaji ambao wanaingia mikataba na Serikali ambapo

tunawakilishwa na Shirika letu la utafutaji wa mafuta na petroli *TPDC* ni makubaliano maalum ambayo hayaondoi ukweli kwamba Serikali ndiyo mmiliki wa gesi yote.

Lakini niseme kwamba katika makubaliano hayo mwendelezaji ama yoyote anayeingia mkataba na Serikali kupitia *TPDC* anakuwa analipia gharama zote za utafutaji na gharama zake anazirudisha baada ya kuanza kupatikana kwa gesi kwa makubaliano maalum. Lakini jambo jingine ni kwamba mikataba ya utafutaji wa mafuta na gesi ni mizuri, inahitaja na maslahi ya taifa yamezingatiwa.

Na. 214

**Tatizo la Maji Kawe.**

**MHE. RITA L. MLAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Kawe lina matatizo ya maji kwenye maeneo mengi; na kwa kuwa Serikali ilipata mkopo wa takriban shilingi bilioni 162 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji na kuhakikikisha upatikanaji wa maji kwenye Jiji la Dar es Salaam; na kwa kuwa Serikali iliwatangazia wananchi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2000 na 2005.

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maeneo ya Kawe, Mbezi Juu, Makongo, Changanyikeni, Kunduchi Mtongani, Wazo, Bunju na Mabwe Pande yanapata maji ya uhakika?

(b)Je, kuna uhusiano gani kati ya Manispaa ya kinondoni na *DAWASA* katika kutekeleza jukumu la kuhakikisha kuwa maji yanapatikana?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki Mbunge wa Jimbo la Kawe lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia DAWASA inatekeleza mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka Jijini Dar es Salaam tangu mwaka 2003 na unatarajiwa kukamilika Desemba 2008. Mradi huu unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Benki ya Rasilimali ya Nchi za Ulaya na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa gharama ya shilingi bilioni 164.6. Kupitia mradi huu mitambo ya kusafisha na kusukuma maji ya Ruvu Chini, Ruvu Juu na Mtoni imekarabatiwa. Aidha matanki ya kuhifadhi maji na mtandao wa mabomba ya kusambazia maji umekarabatiwa. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi niliouelezea, tayari kazi kukarabati mabomba na ulazaji wa mabomba mapya imeanza tangu mwezi Mei mwaka huu, kwenye maeneo niliyoyataja. Mkandarasi China Hunan yupo kwenye eneo la mradi.

Kazi hizi zinatarajiwa kukamilika ifikiapo Mei 2009. Aidha maeneo ya Wazo, Bunju na Mabwepande yatashughulikiwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia mfuko maalum wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)*. Chini ya Mradi huo mabomba mapya ya usambazaji maji katika maeneo hayo yatalazwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano kati ya DAWASA na Manispaa ya Kinondoni unahusu maeneo yafuatayo:-

(i) Kubuni kwa pamoja miradi ya maji safi na usafi wa mazingira;

(ii) Kuchangia na kuratibu na kujenga na kuendesha miradi hiyo kwa pamoja;

(iii)Manispiaa hutoa maeneo ya ardhi ya miradi; na

(iv) Manispaa huwakilishwa na Mkurugenzi wa Jiji katika Bodi ya *DAWASA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rita Mlaki ni mfuatiliaji makini wa masuala yanayowahusu wananchi wa Kawe na Dar es Salaam hasa masuala ya maji kwa ujumla. Tuna mpongeza na tunamshukuru.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika maeneo kadhaa ya Jimbo langu la Kawe kuna Miundombinu ambayo imekwishaweka usambazaji maji hususan Kawe, Mikocheni, *Mbezi Beach*, Msasani lakini hadi sasa maji hayatoki na wakandarasi wanasema kuwa kazi yao ni kusambaza miundombinu na sio kuzingatia vyanzo vya maji. Je, Serikali itatuhakikishiaje kuwa maeneo hayo yaliyotajwa yanapata maji ya uhakika?

La pili, kwa kuwa katika maeneo ya Madale, Kisauke, Mvumoni Lakasangwe ambako ndiko anakoishi Mheshimiwa Mzee wetu Rashid Kawawa wananchi wamejitahidi wamechanga pesa, Manispaa imejitahidi imetoa pesa lakini haitoshi na sasa kuna tanki limejengwa ambalo halijakamilika. Je, Serikali inatusaidiaje katika eneo hilo kuhakikisha kwamba wanapata maji ya uhakika?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalotukabili Dar es Salaam ni uchache wa maji yanayotoka kwenye vyanzo vya maji. Tutakapoweza kulihimili hilo tatizo basi tutakuwa tumetatua tatizo kubwa la maji Dar es Salaam. Tatizo la pili ni uvujaji wa maji, maji yanayozalishwa na yanayofika kwa mtumiaji ni kama asilimia 50 ya yale yanayozalishwa. Kwa maana hiyo naomba nieleze kwa kifupi tu yafuatayo.

Uzalishaji wa maji Dar es Salaam, Ruvu Juu lita milioni 80, Ruvu chini lita 180, Mtoni lita milioni 9 na visima ni milioni 30. Kwa hiyo, ni kama lita milioni 300 kwa siku. Lakini mahitaji ni lita milioni 400 kwa siku. Kwa hiyo kuna *short fall* ya kama lita

milioni 100 na upotevu ni asilimia 50. Sasa tunafanya nini, tuna miradi ambayo itazuia upotevu wa maji kwenye hii miradi ambayo nimeitaja kwenye jibu langu la msingi. Lakini vilevile tuna mradi wa maji kutoka chini ya ardhi katika maeneo ya Mpera na Kimbiji ambapo tunatarajia ifikapo 2011 tutakuwa tumepata karibu lita milioni 180 kuingia katika mfumo wa maji Dar es Salaam hasa kusaidia maeneo ya kusini. Tutajenga Bwawa Kitunda ambalo litasaidia kurekebisha mfumo wa maji ambayo yanapatikana Ruvu Juu na Ruvu chini mwaka.

La pili kuhusu mradi wa maji wa Wazo, Madale Kisauke eneo ambalo Mheshimiwa Mzee wetu Kawawa anaishi niseme tu kwamba kwa kweli huu mradi ni wa zamani ulianza mwaka 1994 kwa maana ya usanifu lakini utekelezaji wake umeanza 2006. Tanki tayari limeshajengwa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na tutalaza bomba karibu kilomita tisa kutoka Wazo, bomba limepatikana ulazaji umeanza na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwanzo mwa mwaka 2009. Kwa hiyo, tunamhakikishia Mzee wetu Rashid Mfaume Kawawa maji safi, maji salama na maji ya uhakika.

Na. 215

**Wezi wa Ng'ombe Wilaya ya Singida Vijijini**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo tarehe 28/10/2006 wananchi wa Kijiji cha Mnang'ana Kata ya Sepuka Wilaya ya Singida Vijijini waliwakamata wezi wa ng'ombe pamoja na ng'ombe 25 na kuwakabidhi kwenye Kituo cha Polisi Sepuka na Polisi nao wakakabidhi ng'ombe na wezi hao kwa *OCD* wa Wilaya ya Singida; na kwa kuwa baada ya siku moja wezi hao pamoja na ng'ombe wote 25 walipotelea mikononi mwa Polisi na mmiliki wa ng'ombe hao hakupewa ng'ombe wake hadi leo:-

(a)Je, ni kwa nini mmiliki wa ng'ombe hao hakukaboidhiwa ng'ombe wake wakati walipatikana na kukabidhiwa kwa vyombo vya usalama wa Taifa.

(b)Je, wananchi wa Kijiji hicho watalipwa lini fedha zao walizoahidiwa na OCD kiasi cha shilingi 200,000/- kwa kazi waliyoifanya ya kuwakamata wazi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wa kijiji cha Mnang'ana walikamata ng'ombe 25 na watu wanaodhaniwa kuwa ni wezi na kuwakabidhi kwa aliyekuwa Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Sepuka *Ex. No. D7810 CPL* Julias ambaye alikuwa na askari *No. Ex E. 138 PC Tunga.* Askari hao waliokabidhiwa ng'ombe na wananchi. Aidha kwa makusudi au kwa kukosa umakini waliwarejesha

ng'ombe hao kwa watuhumiwa wa wizi wa ng'ombe hao badala ya kufuata utaratibu wa kisheria wa kushughulikia matukio ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lilichukua hatua za kuwafukuza kazi askari hao kwa kukiuka maadili ya kazi na pia walifikishwa Mahakamani kwa kosa la wizi wa ng'ombe hao.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu baada ya kupata taarifa kuhusu suala hili, iliwasiliana na ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi ambaye tayari amemwelekeza Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Singida kulipa fedha hizo kiasi Tshs 200,000/- kwa wanakijiji waliofanikisha kukamatwa kwa ng'ombe hao. Hivyo nawaomba wananchi hao kuwasiliana na uongozi wa Polisi Mkoa wa Singida ili waweze kulipwa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwamba hivi karibuni Inspekta Jenerali wa Polisi amemteua Kamanda Mpya wa Kikosi Maalum cha Polisi cha kuzuia Wizi wa Mifugo (STPU) Kamashna Msaidizi wa Polisi Ray Kalama. Pamoja na majukumu yale kikosi hiki kitaimarishwa zaidi kwa kuongezewa uwezo wa kupambana na wezi wa mifugo katika Mikoa yote hapa nchini. Aidha *operation* maalum za kusaka wezi wa mifugo zitaendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Jeshi la Polisi yanategemea sana ushirikiano wa wananchi na wadau wengine wa usalama wa Raia katika kupambana na uhalifu nchini. Aidha, tunaomba wananchi waendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za wahalifu na uhalifu ili kutokomeza vitendo hivyo. Nachukua fursa hii kuwapongeza sana wananchi wa kijiji cha Sepuka kwa ushirikiano wao wa dhati katika utekelezaji wa vitendo vya dhana nzima ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naomba Mheshimiwa Waziri ajue kwamba mwenye ng'ombe hao Mzee wa watu wa kisukuma kutoka Meatu Mzee Mahola yupo ndani ya ukumbi na anamsikia na kwamba hajasema lolote kuhusu wale ng'ombe 25.

Katika swali langu la msingi nimeuliza ng'ombe 25 wamekatwa wamekabidhiwa Polisi na amekiri kwamba Polisi waliwapokea. Hazungumzii sasa huyu Mzee wa watu wale ng'ombe atapewa lini ndiyo swali la msingi? Kwa hiyo, ni wajibu wa Polisi kurudisha wale ng'ombe kwa Mzee Mahola ambaye yupo hapa kwenye ukumbi huu mapema iwezekanavyo?

Swali la pili, kama wananchi wanakamata wezi na ng'ombe na kuwakabidhi kwenye Kituo cha Usalama cha Polisi na kuacha kuchukua Sheria mkononi, halafu ng'ombe wale wanapotelea Polisi hivi kesho na kesho kutwa kuna sababu ya kutokuchukua Sheria mkononi kwa sababu Polisi hawafanyi kazi yao vizuri? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na makini.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Tanzania kwa ujumla wao kwamba Jeshi la Polisi liko makini na matukio kama haya ambayo yametokea. Ni matukio ambayo ni bahati mbaya na ndiyo maana Jeshi la Polisi limechukua hatua kuwatia hatiani wale Askari ambao wamefanya kosa hilo lililofanyika.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mzee Mahola ambaye yupo hapa ndani ya Bunge siku hii ya leo kwamba mimi mwenyewe kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi nitaenda katika Kijiji cha Sepuka baada tu ya kipindi cha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafanya kazi na Polisi kuhakikisha kwamba hao ng'ombe ambao wamechukuliwa wanarudishwa kwa Mzee Mahola na kuwathibitishia Watanzania kwamba Jeshi la Polisi lipo makini na linafanya kazi yake vizuri sana. *(Makofi)*

Kama alivyoeleza Naibu Waziri, Jeshi la Polisi limeimarisha kikosi cha (STPU) na tutafanya *operation* nchi nzima kuhakikisha kwamba wahalifu wote ambao wanajihusisha na wizi wa mifugo wanachukuliwa hatua mara moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mzee Mahola naomba usimame pale ulipo. Hayupo!

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa Barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Wilaya hizi mbili Mpwapwa na Kongwa na kwa kuwa fedha zinazotengwa kwa mfano katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 ni shilingi milioni 600 tu ndiyo zimetengwa kwa ajili ya kutengeneza barabara hii na matengenezo ni madogo.

Je, sasa Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kutenga fedha za kutosha ili barabara hii ifanyiwe matengenezo makubwa kwa sababu barabara

hii ndiyo inayounganisha majimbo matatu, Jimbo la Kongwa, Mpwapwa, pamoja na Kibakwe?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa barabara hii na hasa kwa vile ni barabara ambayo inaunganisha majimbo haya mawili na kwamba katika Jimbo la Mpwapwa kuna Kituo cha Utafiti wa Mifugo, Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo, Chuo cha Mifugo, Chuo cha Ualimu Mpwapwa, shule za Sekondari zinazozidi 20, Chuo cha Maafisa wa Afya na kadhalika. Hii ni barabara muhimu tutajitahidi katika miaka inayofuata kuweza kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuitengeneza.

Na. 221

**Ununuzi wa Boti Badala ya Mitumbwi**

**MHE. MOHAMED ALI SAID** aliuliza**:-**

Kwa kuwa kivuko cha Serikali kinachoitwa *MV Geita* ambacho kinavusha watu kati ya Nyakalilo na Kome, kimeharibika kwa muda mrefu sasa bila kufanyiwa matengenezo na kwa kuwa kwa muda mrefu wananchi wamekuwa wakivuka kwa kutumia mitumbwi na kwamba ajali nyingi zimekuwa zikitokea na watu kupoteza maisha yao:-

(a) Je, kwa nini Serikali sasa hainunui boti mpya ili kuokoa maisha ya wananchi wake hasa ikizingatiwa kuwa vivuko vya mitumbwi ni kubahatisha na ni hatari kwa maisha?

(b) Je, Serikali inasimamia vipi usafiri huo wa mitumbwi kuhakikisha kuwa vinachukua abiria wanaostahiki na hivyo kupunguza ajali za mara kwa mara?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kivuko cha *MV Geita* chenye ukubwa wa tani 65 na uwezo wa kubeba magari madogo 6 na abiria 210 kwa mara moja, kilikuwa kinatoa huduma ya kuvusha abiria na magari kati ya Nyakalilo na Kome kabla ya kuharibika mwaka 2003.

Kivuko hiki tayari kilifanyiwa ukarabati wa bodi na sasa Serikali kupitia wakala wa ufundi a umeme (*TEMESA*) inatengeneza injini na mitambo ya uendeshaji kwa ajili ya kivuko hicho.

Katika kuimarisha zaidi huduma ya kuvusha abiria na magari kati ya Nyakalilo na Kome, Wizara kupitia wakala wa barabara (*TANROAD*) imenunua kivuko kipya cha Kome kutoka Uholanzi chenye uwezo wa kubeba tani 45 yaani magari madogo 4 na abiria 100. Ujenzi wa kivuko hiki tayari umekamilika na kivuko kitawasili nchini mwezi Agosti 2008. Aidha, kivuko hiki kipya kitafanya kazi pamoja na kivuko cha *MV Geita* mara baada ya matengenezo yake kukamilika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *SUMATRA* inafuatilia kuhakikisha mitumbwi inayotoa huduma katika eneo hilo imesajiliwa na inakidhi matakwa ya usalama wa vyombo vya majini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yameisha. Waheshimiwa Wabunge wageni wetu leo, kwanza kabisa nina wageni wa Mheshimiwa Lawrence Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi Ndugu Amani Muria na Mke wake Bibi Rose Amani kutoka *Kopcom Tanzania Limited* karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Capt. John Chiligati Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wabunge wote wa Mkoa wa Singida wageni hawa ni Ndugu Bora Lumaza, Katibu wa UWT Mkoa na Ndugu Bahati Makalanzi, Katibu wa Vijana Mkoa na Ndugu Alfonso Swale, Katibu wa Wazazi Mkoa wa Singida, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wa Mheshimiwa Gaudensia Kabaka, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao ni Ndugu John Marwa Kabaka, ambaye ni Mume wake. Bahati nzuri tumesoma wote huyu karibu, Tuna wageni wa Mheshimiwa Philip Marmo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, uratibu na Bunge hawa ni Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kumi za Wilaya ya Mbulu zilizofanya vizuri katika mtihani wa darasa la saba mwaka 2007 naomba wote wasimame mahali walipo. Hongereni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya tunajivunia kazi yenu ahsante sana.

*T*una wageni wa Mheshimiwa Marmo tena, shule zenyewe zilizoongoza Kimkoa na Kiwilaya ni shule ya Msingi Natahalali Mwalimu Mkuu wake ni Blasio Sanya, Shule ya Mchida Mwalimu Mkuu wake ni Julius Habie, Shule ya Msingi Hasha Mwalimu Mkuu wake ni Leonard Malisa, Shule ya Msingi ya Yedahampa Mwalimu Mkuu wake Wilbord Jorijiki, Waheshimiwa haya majina ni magumu sana. Kuna shule ya Msingi inaitwa Jaranja, Kwadachi, Endamilae, Getanyamba, Mewadani, Gidimondan, wote hawa ni walimu wakuu wamefuatana na waratibu wa elimu Kata na Maafisa Taaluma wa Wilaya Ndugu Modesti Matire na Veronica Mushi naomba wasimame, Ahsanteni sana na karibuni.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Magembe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambao ni maafisa 72 kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nadhani watakuwa kwenye *basement*. Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ambaye ni shemeji yake na rafiki wa familia yake Mchungaji Mstaafu wa Kanisa la Katoliki la *St. Francisco,* yuko na *Father Nasis Kabip* wa Parokia ya Murutunguru *Ukerewe Diocese* karibuni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, ambao ni wanafunzi wa Udaktari wa mwaka wa nne wa chuo kikuu cha *IMTU* wapo 25 madaktari wetu wa kesho wako wapi, karibuni sana, wageni maalum wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam naomba wote wasimame, karibuni.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni 12 wa Mheshimiwa John Lwanji, ambao ni Wenyeviti na Makatibu Kata wa Agondi.

Waheshimiwa Wabunge wale wa Dar es Salaam ni Alexander Chalamila, Isaya Mwakilasa, Mujuni Sylivester, Joseph Shamba Mgaya.

**MBUNGE FULANI:** *The comedy* hao!

**NAIBU SPIKA:** Ahaa, nimeambiwa tu wageni maalum sikuambiwa ni *The Comedy*. Sasa nakuta majina yao, karibuni sana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Lwanji ambao ni Wenyeviti na Makatibu Kata wa Agondi Jimbo la Manyoni Magharibi. Wageni hawa wameongozana na Diwani Jackson Majendo. Naomba wasimame hapo walipo. Ahsanteni sana na karibuni sana. *The comedy* mmehamia Bungeni! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nina wanafunzi 15 kutoka *Ardhi University Stundents Organisation* (*ARUSO*) nafikiri wamekosa nafasi, wanafunzi watano kutoka *Save the Children*, kuna wanafunzi 60 kutoka Makole Sekondari. Wako wapi wasimame na walimu wao karibuni sana na Ahsante sana. Kuna wanafunzi 20 kutoka chuo cha ualimu cha Mpwapwa wasimame mahali walipo, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tuna shughuli zingine pia, kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge huduma za Jamii Mheshimiwa Omar Kwaangw' anaomba Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo tarehe 15 Julai kutakuwa na kikao cha Kamati saa saba mchana katika ukumbi 231.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Bunge na Maendeleo ya Jamii na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha pamoja na Baraza la Watoto wa Wilaya ya Lindi katika

ukumbi namba 231. Naona ukumbi hapa mnagongana. Kwa hiyo, mtapata ufafanuzi kule mtakapokuwa.

Mheshimiwa Misanga Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya miundombinu kuwa watakuwa na Kikao leo saa sita na nusu mchana katika ukumbi namba 227, Katibu Msaidizi wa Bunge anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi pamoja na kuwasilisha hotuba yake ya Bajeti hii pia inawaarifu Waheshimiwa Wabunge kuwa ina dawati la taarifa katika viwanja vya Bunge, mnakaribishwa ili kuona na kupata taarifa mbalimbali za elimu kupitia taasisi ya elimu ya watu wazima, Taasisi ya Elimu Tanzania, Chuo Kikuu cha Mzumbe na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, katika eneo letu la Maonyesho pale kuna shughuli hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, pia Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Wabunge anapenda niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe leo kutakuwa na maonyesho haya ninayosema pia upimaji wa afya utakaotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika ukumbi wa Pius Msekwa uchunguzi utakaofanywa ni wa sukari, moyo na saratani ya kizazi kwa wanawake. Aidha, watakaopima sukari wanatakiwa kutokula kitu chochote kabla hawajachuliwa vipimo, mnafahamu kesho Wizara hiyo inawasilisha Bajeti yake na kila mwaka huwa wanatoa huduma za namna hiyo.

**MBUNGE FULANI:** UKIMWI..?

**NAIBU SPIKA:** Nadhani itakuwa kesho. Kwa hiyo, wale wabunge watakaopima kisukari wasile kitu kabla ya kwenda huko, kupima. Ni muhimu kwenda kufanya hivyo, ni nafasi ya pekee hiyo. Waheshimiwa Wabunge, tarehe 16 na 17 Julai, 2008 kutakuwa na maonyesho ya shughuli za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Bohari Dawa na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* kwenye viwanja vya Tafrija vya Bunge.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009
### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge jana tulipoahirisha shughuli za Bunge wafuatao walitajwa kujadili, Mheshimiwa Mercy Emmanuel, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Mzee Zuberi na Mheshimiwa Abdul Marombwa.

**MHE. MERCEY M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii muhimu ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii lakini,  nina machache tu ya kuweza kuongezea juu ya hotuba nzuri waliyoiwasilisha Mawaziri wetu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitaanza na masikitiko makubwa ya matokeo ya mitihani ya darasa la saba ya mwaka jana, ni kweli kabisa matokeo ya mitihani mwaka jana Tanzania nzima kumekuwa na rekodi ya wanafunzi wengi kutofaulu kabisa, mimi nilikuwa nafikiri kwamba ni lazima Wizara itakuwa imeshajaribu kufuatilia ni kitu gani kimesababisha wanafunzi wengi kutofaulu kuingia *form one*, kama tulivyokuwa tumeandaa madarasa ni kweli madarasa mengi yamebaki tupu wanafunzi hakuna wamefeli na waliofaulu ni wachache, sasa nilikuwa nafikiri labda Wizara inayo majibu ni kwa sababu gani hiki kitu kilijitokeza na tunafanyeje mwaka huu ili kurekebisha matatizo yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kujua labda mtihani ulikuwa ni mgumu au ni kitu gani kilijitokeza lakini kimsingi....

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge *order*, wanaotoka nje watoke kimya.

**MHE. MERCEY M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza lilikuwa ni hilo ambalo nilikuwa nafikiri kwamba ninahitaji ufafanuzi mzuri kabla ya kufika kipindi cha mitihani ili tuweze kuona ni jinsi gani watoto wetu wanafaulu vizuri na madarasa yetu tuliyoandaa watoto wanapata nafasi ya kuingia.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine cha pili nilitaka kuchangia kuhusu madarasa ya awali, (watoto wanaojifunza kuanzia miaka mitano, sita yaani chekechea) naweza nikasema kwamba watoto hawa mara nyingi wanakuwa na walimu ambao kwa kweli hawastahili kabisa kuwafundisha na ninaweza nikasema shule nyingi zinawachukua walimu majumbani na wanakuja kufundisha kwa hiyo unakuta mwalimu anapata uzoefu kutokana na wale watoto wanaoanza masomo lakani kimsingi tunaweza tukasema kwamba hawa watoto wasipoanza kwa msingi mzuri inawezekana wasifanye vizuri hata kule mbele wanakokwenda kwa sababu lengo la Wizara nadhani ni kuhakikisha kwamba mtoto anapoingia darasa la kwanza anakuwa ameiva vizuri angalau asije akasumbua sana anapokuwa anaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema na nimeona maeneo mengi walimu wamekuwa ni wachache, na hawapatikani na imeonekana kabisa kwamba labda hakuna umuhimu sana wa kupata walimu wazuri wa kuwapatia watoto hawa wa chekechea, kwa hiyo nilikuwa nashauri kwamba Wizara ijaribu kufanya utaratibu mzuri watoto hawa waweze kuanza vizuri, wapate walimu wazuri nafikiri watafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikasema hata hizi shule za *international* ukiangalia sana watoto wanaoanza chekechea kusema kweli wanakwenda vizuri sana, kwa sababu wameanza na msingi mzuri na walimu ni wazuri wame-qualify vizuri wanachukua walimu walioiva wanawaanzishia msingi mzuri kwa hiyo unakuta watoto wanakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri kwamba hata sisi Wizara ijaribu kufanya hivyo ili tuweze kuchukua watoto wazuri waweze kwenda katika msingi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nilikuwa nataka kusema ni posho ya kufundisha katika mazingira magumu. Ni kweli kabisa walimu wanafundisha katika mazingira magumu sana, wako vijijini sana, walimu wanawajibika kuongeza nguvu za ziada ili waweze kuona ni jinsi gani watoto wanafanya vizuri, kwa mfano kipindi hiki kuna shule nyingi ambazo walimu kwa kweli wanajituma sana kwa sababu mitihani ya darasa la saba imekaribia sana kwa hiyo unakuta watoto wanasoma sana, mwezi wa sita hawakufunga, wanakwenda shule mpaka Jumamosi, Jumapili lakini juhudi hizi mwalimu anazifanya ili aweze kutoa watoto wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hawa watoto siyo wa kwake na wala hapati zawadi yeyote wanapokuwa wamefaulu. Lakini unakuta anapokuwa anajituma hapati motisha yeyote ya kumtia moyo. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba Wizara ijaribu kuangalia Walimu wapo wengi rekodi zipo nyingi maeneo mbalimbali, utakuta watoto wanaofanya hivyo watoto wao kwa kweli wanafaulu vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanaweza wakafaulu wakabaki watatu au wanne lakini wanafaulu kwa sababu ya juhudi za walimu wanaojitolea kufundisha, kwa hiyo nilikuwa nafikiri kwamba Wizara ijaribu kuangalia posho za hao walimu wanaojitolea katika kipindi hiki, walimu wapo kijijini na wanafundisha katika mazingira magumu kwa hiyo nafikiri kwamba Wizara ijaribu kufuatilia ni jinsi gani ya kuwasaidia walimu hawa ili waweze kufundisha kwa moyo na kwa juhudi kwa sababu angalau Serikali inajaribu kuwajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie suala la watoto wa kike, hawa watoto wa kike kweli limekuwa ni tatizo kubwa, watoto wetu wanakuwa hawamalizi shule, lakini kinachojitokeza wanapata ujauzito kabla ya watoto, kweli kabisa hata walimu wanahusika lakini pia si walimu tu kuna watu wengine wa nje wanahusika lakini kingine hata wanafunzi kwa wanafunzi wanahusika kubebeshana mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naweza nikasema kwamba ni tatizo kubwa tunahitaji kila mtu abebe mzigo licha tu ya kuiambia serikali kwa sababu hawa watoto na shule tunazo kule tunakoishi. pia ninafikiri kuna haja ya kutafuta ni kwa jisi gani tunawasaidia watoto wetu ili waweze kuepukana na suala hili la kubeba mimba au kupata ujauzito kabla ya kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kitu kimoja kingine kinachojitokeza katika suala hili, ni kweli kabisa hawa watoto wakishapata ujauzito kwa mfano mwanafunzi amebebesha mimba mwanafunzi mwenzie wanasoma pamoja au shule tofauti, kimsingi watoto hawa wote ni wanafunzi ninachotaka kusema imefikia mahala hata watoto wa kike sasa wamekuwa wanaendekeza suala hili, ninaposema hivyo

ninamaana kwamba mtoto wa kike anapopata ujauzito anayebeba mzigo ni mtoto wa kiume mwanafunzi mwenzie kwa sababu amembebesha mimba. *(Makofi)*

Ukichukua historia ya huyu mtoto hata ukiongea naye anakuambia ametembea naye mara ya kwanza, ya pili, tatu na nne hajamwambia mwalimu, hajamwambia mama, hajamwambia rafiki yake hajamwambia mtu yeyote. Ninachotaka kujiuliza kwa nini na yule binti asiwajibike, mimi nina mtoto wa kike mzuri tu kama watoto wengine walivyo wa wazazi wengine. Kwa hiyo, mimi ninavyosema hivi si kwamba sina mtoto wa kike labda nina mtoto wa kiume, nina mtoto wa kike safi hata nikimleta hapa watachumbia mapema wanaotaka. (*kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema mimi sioni sababu mtoto wa kike akibeba mimba akibebeshwa mimba na wanafunzi mwenzie eti anawajibishwa mtoto wa kiume, mtoto wa kike naye awajibishwe kwa sababu hasemi ananyamaza kimya na imefikia mahala hata mzazi kwa mfano mimi mtoto wangu akipata ujauzito basi nitakimbia kwa yule mzazi nitamwambia kwamba haiwezekani, mtoto wangu hawezi kubebeshwa mimba ni lazima useme kwa nini ambebeshe mimba.

Sasa mimi ndiye ninayekuwa na uchungu sana sijiulizi kwa nini mimi mtoto wangu hajawahi kuniambia naishi naye, mimi nafikiri kwamba ifikie mahala hata Wizara ichukue pande zote mbili, mtoto wa kiume aliyebebesha mwenzie mimba na yeye awajibishwe na huyu mbebeshwa aliona ni vema inapendeza, kwa hiyo na yeye ifikie mahala awajibike aulizwe ni kwa nini unakubali mra zote hujasema, na wewe unatakiwa uadhibiwe, itafikia mahala watoto wa kike wataogopa, lakini sasa hivi wanajua mimi nitamsema, si yeye mwenyewe aliniambia, alikuambia ukamwambia nani, nafikiri Wizara ijaribu kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda watu wazima, watu wazima naweza nikasema kwa mfano mwalimu, mtu wa mitaani huyo kwa kweli kafanya makusudi kwa sababu anamwona huyu ni mtoto, huyo vyovyote itakavyokuwa lakini ninachosema ni mwanafunzi na mwanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia Ofisi ya ya Waziri Mkuu nilizungumzia juu ya suala la michango. Jana nilikuwa nimefurahi sana nilimwona Waziri wa *East Africa Community* alikuwa hapa nikadhani kwamba huu ujumbe akiupata nadhani ataufanyia kazi, unajua kama nilivyosema kipindi kile tunapokuwa tunachangia tunachangia kwa maslahi ya wananchi, na tunasaidiana sisi kwa sisi, mimi nikikuta tatizo Mtwara nikaja kulisema hapa ina maana ninamsaidia mtu wa Mtwara.

Lakini si kitu kwa sababu naona leo ndiyo mahali pake, nilichokuwa nataka kusema ile michango ya Nkenge, wakati ule ilikuwa kama mzaha sijui nini lakini narudia tena ile michango ni mikubwa, nilizungumza kwamba ndaninya familia kuna baba na mama wale wameoana, lakini mchango unaotakiwa labda ztuseme ni shilingi 28,000 lakini kinachokuja ni kitu kimoja mama anatakiwa achange, mama anatakiwa achange, sasa mimi nilikuwa nafikiri siyo sahihi kwa sababu baba akishachanga ina maana ile familia imechanga tayari kwa hiyo hakuna haja ya kuchanga baba na mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado hata ile michango ya sijui ya matofali wanakata katikati, mama anatakiwa apelike, na baba anatakiwa apelike, kwa hiyo wale ukipiga hesabu nilikuwa nafikiri kwamba kuna haja ya kufuatailia pesa ile ni kubwa mno na iayoliwa ni kubwa sana na ninasikitika kusema kwamba wanaofuatilia hivyo ni Madiwani, Diwani wa kata ya Nkenge naongea kwa ujasiri namfahamu sura na anakimbiza watu majumbani suala hili siyo zuri naomba Wizara ifuatilie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwamba kama litafuatiliwa mapema litasaidia hata ujenzi unaoendelea mbele lakini kama litanyamaziwa kwa kweli litaleta athari na sisi kama wawakilishi wa wananchi bahati nzuri sisi wapinzani tunatangatanga mno ndiyo maana tukileta habari watu wanafikiri zinatoka wapi, sisi kazi yetu ni kukusanya yale tunayoyaona hayafai, kwa hiyo ukisikia tumeenda sehemu Fulani ni kweli tumekwenda na tumeona na tunaiambia Serikali ijaribu kurekebisha, naomba Wizara ijaribu kufuatilia hili suala ili watu waweze kuchanga michango inayotakiwa tuweze kufanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nizungumzie suala la pesa za walimu, wenzangu wameshazungumza madni mengi, ni kweli kabisa wanadai maeneo mengi, likizo, uhamisho, sijui vitu gani na kadhalika, lakini ninachotaka kusema na kinachonisikitisha kikubwa zaidi ni pale mwalimu anapokuwa anaumwa anatakiwa kwenda kutibiwa, hili ni tatizo kubwa nasikitika kuna kwamba anapokuwa anahitaji kwenda kutibiwa inakuwa ni shida sana kupata pesa ya matibabu, wanamwambia kwamba chukua pesa yeyote sisi tukija tutakurudishia hawezi kupata hii pesa sasa huyu mwalimu ataendelea vipi kufanya kazi, mimi nilikuwa nafikiri ifikie mahala matatizo mengine yatatuliwe moja baada ya jingine, kama Mwalimu anaumwa asaidiwe, mifano hii ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wanazunguka na wanakuta kesi hizi Wilayani si kwamba ni uwongo naiomba Serikali ijaribu kufuatilia, walimu hawa malimbikizo yapungue kila siku nikisimama hapa huwa nazungumza jambo moja kwamba unapofika wakati wa uchaguzi kwa mfano mwaka kesho.

Kusema kweli marekebisho yanarekebishwa hasa kwa walimu na ninaweza nikasema wanarekebishiwa kwa sababu wanasimamia uchaguzi ili waweze kufumba macho mimi sikubaliani na suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama ni kurekebisha inatakiwa marekebisho yaanze mapema lakini kwa sababu wanajua walimu watasimamia uchaguzi basi wanawafunika funika na ninaweza nikasema na kwa sababu walimu masikini na wenyewe Mungu kawapa roho kama ya watoto basi wanaachilia lakini naomba Wizara inauwezo mkubwa wa kuekebisha haya madeni, ili mjaribu kufanya vizuri walimu wetu waweze kufundisha katika mazingira mazuri.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kuzungumza pia suala la mafunzo juu ya walimu…

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja lakini…eeh! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii muhimu sana, naanza na kwa kumpongeza Waziri na wasaidizi wake wote kwa kazi ngumu ya kuandaa hotuba kama hii na kuiwasilisha Bungeni maana Wizara hii sasa inashughulikia kuanzia *pre school* mpaka *post graduate studies* ni eneo kubwa sana wanaloshughulikia nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugomvi wangu wa kwanza kabisa ni hili suala la mitihani, kufutwa au kubadilishwa kwa mtihani wa darasa la nne na mtihani wa kidato cha pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipita humu nchini unasikia malalamiko mengi sana ya wazazi kwamba mtoto anamaliza darasa la saba hajui kusoma hajui kuandika hajui kuhesabu, maana yake ni kwamba mtoto huyu ametumia miaka saba lakini hakupata kile alichoendea shuleni.

Mitihani hii ni njia ya kutambua kama mtoto huyu kweli anafaidika na masomo yale anayopewa ama hafaidiki nayo, kama hafaidiki apewe fursa ya kurudia masomo yale mpaka afaidike nayo, sasa unaposema unaondoa mtihani mtoto aanze tu darasa la kwanza mpaka darasa la saba unasema nini, unasema huyu mtoto atumie tu muda wake shuleni miaka saba akipata ama akikosa shauri lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi wazazi tunasema hapana hiyo si sahihi, huyu mtoto apimwe tujue kama anapata kile kinachotakiwa kama hapati tumrudishe asome mpaka akipate, *form two* hivyohivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu jana nimeletewa meseji kutoka kwa walimu hapa wakikataa kata kata kwamba mitihani hii isifutwe inawasaidia kuwafundisha watoto wao na kuwawezesha kufanya vizuri wanapofika kidato cha nne na huko mbele ya safari.

Kwa hiyo mimi naomba Wizara isiwe na hii tabia ya kubadilisha badilisha mambo na wanapotaka kubadilisha wafanye *studies* kwanza na wathibitishe kwamba hiyo ndiyo njia pekee iliyopo ndipo wabadilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka tulikuwa na ugomvi hapa wa kufutwa kwa michezo mashuleni, tukapiga kelele hapa Bungeni haikurudishwa, katika hili tunaomba msifanye mabadiliko mpaka tukae tuelewane.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitihani hii ni *insentive* kubwa sana kwa walimu kufundisha watoto wao kwa bidii kwa kutaka wafaulu, ni *insentive* kubwa sana kwa wanafunzi kufanya bidii sana ili wafaulu mitihani yao, sasa tunapofuta badala yake nini, ni kwamba tukae tu miaka mine halafu mtoto huyo anarudi nyumbani kama alivyokwenda shule.

Mimi nafikiri hilo siyo sahihi. Naomba tusiwalaumu Wakoloni juu ya hili maana tumeshajitawala miaka karibu 50, hivi baada ya miaka 50 bado Mkoloni ndiye anayetuamulia mambo ya kufanya? Kwa hiyo, naomba Wizara isifute wala kubadilisha mitihani hii. Sisi ndiyo wazazi, sisi ndiyo wenye shule na tunafikiri mitihani hii inasaidia watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni pongezi, ninapenda niipongeze sana Serikali, niwapongeze wananchi wa nchi hii kwa haya maendeleo makubwa sana tuliyopata ya elimu katika miaka hii michache iliyopita. Sasa hivi wanafunzi wameongezeka katika shule za msingi kwa malaki, wameongezeka kwenye shule za sekondari kwa malaki. Hii ni juhudi nzuri sana na naomba kwa kweli tujipongeze sana kwa haya mafanikio tuliyopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa linakuja suala ambalo linazungumzwa la *(quality)* ubora wa elimu, je, shule hizi zinaweza kutoa elimu iliyo bora? Jibu ni ndiyo! Unahitaji shule kwanza, ukishapata hiyo shule ndiyo uzungumzie ubora. Hivi unaweza kuzungumzia ubora wakati huna shule? Mtoto yuko nyumbani, wewe unazungumzia ubora wa elimu yake, ana elimu gani wakati huo yuko nyumbani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo la kwanza tulilofanya ni kujenga shule halafu baada ya kujenga shule tumejiundia matatizo mengi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa Walimu, vitabu, vifaa na kadhalika ili tufikie huo ubora. Sasa ndiyo kazi tunayofanya sasa hivi ya kuhakikisha kwamba hayo mahitaji sasa ya kupata ubora yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika hili tuungane Wabunge wote na wananchi wote tuhakikishe kwamba zile shule zilizojengwa, zinapata mahitaji yake ili ziweze kutoa elimu bora. Hivi ni lipi bora, mtoto kukaa nyumbani ama kwenda shuleni hata kama ubora wa elimu inayotolewa katika shule hiyo siyo mzuri? Maana ni bora kukosa kabisa kuliko kupata kiasi? Nafikiri *thinking* hiyo siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri kazi iliyofanyika ni nzuri tuendelee kuifanya ili ikamilike na kwa ubora huo tunaotaka. Wala tusifike mahali tukasita kwamba hivi kukosekana kwa mambo haya yote je, bado tuko katika njia ile tuliyotaka kwenda?

Tuko katika njia, tunachohitaji ni juhudi zaidi, ni maarifa zaidi, ni kuelekeza vizuri zaidi *resources* zetu ili tuweze kupata elimu iliyo nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napongeza sana Serikali kwa maamuzi yake haya kwamba watoto wote wapatr elimu ya msingi kwamba watoto wanaofaulu shule za msingi wote waende sekondari na nategemea watakaofaulu shule za sekondari wote waende Chuo Kikuu, halafu baada ya hapo tutazungumza juu ya hayo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nafikiri fadhila huanza nyumbani, naomba nirudi Dar es Salaam. Sisi wa Mkoa wa Dar es Salaam, tuko katika hali ngumu kweli kweli na hali ya kipekee kabisa. Asilimia 10 ya Watanzania wanaishi Dar es Salaam, kwa hiyo watoto tunaozungumzia Dar es Salaam ni watoto wengi. Mahitaji yetu ya shule ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi sana tulizembea, hatukujenga shule kwa kasi iliyotakiwa. Kwa hiyo, tulikuwa na upungufu mkubwa sana wa shule za msingi, tulikuwa hatuna shule za sekondari, tulikuwa na shule chache sana. Ijapokuwa huko Mikoani walikuwa wanaamini kwamba Dar es Salaam ndiko kwenye shule, ndiko kwa kupeleka watoto lakini ukweli ni kwamba Dar es Salaam tulikuwa nyuma sana katika hili suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa MMEM imetusaidia, tumejenga shule za msingi lakini kabla ya kukamilisha kukidhi mahitaji ya shule za msingi ikaja MMES sasa ilipokuja MMES kwa kweli shule za msingi zimesahaulika na sasa hivi karibu robo tatu ya shule zilizoko katika Jimbo langu zina watoto zaidi 100 kwa kila chumba cha darasa. Tumerudia katika matatizo yale yale tuliyokuwa nayo. Naomba Wizara ihakikishe kwamba MMEM inaendelea mpaka tukamilishe mahitaji ya shule za msingi, kwa kutupatia ule mchango ambao Serikali inatoa na sisi na wazazi wenzetu tujitahidi kujaza lile pengo linalobaki. Naomba sana Waziri hili ulizingatie vinginevyo tunapata matatizo makubwa si rahisi Mwalimu kufundisha watoto 100 au 80, lengo la Wizara ni watoto 40 au 45 kwa kila darasa. Naomba mtusaidie tufikie lengo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni shule za sekondari. Dar es Salaam tumejenga shule za sekondari nyingi sana, hii shule za sekondari moja kwa kila kata inawezekana pengine Mikoani. Dar es Salaam kata moja ina watu wengi karibu kama baadhi ya Wilaya katika nchi hii. Kwa hiyo, haiwezekani kujenga shule moja. Ukienda maeneo kama Kibamba unakuta zimejengwa shule za sekondari mpya 8, Mbezi wamejenga shule za sekonadari 3, Goba wamejenga 5 na kadhalika. Kwa hiyo, tumejenga shule nyingi sana za sekondari katika kipindi hiki. Lakini tumejiundia matatizo makubwa sana pia. Maeneo ya kujenga yanapatikana pembezoni mwa Jiji siyo katikati ya Jiji. Ndiyo maana shule hizi zimejengwa kwa wingi Kibamba ambako maeneo ya kujenga yanaweza yakapatikana, Goba ambako maeneo ya kujenga yanaweza yakapatika, Mbezi, Kimara na Makuburi na kadhalika. Kata za katikati ya Jiji, tulipojitahidi sana tukaweza kujenga shule moja ya sekondari. Sasa matatizo ya kwanza ni kwamba watoto karibu wote katika shule hizi wanatoka nje ya mitaa zilikojengwa shule hizi. Kwa hiyo, kuna tatizo kubwa sana la usafiri kupeleka watoto hawa shule. Tatizo hili ni kubwa sana na kutokana na nauli ndogo ambayo watoto hawa wanatakiwa walipwe kwenda shule kwa sababu mabasi

yanawakataa, kwa hiyo, watoto wengi sana wanachelewa kufika shuleni hilo ni tatizo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu mmoja wa shule ya Sekondari ya Goba, anachofanya ni kwamba kila siku asubuhi anakwenda Tangibovu anakodisha mabasi ya kusafirisha watoto wake kwenda shule na yeye anachukua basi la mwisho kwenda shuleni kwenda kuwafundisha hawa watoto wanapokuwa wamefika. Lakini nauli wanayowalipisha wale watoto kwa njia hiyo ni shilingi 100 kwa kila mmoja siyo shilingi 50 anawafikisha shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna tatizo kubwa sana. Hizi shule tumezijenga lakini kuwafikisha watoto hawa katika shule hizo ni tatizo kubwa kweli kweli. Mimi naamini tatizo hili liko huko Mikoani pia. Maana kama katika kijiji kimoja pana shule ina maana watoto wasafiri kutoka katika vijiji vingine kwenda katika shule katika kijiji hicho. Sasa kuna mambo ambayo tunaomba Serikali itusaidie, la kwanza kadri itakavyowezekana tujenge hosteli za hawa watoto hasa wa kike hasa katika shule hizi mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zijengwe hosteli ili kuwapunguzia watoto adha ya kusafiri kutoka nyumbani mpaka shuleni na hatari zote wanazokutana nazo barabarani. Kwa hiyo, tunaomba sana suala hili litiliwe mkazo na kwa kweli tuhakikishe kwamba hawa watoto wa kike wanalala shuleni. Baadhi ya shule zimekuwa bunifu zimetafuta watu wenye majengo yao wamekodisha majengo yale wanaweka huko watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo langu ni kwamba sasa wanalelewaje hawa watoto? Nani anayewatunza? Nani anahakikisha kwamba wanakula sawa sawa? Kwa hiyo, tatizo hili ni kubwa na ninaomba lifikiriwe na Wizara itusaidie tuweze kujenga hosteli hizi ili watoto hawa waweze kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili, ni Walimu. Katika shule hizi hakuna nyumba za Walimu, kwa hiyo Walimu wanaishi mbali kutoka kwenye shule zao, wanasafiri kila siku asubuhi kwenda shuleni, wakimaliza kufundisha wanasafiri kurudi nyumbani, ni kazi ngumu kweli na ukifikiria kwamba Mwalimu huyu gharama zote hizi anajilipia na hakuna utaratibu wa kumfidia. Utakubaliana na mimi kwamba hawa Walimu wanafanya kazi ya wito, kazi ya kujitolea, naomba tuchukue nafasi hii kuwapongeza sana na kuwashukuru kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuombe basi Serikali ione hili tatizo na itusaidie tujenge nyumba za Walimu nyingi kadri inavyowezekana ili Walimu waweze kuishi karibu na maeneo yale wanakofundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuangalie maslahi ya Walimu hao maana tunalalamika kwamba Walimu hawatoshi na kwamba tutajitahidi tupate Walimu wa kutosha, lazima tuwape hawa Walimu vivutio vitakavyowafanya wakubali kufundisha kwa moyo. Hii ya kusema kwamba Ualimu ni wito, kweli ni wito lakini kama una njaa huu wito bado upo? Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iangalie suala hili. Hili suala la

maslahi ya Walimu, mahali watakapoishi na mahitaji yao mengine, lizingatiwe ili Walimu wetu waweze kukaa katika shule zile na kufundisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia watumishi wa Serikali waruhusiwe kukopa vyombo ya usafiri. Kwa mfano, Walimu nao waruhusiwe kukopa vyombo vya usafiri kama magari, pikipiki na vifaa vingine ili waweze kusafiri katika maeneo yao ya kufundishia. Nafikiri tukiweka mambo haya yote pamoja, watu watavutika kwenda katika kazi ya Ualimu, watu watavutika kufundisha kwa bidii na watoto wetu watapata elimu ile ambayo tunakusudia kuwapatia. Naomba sana Wizara iangalie masuala haya na iangalie ni jinsi gani tunavyoweza kuyatekeleza ili kuhakikisha kwamba elimu katika nchi yetu hii inaendelea vizuri inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru sana kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa siku hii ya leo.

Kwanza, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Waziri kwa hotuba yao nzuri waliyowasilisha jana kwa umakini tu ambayo inaleta mwangaza katika elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunachangia lazima tusaidiwe maji au tukikosa maji hata ule uyoga, unatufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nataka kulichangia leo, ni kuhusu Sheria ambayo imeanzisha Vyuo Vikuu Tanzania. Sheria ambayo imeanzisha Vyuo Vikuu Tanzania, ni sheria ambayo imepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatumika na vyuo vyote Tanzania pale wanapotaka kuanzisha vyuo vikuu. Wakati huo huo, Baraza la Wawakilishi nalo limepitisha Sheria ya Chuo cha Suza kuhakikisha kuwa nacho kinafanya kazi katika Tanzania hii hii. Sasa cha msingi ambacho nataka kuzungumzia hapa, lipo tatizo nafikiri linaweza likajitokeza, vyombo viwili au taasisi mbili zinaidhinisha chombo kimoja ambacho kinaweza kikafanya kazi katika nchi hiyo hiyo moja, huku Baraza la Wawakilishi limeweka Sheria dhidi ya Chuo Kikuu cha Suza na Bunge la Tanzania limeweka Sheria juu ya Vyuo Vikuu. Sasa je, katika suala hili, Suza ni mwanachama wa TCU? Je, Suza ina *charter* yake ya kuhakikisha kuwa mambo yake yanakwenda katika utaratibu uliopangiwa? Naomba ufafanuzi zaidi kuhakikisha kuwa je, katika makubaliano yenu mliyokubaliana katika suala hili tunakwenda sambamba katika kutoa elimu ya Chuo Kikuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni kuhusu mitaala yetu. Ukweli suala hili nalipigia kelele sana hapa Bungeni katika bajeti zote hizi. Suala la mitaala Zanzibar au Tanzania, lina matatizo. Elimu ya msingi Zanzibar ina mitaala yake lakini wanapofika juu wana mtaala wa Muungano. Ni suala ambalo kwa kweli linatuyumbisha sana. Wanatoka darasa la kwanza mpaka darasa la saba, wanafanya mtihani ambao unatayarishwa na Wizara ya Elimu ya Zanzibar lakini wakifika *Form One*

mitihani yao inatayarishwa na Baraza la Mitihani. Ni tatizo kwa kweli lazima mliangalie kama tunakwenda sambamba katika elimu tuanze kutoka mwanzo tusikutane juu. Kwa nini tusikutane hapa mwanzo ndiyo tukaanza pamoja tusiwayumbishe hawa watoto. Kwa sababu unapoanza chini mpaka juu katika mfululizo wa aina moja tunakwenda sambamba lakini utaanza darasa la tisa lakini huku chini kila mtu mmoja anakwenda kivyake, ni tatizo kubwa ambalo linatukabili hivi sasa katika kutoa elimu Zanzibar. Hili nalipigia kelele sana kuwa tuliangalie. Katika mfumo huu ni wapi elimu bora inatoka, Tanzania Bara au Tanzania Visiwani? Tuunganishe mawazo yetu, tuhakikishe kuwa tunakwenda sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni katika mitihani ambayo inafanywa ya *Form Four*, *Form Six* na kuendelea, kwa uhakika Zanzibar tunafanya vibaya sana mitihani. Ukiangalia matokeo, miaka yote Zanzibar inafanya vibaya. Sasa Mheshimiwa Waziri tatizo ni sera, mitaala au mfumo wenyewe? Mbona hatuelewi kwa sababu mara zote Zanzibar inafanya vibaya lakini maelezo ya kimsingi hakuna. Kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Waziri mnapokaa na Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mliangalie hili suala je, tatizo nini? Kama sera mbaya tuzibadilishe, tatizo mfumo mbaya tuubadilishe, mitaala yetu mibaya tuibadilishe, tuhakikishe kuwa na wao Zanzibar wanafanya vizuri au kama tatizo ni Walimu, tuhakikishe kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inasomesha Walimu wengi zaidi au inatoa mafunzo zaidi kwa Walimu, naomba tuhakikishe hili tatizo linakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukweli uliopo Zanzibar katika mitihani yote ya *Form Four* au *Form Six*, wanafanya vibaya kwa kuangalia takwimu za Wizara ya Elimu. Dawa ni kuhakikisha kuwa suala hili tunalitafutia ufumbuzi ili wanafunzi wa Zanzibar nao wafanye vizuri katika mitihani yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni mitihani ya maarifa. Uko mtihani wa maarifa lakini huu mitihani wa maarifa ni maarifa kweli hauna *limit*, uko tu. Mtihani huu hauna sera, hauna *syllabus*, wala hauna muda wa kukaa katika darasa, ni lazima tuuangalie huu mtihani. Kama huu mtihani hauna maana, tuuondoshe kabisa kwa sababu ni mtihani wa maarifa sasa maarifa hayapatikani, unamuweka pale mtu miaka miwili, miaka mitatu au miaka minne yaani hujambadilishia elimu yake lakini bado unasema ni mtihani wa maarifa. Kwa hiyo, kama ni maarifa anayapata tuhakikishe kuwa anawekewa na mipango mizuri. Kuwepo na *syllabus* ambayo inaweza ikamuongoza, kuwe na sera ambayo inamuongoza. Lakini hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kikamuongoza kwa hiyo wanafanya vibaya sana au wanakaa muda mwingi hawajapanda daraja wala hawajafanikiwa katika hayo maarifa yao kuhakikisha kuwa wanavuka hilo lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia, ni kuhusu *TCU*. Katika hotuba ya Waziri amesema kuwa wanafanya ukarabati katika jengo la *Post House*. Wanatumia fedha nyingi sana hivi sasa katika kuhakikisha kuwa wanafanya ukarabati kwa nini wasitafute nafasi ya kuhakikisha kuwa wanajenga ofisi zao wenyewe za kujitegemea? Hili tatizo kwa kweli Tanzania tunalo ukiliangalia katika Wizara tofauti tofauti hata Wizara ya Fedha yenyewe inatumia hela nyingi katika kupanga majengo ya

taasisi mbalimbali lakini hawawezi kujenga ofisi zao wakahakikisha kuwa wanakidhi haja ya zile taasisi. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kuwa badala ya kutumia hela nyingi kukarabati, kupanga lazima tutumie hela nyingi katika kujenga ofisi zetu ambazo tunaweza tukajitegemea tuhakikishe kuwa hizi ofisi ni zetu na wakati mwingine mnaweza mkapangisha na kupata hela ambayo inaweza ikakusaidia wewe mwenyewe vizuri tu. Kwa hiyo, ipo haja kuhakikisha kuwa tunabadilika hivi sasa baada ya kuhakikisha kuwa tunapanga badala yake tunajenga ofisi zetu na kuhakikisha kuwa zinatusaidia katika mambo yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Chuo cha Mwalimu Nyerere. Nililizungumzia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nalirudia tena, wamesema wanakarabati majengo yaliyopo. Lakini hivi sasa Chuo cha Mwalimu si cha kukarabati mabweni yaliyopo, hivi sasa ni kuhakikisha kuwa wanaongeza mabweni yaliyopo, kwa sababu wanaongeza idadi ya wanafunzi kwa kiwango kikubwa sana lakini idadi ya mabweni ni ile ile. Hivi sasa wanafunzi waliopo pale wanabebana wanalala wawili wawili, kwa hiyo, ipo haja hali hii kuibadilisha. Kwa hiyo, wanavyoongeza idadi ya wanafunzi wahakikishe na miundombinu wanaibadilisha, inakuwa ni bora. Kwa hiyo, nashauri wahakikishe mabweni ya pale yanaongezeka siyo kufanya ukarabati tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zile fedha ambazo wametengewa kwa ajili ya kufanya ukarabati wahakikishe kuwa na ujenzi wa mabweni unaenda sambamba na idadi ya wanafunzi, kwa kweli inavyoongezeka na mabweni yaongezeke ili kuondoa usumbufu uliopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu *Science Marine* na hili nililizungumzia sana, nikatoa takwimu ya jinsi suala hili linavyokwenda hivi sasa. Lakini kwa kweli hatujawa *serious* na hili suala na kwa kweli kama tupo *serious* lazima *Science Marine* ianze vizuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Taasisi ambazo zipo Zanzibar hivi sasa na juzi tu uliwekwa mkataba wa Ofisi ya Makamu wa Rais, nafurahi sana kwa kweli umekwishawekwa. Haya mambo mengine kama tunayachukulia *serious* namna hii, tutaenda vizuri na tuhakikishe kuwa hii *Science Marine* inakwisha isiwe ni historia na ndoto za kila siku ambazo tunakuja hapa tunapiga kelele kila siku wakati fedha inayotengwa ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni Baraza la Mitihani. Kwa kweli Baraza la Mitihani, ni Baraza ambalo linafanya kazi katika mazingira magumu sana. Nawapongeza sana, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na wanafikia mahali kwa kweli wanakwazwa sana, kwa sababu wanatunga mtihani wa darasa la nne, wanatunga mtihani wa darasa la saba, wanatunga mtihani wa kidato cha pili, yaani hawapumziki wanafanya kazi katika mazingira magumu. Lakini wana uchakavu wa vifaa vilevile, hatuoni Serikali kupunguza ushuru wa vile vifaa ambavyo vinaingia nchini katika Baraza la Mitihani. Serikali ipunguze ushuru kuhakikisha kwamba wale wanafanya kazi vizuri sana na kwa ufanisi. Kwa hiyo, Serikali ipunguze

ushuru kuhakikisha kwamba vile vifaa vinavyoingia nchini hawatozwi ushuru na kuvigharamia fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nimefurahi sana kuwa Baraza la Mitihani linajenga ofisi Zanzibar. Kwa kweli hili ni suala zuri sana na kuacha yale mambo ya kupanga kwa sababu wanaanza kujenga ofisi yao ambayo itawasaidia wao wenyewe kuhakikisha kuwa wanakuwa na ofisi zao za kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la wanafunzi kuzuiliwa kufanya mitihani, wengine wanafutiwa kabisa kwa udanganyifu yaani kila mmoja anafutiwa yale matokeo kulingana na vile alivyodanganya Baraza la Mitihani lakini tatizo lipo wapi? Wale wanafunzi ambao wanafanyiwa uchunguzi, uchunguzi ufanyike haraka, kuna wengine wanafutiwa matokeo halafu wanaambiwa wanafanyiwa uchunguzi, lakini uchunguzi huo unachukua muda mrefu. Kwa hiyo, kama ni uchunguzi, uchukue muda mfupi ili kuhakikisha kwamba wale wanafunzi wanapata nafasi ya kujiweka katika mazingira ambayo kwa kweli yanaweza yakawasaidia katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu walemavu. Katika utafiti uliofanywa mwaka 2006/2007, ulionyesha kuwa katika ujenzi wa madarasa katika Halmashauri nyingi nchini haukidhi mahitaji ya walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisoma hiyo taarifa inavyosema hali ya majengo katika Halmashauri zilizofanyiwa utafiti katika Wilaya nne, zinaonyesha madarasa 414 lakini hakuna hata darasa moja ambalo lilijali maslahi ya walemavu. Kwa kweli huu ni udhaifu. Kwa kweli hakuna mlemavu aliyejaliwa katika Halmashauri kwa kuhakikisha kuwa katika madarasa hayo na walemavu nao wanaweza wakaingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na kingine ambacho kinasikitisha zaidi ni huduma za shuleni kama chakula, mashine, usafiri, fimbo nyeupe na mambo mengine, hakuna shule ambazo zinajali matatizo ya wale walemavu. Kwa hiyo, hilo ni tatizo la msingi ambalo kwa kweli inabidi waliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine la hatari zaidi katika hizo Halmashauri ambazo zilifanyiwa utafiti ni vyoo yaani mlemavu utampelekaje shuleni kama hakuna huduma ambayo inamhakikisha kuwa anaweza akafika vizuri katika vyoo? Hili ni tatizo sugu kwa kweli Halmashauri zetu zinapojenga majengo ya madarasa zizingatie kuwa kuna jamii ya walemavu ambao wanahitaji hiyo huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la kumalizia ni suala zima la Walimu. Mimi nilikuwa Mwalimu nashukuru sana na ninazijua shida za Walimu zilivyokuwa, lakini Walimu wana kero nyingi kweli. Lakini kero hizo zinaonekana kama ni za kawaida, na fadhila za Mwalimu ni kujisifia tu, Profesa yule nimefundisha mimi, Waziri yule nimemfundisha mimi, ili mradi tu, hiyo ndiyo sifa ya Mwalimu. Lakini hakuna kitu

kingine ambacho anafanyiwa mpaka wakati anastaafu afanyiwe tafrija. Wanaofanyiwa tafrija basi wanapewa cherehani na baiskeli, hiyo ndiyo tija ya Mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine cha kuzingatia katika kero za Walimu ni kuhusu mishahara. Katika mishahara yao, michango ipo mingi sana ambayo wanakatwa bila ridhaa yao, hawashirikishwi katika kukata michango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vilevile kauli ya Mheshimiwa Rais, inasema kuwa mishahara ianze kulipwa kuanzia tarehe 25 ya kila mwezi na kuendelea, lakini bado mishahara inaweza kulipwa zaidi ya tarehe hizo. Kwa hiyo, hili ni kero kwa Walimu ambalo lazima lishughulikiwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akinijibu swali langu, tarehe 26 Juni, 2008, alieleza wazi kuwa hakuna masuala ya siasa katika taaluma au katika elimu. Mimi nilifurahi sana kwa sababu siku zote unapoleta siasa kwenye taaaluma au kwenye elimu, basi ujue hiyo elimu itakuwa siyo sahihi na haitowasaidia wananchi wa eneo hilo au wa nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nachangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilizungumza kwa zaidi ya dakika kumi kuhusiana na Mtihani wa Darasa la Nne. Mheshimiwa Waziri katika Bunge lililopita alisema Mtihani wa Darasa la Nne umeondolewa na sasa hivi amethibitisha tena kwamba hiyo mitihani itakuwepo tu, mwanafunzi atafanya huo mtihani akifaulu ataendelea na masomo na akifeli ataendelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala zima la mtihani, ukichukua mwongozo wetu hasa kwa upande wa mtihani wa elimu ya msingi, ukichukua huu Muhtasari wa Elimu ya Msingi, una mambo mengi. Kwanza, unaeleza madhumuni ya elimu ya msingi ni nini. Dhumuni la kwanza kwa idhini yako naomba nisome.

*“Dhumuni la Elimu ya Msingi kwa nchi yetu hii ya Tanzania, ni kupata stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, ubunifu na kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndiyo dhumuni. Yapo mengine mengi lakini dhumuni namba moja ni hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa pili, ni upimaji wa wanafunzi? Mwanafunzi tunampima nini? Katika muhtasari huo huo uliondaliwa na Wizara yetu,

unaeleza wazi kuwa safu ya upimaji inamwelekeza Mwalimu kuhusu aina ya maswali ya kujiuliza katika kupima iwapo lengo husika limefikiwa au laa! Lakini inasema maswali ya upimaji yanatokana na malengo mahsusi yaliyowekwa na Mwalimu. Mwalimu anashauriwa azingatie maswali hayo ya upimaji kila anapomtathmini mwanafunzi alikofikia katika malengo mahsusi. Hayo ndiyo malengo ya upimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba sana Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, iangalie kwa nini ilileta Mtihani wa Darasa la Nne. Kwa nini Mtihani wa Kidato cha Pili, ulilетwa katika Wizara yetu hii? Waangalie sababu zilizopelekea mpaka hiyo mitihani ikawepo. Je, kwa wakati huu tuliokuwa nao sababu hizo zimeondoka? Hivi katika shule zetu tuna wanafunzi 40 au 45 katika kila darasa? Hivi katika shule zetu tuna Walimu wa kutosha? Kila shule ya msingi katika nchi yetu ina Walimu wa kutosha? Hivi katika shule zetu kuna madarasa ya kutosha? Hivi katika shule zetu kuna vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyolingana na idadi ya Walimu walikuwepo na wanafunzi waliokuwepo? Hivi katika shule zetu Walimu wetu wanaishi katika nyumba nzuri au wanahangaika hangaika tu katika nyumba za kupanga, leo wako hapa na kesho wako pale, wanaandaa vizuri kweli masomo yao, wanaandaa vizuri maazimio ya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama haya ambayo yalipelekea wakati ule wakasema hapana, kutokana na ukubwa wa madarasa yetu hayo, tuna upungufu mkubwa sana wa Walimu, tuna upungufu mkubwa sana wa madarasa, darasa linakuwa na wanafunzi 100, ni vizuri tuamue tuweke hiyo mitihani ili wale watakaokuwa na uwezo wa kufaulu ule mtihani, waendelee na masomo na hao ambao hawana uwezo basi wapatiwe nafasi ya kurudia kwa mwaka moja, mwaka wa pili wakifeli wataendelea na masomo kama kawaida, Wizara hiyo inaona haifai?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hii sikubaliani nayo na niseme tu endapo leo itapitishwa basi mimi nitaleta Hoja Binafsi kuhusiana na suala hili. Wanaotakiwa kuamua suala hili, hebu washirikishe wadau wa elimu, wasikae watu wawili, watatu wakaamua mawazo kama hayo ambayo yanaumiza. Mwanafunzi anaporudia darasa, unamsaidia kumrekebisha zaidi ili masomo yale aweze kuyaelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika saikolojia ya ukuaji, mtoto anaweza kukua kiakili lakini kimwili anaweza kudumaa lakini mtoto mwingine anaweza kukua kimwili, kiakili akadumaa. Lakini kwa kurudiarudia jambo hilo, uwezekano wa huyo mtoto kuendelea vizuri na masomo upo. Kukariri au kurudia, ni mojawapo ya njia nzuri kabisa ya kufundishia kama wewe ni Mwalimu mzuri. Sasa unapoondoa kukariri, ili mradi watoto waweze kumaliza Darasa la Saba *then what*? Wamalize Darasa la Saba, basi? Hapa tunakwenda kisiasa, hatwendi kitaaluma na hatuwatendei haki wananchi na wanafunzi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sana watu wanasema kwamba elimu ya Tanzania ukiilinganisha na elimu ya nchi zote za Afrika Mashariki, hakuna Mtihani wa Darasa la Nne, hakuna Mtihani wa Kidato cha Pili, ni kweli kwa sababu elimu yao ni bora. Ukienda kwenye darasa la Kenya huoni darasa lenye wanafunzi 100. Ukienda Uganda, hulioni hilo darasa lenye wanafunzi 100 kama la kwetu! Wao madarasa yao

yako *intact,* Walimu wanapata marupurupu ya kutosha. Unaposema kwamba hawa Walimu wetu watafundisha masomo haya baada ya kufeli, wale watoto watachaguliwa, watachambuliwa na watawekwa kwenye madarasa ya *remedial*, yaani ufundishaji ule wa ziada, tumewaandaa hawa Walimu? Shule za kwangu kule Walimu watatu, madarasa 7, huyo Mwalimu atapata muda wapi wa hiyo *remedial teaching?* Nani atakayefundisha? Kwa Mwalimu wa aina hiyo, tunaongopeana. Hebu tueleze ukweli kuhusiana na suala hili. Tusilipeleke hivi hivi tu, wadau wakae, waone na watafakari, tusiamue sisi wenyewe moja kwa moja. Hilo ni langu la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni mpango wa elimu ya msingi kwa aliyeikosa MEMKWA. Mpango huu katika nchi yetu siyo mbaya ni mpango mzuri lakini utekelezaji wake umejaa matatizo mengi. Wale Walimu wanaofundisha wanafunzi hawa wa MEMKWA posho yao ile ya Sh.20,000 imepitwa na wakati. Leo Mwalimu anafundisha mwezi mzima unampa Sh.20,000 hata kununua sabuni anashindwa huyu mtu, anakaa pale kwa zaidi ya masaa matatu, manne anafundisha. Sasa naomba posho kwa wale Walimu wanaofundisha masomo ya MEMKWA ziangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, ni kuhusiana na mitaala. Wizara ya Elimu miaka yote inaenda kwenye mabadiliko ya mitaala, kila mwaka mabadiliko yanatokea. Mabadiliko haya, semina zake zinafanyika kwa viongozi wa juu tu, lakini wale ambao wana-*implement* mabadiliko hayo ambao ni Walimu wa Shule za Msingi, hawahusishwi. Semina zinamalizika huko juu lakini huku chini hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kifungu cha *training* katika Halmashauri, unapewa Sh.6mil, una Walimu 2,000, unaleta mabadiliko ya mitaala, unapoleta mabadiliko Sh.6mil zitasaidia nini? Semina gani zitakazofanyika ili hawa Walimu waelewe huu mtaala mpya ambao unatolewa? Naiomba tena Wizara wanapotaka kubadili mitaala, wajiandae kwa kuwa na fedha za kutosha pamoja na kuwafanyia semina wale viongozi wa kule juu lakini waweke fedha kwa ajili ya Walimu ambao wana kazi ya ku-*implement* hiyo mitaala kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni mgawanyo wa Walimu. Katika nchi yetu, mgawanyo siyo mzuri hata kidogo. Ukikiangalia kitabu hiki cha *Basic Education Statistics in Tanzania (BEST)* cha mwaka 2004 mpaka 2008 kwa mfano, Mkoa wa Shinyanga, nilikuwa najiuliza hivi hawa Wasukuma hawana akili wajukuu zangu? Kwa nini miaka yote Wasukuma wanakuwa wa mwisho katika mitihani ya Kitaifa? Lakini ukiangalia ndiyo Mkoa wenye uwiano mdogo kabisa baina ya Mwalimu na Mwanafunzi. Mkoa wa Shinyanga kwenye kitabu hiki, ukurasa wa 34, inaeleza wazi kwamba kila Mwalimu mmoja wa Shinyanga anafundisha Wanafunzi 74 na mwaka jana Mkoa wa Shinyanga ulifaulisha kwa asilimia 33 tu, Wanafunzi 74 kwa Mwalimu mmoja tu kama wewe ni Mwalimu kweli, huwezi kufundisha! Mkoa wa Tabora ni Wanafunzi 68 kwa Mwalimu mmoja. Mkoa wa Mwanza, Wanafunzi 66 kwa Mwalimu mmoja. Kigoma, Wanafunzi 60 kwa Mwalimu mmoja. Rukwa, Wanafunzi 60 vile vile kwa Mwalimu mmoja. Mikoa hii yote *performance* yao siyo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ilione suala hili kwamba kwa sasa tusipeleke Walimu katika Mikoa ambayo ina Walimu wa kutosha na kwa nchi yetu iko miwili tu, Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Dar es Salaam, tusipeleke Walimu huko. Kwa sababu *pupil teacher ratial* ya Mkoa wa Dar es Salaam ni Wanafunzi 38 kwa Mwalimu mmoja vile vile na Mkoa wa Kilimanjaro. Sasa utakapoona kuna shule ambazo zina upungufu wa Walimu, ni kutokana na *poor distribution of Teachers* katika Mikoa hiyo lakini siyo kwamba Walimu hawatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaangalia huu mgawanyo wa Walimu ambao tunaletewa tukiona Walimu wanakwenda katika Mikoa hiyo bila kuzingatia ile Mikoa ambayo ina upungufu mkubwa wa Walimu kwa kweli sitaunga mkono mgawanyo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie suala la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dr. Siyame na Mheshimiwa Dr. Mlingwa ajiandae na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed naye ajiandae.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nipate kushiriki katika kuchangia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba yao mahiri, yenye ku-*cover* karibu kila eneo la Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza niseme nimefurahishwa na nukuu yao ya dira kwa maana ndoto yetu ya kufikia mwaka 2025 inayosema kwamba ndoto yetu ama dira yetu, ni kuwa na Mtanzania aliyekamilika kwa kiwango cha juu, mwenye maarifa, mahiri na aliyekomaa kiutamaduni ili aweze kukabiliana na changamoto za kitaifa na kimataifa katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi ifikapo huo mwaka 2025. Ni namna gani tutafika hapo kwa maana ya dhima, wanatamka bayana kwamba inabidi kutoa fursa sawa ya elimu bora kwa wote na kuhakikisha kuwepo kwa mazingira ya kisheria na kiutendaji yenye mvuto kwa wadau wote, nia na uwezo wa kutoa elimu iliyo bora ili washiriki kupanua elimu iliyo katika ngazi zote pamoja na kuimarisha uendeshaji kwa kukuza utamaduni wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba nianze na nukuu ambayo ni tafsiri ya mwandishi mmoja wa hizi *poems* anayeitwa Robert Prouty, katika poems zinazoitwa '*Voice in the Wilderness*' kwa Kiswahili ni 'Sauti Nyikani'. Anaanza kwa kusema:-

*"Sihitaji kusulubikia, haki yangu ya kujifunza, ni yangu, na kama ni kutokana na sheria mbovu na makosa ya kiusanifu na maeneo mengi mno ambapo watu wengi sana hawajali, kama ni kutokana na sababu hizi zote na nyinginezo, kwangu mimi mlango wa darasa bado siufikii, bado siuoni, kasoro hizo haziniondolei haki yangu. Hivyo nipo hapa nami pia ni mmoja wenu. Kwa baraka za Maanani na zenu nitapata fursa yangu. Hatujawahi kukutana, bado hujanijua na hivyo bado hujajua kuwa kuna mengi unaweza kupata kutoka kwangu. Jina langu ndiyo kesho yangu na ninachodai ni haki, haki yangu ya kujifunza".*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimenukuu mambo haya kwa makusudi tu. Katika utafiti uliofanywa mwanzoni mwa mwaka huu, kati ya Januari na Juni kuhusiana na suala la kuandikisha na kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanabakia shuleni.

**NAIBU SPIKA:** Sogea kwenye chombo, ama sogeza chombo.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la kuandikisha na kuhakikisha wanabakia shuleni watoto wenye mahitaji maalum, inaonekana wazi kwamba katika ile Mikoa miwili ya Dodoma na Morogoro ambapo utafiti huu ulifanywa, hawa watu hawakupewa haki yao na inaonekana kwamba kile kiwango cha uandikishwaji cha hawa watoto hakikuzingatia wingi wao katika ile jamii wanayoishi. Hii inadhihirishwa kabisa na hata taarifa iliyomo kwenye hotuba hii ambayo kitakwimu kati ya watoto wote zaidi ya 8,800,000 waliojiandikisha si zaidi ya watoto 34,000 wenye ulemavu ambao walijiandikisha, ambao ni sawa sawa na asilimia 0.4 wakati katika jamii hii walemavu ni takribani asilimia 10. kwa hiyo, kilio cha hawa walemavu ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi ni vema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambayo, mimi kwa bahati nzuri ni mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, naomba niseme mapema, nilishiriki katika kuishauri kutayarisha hotuba hii, napenda niseme kwamba baada ya kuipata taarifa hii naona tuangalie upya mwenendo mzima wa utoaji haki sawa katika kuandikisha hawa watoto walemavu. Inadaiwa na hawa watafiti kwamba hakuna mafanikio katika kushawishi mabadiliko ya kisera kuelekea utoaji wa elimu jumuishi katika jamii hii na pia hakuna utashi wa kisiasa, kwa maana hata sisi Waheshimiwa Wabunge tunahusika katika kutowatendea haki. Hawa walemavu wanadai kwamba hata baada ya kuwa wameandikishwa kwenye hizo shule zao wanashindwa kuendelea na masomo yao kwa sababu hakuna vile vifaa maalum kwa mfano kitu wanaita shime sikio, nina hakika ni *hearing device* pia kuna fimbo nyeupe, kuna mashine za kuchapia nukta nundu kwa maana ya *braille*. Wanasema kwamba hata pale ambapo wanakuwa wametengewa hizo pesa kwa ajili ya kununulia hivyo vifaa, hizo pesa haziwafikii walengwa, zinatumika kama *general budget* ya hizo shule. Hivyo basi inabidi tuli-*address* hili suala kwa upya ili tuweze kuwatendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda baada ya kusema hayo, nije kwenye mfumo mzima wa *enrollment* ya watoto wetu wa shule hususan *net enrollment* yetu. Kufuatana na hotuba ya bajeti hii yaWizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tunaona kwamba kati ya darasa la kwanza hadi la saba, kuna watoto zaidi ya milioni nane lakini Walimu ni 154,000. Bila kujali uwiano mbaya wa mgao wa Walimu uliopo kati ya vijiji vya pembezoni kama kule kwangu na mijini kama Dar es Salaam, tunakuta kwamba Mwalimu mmoja anafundisha watoto 54. Hii ni kwa mijini tu kwa bahati mbaya ukija kule Mbozi Magharibi, Mwalimu mmoja ana watoto 200 ambapo ni hali ya hatari kabisa, inatakiwa iangaliwe upya. Tunahitaji kuhakikisha kwamba hawa watoto wanapewa elimu iliyo bora kwa kupanua milango ya kuwapatia mafunzo Walimu zaidi ili waweze kufikisha kile kiwango angalau Mwalimu mmoja aangalie watoto kati ya 35 na 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwenye elimu ya sekondari, tupongeze pia hatua ya Serikali ya kufanya ufanisi wa kujenga shule karibu kila Kata ambazo kwa kweli imetufanya tupige hatua mbele katika kutoa elimu ya sekondari. Lakini bado tatizo ni lile lile la Walimu kwamba tuna Walimu wachache. Mfano, pale kwangu Mbozi Magharibi, kwenye Kata zangu 11, nashukuru kwamba ndani ya miaka miwili tumeweza kujenga shule zaidi ya 10 wakati hapo mwanzo kulikuwa na shule zisizozidi nne lakini tatizo bado ni Walimu. Shule nyingi kati ya hizo zina Walimu watatu, wakati tuna vyumba vya madarasa vya mikondo 16, 16, ina maana kuna *shortage* kubwa mno ambayo inafanya watoto wetu wasipate elimu iliyo bora. Bahati mbaya kuna shule ambazo tulikuwa tumekamilisha mwanzoni mwa mwaka huu lakini kutokana na elimu duni inayotolewa kwenye shule za msingi pale kutokana na upungufu wa Walimu, shule zile tumeshindwa kuzifungua pamoja na kwamba watoto katika shule za msingi walianza 190 lakini wanaofanya mtihani ni 20 na kati ya hao walioshinda ni 18 ambao hawawezi kujaza hata mkondo mmoja wa darasa. Katika hilo, ninaomba Serikali iji-*address* tena upya kuweza kutoa upendeleo, kama alivyokwisha kusema msemaji aliyenitangulia kwamba, kwenye ile Mikoa ambayo uwiano wa Walimu sasa hivi ni Mwalimu mmoja kwa watoto 38 basi kwa muda na kwa makusudi tu tusimamishe upelekaji wa Walimu wapya ili tuweze kujaza zile sehemu ambazo zina upungufu kama kwangu ambako Mwalimu mmoja anashughulikia watoto 200 na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye elimu ya Vyuo Vikuu, nachelea kusema kwamba tutakuwa na matatizo makubwa kati ya miaka saba na 14 ijayo. Leo hii kati ya Darasa la Kwanza na Darasa la Saba, kuna watoto zaidi ya milioni nane, hawa ndiyo watoto ambao miaka saba hadi 14 ijayo watakuwa wako Chuo Kikuu. Kufuatana na hali halisi ambapo hawa watoto wa Shule za Msingi walioko kwenye shule zetu na jinsi tulivyojiwekea utaratibu wa kujenga shule zetu, milioni sita karibu na laki tatu hivi, watakwenda sekondari na nusu yao kwa maana ya milioni tatu wataingia *high school* na baada ya hapo nusu yao ambao ni zaidi ya milioni moja na nusu, watatakiwa kwenda Vyuo Vikuu. Nafasi zetu za Vyuo Vikuu kwa nchi nzima hazizidi 60,000. Sidhani kama katika miaka saba ijayo tutakuwa tumefikisha uwezo wa kuchukua hata nusu ya hawa watoto milioni moja na nusu ambao watakuwa wanahitajika kuingia Vyuo Vikuu. Hivyo hapa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ina kazi kubwa ya kuhakikisha hawa watoto hatuwaachi bila kuwatendea haki vinginevyo hawa ndio watageuka kuwa majambazi na watatudai sisi kutowatendea haki kwa namna ile isiyokuwa ya kawaida.

Kwa hiyo, inabidi kujipanga upya kuhakikisha kila mdau anashirikishwa ili aweze kutoa mchango wake katika kuhakikisha elimu ya juu inafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme hivi, sasa inasikitisha, Vyuo vyetu Vikuu kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo sisi wakati tunaingia kila chumba walikuwa wanalala wanafunzi wawili lakini nasikia siku hizi wanalala chumba kimoja wanafunzi hadi 10 kiasi kwamba wanapeana zamu ya kulala masaa mawili mawili vinginevyo wengine wanalala chini ya mti wakisubiri wenzao wamalize hiyo zamu. Hivyo basi, tunahitaji kufanya juhudi ya ziada ili kuweza kuongeza idadi ya vyumba vya malazi kwa sababu mtu asiyelala usingizi wa kutosha naamini hawezi ku-*perform* vizuri hata kwenye shule yake, tuwape nafasi waweze kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kitu kingine kwa upande wa Vyuo Vikuu hivi. Katika hali ambayo nafikiri pengine Serikali yetu haijaangalia vizuri, ni ule mgawanyo wa zile *environmental motivation services.* Naamini kabisa katika ngazi ya Chuo Kikuu, tuna Maprofesa, tuna *Associate Professors,* tuna *Senior Lecturers, Lecturers, Tutorial Assistants* na wafanyakazi wengine, katika hali yetu kutokana na mazingira yasiyokuwa ya kuridhisha kila mtu anafanya juhudi awe *Professor* ili aweze kupata maslahi mazuri, katika kila Idara kunakuwa na *Professor* mmoja ambaye yeye kazi yake anakuwa ni kama *think tank* wa ile Idara. Lakini sisi kwetu unaweza kukuta Idara moja yenye wanafunzi 100 ina ma-Profesa watano ambao kikawaida kila mmoja atabidi awe kiongozi wa hiyo Idara, hivyo basi hakutakuwa na Mwalimu wa kufundisha hawa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea sasa hivi, ni kwamba wale watu ambao wamekaa kwenye ngazi za kawaida kwa sababu maslahi yao si mazuri, hawaridhiki na hayo mazingira …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Oooh! Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ni Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshismiwa Ali Seif, ajiandae na Mheshimiwa Musalika ajiandae.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Wasaidizi wake na Watendaji Wakuu wote pamoja na Ma-Profesa wote kwa sababu Wizara hii ndiyo yenye Maprofesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga Mjini, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusema kuwa mapinduzi yoyote ya maendeleo tunayoweza kuyazungumzia hayawezi kuwepo bila ya elimu. Kwa hiyo, ni matumaini yangu na naiomba Serikali miaka mingi kadhaa ijayo elimu iendelee kuwa ni ya kwanza katika mgao wa fedha za Serikali ili kusudi suala hili muhimu liweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuuliza swali. Hivi mtoto akikwama Darasa la Saba kwa sababu ya mtihani, faida ni kwetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza mchango wangu. Kwanza, pongezi kwa wananchi wa Shinyanga Mjini kwa ujenzi wa shule nyingi za sekondari, takribani 15 hivi ndani ya miaka miwili. Pili, naishukuru sana Serikali kwa kukifanya Chuo cha Biashara *(SHYCOM)*, kuwa Chuo Kikuu cha Ualimu wa Biashara. Naiomba Serikali ikiboreshe Chuo hiki ili kusudi kiweze kufanya kazi inayotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, shule ya Rajani iwe ya Kidato cha Tano na Sita kwa sababu inazo sifa zote na madarasa Kidato cha Tano na Sita yapo. Tumeshaomba muda mrefu, ni matumaini yangu kuwa sasa mwaka huu itakuwa ni kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni kuhusu elimu ya msingi. Mpango wa elimu ya msingi kwa wote iliyojulikana kama *UPE* mwaka 1974 ilipotayarishwa, ilikuwa na lengo la kumfanya kila mtoto afike Darasa la Saba. Sasa najiuliza, mtoto akiishia Darasa la Nne, ni ili awe kitu gani? Fedha za Mtihani wa Darasa la Nne zinazotumika kwa ajili mitihani hiyo, ni sawa? Sidhani kama ni sawa kwa sababu tunatumia pesa kumwekea kizingiti mtoto ili asifike Darasa la Saba kwa nini? Nadhani mtazamo mpya unahitajika ili kuondoa kikwazo hiki ili kusudi kila mtoto anayeingia Darasa la Kwanza afike Darasa la Saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, kuhusu elimu ya sekondari, nianze kuipongeza sana Serikali kwa kuvuka lengo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kwa ujenzi wa shule za sekondari. Hii ni hatua moja muhimu sana na haina sababu ya kuibeza kwa sababu hatuwezi kupiga hatua mbele kwenye elimu ya sekondari bila ya kuanza ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kwa kufanya miujiza katika miaka miwili. Shinyanga ilikuwa na shule za 78 kwa miaka 44 ya uhuru. Mpaka mwaka 2005 walikuwa na shule 78 tu lakini sasa Shinyanga ina shule 272. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyote vile lazima tuwapongeze wananchi hawa, chini ya Uongozi wa Mkuu wa Mkoa, Ndugu Brigedia Generali Dr. Johanes

Balele. Ujenzi wa shule zote za sekondari tunazozishuhudia sasa, ni hatua muhimu sana. Kinachotakiwa sasa tuziboreshe kuliko kubeza kwa sababu tunazihitaji. Nafikiri tushirikishe zaidi wazazi, wananchi wote na wadau wa aina mbalimbali ili kuhakikisha kuwa shule hizi tunazikamilisha, tunaziboresha ili kusudi watoto wetu waweze kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa, wenzetu wa Kenya wana shule za sekondari 4,500 lakini ni wachache kuliko sisi sisi ndio tunakaribia shule 4,000. Kwa hiyo, tunahitaji juhudi za ziada ili kuhakikisha kuwa kila mtoto anayeingia sekondari afike Kidato cha Nne na mimi naungana na Waheshimiwa Wabunge ambao wanajiuliza je, kuna haja kweli ya kuwa na Mtihani wa Kidato cha Pili. Mimi siamini kama kuna haja, kwa sababu tunajaribu kuweka kikwazo ambacho hakina maana yoyote. Nadhani hatua ambayo tunapaswa sasa kuichukua ni kuwa na *Universal Secondary Education,* Elimu ya Sekondari kwa Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, ni kuhusu mfumo wa usimamizi wa elimu ya msingi na ya sekondari. Nadhani kunahitajika kuangaliwa upya ili kusudi tuhakikishe kuwa tuna viwango vinavyofanana nchi nzima. Kwa sababu nilipokuwa naangalia kwenye vitabu vya Mheshimiwa Waziri, nilikuta kuna shule zinaitwa za sekondari za Serikali na shule za jamii. Sasa hii ni hatari kidogo kama tuna maana kuwa usimamizi wa shule hizi utatofautiana. Shule zinazoitwa za Serikali zisimamiwe na Serikali Kuu na shule zinazoitwa za jamii zisimamiwe na mamlaka nyingine. Sidhani kama hili suala ni sawa kwa sababu hatuwezi kuhakikisha kuwa viwango vya elimu nchi nzima vinakuwa ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hapa ni mtalaamu wa kutengeneza miundo ya mashirika na utumishi wa aina mbalimbali. Nimeshaanza hata kuchora *Organization Chart* inavyopaswa iwe ili kusudi usimamizi huu uwe ni wa aina moja kuhakikisha kuwa viwango vya elimu nchi nzima zinakuwa ni sawa. Niko tayari kumwonyesha Mheshimiwa Waziri ili kusudi pengine aweze kunielewa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tano ni kuhusu elimu ya juu, tupanue haraka mafunzo ya elimu ya juu kwa sababu bado tuko nyuma na bahati nzuri takwimu zinajieleza hapa. Kwa mfano, napendekeza, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika cha Moshi, kianzishwe kuwa Chuo Kikuu mapema si zaidi ya mwaka 2009/2010 ili kusudi *campus* ya Kizumbi iliyoko kwenye Jimbo langu itumike na ni kubwa, itumike kwa usahihi kuinua elimu ya ushirika na biashara ili kusudi Vyama vyetu vya Ushirika ikiwa ni pamoja na *SACCOS,* viweze kuendeshwa na watu wenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iendelee kuboresha vyuo vikuu vya zamani kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Kusema kweli, miundombinu ya Vyuo Vikuu vya zamani hususan Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sihitaji kusema sana kuhusu hali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa sasa. Mimi nimekuwa mwanafunzi pale na

nimekuwa mwalimu pale, hali siyo nzuri, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, anafahamu, iwe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini uangalie na *SUA*, kuna matatizo kidogo. Maisha ya Wahadhiri na Watafiti ambao ndio wanatengeneza watu, wanao uwezo wa kuibadili dunia kwa kuleta maendeleo, hawajaangaliwa ipasavyo, hivyo maisha yao naomba yaboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyuo vikuu, napendekeza, vihamasishwe zaidi kuwekeza katika miradi ya uwekezaji na hii inafanywa dunia uzima. Nenda dunia nzima utaona wana Vitengo hata vya kutafuta pesa tu kwa ajili ya uendeshaji wa Vyuo Vikuu. Sasa sisi hapa kila kitu tunataka Vyuo Vikuu vya Umma viendelee kutegemea Serikali pekee. Sawa vitaendelea kuitegemea Serikali lakini ni lazima tubuni mbinu mpya, kwa mfano ule mradi wa *Mlimani City* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni mfano mzuri ambao unapaswa kutafsiriwa katika maana ya kupanua Chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naupongeza sana Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mfano huo wa mradi mzuri ambao si tu unawaingizia pesa lakini pia angalia huduma inayotolewa kwa wakazi wa Dar es Salaam na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunahitaji kupanua hii elimu ya juu na sekta binafsi inahusika, naomba Serikali ihamasishe uwekezaji katika ujenzi wa Vyuo Vikuu ili kusudi watoto wa Kitanzania wale wenye sifa waweze kuwa na uhakika wa kwenda Vyuo Vikuu vinginevyo maendeleo haya tunayoyasema tunayalilia, hatuwezi kuyapata kama watu hawakusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni sera za elimu. Nadhani, tunahitaji sera ya elimu ya msingi, elimu ya sekondari na ya elimu ya juu. Katika maandalizi ya sera hizi, watumike…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Kengele ya ngapi hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ya kwanza!

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Ooh! Safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya sera hizi, watumike wahusika wakuu, Walimu kwa upande wa shule za msingi, Walimu kwa upande wa shule za sekondari na Wahadhiri kwa upande wa Vyuo Vikuu. Hawa ndio wanajua mazingira, hawa ndio wenye mtazamo, hawa ndio akili yao tunaitegemea. Wewe zungumzia maendeleo yoyote hapa Tanzania au nchi yoyote, sasa mimi nazungumzia Tanzania hapa, Maprofesa unaowaona na Wahadhiri walioko kwenye Vyuo Vikuu, ndio wanaotengeneza watu watakaowezesha kuitoa Tanzania hapa ilipo na kuipeleka mbele. Kwa hiyo, ni lazima hawa watu wana mtazamo. Sasa ni suala tu la kuhakikisha kuwa tusitengeneze sera kwa kujifungia sisi wenyewe kwenye Mawizara yetu, bali tufungue milango, tuwaambie kazi ni hii hapa, lete mambo, watayafanya haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dira, mimi hii dira ya Wizara ya Elimu, naikubali, hamna matatizo, lakini siamini kama hii dira inaeleza kwa usahihi dira mahususi ya elimu ya msingi, ya elimu ya sekondari na ya elimu ya juu. Mimi nimeisoma hii dira na ninaipongeza sana kwamba ni dira ya ujumla, lakini tunahitaji dira ya elimu ya msingi, elimu ya sekondari na dira ya elimu ya juu. Hivyo ndivyo tutakavyoweza kujipanga vizuri ili kuhakikisha kuwa kweli tunakuwa kwenye mstari ulio sahihi na hawa Maprofesa watumike kutengeneza hizi dira. Nasema hivi, ukitaka kukoseakosea ni katika kutengeneza dira, basi mambo yote yanakosewa, mambo mengine mengi tuliyonayo tumeyakosea kwa sababu dira tumezikosea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kurudia kuunga mkono hoja hii na nirudie kuwashukuru wananchi wangu wa Shinyanga Mjini. Leo nimeamua kuwasemea kwa mtindo huu kwa sababu najua bila ya elimu, utajiri wote ule wa Shinyanga unaosemwa kule, hakuna kitu hapa. Madini yapo, pamba ipo na pamba Mkoa wa Shinyanga ndio wa kwanza, dengu ndiyo ya kwanza, lakini hakuna elimu. Ng’ombe sisi ndio tunaoongoza lakini angalia hali ya wananchi wa Shinyanga!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naungana na wenzangu kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri na hotuba nzuri. Nampongeza vilevile Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye kwa kweli amefanya kazi nzuri sana ya kueleza upungufu uliopo katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nataka tu kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri, ni vipi wanahusiana na wenzetu wa Zanzibar, kwa sababu zamani Wizara ya Elimu ya Juu, ni sehemu ya Muungano na sasa imechanganywa pamoja na Elimu ya Msingi ambayo si ya Muungano, sasa hivi wanafanyaje kazi? Wakati ule mipaka ilikuwa inaonekana waziwazi, hilo ni jambo langu la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nimeangalia hiki kitabu cha *Basic Education Statistics,* naona kuna matatizo kidogo, ninataka nipate ufafanuzi. Kwanza, ni suala la *Teachers’ Education enrolment.* Nimeona katika *Government institutions,*

kunaonekana kwamba zinapungua ukiangalia na zile za binafsi wakati tunapanua elimu kwa *secondary schools, primary schools* na vyuo vikuu lakini vyuo ambavyo ni vya Serikali vya kufundisha Walimu *enrolment* imeteremka sana. Kwa mfano, katika mwaka 2008 kwenye *Government institution,* kuna Walimu 16,700 wakati kwenye *private institution* walianzia 1,000 wako kwenye 5,188. Nilitegemea katika hii elimu tunayokuza sasa hivi basi Vyuo vya Ualimu navyo vingekuwa vinaenda vilevile sambamba na kuongezeka kwa elimu yenyewe kwa sababu tutahitaji Walimu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitabu hiki vilevile hakioneshi Walimu wangapi wamekufa, wangapi wameacha kazi, unaona tu idadi ya Walimu wapo, lakini wangapi wamepungua kwa mazingira mbalimbali takwimu hizo hapa hazipo. Kwa hiyo, hizi *data* hazitupi kipimo kizuri cha kutusaidia, hili lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la Katiba. Haki ya raia kupata elimu inatokana na Ibara ya 11 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hutegemei kwamba kutatokea sheria yoyote ambayo itamnyima raia elimu inayopingana na msingi wa Katiba. Sasa chukua mfano wa hii Sheria yetu ya Mikopo, inasema lazima mwanafunzi alipe mkopo na kama ile 20% au 40% aliyopedekezewa kupewa kama hakulipa hapewi *Statement of Results.* Usipompa *Statement of Results* maana yake unamkosesha haki ya kupata ajira, itakuwa tayari umevunja misingi ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ile 60% iliyobaki ambayo anatakiwa kuilipa hawezi kuilipa kwa sababu tayari umeshamzuia kupata ajira. Kwa hiyo, nafikiri hapa kuna mgongano kidogo. Mtazamo wa Katiba wa kumpa haki mwanafunzi apate elimu na apate ajira halafu wajibu wake wa kuja kulipa mikopo yenyewe, mimi hapa nafikiri kuna mgongano wa sheria na Katiba, pengine ni vizuri tukaangalia upya tunafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, unamnyima *Statement of Results* halafu unamwambia lakini unatakiwa uje ulipe na yeye uwezo wake wa kulipa ni mpaka apate kazi, kazi hawezi kupata kama hakupeleka Shahada ambazo zinatakiwa katika ajira, anafanyaje mtu huyu? Kwa hiyo, nasema upande mmoja unampa haki upande wa pili unamnyng’anya haki. Nafikiri tungeangalia tafsiri sahihi ya Katiba na kama sheria hii ina matatizo basi tuilete tena hapa Bungeni, tuifanyie marekebisho, tusiwanyime watoto wetu haki yao ya kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukamkosesha elimu kijana eti kwa sababu hakulipa Sh.100,000/= anazotakiwa kulipa katika ule utaratibu wa mchanganuo wa kusema alipe 20% au 40%, hilo limetokea na ni tatizo la msingi sana. Nafikiri hili liangaliwe upya ili tuone kwa nini Mtanzania ambaye kipato chake cha siku tunakielewa kabisa hakizidi hata Sh.1,000/= halafu unamwambia mtoto wake anapoingia tu shule alipe Sh.1,000,000/=, ataitoa wapi Mtanzania huyu? Nafikiri hapa kuna matatizo ya msingi, kama ni *policy,* tunahitaji kuiangalia upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lililo baya zaidi, ni kwamba hii *Loan Board* imewekewa vigezo fulani fulani vya kusema mwanafunzi huyu anapimwa ili apate msaada wa kiasi fulani. Sasa wana *feed computer*, *computer* ndiyo inayotoa *results*, sasa *computer* inakuwa-*feed* na binadamu, sina uhakika wa usahihi wa taarifa zinazowekwa na kusema yule mtoto ni maskini sana au yule ni kilema au huyu hali yao ya maisha ni mbaya sana, sina hakika kama zile taarifa ni sahihi na ndio maana bado utakuta watoto wengi wa kimaskini wanakosa elimu kwa sababu ya utaratibu unaotumika hivi sasa. Sasa nataka niulize tu kwa sababu bahati nzuri Wizara hii ndio kichwa chetu, ndio wenye taaluma zote, je, tumefanya utafiti kuona hii *information* tunayoi-*feed* katika *computer* inatupa *result* sahihi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hili linatakiwa kufanyiwa kazi. Wako vijana wengi sana, watoto wa kimaskini kabisa, wamekosa nafasi za kusoma au wamekosa kupewa viwango sahihi vya malipo wanayotakiwa kulipwa kwa sababu ya taarifa zinazotokana na hii *computer* kuwa-*fed* na *wrong information.* Nafikiri hilo linatakiwa kufanyiwa kazi ili tupate majibu sahihi. Naomba kwa hili washirikishwe vilevile zile Bodi za Vyuo, wanafunzi nao washirikishwe katika kupata taarifa sahihi juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni suala la viwango vya hii mikopo inayotoka. Nafikiri hakuna uwiano, ukichukua wanafunzi wa Sayansi na wanafunzi wa *Arts*, utakuta wanafunzi wa Sayansi wanabebeshwa mzigo mkubwa zaidi kuliko wanafunzi wa *Arts.* Chukua tu Chuo cha Ardhi, mwanafunzi wa Chuo cha Ardhi atatakiwa kulipa si chini ya shilingi milioni moja na zaidi lakini mwanafunzi wa *Arts* wa *same category* ya D, analipa kama shilingi 560, sasa nasema hapa hakuna uwiano, aina moja ya …

**NAIBU SPIKA:** Laki tano?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema laki tano, kwa hiyo, nafikiri hapa kuna tatizo la uwiano. Nafikiri ni muhimu tutazame suala hili kama kweli tunahimiza watu wasome Sayansi halafu tena unawapa mzigo mkubwa zaidi, hivi kweli watu watakwenda kwenye Sayansi? *Take into account* kwamba wazazi wao ni maskini sana, hao unaowaambia wakafanye hivyo, wazazi wao ni maskini sana ndio maana watu wame-*opt* kuchukua *Arts subjects* kwa sababu ya matatizo makubwa yaliyoko ya uwezo wa kulipia masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hilo tu, watu wanaosoma masomo ya sayansi wana kazi kubwa zaidi, wanafanya utafiti mkubwa. Kwa ruksa yako, naomba nitoe mfano mmoja. Huyu ni mwanafunzi wa Chuo cha Ardhi, ametakiwa atengeneze *project.* Amepewa Sh.195,000/=, *paper* moja tu peke yake ina *cost* Sh.10,000/=, hii ni *project* moja tu, hajatengeneza *dissertation,* ngoja tu nikuoneshe. Tena huyu kijana ni *very intelligent.* Hii ndio *dessertation* yake aliyopeleka Chuoni, ametengeneza *AIC Complex* nzuri kule Arusha, *it worth about 47 billion,* amejitolea amefanya kazi kubwa. Hii kazi

peke yake ukichukua *Architect* wa nje akuchoree, ni *two percent* ya malipo ya hii kazi aliyoifanya. Wewe unampa Sh.*195,000/=* akafanye kazi hii, anaweza kufanya kweli? Akimaliza hapo, anatakiwa apeleke *Thesis* yake, anaitengeneza kama hivi, nzuri sana, ukiziona hizo picha zilizoko ndani utafurahi kweli. Lakini huyu lazima ametumia pesa zake za ziada kufanya hii kazi. Sasa baada ya yote haya huyu kijana kwa sababu hakuweza kulipa ile 20% anayotakiwa, anaambiwa hapati cheti, *all of this work,* aliyofanya ni bure. Kwa hiyo, hawezi kuajiriwa, hawezi kulipa mkopo, hawezi kufanya chochote kingine, *what are we doing? Are we serious* kwamba tunataka kuwasomesha watoto au tunataka kuwatesa watoto? Nafikiri kuna tatizo la msingi, tunahitaji kukaa kitako kuangalia upya kama hii Sheria ya Mikopo tuliyoipitisha haisaidii basi ije Bungeni, tuirekebishe lakini wanafunzi wetu wa Kitanzania wapate elimu, hatuwezi kwenda namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano, kuna vijana wanaokaa kwenye *hostels* na kuna vijana wanokaa nje ya *hostels.* Anayekaa kwenye *hostels* analipa kama Sh.450/=, anayekaa nje ya *hostel,* wamepata vyumba vya kusaidianasaidiana, wanalipa analipa Sh.1,000/= lakini *rate* yao ya mkopo ni aina moja.

**NAIBU SPIKA:** Mia nne hamsini?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sh.450/= kwa wanaokaa *hostel* pale Chuoni.

**NAIBU SPIKA:** Kwa siku?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sh.450/= kwa siku, nje analipa Sh.1,000/= lakini *rate* yao ya mkopo ni hiyo hiyo moja. Sasa najiuliza na huyu aliyeko kwenye *hostel* ana *advantage* kwa sababu kwanza anakaa mahali pazuri kidogo, anapata nafasi ya kufanya *research,* huyu mwingine lazima apande daladala, pesa yenyewe ya daladala haimiliki, hivyo ni matatizo lakini *facilities* anazozitumia yule aliyeko kwenye *hostel* na yeye ni tofauti na unawategemea watoto hawa wa-*perform* sawasawa? Nasema hapa napo kuna tatizo. Kwa hiyo, nafikiri nalo hili linatakiwa liangaliwe. Ndio tunasema pengine hii Bodi yote tulitakiwa kwanza tui-*review,* tuangalie sheria, tuangalie na utendaji wenyewe, tuangalie kama kweli inasaidia wanafunzi kuweza kulipa haya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri hizi fedha za awali za 20% ambazo mwanafunzi anatakiwa kulipa, ziwe ni sehemu tu ya mkopo akipata ajira huko mbele ya safari, alipe. Huwezi kumwambia mtoto wa mzazi, amelipa kuanzia *primary school, secondary school, high schools,* halafu mwanaye anaingia *University* umwambie anatakiwa alipe Sh.1,000,000/=, atazitoa wapi Mtanzania huyu anayepata Sh.1,000/= kwa siku? Sasa nafikiri tungeiondoa hii kabisa tukaiingiza tu katika *basket* nzima ya mkopo ili akipata ajira, yeye mwenyewe aweze kulipa Serikalini, hiyo inaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Walimu. Walimu wanapelekewa fedha zao nyingi kule chini kwenye *OC*. Katika mazingira kama ya Wilaya ya Kasulu, wamejitahidi sana kukishirikisha Chama cha Walimu na ile *OC* bahati nzuri haina matatizo sana. Wanajua matumizi yao yanavyokwenda lakini Wilaya nyingine bado kuna matatizo. Nafikiri Wizara ikajifundishe pale Kasulu walifanyaje hata matatizo yakapungua kuliko sehemu nyingine? Ndio maana huu mlundikano wa madeni umekuwa mkubwa sio kwamba wakati mwingine pesa zinakuwa hazipo bali ni kwa sababu kuna *accounts* 500 kule zimekuwa *mismanaged* kwa sababu pengine hakuna ufuatiliaji mzuri. Pengine haya madeni ndio yamebaki, lakini inawezekana vilevile na Wizara ina mzigo mkubwa wa fedha inaotaka kutumia, pesa hazitoshi. Sina hakika katika bajeti hii wamepewa asilimia ngapi ya *total budget*, pengine ni 58%, 59% au 60% au 70% pesa nyingine bado hazijatoka. Sasa nasema kuna matatizo yanahitaji kuangaliwa. Ni namna gani tutaondoa matatizo ya Walimu juu ya madeni yao? Sasa hivi wanadai zaidi ya Sh.*12,000,000,000/=* na wale Wakaguzi wanadai *4.2 billion*, nasema ni pesa nyingi sana hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi naiuliza Serikali kila siku, tunatumia *cash budget* inakuwaje watu hawa tuwakope? *What is the meaning of the cash budget?* Kwa nini wakopwe watu wakati Serikali bado inaendelea kutumia *cash budget?* Haya ni maswali ambayo bado hayajapata majibu ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka kujua juu ya hii *Loan Board,* fedha zao za *administration* zinatokana na ile *hundred and seventeen billion* waliyopata au ziko nyingine? Maana ukitizama katika kitabu hiki, kuna *about two hundred and twenty billion,* sasa nina hakika hizo ni pamoja na zile za *administration* au ni mbali na zile za *administration?* Wasiwasi wangu ni kwamba inawezekana pesa hizi nyingi zikaingia kwenye *administration* na kidogo zikaenda kwenye mkopo. Bahati mbaya mwaka huu fedha yenyewe imepunguzwa zaidi, kwa hivyo wanafunzi wengi watabaki nje hawaendi shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Chuo Kikuu Cha Dar-es-Saalam, ndio chuo mama. Chuo Kikuu cha Dodoma kitakaa mpaka miaka 10 ndio kitaweza kuzalisha Walimu wake, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, ndicho kitakachoweza kutusaidia kutupatia Walimu wa vyuo vingine. Mbona tumekiacha kama mtoto wa kambo? Ndio maana tunakosa hata Madaktari kwa sababu tunakwenda ku-*invest* sehemu mpya huyu mama mzee tunamwacha na akifa huyu mama mzee, hao wengine hawata-*survive.* Unaanzisha Chuo Kikuu kipya cha Dodoma lakini unategemea *Lectures* kutoka Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam. Kwa hivyo, lazima ukiimarishe vizuri, ukiendeleze vizuri ili kiweze kukusaidia kwa hawa wachanga wanaokuja ili nao waweze kupata watu wa kuwafundisha lakini sasa tumekiacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ardhi pale wamejenga *hostel* nzuri pale nje lakini mpaka sasa hivi hakuna *restaurant*, maana yake lile jengo litakuwa limebaki tu. Katika bajeti ya safari hii hakuna fedha. Sasa tunafanyaje, mbona tunafanya mambo nusu nusu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninapenda Mheshimiwa Waziri, atueleze katika *2025 vision,* maana mara nyingi tuna *quote* Ilani ya Uchaguzi, hebu tuangalie hizi *target* zetu zilikuwa zinasema nini? Tanzania tulitaka ma-*scientist, Medical doctors*, *Architects* na *Lecturers* wangapi? Mbona hatuoni mahali popote inapozungumziwa? Kila mahali ukisoma wanasema mwaka huu Walimu hawa lakini idadi hasa tunayoitaka ni ngapi na tutaifikiaje? Mimi sijaona katika kitabu chochote mambo haya yakielezwa, ninaomba kwa kweli tupate ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu.

**NAIBU SPIKA:** Sauti yako haisikiki vizuri.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kukupa shukrani kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya maelezo ambayo kayatoa kiongozi wangu wa upinzani kuhusiana na kuzuiliwa kwa matokeo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwa kutolipa 20% ya mkopo wao lakini pia imedhihirika kuwa wanafunzi wanazuiliwa kupewa matokeo katika vyuo fulani kutokana na kutolipa hata ada za Vyuo Vikuu. Ushahidi nilionao huu hapa wa Chuo Kikuu cha Ardhi, unaonesha kuwa kuna wanafunzi wamezuiliwa matokeo yao kwa sababu hawajalipa ada ya Chuo Kikuu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani dhana ya Serikali kutoa mkopo kwa wanafunzi ni kuwawezesha kupata elimu, sasa leo Serikali inapochukua juhudi kubwa ya kuwakopesha wanafunzi halafu kukawa na ada ndogo kama hizi za vyuo zikazuia matokeo, kwa kweli hili tutakuwa hatuwatendei haki wanafunzi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuangalie mtu ameshasoma miaka minne, leo unamzuilia matokeo yake kwa ada ya Chuo Kikuu, hajui kama amefanikiwa katika masomo yake yale au hakufanikiwa. Leo huyu anapokwenda katika mazingira ya kawaida ya maisha ya nyumbani, ule uwezo wa kuweza kukabili mtihani ule unapungua. Sasa leo unapomrejesha baada ya kulipa ada hiyo, inawezekana somo alilofeli akalifeli tena. Leo unamchafulia mwanafunzi maisha yake kwa kutolipa kwa mfano Sh.100,000/=, kwa kweli nadhani hatuwatendei haki wananchi wetu, wanafunzi wetu, kwa hiyo, ipo haja ya Wizara kuhakikisha kuwa suala hili linaondoshwa mara moja. Hapa ninayo orodha ya wanafunzi wa kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi na wengi wao wako katika hali

hiyo. Kwa hiyo, ipo haja ya Wizara kuona ni nini wanafanya kuhusiana na suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Mbunge, kwa kweli inaonekana anazungumzia suala la elimu bora na hili ni tatizo linaloonekana linatukabili Tanzania, lakini kilichopo ni kuwa je, hii elimu bora ni ipi? Kwa hiyo, ipo haja kwa kweli kwa Wizara ya Elimu, kuanzisha Mjadala wa Kitaifa wa kujua au wa kutambua maana ya neno elimu bora. Vile vile ipo haja ya kuanzisha Mjadala wa Kitaifa kuhusiana na hiyo elimu bora, tukishajua ni nini, basi ni vipi, tutaifikia. Kwa sababu inavyoonekana, utafiti uliofanywa na taasisi moja ya elimu, ni kuwa kila mmoja katika watu waliofanyiwa utafiti ambao walikuwa ni Walimu, Walimu Wakuu, Maafisa Elimu na Kamati za Shule, hawa walipohojiwa ilionekana ni watu waliogawanyika katika makundi manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo waliosema elimu bora wakiihusisha na vitendea kazi, Walimu, madarasa, maabara na makataba. Hawa walisema kwa mazingira hayo, utapata elimu bora. Lakini vilevile wako waliosema kuwa elimu bora inapatikana pale ambapo wanafunzi wanapasi wengi zaidi katika elimu ya msingi kwenda kidato cha kwanza, kidato cha nne kwenda kidato cha tano. Kwa hiyo, kwa wao kigezo cha elimu bora ni kupasi zaidi kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo ambao wamehusisha elimu bora ni kuwepo kwa Walimu, kwa maana unapokuwa huna Walimu wenye sifa basi elimu bora itakuwa haipo. Wako waliohusisha kuwa elimu bora lazima imtayarishe mwanafunzi aweze kukabili maisha ya baadaye lakini tatizo lenyewe ni sawa lakini kwa misingi kuwa aajiriwe. Kwa hiyo, hawa walisema kuwa bila kuajiriwa ina maana elimu uliyopata wewe si bora. Kwa hiyo, kutokana na tofauti hizo za tafsiri ya elimu bora, Wizara ya Elimu ambayo ndiyo inasimamia sera na sheria za elimu, ipo haja ya kuanzisha Mjadala wa Kitaifa, unaohusiana na ni nini elimu bora na ni vipi elimu bora itafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi ambayo imefanya utafiti kuhusiana na elimu stadi. Inaeleweka katika elimu ya msingi na katika elimu ya sekondari, wanafunzi wanasoma masomo mengi lakini kuna masomo hayo ambayo tunaweza kuyaita *basic skills* ambayo hayo ni lazima mwanafunzi ayapate ili aweze kuendelea na masomo mengine. Masomo hayo ni hisabati na lugha, tunaposema lugha kwa maana ya Kiswahili na Kingereza. Sasa bila ya kuyamudu masomo haya, kwa kweli itakuwa ni matatizo na itaendelea kupigwa kelele kuwa elimu yetu inazidi kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuone utafiti ulituambiaje kuhusiana kwanza na hisabati. Watafiti hawa walijaribu kuchukua wanafunzi wa darasa la 10, kwa maana ya elimu ya sekondari na wanafunzi wa darasa la sita kwa elimu ya msingi. Waliwapa hesabu zinazofika saba ambazo zilifanywa na wanafunzi wa darasa la 10 na darasa la sita. Tofauti iliyokuwepo ni kuwa wanafunzi wa darasa la sita, hesabu zile waliandika kwa lugha ya Kiswahili na darasa la 10 kwa Kingereza. Walipozifanya hesabu hizi ambazo

zilikuwa ni rahisi kwa kiasi fulani, kwa ujumla matokeo kwa kweli yalikuwa ni mabaya. Mfano ni kama huu, katika hesabu hizo saba hesabu namba tatu kulikuwa na jamaa ana machungwa 30, swali lilikuja hivyo, anataka kuwagawia wanafunzi saba, ili wapate machungwa sawasawa apate nyongeza ya machungwa mangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo. Wanafunzi wa msingi waliofanya mtihani huo wa hesabu hizo saba, walikuwa 549 hawa wa darasa la sita na wanafunzi 491 walikuwa ni wa kidato cha pili, kitabu kilichotumika kutoa maswali hayo ni kitabu cha darasa la tano. Kwa hiyo, darasa la tano kilitumiwa kumpima mwanafunzi wa darasa la sita na darasa la 10 na umuhimu wa hisabati kila mmoja anauelewa. Matokeo ni kuwa katika wanafunzi 549 wa elimu ya msingi katika suala hili, 45% walilijibu sahihi, ambao ni sawa sawa na wanafunzi 247 na wanafunzi 491 wa darasa la 10 ambao wameshalipita karibu miaka mitatu, anatolewa mtihani wa darasa la tano, wanafunzi waliopasi hesabu hiyo niliyoieleza ni 33% ambayo ni sawasawa na wanafunzi 162, hii ndio hali iliyojitokeza katika swali la hisabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kulikuwa na swali namba tatu ambalo linaeleza kuwa kuna mzee alimpa mwanawe Sh.10,000/= ya noti akanunue sukari kilo moja ambayo bei yake ni 1,300/= na majani ya chai ambayo kila pakti ilikuwa ni Sh.500/=, kwa hiyo, swali lilikuwa huyu atarudishiwa chenji ya kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake kwa swali hilo ambalo lilikuwa ni nambari tatu ni kama ifuatavyo. Katika wanafunzi wa elimu ya msingi au darasa la sita ambao ni 549 waliolijibu sahihi swali hili ni 43% ambao ni wanafunzi 269. Hapa kwa wanafunzi wa kidato cha pili, ambao walikuwa 491, walijibu afadhali 70% ambao walikuwa ni sawasawa na wanafunzi 344. Hii ndio hali ya hisabati na umuhimu wa hisabati unaeleweka katika shule zetu za msingi na shule zetu za sekondari. Kwa hiyo, ipo haja kwa Mheshimiwa Waziri, kuona kuwa suala hili linapewa uzito ili ionekane kuwa hisabati inapata nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tena kuwa katika lugha, ni stadi nyingine ambayo ina umuhimu wake katika kutoa elimu. Lugha hapa ni Kingereza na Kiswahili, Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa, Kiswahili ndio inayotumika katika kuwasilisha elimu katika madarasa ya msingi. Lakini pia na Kingereza nayo ndiyo inayotumika katika kusomesha wanafunzi wetu katika elimu ya sekondari na ndiyo inayotuunganisha sisi na dunia. Katika hili, wanafunzi walijaribiwa katika kusoma *(reading), translation* (tafsiri) na *dictation (*imla). Katika kusoma, walichukuliwa wanafunzi 10 kutoka darasa la sita na wanafunzi 10 kutoka darasa la 10. Katika kusoma Kiswahili, ilionekana kuna afadhali lakini matatizo yakaja kwenye Kingereza, kwa hiyo, hii inadhihirisha kuwa Kingereza nacho kinahitaji kushugulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika tafsiri ambayo ilichukuliwa, aya moja katika kitabu cha darasa la tano, kwa sababu vigezo vyote ilikuwa ni darasa la tano, ilipotafsiriwa aya hiyo kutoka Kingereza kwenda katika Kiswahili, ambapo ilikuwa ni wanafunzi 476 wa elimu ya msingi, waliopata nzuri kutoka Kingereza kwenda Kiswahili,

walikuwa ni 13% ambao ni sawasawa na wanafunzi 62. Waliopata maksi za wastani ilikuwa ni 21% ilikuwa ni wanafunzi 100 na waliopata mbaya ni 66%. Ilipokuja tafsiri ya Kiswahili kwenda Kingereza, Kiswahili kwa Kingereza, aya inayotoka katika kitabu cha darasa la tano, 4% walipata nzuri, 4% walipata haijambo na 92% mbaya ambayo ni sawasawa na wanafunzi 438 walipata mbaya. Hiyo ni elimu ya msingi ya wanafunzi wa darasa la sita. Lakini ilipotokezea matokeo ya waliyofanyiwa wanafunzi wa sekondari, Kingereza kwa Kiswahili 22% ambayo ni sawasawa na wanafunzi 102 walipata nzuri, wasatani 44% ni sawasawa na wanafunzi 205 na waliopata mbaya ni 34% sawasawa na wanafunzi 58.

Kutafsiri kiswahili kwa Kiingereza 10% walipata nzuri ambao walikuwa ni wanafunzi 47, wastani ni 31 ambao ni sawasawa na wanafunzi 144 na 59% ni mbaya ambao ni 274.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inadhihirisha kuwa Kiingereza kinatupa matatizo na tatizo lililopo ni kuwa wanafunzi wanasomeshwa kwa lugha ya Kiswahili wanapotoka shule ya msingi kwenda sekondari, masomo yote karibu kwa kweli ni kwa lugha ya Kiingereza na hali ni kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni *dictation*, yaani walichukuliwa wanafunzi 483 wa elimu ya msingi na wanafunzi 559 wa sekondari waliofanyiwa imla ya Kiswahili 38% ambao ni sawa sawa na wanafunzi 184 waliopata nzuri ni, 37%

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana umefanya utafiti kwelikweli. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Musalika.

**MHE. JAMES P. MSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tangu niwe Mbunge, miaka yote huwa napongeza na kuunga mkono asilimia mia moja hoja za Mawaziri wa Elimu, lakini kwa leo nataka niseme kwamba sitapongeza au kuunga mkono hoja hii mpaka nitakapokuwa nimepata maelezo ya kina kwamba ni kigezo gani kimetumika wakati wa kugawa vyuo vya ufundi stadi katika Wilaya zile 25 katika Kanda ya Ziwa? Kwa nini Wilaya ya Geita haikupewa chuo hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukisema hapa matatizo ya Geita ni idadi ya watu. Geita ina watu sawasawa na Mkoa wa Lindi au sawasawa inakaribi Zanzibar. Geita ni sawasawa na wananchi waliopo Wilaya ya Kinondoni, Geita ni Mkoa. Geita kuna watu wamekuja pale ambao wameletwa na Serikali kwa maana ya kwamba wamefuata wawekezaji wa Madini, wamekuja kutafuta kazi na shughuli zote za madini na wengi hawana kazi, lakini mtu anapokuwa hana kazi na kwamba hana umeme analazimika kulala mapema na anapolala mapema kazi inayofuata ni kuzaa. Sasa tuko wengi Geita.

Watu hawa milioni moja na zaidi, fikiria ni vijana wangapi katika hawa hawana kazi na kwa nini sasa tulaumu kwamba wanajiingiza kwenye vitendo vya ujambazi au vitendo vingine vibaya? Leo Serikali ina wazo zuri la kujenga hivi vyuo ili hawa vijana

ambao hawana kazi waweze kupata elimu hiyo katika vyuo vya ufundistadi, lakini Serikali haikuona hili. Hapa hapahitaji mtu kuwa Profesa kuliona hili. Baya sana, Mheshimiwa Waziri ni Profesa, Katibu Mkuu ni Profesa pia, *logic* hapa *says no*! Walipaswa kuwa wameliona hili.

Sasa nasema, nitataka maelezo ya kina, kwa nini sina tatizo na kwa mfano hapa kwenye ukurasa wa 103 Kanda ya Ziwa Mkoa wa Kagera wamepeleka vyuo hivyo Chato na Misenye sina tatizo. Lakini Mwanza, Ukerewe na Kwimba sina tatizo. Tatizo langu ni kwamba hivi hawa Maprofesa wawili na watendaji wazuri kabisa, mahiri, katika Wizara hawakuona kwamba watu milioni moja kuna vijana ambao wana matatizo makubwa zaidi ambao wangeweza kupata ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tukumbuke ndiyo maana wakati wa uchaguzi wanatupa taabu sana Serikali. Wakati wa uchaguzi sehemu nyingi ukikuta vijana ambao hawana kazi kwenye mikutano wanakaa pembeni, utasema wakati mwingine wananuna na wakati mwingine wanazomea kwa sababu ya mambo haya haya kwamba tukishapata Serikali hatuwakumbuki.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri, atafute pesa sehemu yoyote angalau akaiweke Wilaya ya Geita katika mchakato huu na mimi nitakuwa tayari kutoa shilingi na nitawashawishi hata Wabunge wenzangu wa Geita tupo watatu tukitoa shilingi tatu kwa Mshahara wa Waziri na pengine na Manaibu wake na Katibu Mkuu tunaweza kupata hela pengine ya kuanza kujenga msingi kule ili mwaka kesho wakumbuke.

**NAIBU SPIKA:** Haiwezekani! Utaondoa shilingi moja tu kwa *item*.

**MHE. JAMES P. MSALIKA:** Basi shilingi moja hiyo inaweza kutosha, tutajua namna ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nataka nije kwenye mpango wa *MMEM* na M*MES* awamu ya tatu Wilaya ya Geita ilifanya vizuri sana katika kujenga maboma ya madarasa pamoja na nyumba za Walimu kama Serikali ilivyokuwa imeelekeza kwamba wananchi wachangie nguvu na Serikali itaweka pesa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wote huu Wabunge wa Geita tumekuwa tukitoa kilio hapa kwamba wananchi wa Geita walifanya juhudi sana, walijenga zaidi ya madarasa 200 na zaidi ya nyumba za Walimu 850. Lakini Serikali haikutimiza lengo lake na kazi hii ilifikiwa baada ya wananchi kujitoa walichonacho na wakati mwingine walijilazimisha kutoa na wakati mwingine Serikali iliwasukuma kidogo na kuwaweka ndani wengine ndiyo tukafikia hapa na ndiyo tukafikia hapa na tukawa sasa mfano Wilaya ya Geita kwamba Wilaya nyingine wajifunze kule. Sasa ilipofika Serikali sasa itimize wajibu wake wa kujenga maboma haya ndiyo kukawa na Kiswahili kwamba hela haitoshi mpaka leo hali hiyo bado ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari zake ni kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, bado kuna maboma haya ya *MMEM,* kwa hiyo, yanaathiri mpango wa *MMES* kwamba nguvu zinazohitajika kuweka kwenye *MMES* au Shule za Kata inabidi sasa zigawanywe kwa sababu maboma haya bado wananchi wanayajenga taratibu. Hata mradi ule wa *TASAF*, kuna maeneo yana matatizo kweli. Kwa mfano Zahanati, Visima au Malambo lakini wananchi wanaona afadhali wachague madarasa ya shule au nyumba za Walimu ili wapumzike michango kwa sababu sasa hivi kule wananchi wa Wilaya ya Geita inabidi wachangie hiyo *TASAF,MMES*, shule za sekondari lakini ni pamoja na maboma hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi Serikali *so far* tangu mpango wa *MMEM* uanze wamejenga madarasa 184 tu na nyumba za Walimu 62. Wananchi wameyapunguza na sasa hivi ninavyozungumza kwa taarifa ambazo nimezipata jana kutoka kwa Afisa Elimu wa Wilaya, Ndugu Kitatumwa amesema maboma ya vyumba vya madarasa yaliyobakia mpaka sasa hivi ni maboma 632 baada ya wananchi kuyapunguza na nyumba za Walimu 246. Kwa hiyo, naomba ombi maalum kwamba wananchi wa Geita wanaomba Serikali ione hali halisi hii na iwaonee imani na Serikali ione aibu kwa wananchi hao itenge pesa ili ikamilishe maboma haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wakati nikichangia hotuba ya Waziri Mkuu nilikumbushia maelekezo ya Waziri Mkuu ambaye ameshayasema na kutoa maelekezo kwamba utaratibu lazima uwepo mzuri wa kuchangia hizi shule za kata pamoja na michango mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sipendi kulirudia, lakini kwa sababu ni kero kwa wananchi na Serikali haipendi kero kwa wananchi wake ni vizuri nikairudia hapa ili nisaidiwe na wananchi wangu waisikie kwamba kipindi ambacho si cha msimu kumchangisha mwananchi michango hii ni kurudisha zile kero ambazo tuliziondoa za kodi ya maendeleo ya kodi ya mifugo.

Kipindi cha mwezi wa kwanza kwa mfano kwenye maeneo yetu kwenye Jimbo langu la Geita kipindi cha mwezi Desemba au Januari, wananchi wanakuwa hawana akiba ya chakula, pesa, ndiyo wakati wanapeleka watoto wao shule na ndiyo wakati wako kwenye shughuli za kilimo. Sasa unapowapelekea michango, matokeo yake wanakimbia familia . Ni mara nyingi mimi nimeletewa kesi kwamba wanaume wanakimbia familia, lakini bado hawa akina mama wanaoachwa pale wanakamatwa na michango hii inafanywa kwa mtindo wa misako.

Kwa hiyo, naomba sana hapa Serikali itoe waraka kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi na sisi Wabunge watupe nakala kwamba michango hiyo kufuatana na maeneo yafanyike wakati wa msimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikitoka hapa nakwenda kufanya vikao kwenye vijiji vyangu. Ni vizuri kama kweli Serikali imemsikiliza Waziri Mkuu nipate nakala hiyo ya waraka kwa hawa ambao nimewasema ili wananchi nikawaeleze ili wafanye kazi kwa furaha faida yao ni faida ya nchi, lakini wanafanya wanaona kama ni kero kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije na mimi kwenye matatizo ya Walimu. Walimu wana malalamiko yao hapa ya madai na haya yanatokana na kama walivyosema wenzangu na mishahara isipolipwa kwa wakati marekebisho ya mishahara baada ya kupanda vyeo na fedha za matibabu, likizo, uhamisho na mengine mengi na mpaka uhakiki mbalimbali ulipofanyika kama walivyosema wenzangu zimepatikana shilingi bilioni tisa kufikia Julai na pesa hizi Serikali haikulipa mpaka walipotishia kugoma tarehe 1 Mei, 2008 na zikalipwa shilingi bilioni 7.1. Sasa madai mapya yapo ambayo sasa hivi yanafikia shilingi bilioni 12.

Mwanza peke yake Walimu wa shule ya msingi peke yake wana madai mapya ambayo ni jumla ya shilingi bilioni 1.1, hayo ni madai ya shule zamsingi peke yake, wale wa Sekondari na ukaguzi wanadai shilingi bilioni 4.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu pamoja na kwamba wanaondoa ujinga katika Taifa lakini sisi kama wanasiasa akiwemo na Mheshimiwa Waziri akumbuke kwamba ni watu muhimu sana wakati wa uchaguzi. Wakati wa Uchaguzi. Walimu hawa huwa hawalali. Saa nane wana maboksi ya kura zetu, ni waaminifu! Kama ni kura ya CCM utaikuta ni kura ya CCM, kama ni ya *CUF* ni hivyo hivyo, kama ni ya *UDP* ni hivyo hivyo hawalali na ni waaminifu, wanatufanyia kazi hata za uchaguzi. Sasa baada ya sisi kupata Serikali ndiyo tunasahau kweli. Ninaomba sana Walimu hawa walipwe madai yao.

Zipo athari nyingi sana zinazotokana na kutolipwa hususan kwa Walimu wapya wale akina mama, wasichana, wanapata matatizo sana ikiwemo na kuvunjika moyo wa kufundisha, kufanya biashara ndogo ndogo kama maandazi na michicha na mbaya zaidi wanalazimika kuolewa hata na watu wenye umri mkubwa kama baba zao.

Mimi kwenye kijiji changu kimoja kuna msichana mmoja alipangiwa kwangu baada ya miezi miwili alikuwa anaomba ahame na mimi nikamdanganya kwamba nakushughulikia. Baada ya mwaka mmoja nikiwa kwenye mkutano wa hadhara nikamwuliza Mwenyekiti wa kijiji kwamba yule Mwalimu aliyekuwa ahame mbona naona kama hana tatizo siku hizi? Yule Mwenyekiti wa kijiji akaninong’oneza taratibu akaniambia Mtendaji wa Kijiji maana yake ni kwamba yule mama tayari alikuwa ameshapata pale mume, ameolewa na Mtendaji wa Kijiji. Sasa huo ni mfano si mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mfano mbaya mwingine ni kwamba yupo Mwalimu mmoja amekwenda ameripoti kijiji kimoja kwa sababu ya kutaka kujikimu, kapata bwana. Yule bwana hakujua, wamekaa wote baada ya muda akampa mimba kumbe yule bwana ni kibaka, jambazi na anavuta bangi. Ndugu zake wamefanya utaratibu wa kufanya *send off* kuhalalisha ndoa. Siku ya *send off* yule bwana harusi mtarajiwa amekuja amevuta bangi na wenzake mashati yamechanika, kofia hovyo hovyo, wale wazazi wake wakasema, *full stop!* Hakuna kitu kuendelea hapa! Lakini yule jamaa akaja kumtishia yule mwanamke kwamba kitakachoendelea hapo ukinikataa nakuua. Si umeshajua mambo yangu! Sasa Mwalimu yuko kule, anahangaika, siwezi kusema ni

sehemu gani, lakini ni maeneo ya huko kwetu. Kwa hiyo, kuwacheleweshea mishahara kunawaingiza kwenye matatizo walimu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba, mimi sitaunga mkono mpaka nipewe maelezo ya kina kwa nini Geita haina Chuo cha Ufundi Stadi?  Ahsante sana.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza na mimi kuchangia machache kuhusu hotuba ya Waziri wa Elimu.

Napenda vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake hii nzuri pamoja na Manaibu wake na vilevile nawapongeze kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuendesha Wizara hii. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa ujumla, Serikali kupitia Wizara hii imejitahidi sana kufanya mambo mengi mazuri katika kuhakikisha kwamba tunaendeleza elimu katika nchi yetu na imejitahidi kuweka mipango mizuri sana ambayo nafikiri kama itatekelezeka, Taifa letu litakuwa moja ya Mataifa katika nchi za kiafrika ambazo zinaongoza katika utoaji mzuri wa elimu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo na pamoja na kwamba malengo ya MKUKUTA yanataka tuimarishe elimu iliyo bora, lakini kuna vikwazo mbalimbali ambavyo kwa kweli tunakwenda navyo, ni vingi sana, lakini nitapenda kwa nafasi hii finyu niweze kuzungumzia machache kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kuhusu Walimu. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia  sana kuhusu masuala ya Walimu, kwanza ni kuhusu mchango wao katika kuhakikisha kwamba  wanakuwa vinara katika utoaji wa elimu iliyo bora. Sasa hatuwezi kufikia azma hiyo kama Walimu hawa ambao ndiyo tunawategemea hali zao zinapata matatizo hayo au vikwazo vya maisha yao havitatuliwi kwa haraka.

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa malalamiko ya Walimu ni mengi na kwa kuwa Waziri ndiyo kwanza ameingia katika Wizara hii pamoja na wenzake, naomba wakae chini watafakari matatizo haya ambayo mengi wameyakuta, wajitahidi kuyarekebisha katika muda wao ambao watakuwa wanaongoza Wizara hii, na sisi tutakuwa nyuma yao katika kuwapa *inputs* ya mambo mbalimbali ambayo wanatakiwa kuyarekebisha.

La pili, ni kuhakikisha kwamba hao Walimu wanapata mafunzo mazuri, mafunzo yatakayowawezesha kutoa elimu iliyo bora. Mimi napata shaka sana, unapomwacha Mwalimu akafundisha kwa miaka 15 bila kurudia kupata mafunzo ya *refresher courses.* Kwa kweli Mwalimu huyo anapata matatizo, kwani ufundishaji wake unakuwa duni sana. Kwa hiyo, ningependa kushauri kwamba kuwepo na utaratibu wa mara kwa mara wa kuhakikisha kwamba Walimu wanapewa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu masomo wanayoyafundisha na hili litaligusia tena baadaye kidogo.

Lakini vilevile ni muda wao wa mafunzo katika vyuo. Mimi ni Mwalimu. Huwezi kuwa Mwalimu uliyekamilika, kama utakuwa umepata mafunzo chini ya miaka miwili wewe siyo Mwalimu hata kidogo! Kwa hiyo, mpango wa *crush program* mimi naupinga. Mpango wa kufundisha Walimu miezi sita mimi naupinga, siyo mpango mzuri. Kwa hakika kama tunataka Walimu waliobora watusaidie katika kuendesha elimu hapa nchini ni lazima tuweke utaratibu wa kuwafundisha kwa miaka inayozidi miwili.

Tumehakikisha na tumeona hawa vijana waliomaliza *form six* kipindi kifupi kilichopita wamepitia mafunzo ya ualimu wa miezi sita. Wako huko mashuleni eti na wao wanaitwa Walimu. Walimu gani wa miezi sita? Hao ndiyo ambao sasa hivi tunashuhudia wakiingia katika mitego ya kufanya mapenzi na wanafunzi wenzao huko mashuleni.

Kwa hiyo, naomba sana tuwaimarishe hawa vijana wawe wamekomaa waende kufundisha katika shule zetu wakiwa wamekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia katika azma hii ya kuboresha elimu ni suala la mikondo mashuleni. Mimi nakubaliana kabisa kwamba tuna matatizo kwamba tunahitaji kuwa na wanafunzi wengi wanaoingia *form one*. Tunahitaji kuwa na wanafunzi wengi wanaohitaji kuingia katika madarasa ya *form five na form six*. Lakini unapoweka mikondo nane katika shule ya *form one* mpaka *form four* maana yake mikondo nane *form one, form two, form three na form four*. Unatengeneza mikondo 32 yenye wanafunzi 1,280 katika shule moja. Kweli inatawalika shule hiyo? Hiyo haiwezi kutawalika. Lazima Waziri aliangalie hili suala vizuri zaidi. Ni *crush program* ndiyo, lakini lazima tuende na sera tulizojiwekea ili tuweze kuwa na Walimu wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufundishaji wa masomo ya lugha. Watu wengi hapa wamezungumzia kuhusu masuala ya lugha. Ni muhimu sana. Ili twende vizuri na watoto hawa katika azma yao ya kujifunza. Unapoamua kwa mfano kwamba wewe unafundisha lugha ya Kiingereza shuleni lazima kweli uamue kukifundisha Kiingereza, siyo vinginevyo hata kidogo! Siyo kuchanganya masuala ya Kiswahili humo humo, *vocabulary* hazieleweki na Mwalimu huyo ambaye unampa kazi ya kufundisha lugha ya Kiingereza hujamuandaa vizuri. Leo anaitoa elimu hiyo kwa wanafunzi, kwa kweli haieleweki. Matokeo yake sasa ndiyo tunaona Walimu na wanafunzi hawatofautiani katika kuzungumza lugha ya Kingereza. Kwa hiyo, naomba hili Wizara iliangalie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri basi kuwapeleka kwenye vyuo kama Waziri alivyolizungumzia katika hotuba yake. Walimu wawe *categorised na specialised* kufundisha masomo fulani fulani ambayo tunajua kabisa kwamba leo hapa Mheshimiwa Masilingi au Mheshimiwa Shally ni Mwalimu wa Kiingereza kweli awe ni Mwalimu wa Kiingereza tunayemtuminia na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa elimu ni pamoja na masomo ya Sayansi, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri kwamba ni azma ya Serikali sasa kuhakikisha kwamba tunajitahidi kupeleka watoto wetu ili waweze kusoma masomo ya Sayansi na hili tumechelewa sana. Mataifa mengine wanakimbia katika suala hili ili

waendane na Sayansi na Teknolojia ya hivi sasa. Vikwazo vikubwa tunavyopambana navyo hivi sasa ni ujenzi wa maabara na hili nafurahi kwamba wengi wameliona. Maabara kwa kweli ni lazima Serikali itekeleze wajibu wake. Miaka kama mitatu hivi nyuma Serikali ilishaamua kwamba yenyewe itajenga maabara kwa sababu inajua kabisa kwamba maabara ni majengo ambayo ni gharama sana kwa wananchi kujenga. Kwa hiyo, mimi nashukuru kwamba Serikali imeliona hilo na kwamba Serikali itajenga maabara.

Lakini kwa kasi hii na kwa mwendo huu wa kutoa maabara moja kwa Wilaya moja tutafika lini? Hatutaweza. Mimi nathubutu kusema kwamba pengine azma yetu tunayo na ni nzuri, ni vizuri basi tukae chini tuangalie: Je, tunaweza tukakopa? Serikali iamue kukopa kutoka kwa Wahisani wengine ili tujenge maabara ili watoto wetu waweze kufundishwa na sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tu kusema kwamba lile suala la nafasi katika *form five na form six*. Tumechelewa sana katika ujenzi wa madarasa ya *form five* na *form six*. Hivi sasa tunavyozungumza, wanafanya vizuri sana *form four* lakini hawaendi *form five*, hawaendi kwa sababu hakuna madarasa, sasa tunafanya nini? Ni vizuri tukaongeza idadi ya haya madarasa ya *form five na form six*. Tumejitahidi kufanya vizuri sana *form one* mpaka *form four* na wananchi wamefanya kazi nzuri sana, lakini katika hayo madarasa ya *form five* na *form six* ni lazima tuamue vizuri na vilevile tuamue kuhakikisha kwamba hawa watoto wanaofaulu *form four* wanakwenda *form five*.

Nikitoa mfano wa Mkoa wa Mbeya tu peke yake, Mkoa wa Mbeya mwaka jana ulifanikiwa kufaulisha watoto 4,500 wa *form four* kwenda *form five* lakini watoto 1,675 hawajapata nafsi mpaka sasa. Kielimu tunaweza kusema hawa wako nyumbani, lakini kwa wale wenye bahati labda wana wazazi ambao ni wazuri kidogo kifedha, wamewapeleka labda kwenye *private schools*. Lakini wananchi tunasema wako huko Mitaani. Tunafanya nao nini? Kwa hiyo, hili naomba lizungumziwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie suala la mimba mashuleni kwa sababu linaniuma sana. Ni tatizo kubwa sana! Sitaki kurudia maagizo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Mbeya, lakini kipindi cha mwaka mmoja tu wasichana wa *form one* mpaka *form four na form five* baadhi yao, jumla ya wanafunzi 703 wamepata mamba. Hivi Sheria ile ya Kujamiiana inafanya kazi gani? Pamoja n sheria, lakini wakati huo huo iwekwe *program* maalum ya kwenda huko kwenye Kata na vijiji kutoa elimu. Tutoe elimu kwa wale wadau wote, vyombo vya dola, Watendaji wa Kata wote wapewe elimu hii kwamba mwanamke ni maendeleo ya nchi. Ukikatisha watoto 703, umeua kabisa Taifa, umeua nafasi nyingi sana za wanawake ambao wangeweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa shule ni muhimu sana. Ni muhimu mno! Naomba sana tujielekeze katika kuwasaidia wakaguzi. Pale Wilaya ya Rungwe waliahidiwa kujengewa Ofisi ya Wakaguzi. Ramani ipo, kiwanja kipo na bahati nzuri Halmashauri ya Wilaya waliahidiwa kwamba wakijengewa, wafadhili wao watawapa vifaa vyote vya kuweza kusaidia wakaguzi waweze kupata nafasi na unafuu mzuri wa utendaji kazi. Sasa hiyo ofisi itajengwa lini? Ninaomba Mheshimiwa Waziri atueleze

hapa, hiyo ofisi itajengwa lini?  Kwa sababu sasa ni miaka miwili imepita ofisi hiyo haijajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nigusie kuhusu mishahara ya Ma-*REO*.  Ma-*REO* ni watumishi wa Wizara na hao ndiyo wanaoratibu masuala ya elimu katika Mikoa, lakini mishahara yao ni midogo kuliko Ma-*DEO*. Ma-*REO* ndio wanaotakiwa kusimamia kazi za Ma-*DEO*. Kuanzia Januari, 2008 DEO anapata shilingi milioni 1.2. Lakini *REO* alipwe mshahara wa Walimu kama kawaida Sh.300,000/= au Sh.400,000/=.  Hivi kweli atatoa mwongozo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuzungumza niliyonayo moyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru Waziri wa Miundombinu na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kuweza kuwaona au kuwajali wanakigoma ambao walikuwa wanasumbuka sana wakati wa usafiri. Wamewaongezea siku moja, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nisiache....

**NAIBU SPIKA:** Wamewaongezea kitu gani?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Wameongeza safari moja ya treni, zimekuwa safari tatu.

**NAIBU SPIKA:** *Okay*.  Ahsante sana.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Kwa hiyo, tunasubiri zile siku sita ambazo zitawekwa mwezi wa Nane.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiache tena kumshukuru Waziri wa Elimu Mheshimiwa Maghembe na Manaibu wake kwa kutuletea hotuba nzuri ambayo wote tunaifurahia. Nawapongeza sana.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kuhusu watoto wanaosomeshwa na Halmashauri.  Watoto wanaosomeshwa na Halmashauri, wale wenye mazingira magumu pamoja na watoto yatima, kwa kweli Halmashauri mfano ya Kigoma Vijijini haiwatendei haki. Watoto hao wanapokuwa wamechaguliwa kwenda shule za Sekondari huwa wanawachangisha michango mingi sana, wanawaambia wapeleke majembe, mafyekeo, ndoo, mapanga na vile vile wanunue *ream* ya karatasi na inatakiwa wale watoto wawe na sare aina mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao watoto ambao wapo katika mazingira magumu na mayatima hivyo vitu vyote watavitoa wapi? Naomba Serikali leo iweze kunipa majibu haya. Vilevile watoto hawa wamekuwa wanakatazwa kufanya mitihani mpaka kwanza wapeleke pesa. Hizo pesa watazitoa wapi wakati wanasomeshwa na Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli watoto hawa wanasumbuka sana. Kuna wengine wamemaliza kidato cha nne, lakini kwa sasa wameambiwa hawawezi kupewa majibu mpaka kwanza watoe pesa na Halmashauri haitaki kutoa pesa. Je, hizo pesa za kusomesha hao watoto, hao viongozi wanazipeleka wapi kama sio mafisadi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitazungumzia walimu wapya ambao wanapangiwa Mkoa wa Kigoma na hawataki kwenda. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kuwa, tufuate mfano kama vile Mkoa wa Rukwa, tukasema sawa tutafuata mfano, kwa sababu walimu wanaporipoti Mkoa wa Kigoma wanakwenda kwanza kuangalia sehemu ambako lazima wapelekwe. Wanapelekwa sehemu ambayo hakuna barabara, maji, nyumba ya kulala, mtu ana simu, lakini mtandao hakuna. Je, huyo mwalimu akishatoka atarudi tena huko? Si inabidi arudi katika Mkoa ambao una vitu vyote hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiambia Serikali, kwanza iweke maji vijijini, ipeleke barabara, ijenge nyumba za walimu. Nadhani walimu watakapokwenda kuona yote hayo hawataacha kufanya kazi Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama amepangiwa Mgambo, inabidi atumie meli na akitumia meli ukifika wakati wa kusafiri kuja Kigoma Mjini kuchukua mshahara anatoa elfu thelathini kwenda na kurudi elfu sitini na mshahara wake hapo ni shilingi elfu themanini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwalimu gani wa leo atakwenda sehemu hiyo ambayo usafiri ni wa shida, ambayo inatakiwa atoe zaidi ya nusu ya mshahara wake abaki na shilingi elfu ishirini, elfu ishirini zitamsaidia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba walimu wanapokwenda kuchukua mshahara wapate *night allowance*, lakini kwa sasa hakuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ambao wanafikia umri wa kustaafu, wanapostaafu hawana mahali pa kulala. Mtu anajisahau kabisa au mshahara unakuwa ni mdogo kuweza kusomesha watoto shule, malazi, halafu ajenge! Kwa hiyo, unapofika wakati wa kustaafu hana pa kwenda, wakati viongozi wote mlioko hapa na wale walioko katika majukwaa bila mwalimu wasingekuwa *engineers*, Makatibu Wakuu, tumeweza kufikia kote huko kwa sababu ya walimu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iwajengee nyumba halafu iwe inawakata kidogo kidogo kwenye mishahara yao ili watakapostaafu wapate pa kuishi kuliko mwalimu anastaafu, halafu anaanza kwenda kufanya kibarua kwa mwanakijiji. Naomba Serikali ilisikie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya ziara katika Mkoa wa Kigoma nikaenda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Msambya, Kigoma Kusini, nikatembelea shule moja ambayo ina mtoto ambaye hasikii, wala hasemi, mwalimu ndiye alinipa taarifa za huyo mtoto, nikasema sawa. Nikaja kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, lakini sasa hivi amehamia Wizara nyingine akanielekeza akasema peleka hili jina kwa mwenye Kitengo cha Elimu Maalum, lile jina likapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaona majibu hayaji, nikawa napiga simu wakawa wananiambia mengine mengine, ikabidi niende Wizarani kwa Katibu Mkuu nikamwambia. Nilivyomwambia akasema usiwe na wasiwasi huyo mtoto atasoma. Umefika mwezi wa Tano wakanipa taarifa wakaniambia kuwa, yule mtoto sasa amepangiwa shule kwenda Tabora, huyu mtoto ni mtoto wa kike. Kwa hiyo, barua utaikuta imeshafika kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyokwenda kweli nikaikuta ile barua, lakini yule mtoto amepewa barua tu, Serikali imemwacha hivyo hivyo bila kumsomesha. Je, huyo mtoto atasomeshwa na nani bila Serikali? Kwa sababu mama yake hana uwezo, yuko katika mazingira magumu. Jamani wahusika naomba mumsaidie huyo mtoto, hana mbele wala nyuma. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtoto ni mlemavu, hasikii wala hasemi, lakini ameshinda kwenda *form one*. Hamwoni kama ni miujiza mikubwa! Jamani nilikuwa naomba Serikali iweze kumsaidia. Katika kufanya majumuisho kwa haya tuliyoongea na ambayo tumeandika, naomba Serikali inipe jibu: Je, huyu mtoto atasomeshwa au hasomeshwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilifikiri wewe ulimchangia nauli, kumbe hapana! *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri wa Elimu - Mheshimiwa Jumanne Maghembe; Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Kabaka; Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu. Hongereni sana kwa kuandaa hotuba nzuri, inayoeleweka na yenye kulenga mafanikio mazuri ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi zangu, kabla sijaendelea, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na mafanikio yaliyopatikana baada ya kuanza ujenzi wa sekondari hizi za Kata. Mafanikio makubwa yamepatikana baada ya

mipango hii ya *MMEM* na *MMES*. Mkoa wetu wa Kigoma kabla ya kuchukua jukumu hili la kuanza kujenga shule za Kata tulikuwa na shule thelathini na nne, lakini baada ya mpango huu wa ujenzi wa shule za Kata mpaka sasa tuna shule themanini na nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali yetu na wananchi kwa kujitolea kushiriki katika shughuli za ujenzi wa shule za sekondari, lakini shukrani zangu pia naomba zimwendee Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Simbakalia, Wakuu wa Wilaya zote tatu kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuwahimiza wananchi kushirikiana na Wakurugenzi, Madiwani na viongozi wote wa Mkoa ule kwa kuhakikisha shule zinajengwa na sasa hivi watoto wetu wanapata shule za kusomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ambayo tumeyapata, bado kuna matatizo madogo madogo ambayo yanajitokeza. Shule nzuri zimejengwa za msingi na za sekondari, lakini matatizo makubwa ni walimu. Ukosefu wa walimu ni tatizo kubwa sana. Kila tunapokwenda vijijini kufanya ziara, unapomaliza kufanya kikao, wananchi wananyoosha mikono swali la kwanza litakalojitokeza, Mheshimiwa Mbunge, shule tumejenga, walimu hawatoshi. Tunaomba mtupie Mkoa wa Kigoma macho kwa sababu ni Mkoa ambao upo pembezoni, kwa hiyo, walimu wanaopangiwa Mkoa huu hawaendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wale walimu wanaopelekwa kule wapangiwe *hardship allowance* ili wasiache kwenda katika Mkoa wetu kufundisha, kwani Mkoa wetu ni Mkoa ulioachwa nyuma kwa muda mrefu kwa sababu ya miundombinu. Naamini kabisa ikifanyika hivyo, walimu watakwenda kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba muendelee kuuangalia mkoa wetu kwa kushirikiana na viongozi wengine, Waziri Mkuu, watu wanaohusika na Miundombinu barabara. Wote kwa pamoja mkishirikiana mtauweka Mkoa wetu mahali pazuri, walimu watakuja, hawataona sababu za kutokuja kufanya kazi Kigoma. Kwa hiyo, naomba Mkoa wetu uangaliwe kwa jicho la huruma kwa sababu ni Mkoa ambao upo pembezoni, umesahaulika kwa muda mrefu, walimu wakipangiwa kule hawaendi kwa sababu ya matatizo ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ya shule zilizojengwa, lakini bado kuna matatizo ya maabara. Wenzangu wameshazungumza, lakini inabidi nizungumze kwa sababu tatizo hili ni kubwa sana. Tunaomba Serikali kwa kuunganisha na nguvu za wananchi. Najua tukianza, wananchi wakajenga, Serikali ikaunga mkono, tutaweza kupata maabara. Tunaomba Wizara itupie macho Mkoa huo kwa kuwekeza katika ujenzi wa maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zinajengwa, nyingine utakuta ziko mbali na maeneo ambayo watoto wanaishi. Kwa hiyo, utakuta watoto wa kike mara nyingi wanapata shida, wanapokwenda shuleni, wanakutana na vikwazo na vishawishi mbalimbali vinavyowafanya waweze kujiingiza kwenye janga kubwa la kutenda vitendo ambavyo sio vizuri kutokana na mazingira yanayowazunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba hosteli zijengwe katika shule zetu za Kata. Wananchi ni wasikivu, wanapenda maendeleo. Tukienda kuwaambia kwamba tukiweka nguvu zetu Serikali itatuunga mkono tutaweza kupata hosteli, watatekeleza. Kwa sababu kwanza watakuwa wamepunguziwa mzigo mkubwa kwa watoto, maana yake mtoto anaposoma huku anaishi nyumbani kuna matumizi mengine ambayo yanakuwa ni makubwa zaidi kuliko ambavyo angekuwa anaishi hosteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzia kuhusu uhaba wa walimu. Naiomba Wizara kwa kupitia Maafisa Elimu iweze kuhakikisha mgawanyo wa walimu unakuwa wa uwiano ambao ni mzuri kwa sababu shule nyingi za mjini ndizo zinapata walimu. Walimu vijijini hawaendi, unakuta wote wameishia mjini, vijijini hakuna. Wizara ya Elimu iagize Maafisa Elimu kuhakikisha walimu wapya wanaopelekwa kwenye Wilaya zetu, kwenye Halmashauri zetu wasipangiwe mijini bali wapelekwe vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule vijijini kuna matatizo makubwa sana, walimu hakuna, shule moja unakuta ina mwalimu mmoja. Tunaomba walimu wapelekwe vijijini, ndipo kwenye matatizo makubwa sana mjini kuna unafuu kwa sababu utakuta pengine mwalimu ameolewa, mume wake ni Mkurugenzi atapangiwa mjini. Mwalimu ameolewa pengine mume wake ni Daktari atapangiwa mjini. Kule kijijini unakuta walimu hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye huduma za walimu. Mimi mwenyewe ni mwalimu kwa hiyo, nafahamu adha kubwa wanayoipata walimu kwa sababu huko nyuma nilikuwa nakutana nayo. Naomba tuwaangalie walimu kwa jicho la huruma kwa sababu walimu wanafanya kazi kubwa sana. Ualimu ni kazi ya wito.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba wasaidiwe kupangiwa mishahara ya kutosha, tukumbuke kwamba mishahara haiwatoshi walimu na wao wana familia ambazo zinawategemea kama sisi humu ndani, mwalimu anasomesha watoto shule ya msingi, sekondari, chuoni mpaka chuo kikuu na mshahara wake huo ndio unatakiwa ukidhi mahitaji ya familia yake. Naomba tuwajengee walimu mazingira mazuri kwa kuwapa mishahara inayokidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kuhusu malimbikizo. Naomba Wizara iandae utaratibu mzuri wa kuhakikisha walimu wanalipwa malimbikizo yao kwa wakati unaofaa kwa sababu walimu wengi wameingia kwenye matatizo ya kuingia mikataba na wafanyabiashara wanaokwenda kuwakopesha pesa kwa riba kubwa sana, matokeo yake unakuta mwalimu anahangaika, akianza kuupanga ule mshahara hautoshi kwa sababu tayari wapo wajanja wamekwenda na kumpa lugha nzuri, mwalimu akastukia amekwenda kukopa pesa kwa riba kubwa sana. Baadaye yanakuwa ni matatizo makubwa kwa mwalimu huyu. Anakuta anakatwa pesa yake yote mpaka inayobaki haitoshi tena kwa familia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ipange mipango mizuri ya kuhakikisha walimu wanaishi katika mazingira mazuri. Wakiishi katika mazingira mazuri, naamini

tunaipenda kazi yetu na tukifanyiwa mambo mazuri tutafanya kazi nzuri kabisa bila kinyongo chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara iwakumbuke walimu kwa kuboresha mishahara yao, lakini pia kwa kuhakikisha inalipa malimbikizo ambayo ni ya muda mrefu. Haya malimbikizo ndiyo kilio chao kikubwa. Hawana matatizo na Wizara yao. Serikali ikiwakumbuka na kuwalipa vizuri, walimu ni watu ambao wanajitoa kwa moyo mmoja, wanafanya kazi kwa mapenzi makubwa ya kuhakikisha Taifa letu linakwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie wakaguzi. Baba yangu ni mwalimu, nakumbuka wakati nikiwa mtoto mdogo, ukiona siku hiyo baba ameamka asubuhi, ana hekaheka, ujue leo kuna wakaguzi. Zamani wakaguzi walikuwa wanaogopwa sio siku hizi, wakaguzi siku hizi hawaogopwi kabisa, lakini mwalimu wa zamani mama Margareth Sitta ni shahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani Mkaguzi akiwa anakuja shuleni kwako walimu wanajiandaa, yaani wanahakikisha mazingira yao ni mazuri hadi nyumba zao wanazoishi. Wewe mama nyumba imedekiwa? Mama anahakikisha mazingira ya nyumba ya mwalimu yako safi, lakini siku hizi hawaogopwi kwa sababu mazingira yao sio mazuri. Utakuta wakaguzi wa elimu wamepewa kisamurai. Samurai itaweza kwenda vijijini ambako kuna miundombinu mibovu, haiwezekani!

**NAIBU SPIKA:** Kinini umesema?

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, samurai. Kuna kigari kinaitwa samurai, kipo kama kibiriti vile. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu walikuwa wapo chini ya Katibu Mkuu, lakini juzi wamepelekwa *Local Government*. Kule walikopelekwa sasa, naomba Wizara ihakikishe Wakaguzi wa Elimu wanafanyiwa mambo mazuri ili wapate moyo wa kwenda kufanya kazi kwa kujituma na kwa kuipenda kazi yao. Sio unamkuta mkaguzi amekaa kama vile, yaani anazidiwa hata na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwalimu akihamishwa kutoka kituo hiki kwenda kingine analipwa fedha zake haraka iwezekanavyo, lakini sio Mkaguzi. Yeye fedha zake zinachelewa, atazunguka anasubiri fedha mpaka mwisho anakata tamaa. Naomba maslahi ya wakaguzi wa shule za msingi yaboreshwe. Watengewe fedha za kutosha ili waweze kufanya kazi yao kiufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaguzi wana shida sana. Mafuta ya kuweka kwenye gari ili waweze kuzunguka vijijini, kukagua ni jinsi gani kazi zinafanyika, jinsi gani walimu wanafundisha, hawana. Naomba Wizara iliangalie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi nyuma kule kwenye shule zetu za sekondari. Tunasema tujenge maabara, lakini bila umeme hata tukijenga hakuna kitu. Tunaomba

Wizara na hili iliangalie, tunapojenga maabara tuhakikishe kila kitu kinakuwepo. Tunaomba Wizara itusaidie kuhakikisha kwamba, umeme unapatikana katika shule zinazojengwa, watafute mbinu yoyote hata umeme wa *solar* upo, wasambaze kwenye shule hizi ili ziweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza haya machache, naomba niunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mkoa wa Kigoma umewakilishwa kikamilifu, maana yake nilipata tatizo kwamba niwape hawa wazungumzaji wawili kwa pamoja, lakini nikakuta kila mtu ana haki yake ya kuzungumza. Kwa hiyo, ikabidi niwaruhusu.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu hupata mishahara na upo uwezekano wa kukatwa pale wanapokuwa na deni. Kwa nini Serikali isiwaombe mashirika kama *NSSF*, *PPF*, *NHC* kujenga nyumba za walimu? Ninaamini kuwa fedha za ujenzi wao zitarudi bila ya matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kutoa tamko la Shule ya Sekondari Nanyanje kuendelea, Shule ambayo iko Wilaya ya Lindi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile fedha za *MMES* ambazo zilipaswa kupelekwa katika Sekondari ya Nanyanje na badala yake zikapelekwa Sekondari ya Chikonji zitarudishwa kwa Shule husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna waalimu ambao wamewekwa katika kundi la waalimu hewa kwa sababu wengine walikuwa likizo, masomoni wakati zoezi hili la uhakiki likiwa linafanyika katika vituo vyao vya kazi. Ni nili watarudishwa tena katika *payroll* ya mishahara? Nashauri warudishwe katika *payroll* kwani ikichelewa italeta kero kubwa zaidi, kwani kadri mishahara inavyochelewa ndivyo malimbikizo yanazidi na mateso ya kuishi bila mishahara yanazidi kuzorotesha maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iwaongezee fedha za mafuta Wakaguzi wa Shule za msingi. Kiwango cha mafuta wanachopewa hakitoshi kwa mizunguko yao ya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi Wizara kwa kuwawezesha wakaguzi kupata usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo matatu ambayo ninaomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiw Waziri:-

Mheshimiwa Naibu Spika, takriban Shule zangu zote za msingi katika Jimbo langu la Kibakwe kuna upungufu wa walimu. Kwa sababu hiyo, Walimu Wakuu wanawaomba vijana waliomaliza Kidato cha Nne au Sita kuwasaidia na wanafanya hivyo kwa mafanikio makubwa sana. Je, Serikali inaonaje kama wale wenye moyo wa kufundisha wakawa *assessed* toka Shuleni na Wilayani wakapelekwa vyuo vya Ualimu kwa maana hawa hawawezi kuondoka kwenye maeneo hayo ambapo Shule nyingi ambazo hazina walimu ni zile zilizoko katika mazingara magumu kwa kuwalegezea masharti ya kujiunga na vyuo? Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wa Elimu ya Ufundi na vikwazo vinavyowakabili kimaendeleo. Lipo tatizo linalowakabili walimu wengi wa masomo ya ufundi hali ambayo inawakatisha tamaa sana.

(i) Hawapandishwi madaraja;
(ii) Wahakubaliwi kwenda masomoni; na
(iii)Hawapandishwi vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zinazotolewa ni kama ifuatavyo:-

(a) Kwamba, kuwa mfano wale wenye *Advanced diploma* in *Civil Engineering* wanazuiwa kufanya *Post Graduate* kwa maelezo kwamba hiyo *Post Graduate* sio ya walimu;

(b) Kuhusu madaraja na vyeo, sababu za kutowapandisha ni hivyo hivyo kwamba kama wanataka kupandishwa wakasome *Post Graduate* ya *Education*, vinginevyo kama ni ufundi hawapandi. Je, hivi fundi ni nani? Mwalimu wa mafundi ni nani? Hapa kuna mkanganyiko, naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itoe maelezo rasmi juu ya wigo wa michango ya wanafunzi katika Shule za msingi na Sekondari hapa nchini:

(i) Ni mchango gani halali ya kisheria inayoruhusiwa kuwa Shule ya Msingi na Sekondari hapa nchini?

(ii) Ni michango gani ambayo haipo kisheria, lakini inaweza kuchangiwa/kulipishwa kutokana na makubaliano ya Bodi za Shule na wazazi na mwisho au ukomo wake ni kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITA LOUISE MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi nyingi sana kwa Wizara ya Elimu na Ufundi kwa kazi kubwa wanayoifanya na mchango wao katika nchi hii. Pongezi nyingi sana kwa mpango mzima wa *MMEM* na *MMES*. Napenda kuchangia kwa kuwashauri wasaidie ofisi za Kanda za Ukaguzi, hasa ile ya Dar es Salaam na Pwani. Nafasi waliopo ni ndogo sana na mazingira ya uwekaji wa rekodi sio nzuri. Wanafanya kazi kubwa. Nawashauri wawasiliane na *National*

*Housing Corporation* wapewe ile jumba *floor* ya pili na wawatoe wale wapangaji mmoja mmoja, pale *MAVUNO House.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Wizara imtumie Prof. Maghembe, Mheshimiwa Mahiza, Mheshimiwa Kabaka, Bw. Dihenga na Bw. Mhaiki. *Well done.*

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha siku ya leo kuishika kalamu hali nikiwa *MAUJID*. Pia nakushukuru wewe kwa namna unavyotuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ambayo itawajengea msingi wa maisha Watanzania na kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza, naomba nizungumzie suala la Walimu. Tukimzungumzia mwalimu, tunajua mwalimu ndiye mwenye uwezo wa kumpandisha daraja mtu na akawa na heshima kubwa duniani. Kwa kulijua hili, ni vyema Serikali iwapatie uvumbuzi walimu ili waweze kufanya kazi zao kwa moyo na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hivi, nazungumzia malimbikizo ya madeni ya walimu. Napata wasiwasi mkubwa kwa kuona iko siku kizazi chetu kitakosa walimu, kwani Serikali hadi leo haijaweza kuwaondolea kero na matatizo walimu ambayo yanawaathiri katika kutenda kazi zao. Kero hizi ni pamoja na kutolipwa haki zao kwa wakati, hasa pale ambapo wamekwishatimiza wajibu wao. Mara nyingi malimbikizo ya walimu kutokana na madai ya mishahara isiyolipwa kwa wakati; marekebisho ya mishahara baada ya kupewa vyeo *(Arrears); na* fedha za matibabu, likizo, gharama za masoma na uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2007, Serikali imekuwa ikidaiwa jumla ya Shilingi bilioni 9.5 za Kitanzania. La kusikitisha, walimu walipoazimia kufanya mgomo, ndio wakapewa haki zao. Pamoja na malipo hayo, bado Serikali haijafanikisha deni lote. Yasadikika Shilingi bilioni 7.1 zimelipwa kwa walimu wa shule na vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa Serikali ina malimbikizo mapya ya madeni ya jumla ya Sh.12,266,216,697.99 katika Mikoa 21. Hii ni kasoro kubwa kwa nchi yetu. Kwa nini iwe hivi? Mimi mtazamo wangu nimegundua, Wizara kushindwa kulipa fedha kutokana na uhaba wa bajeti. Hivyo Serikali iandae mikakati ya makusudi ili kuondoa kero hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za walimu. Ni vyema niipongeze Wizara kwa jitihada zake za ujenzi wa madarasa kupitia *MMEM* na *MMES*. Kwa ujenzi wa shule ni mzuri ila dosari iliyopo ni ukosefu wa nyumba za walimu. Ni vizuri Serikali

iongeze nguvu za ziada katika kuhakikisha upatikanaji wa nyumba bora na za kutosha ili walimu waishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa walimu shuleni, tatizo hili linaongezeka siku hadi siku na kuathiri utoaji wa elimu kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mitihani shuleni. Mtihani ni kipimo cha mwanafunzi, ili aweze kutoka na kwenda katika madarasa. Mara nyingi Wizara hufuta matokeo kwa kisingizio mtihani umevuja. Ni aibu kwa Wizara. Suala hili ni vyema Serikali iangalie kwa kina na atakaebainika awajibishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara ya walimu. Pamoja na jitihada za Serikali katika kuhakikisha kuwa watumishi wake wanalipwa mishahara yao kwa wakati, lakini hivi sasa tayari mambo ya kuchelewesha mishahara inaanza kurejea. Walimu hivi sasa wameanza kupokea tarehe 30 hadi 5 ya mwezi unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali, ili Wizara iweze kujikimu, basi iwezeshwe. Bajeti iweze angalau kuondoa haya nilioyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nasita kwa kusema. Ahsante.

**MHE. YONO STANLEY KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Prof. Maghembe na Naibu Waziri na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna tatizo la walimu katika shule za msingi na sekondari, nashauri Serikali iongeze vyuo vya walimu na ikiwezekana kila mkoa kuwe na chuo cha walimu. Gharama za kuendesha vyuo hivyo, Halmashauri zichangie kutokana na vyanzo vya mapato na ikiwezekana hata wafadhili wahisani wasaidie vyuo hivyo. Mashirika ya dini pia yaruhusiwe na yawezeshwe, kujenga vyuo vya walimu ila Wizara ijitahidi kuhakiki na kudhibiti ubora wa elimu itolewayo kwa walimu hao.

Pia muda wa mafunzo wa walimu hao uwe wa kutosha, sio miezi sita, iwe kuanzia miaka miwili na kuendelea.

Ufinyu wa bajeti unaweza kupungua kama Serikali ikiweza kuongeza kwenye vyanzo kutoka taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali hata ikiwezekana kutoka kwa wafadhili kutoka nje ya nchi.

Bodi ya mikopo ya elimu ya juu wajitahidi kukusanya madeni waliyokopesha kwa kutumia mawakala ambao watakuwa waaminifu na mahiri.

Mwisho, naomba Chuo cha Ulembwe – Njombe kilichopo Jimboni kwangu, kiwe Chuo cha Ufundi chini ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi kuliko ilivyo sasa, chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Hakikidhi haja ya wananchi wa Jimbo langu na

Taifa kwa ujumla. Hawana gari, umeme wala vitendea kazi. Eneo ni zuri sana na eneo ni kubwa sana zaidi ya ekari 100.

Pia kuna majengo pale Wanging'ombe, jirani na Wanging'ombe Sekondari, wafadhili walijenga lakini hayatumiki vizuri. Nashauri kwamba, badala ya kutumia wataalam wa kilimo na Katibu Tarafa wa Wanging'ombe, ningeomba Serikali kupitia Wizara yako ichukue majengo hayo na kuwa Chuo cha Ufundi au shule ya *A level* ya Wanging'ombe – Njombe.

Kwa vile katika Wilaya ya Njombe kuna upungufu mkubwa wa kidato cha tano na sita, sisi wananchi wa Njombe tumeona tuanze kujitolea kufanya harambee ya kuchangisha fedha kwa ajili ya kidato cha tano na sita Wanging'ombe, Wawike na Mekoga.

**MHE. ESTHER KABADI NYAWAZWA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndiyo msingi wa maisha. Naendelea kuipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa elimu kwa kutenga fedha kama kipaumbele kwa kuzingatia kazi kubwa inayotakiwa kusimamia elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *MMEM* na *MMES* imefanya mabadiliko makubwa. Kwa shule zote zilizosimamiwa vizuri, naipongeza sana Serikali kwa kuleta mpango mzuri.

Shule za msingi sasa hivi ziko katika hali nzuri, watoto wanasoma vizuri, hawakai tena chini, sekondari za Kata zimepunguza adha kubwa kwa watoto wengi kushinda na kukosa nafasi za kuendelea na masomo ya sekondari. Naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeboresha sana eneo la shule za msingi na sekondari. Naomba mambo yafuatayo yazingatiwe:-

1. Serikali ilete mpango maalum kwa kuanzisha ujenzi wa madarasa ya kidato cha tano na sita, angalau hata kila Tarafa, shule moja ikienda sambasamba na Hosteli.

2. Serikali iweke mpango wa kudumu kusomesha walimu, pia na upanuzi wa vyuo vya ualimu uendane na zoezi hili ili tatizo la walimu liishe.

3. Serikali iendelee, kuongeza vyuo vikuu nchini vya Serikali, ili watoto wengi wasiokuwa na uwezo, wachukuliwe na Serikali.

4. Serikali ilitafutie dawa tatizo la watoto wa kike kupewa mimba kabla ya kumaliza masomo yao.

5. Serikali ipeleke vifaa vya maabara kwa sekondari zote zilizokamilisha hususan shule ya Sekondari ya Ngulla, iko katika Wilaya ya Kwimba Jimbo la Sumve.

6. Serikali isimamie vizuri uchaguzi wa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ili pasiwe na upendeleo kwa watoto wanaotoka katika Kata za vijiji kutopata nafasi za kuingia vyuo vikuu.

7. Bodi ya mikopo izingatie kutoa mikopo kwa wanafunzi waliofaulu vizuri bila upendeleo na migomo iishe, utaratibu uandaliwe mapema kabla ya masomo kuanza.

8. Vyuo vya *VETA* viboreshwe huko mikoani ili tupunguze vijana wengi kukaa bila kazi ya kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi kwa mambo yafuatayo kuhusiana na malengo ya mwaka 2008/2009:-

1. Ni vigezo gani, vitatumiwa kuwapata wanafunzi watakaogharimiwa elimu ya sekondari kwa wanaotoka katika familia zenye kipato duni na yatima?

2. Ruzuku itakayotolewa na Serikali katika ujenzi wa madarasa 200 ya kidato cha sita, madarasa haya yatajengwa katika mikoa pia/au wilaya zipi?

3. Ruzuku itakayotolewa na Serikali kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara, Shule ya Sekondari ya Ngulla itapewa kipaumbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, watumishi wa Wizara na Mashirika yote ya elimu na walimu wote nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuelimisha watoto na vijana wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa Taifa lolote lile hutegemea ubora wa elimu itolewayo kwa watu wa Taifa lile. Je! Mikakati gani imewekwa na inatumika ili kudumisha ubora wa elimu katika mazingira hayo magumu na ya mabadiliko?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanyika katika kupanua au kujenga shule za sekondari nchini, naomba ushauri huu usikilizwe.

(a) Lugha ya kufundishia masomo katika shule za sekondari ni Kiingereza, isipokuwa somo la Kiswahili. Tatizo ni kwamba, walimu wengi hawajui lugha ya Kiingereza vizuri, hivyo kasoro hii inaathiri utoaji bora wa elimu hiyo hadi vyuo vikuu. Nini mkakati wa Wizara ili kutatua tatizo hili?

(b) Kupeleka elimu TAMISEMI ni kuwa elimu TAMISEMI wamelemewa na matatizo mengi. Elimu irudi elimu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuchanganya elimu ya juu na elimu nyingine kunaathiri uongozi wa pande zote juu na chini. Nashauri elimu ya juu itenganishwe na elimu ya chini kama ilivyokuwa kabla.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upanuzi wa elimu ya sekondari (shule nyingi) elimu ya sekondari haiwezi kusimamiwa kutoka Dar es Salaam. Wala matumizi ya Ma-*REO'S* hayatoshelezi kwa sababu hawana uwezo kusimama shule za msingi na za sekondari. Wala matumizi ya maafisa Wilaya hayakidhi mategemeo. Matokeo ni shule za sekondari kukosa uongozi kamili toka juu. Vipi muundo wa Wizara usitazamwe upya ili kukaribisha uratibu na usimamizi wa shule karibu na pale zilipo? Kimkoa au kikanda au kiwilaya au cheo cha *REO* kirudishwe na aongezewe wataalam na madaraka ili asimamie hata elimu ya sekondari, awe na idara tatu: Elimu ya Msingi, Sekondari, ufundi na ualimu.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, maabara na mkataba yajengwe na Wizara na shule chache ziwe na maabara katika Wilaya kwa vile haiwezekani kuwa na maabara imara na katika kila shule. Kwa kubakiza mtihani wa kidatu cha pili, wale watakaofaulu vizuri hisabati na sayansi ndio watakaochaguliwa kwenda *Form III* katika shule zenye maabara.

(f) Mitihani ya darasa la nne na kidato cha pili iendelee na kuimarishwa badala ya kupuuzwa. Tukiipuuza tutaua elimu. Walimu wataacha kufundisha. Tusiongeze matatizo katika matatizo.

(g) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ihusike katika ujenzi wa shule za sekondari ili uweze kuratibu na kuanzisha ujenzi wa shule na mafunzo ya walimu na mahitaji mengine. Shule sio majengo tu au wanafunzi tu. Shule ni majengo bora, walimu wengi na bora na vifaa bora na vingi vya kufundishia na mazingira bora ya kufundishia na kupokelea elimu. Nashauri Wizara ya Elimu iunde Kata za Elimu na Tarafa za Elimu ili iwe rahisi kwake kuratibu elimu nchini. Kata za sasa ni za utawala na zinaundwa kila siku bila kujali uwingi wa watoto katika shule zilizoko katika Kata.

(h) Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro shuleni inaathiri utoaji elimu bora. Kwa kuwa ukosefu wa chakula ni moja ya sababu hizo, Wizara ina mikakati gani ya kutatua tatizo hili? Vipi, mbona Ulaya hakuna migomo ya aina hii shuleni? Sheria itungwe ili shule zisiwe mahali pa kuzalisha vijana manunda na wasio na maadili mema. Madhara ni mengi, tusipoziba ufa tutashindwa kujenga ukuta.

(i) Wizara isiunde Tume au Kamati ndogo ya kuangalia mfumo na maendeleo ya elimu nchini.

(j) Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ni muhimu, lakini mabadiliko yasiyo na dira au mwelekeo thabiti ni hatari kwa nchi yetu. Hatuwezi kubadilisha

magurudumu ya gari huku linatembea. Nia nzuri peke yake haitoshi, lazima nia nzuri iambatane na njia sahihi za kiutekeleza. Njia nzuri ya kuua Taifa ni kuua misingi ya utoaji wa elimu bora.

Twende pamoja;
Tushirikianie;
Tuboreshe elimu;
Tujenge nchi yetu, Tanzania

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLE N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na wasaidizi wake kwa hotuba yake nzuri na kwa kazi nzuri wanazofanya za kuendeleza elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali na wananchi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupanua elimu ya msingi na sekondari. Wapo watu wanaoeleza mafanikio hayo kwa kudai kwamba yanashusha viwango vya elimu kutokana na matatizo mengi yaliyopo. Madai hayo hayana maana kwa kuwa mtoto anayepata elimu hiyo atakuwa na nafuu sana kuliko aliyeikosa. Aidha, mtoto huyo anapata muda wa kukua. Matatizo yaliyopo ya ukosefu wa waalimu na baadhi ya huduma yataendelea kushughulikiwa hatua kwa hatua ili kuboresha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi ulilenga kupunguza idadi ya watoto kwa chumba cha darasa kufikia watoto 40. Kwa Jimbo langu la Ubungo hali ni tofauti kabisa. Zipo shule zenye hadi watoto 150 kwa chumba na karibu shule zote zina wastani wa zaidi ya watoto 80 kwa chumba. Hali hii mbaya haiwezeshi *effective teaching.* Kilichotokea ni kwamba baada ya mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari kuanza, upanuzi wa shule za msingi ulisimama. Tunaiomba Serikali iendelee kuchangia ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata mafanikio makubwa katika ujenzi wa shule za sekondari. Kwa jimbo langu, maeneo ya kujenga shule za sekondari yanapatikana kwenye maeneo ya vijiji vya Goba, Kibamba, Mbezi Luis, Kimara na Makuburi. Katika baadhi ya Kata zimejengwa shule nyingi, kwa mfano: Kibamba 7, Goba 5, Mbezi Luis 3 na kadhalika. Wananchi wa Kata hizi wanahitaji kusaidiwa kwa kuwa wanahitajika kufanya kazi kubwa sana ya kujenga shule hizo na ni kweli kwamba watoto wengi watakaosoma kwenye shule hizo hawatoki kwenye Kata hizo. Kwa mfano, watoto wa Mpaji Magahe walioingia sekondari iliyoko kwenye mtaa wao ni watano tu. Inabidi kuweka utaratibu wa kujenga shule hizo ambao hautakuwa mzigo kwa wananchi wanaoishi kwenye Kata hizi ambao wengi ni maskini sana.

Tatizo lingine linatokana na ukweli kwamba shule hizo zimejengwa pembeni mwa jiji ambako ndiko yanakoweza kupatikana maeneo ya kujenga shule, kutokana na hali hiyo. Watoto wanalazimika kusafiri masafa marefu kutoka Kata za mjini kwenda kusoma kwenye shule hizo. Usafiri ni mgumu sana na watoto huchelewa sana kufika shuleni na baadhi ya watoto wamepata ajali na mmoja wao kufariki.

Kuna ulazima wa kujenga hosteli kwa ajili ya kuwapatia watoto malazi karibu na shule zao ili kuwaondolea adha na hatari wanazopitia kufika shuleni. Serikali inapaswa kutambua mazingira ya kipekee ya Jiji la Dar es Salaam na kujitahidi kulisaidia kugharamia mipango yake ya kuendeleza elimu. Asilimia kumi ya Watanzania wanaishi Dar es Salaam. Kwa hiyo, idadi ya watoto wanaohitaji kupatiwa elimu ni kubwa sana.

Aidha, elimu haikupewa kipaumbele katika miaka iliyopita, jambo ambalo linasababisha kuwapo kwa limbikizo kubwa sana la ukosefu wa huduma (miundombinu) za elimu. Jiji halimudu jukumu hili bila msaada mkubwa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inatumia sehemu kubwa sana ya mapato yake kujenga shule za sekondari. Hii ina maana kwamba huduma nyingine hazipewi umuhimu. Ni kweli kwamba Halmashauri ya Manispaa ina jukumu la kuchangia utekelezaji wa mipango ya kuendeleza elimu. Lakini haikutegemewa kwamba ingeachiwa uzito mkubwa kama huu unaotokana na maamuzi ya Serikali na ambayo hayakuwa miongoni mwa vipaumbele vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna kazi kubwa ya kujenga vyumba vya madarasa, maabara, maktaba na majengo ya utawala kwenye shule za sekondari. Majengo kama hayo yanahitajika kwenye shule za msingi ili kukidhi mahitaji makubwa yaliyopo. Aidha, shule nyingi zina upungufu wa waalimu ambao unasababishwa na mazingira magumu yaliyoko kwenye mitaa zilikojengwa shule hizo. Waalimu wanalazimika kuishi mbali na shule kutokana na ukosefu wa nyumba za waalimu au za kupanga. Hakuna utaratibu wa kuwafidia kwa gharama wanazoingia kusafiri kwenda shuleni na kujihudumia wawapo shuleni. Serikali inapaswa kuliangalia suala hili ili kuwawezesha waalimu kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALIM AL-QASMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kuamka nikiwa mzima na kufika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa hali unavyotulea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yakeambayo kwangu nina hofu kuona utekelezaji wake utakuwa mzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa njia mbili tofauti:

a) Bajeti ya Wizara haiwezi kukidhi mahitaji ya Wizara; na
b) Mabaki ama malimbikizo ya madeni yanayoikabili Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Wizara ya Elimu ina malimbikizo ya madeni kwa walimu wengi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wana chama chao kisheria kijulikanacho kama *CWT*. Chama kiliwasilisha kilio cha madai haya ya madeni ya walimu. Serikali iliunda kamati za uhakiki wa madai hayo. Baada ya uhakiki huo, Kamati mwezi Februari, 2007 jumla ya madai ya walimu hao ilikuwa ni shilingi bilioni 9.5. Madai haya yaliwafikia walengwa, baada ya tamko la walimu kuandaa mgomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imeiwezesha Serikali kulipa deni la walimu kama ifutavyo:- shilingi bilioni 7.1 kwa ajili ya walimu wa shule za msingi na shilingi bilioni 700 kwa walimu wa shule za sekondari na vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Wizara inakabiliwa na matatizo na kwa hali ya bajeti hii Wizara itashindwa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa walimu nchini pamoja na kazi nzuri za Serikali kwa ujenzi wa madarasa kupitia *MMEM*, pamoja na uandikishaji kwa watoto, bado madarasa haya hayana walimu. Ni vyema Serikali ichukue hatua za makusudi ili walimu waweze kutosha madarasa tulionayo. Kukosekana kwa walimu ni hasara kubwa kwa kizazi chetu cha baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna ukosefu wa nyumba bora za walimu. Jambo hili linazorotesha walimu kufanya kazi zao, kwani unapomfanya mwalimu aishi karibu na eneo la kazi yake unamfanya awe na imani na kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara nyingi kitendo cha Serikali kufuta matokeo ya wanafunzi kwa baadhi ya shule zetu. Hii inatokana na ubovu ama uzembe wa makusudi kuvujisha mitihani kwa wanafunzi wetu. Kitendo hiki kinadhoofisha maendeleo ya mwanafunzi ambae hakuhusika. Ni vyema Serikali ilikomeshe tendo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matokeo mbali mbali ya walimu kushambuliwa, kupigwa na wengine kufa wakiwa katika vituo vyao vya kazi. Hii inatokana na jamii kutothamini umuhimu wa kazi za walimu kasoro hizi zinapotokea zinahitaji gharama. Je, Wizara hili wanalijua?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara ya walimu, pamoja na jitihada za Serikali katika kuhakikisha kuwa watumishi wake wanalipwa mishahara yao kwa wakati, mwaka 2007, walimu walikuwa wakilipwa mishahara yao kwa wakati, lakini hivi sasa mishahara hiyo imekuwa ni tatizo kwa walimu, kwani walimu wameanza kupokea mishahara tarehe 30 hadi 5 ya mwezi unaofauata. Kwa mfano hadi tarehe 30 Mei, 2008 walimu walioko chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hawakuwa wamepata mishahara yao ya mwezi Mei, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni ufunguo wa maisha. Ni vyema Wizara hii ipewe uwezo ili iweze kutuzalishia mema juu ya kizazi chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nasema ahsante.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ninaunga mkono hoja hii. Pamoja na hilo, ningependa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Maghembe na Naibu wake, Mheshimiwa Mahiza kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, pia napenda kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara - Prof. Dihenga pamoja na watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti .

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nanyumbu kuna matatizo makubwa sana katika sekta hii ya elimu. Kwanza kabisa, Wilaya ya Nanyumbu ina uhaba mkubwa wa walimu. Hivyo kusababisha wanafunzi kukosa elimu bora inayotakiwa. Mwaka jana Wilaya ya Nanyumbu ilikuwa ni ya mwisho katika mtihani wa darasa la saba. Hii ni kwa sababu ya uhaba wa walimu. Shule nyingi utakuta zina mwalimu mmoja au wawili toka darasa la kwanza hadi la saba. Je, Wizara itatusaidia vipi sisi wa Wilaya ya Nanyumbu kuhusu kero hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine, Wilayani Nanyumbu ni uhaba wa vyumba vya madarasa, uhaba wa nyumba za walimu, matundu ya choo na uchakavu wa madarasa. Wilaya ya Nanyumbu ni wilaya iliyopo pembezoni mwa nchi na inapakana na nchi jirani ya Msumbiji. Wilaya hii ilikosa kupata huduma za jamii ikiwa ni pamoja na madarasa kwa kuwa Nanyumbu ilikuwa ni uwanja wa mapambano wakati wa harakati za kupigania uhuru wa Msumbiji. Hivyo basi, napenda kuiarifu Wizara juu ya matatizo hayo na kwamba hali ni mbaya sana.

Shule kama za Ngalinje, Makanya, Mkwajuni, Mtawatawa, Namaromba, kwa uchache zina hali mbaya sana na hazina hadhi kabisa. Shule za Mkoromwana, Chinyanyira zimeezekwa kwa nyasi. Je, hii ni sawa katika karne hii, tena miaka 47 tangu tupate uhuru? Pia vijiji vya Wanika na Nahawara Chitandi havina hata shule za awali, hivyo watoto wengi kukosa fursa ya kupata elimu ambayo ni haki yao ya msingi.

Ninaomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoa upendeleo kwa kupeleka raslimali fedha nyingi Wilayani Nanyumbu ili kuweza kuinua kiwango cha elimu Wilayani. Wananchi wapo tayari kuchangia nguvu zao kama watawezeshwa na Serikali kutoa fedha kwa mahitaji mengineyo. Naelewa kuwa Halmashauri hupewa mgao wa fedha kwenye sekta hii ya elimu, lakini ninachosema hapa ni kuwa Wilaya ya Nanyumbu ilisahauliwa sana.

Ninachoomba hapa ni upendeleo kwa kupewa mgao zaidi ili wakati wenzetu wanatembea, sisi Nanyumbu tuwe tunakimbia. Ni vigumu kuelezea hali halisi ya mambo yalivyo Wilayani Nanyumbu kuhusu sekta hii ya elimu, hivyo pamoja na kuomba upendeleo wa raslimali fedha na walimu, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Maghembe au Naibu wake waje Wilayani Nanyumbu waone hali ilivyo ili kuthibitisha malalamiko na maombi yangu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu – Mheshimiwa Jumanne Magembe, Naibu Waziri – Mheshimiwa Mwantum Mahiza, Naibu Waziri – Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu na wataalam wote Wizara ya Elimu kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kupitia mpango wa MEM mkoa wa Kigoma tumeweza kufaidika sana, madarasa ya shule za msingi yamejengwa na shule za sekondari zimejengwa na watoto wengi wamefanikiwa kwenda shule. Lakini sasa pamoja na mafanikio yote hayo, bado kuna matatizo mengine kama ukosefu wa walimu na hili ni tatizo kubwa sana katika Mkoa wa Kigoma. Naomba Walimu katika Mkoa wa Kigoma wapewe '*hardship allowance'*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mahitaji makubwa ya maabara. Shule ni nzuri, lakini hazina maabara. Hivyo ni tatizo sana kwa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa hosteli ni kikwazo kikubwa. Watoto wa kike wanaishi katika maisha hatarishi sana. Hivyo, tunaomba Serikali ilitazame hili kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali itilie maanani suala zima la wakaguzi wa shule za msingi, wakaguzi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Wakati mwingine wanazidiwa na walimu wa shule za msingi, kwa sababu mwalimu anapohamishwa, analipwa pesa za uhamisho mapema kabisa, tofauti na wakaguzi. Wakaguzi hucheleweshewa malipo yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wakaguzi nao watolewe kwa Katibu Mkuu warudishe kwenye halmashauri.

**MHE. RUTH BLASIO MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitihani ya darasa la nne na Kidato cha pili sio hoja inayoweza kupita bila kupingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitihani ya darasa la nne, nashauri iwepo hiari kwa watakaoshindwa kufikia alama, wazazi/walezi na watoto wakipenda mtoto arudie darasa, iruhusiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mitihani ya kidato cha pili, napinga utaratibu ambao Serikali inapendekeza. Sio utaratibu utakaoinua elimu ya Tanzania kwa mtindo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitihani ya kidato cha pili ilikuwa na changamoto kubwa sana kwa walimu na wanafunzi. Kilikuwa ni kipindi cha kujifunza kwa bidii na kurekebisha pale ambapo kasoro imetokeza kati ya kidato cha kwanza na kidato cha pili.

Ilikuwa inaleta hofu kwa mwanafunzi na walimu kuona ni aibu kufeli, kwa hiyo, ilikuwepo bidii iliyosaidia kuinua kiwango cha wanafunzi kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ilisaidia hata matokeo mazuri ya kidato cha nne, kwa shule, Wizara na wazazi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini hata kidogo uwezekano wa madarasa ya mafunzo rekebishi kwa walioshindwa kufikia alama; kwa sababu zifuatazo:-

(i) Alama 30 ni ndogo mno, anayeshindwa kuzifikia katika mtihani kumwinua kunahitaji kazi kubwa zaidi.

(ii) Taifa linakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu mfano, wakati wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza wameongezeka kutoka 180, 239 hadi 438, 901; walimu wameongezeka kutoka 18,754 hadi 32,835. Hii pekee inaonyesha zoezi linaloandaliwa na Serikali haliwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hii haitoshi, naishauri Serikali iangalie maeneo mawili.

Kwanza, wanafunzi wa darasa la saba wanaofeli waruhusiwe kurudia mafunzo na watambuliwe (iwapo wanapenda).

Pili, wanaofeli kidato cha nne pia waruhusiwe kurudia bila masharti makubwa yaliyowekwa na Baraza la Mitihani ya kurudia masomo saba kwa mtihani mmoja. Aidha, iwe huru kwa mzazi/mlezi/mwanafunzi na walimu wanaopenda mtoto wao arudie mtihani wa kidato cha pili na kidato cha nne bila masharti magumu yaliyowekwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali haikubaliani nami, napenda wanieleze iwapo wamekisia pesa shilingi ngapi za malipo kwa walimu kwa mafunzo hayo. Rekebishi, maana lazima yatolewe kwa masomo ya ziada, ambayo ni nje ya vipindi vya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiingii akilini, huyu mtoto aliyefeli kidato cha pili kwa masomo hayo ya kidato cha pili: Je, atawezaje kubeba mzigo wa kidato cha pili, kidato cha tatu na kidato cha nne na ukategemea afaulu vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kigezo kilichochukuliwa ni mwanafunzi asiyefanya mtihani wa kidato cha pili asifanye mtihani wa Kidato cha IV. Kumbe hii haifanyi kuboresha elimu yetu, bali inalenga kuongeza idadi ya wahitimu wa kidato cha nne na kuwasukuma watoto mitaani bila uelewa wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu Mheshimiwa Waziri akijibu hoja.

Naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY FIDELIS OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kuhusu ada za shule kwa wanafunzi waliopasi shule za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitueleza kuwa, mwanafunzi aliyepasi anatakiwa kulipa Sh.20,000/= lakini kwa ukweli wanafunzi tunawalipia hadi inafikia hata laki mbili. Wizara itueleze ada halali ni kiasi gani ili kuondoa huu utata?

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya wananchi kwa ajili ya shule za Kata, kwa nia nzuri kabisa ni vizuri wananchi kushiriki katika kuhakikisha kunakuwa na shule za kutosha ili watoto wetu waweze kupata elimu. Lakini shule hizi kuna baadhi ya Tarafa kwa mfano katika Mkoa wa Singida Tarafa ya Sepuka uongozi wa Tarafa ile wanakuwa wakiwanyanyasa wananchi hata kuuza mifugo yao, mazao yao ili shule zijengwe. Lakini wananchi wale hawana shule zilizokamilika. Huu ni ufisadi mkubwa wa kuwanyanyasa Watanzania hawa ambao hata mlo mmoja kwao ni shida. Kwenye ile Tarafa ya Sepuka tayari pana shule, lakini ile shule haina walimu wa kutosha, haina maabara, haina maji, wala matundu ya choo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba zile shule zilizopo, kwanza ziimarishwe kwanza ndio nyingine ziendelee. Elimu nzuri siyo majengo tu, ni pamoja na vifaa kama nilivyotaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule nyingi zimejengwa, lakini hakuna miundombinu ya wenye ulemavu kwa mfano: Kuna walemavu: vipofu, wasiosikia na hata wenye kutembea kwa vibaiskeli vitu kwa vyoo *(special)* na kadhalika, ni wakati muafaka wakati shule hizi zinajengwa, waweke maanani maswali haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa chuo kikuu kupewa mikopo, ni kitu cha kusikitisha. Ni nini jukumu la Serikali katika kutengeneza Taifa la kesho, kinachoweza kuendelea na dunia hii ya teknolojia? Mwanafunzi anatakiwa alipe asilimia 60. Hii ina maana mwanafunzi huyu anajilipia asilimia 100. Hivi mtoto huyu wa mkulima wa kawaida amepasi na wazazi wake hawajui wale nini kwa siku, ataweza kweli kumlipia mtoto huyu kwa asilimia 60? Naomba majibu. Serikali ina wajibu gani kwa watoto hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini malimbikizo ya walimu hayalipwi? Au mpaka waende kwenye mgomo? Pia, katika suala zima la kuwapandisha daraja hivi walimu hasa wa msingi huwa wanapewa motisha gani?

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kusudi langu ni kuongea mambo matatu.

La kwanza ni suala la *VETA* – LINDI. Kwa miaka ya nyuma tumekuwa tukitumia *VETA* ya Mtwara kwa vile Lindi kulikuwa bado hatujajengewa *VETA* yetu na kwamba tuliambiwa kuwa eti watoto wa Lindi sio wengi waendao *VETA*; Kwa hiyo *VETA* ya Mtwara itumike kwa Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kadri siku zinavyozidi kwenda na sisi Lindi tunazidi kuamka na kutaka kwenda kusoma vile vile, tunazidi kuzaliana. Kwa hiyo, shule moja ya *VETA* ya Mtwara peke yake sasa haitoshi, kwani watoto wasomi sasa ni wengi. Elimu ya *UPE (Universal Primary Education)* ambayo ilipitishwa mwaka 1974 na kutekelezwa 1977 na kufanya elimu kuwa haki ya wote ilifanikisha kuongeza idadi ya wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa jamii yetu.

Sasa ni wakati muafaka wa kujenga *VETA* ya Mkoa, Lindi. Uwanja upo na pesa zilitengwa mwaka 2007/2008, tatizo lipo wapi? Haiwazekani muendelee kujenga *VETA* Wilayani kabla ya kumaliza Mkoani. Kama sera ya *VETA* ilivyosema: "Mkoa kwanza." Vinginevyo huo utakuwa ni kuendeleza uonevu. Tusaidieni.

Mheshimiwa Naibu Spika, amini usiamini wamachinga wengi asilimia 45 wanatoka Lindi. Hii ni kwa sababu hawana shughuli za kujiajiri. Nani alaumiwe? Tusaidieni, *VETA* ndio ukombozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya matatizo ya mikoa ya kusini ni elimu, sababu; kila mwaka ninazitaja; kutokana na mfumo wa kikoloni kutotoa elimu kusini ili wazidi kutuchukua kama wakulima wa katani *(cheap labour)* Manamba.

La pili, ni pale ambapo mwaka 1972 walipoamua kuwa na sera mpya ya elimu kuwa, shule zote nchini kuzifanya ziwe shule za kitaifa, hivyo mikoa ile yenye uwezo wa kielimu, kiuchumi ndio waliweza kuwa na nafasi kubwa ya kwenda popote, hivyo kuweza kusoma popote hadi Lindi. Hali ya mazingira, milima ya Ruvuma, Mto Rufiji, barabara mbaya, iliwafanya watu washindwe kwenda mbele zaidi na kwenda kwa miguu kufuata shule na kusoma.

Kwa mambo matatu, elimu kusini ilishuka, tunaomba Serikali kwa makusudi itusaidie kutuongezea pesa zaidi kwa ajili ya kuongeza sekondari na *high school,* hasa ya *Mbekenyera High School* na nyinginezo Lindi.

Shida ya walimu, shule nyingi mkoani Lindi hasa za sekondari hazina walimu wa kutosha, wakipangiwa hawaendi. Tuongezewe waalimu wa sekondari za kutwa. Tafadhali sana. Ahsante sana.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri ya ufafanuzi na kina kuhusu Wizara yake.

Pili, naunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wamehamasishwa na kujenga shule za sekondari kila kata ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa ambayo wamejenga shule za sekondari 24 *(Community Secondary Schools)* na kwa kuwa wananchi hawa kwa kushirikiana na Serikali wamefanya kazi nzuri ya kujenga shule hizo, hata hivyo shule

hizo zinakabiliwa na matatizo makubwa ya upungufu mkubwa wa walimu, vitendea kazi, nyumba za walimu na maabara.

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha kwamba maabara na hosteli zinajengwa kila shule ya sekondari ili wanafunzi wasome masomo ya sayansi kinadharia *(Theory)* na kivitendo *(practicals)* na pia wasichana wakae pamoja kwenye hosteli kwa kuwa mazingira wanayoishi katika shule hizo ni magumu na ndiyo chanzo cha wanafunzi wasichana kupata mimba na kukatishwa masomo yao.

Kwa kuwa shule nyingi za sekondari za bweni zinakabiliwa na matatizo mengi yakiwemo upungufu wa fedha za kuendesha shule hizo na kusababisha shule hizo kuwa na madeni makubwa ya chakula (wazabuni kutolipwa madeni yao) na hata shule kufungwa kwa kukosa chakula na kukatiwa umeme ikiwemo shule ya sekondari ya bweni ya Mpwapwa: Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha kwamba shule hizo zinatengewa fedha za kutosha za uendeshaji ili kupunguza migogoro katika shule hizo kama vile, kuchoma shule, migomo na hujuma mbali mbali katika shule hizo.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ili kupunguza tatizo la upungufu wa walimu wa sekondari, ipo haja kujenga/kuongeza/kapanua vyuo vilivyopo ili kuongeza idadi ya walimu wanafunzi wa *Diploma* kikiwemo Chuo cha Ualimu cha Mpwapwa.  Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati wa nyumba za walimu wa chuo cha ualimu wa Mpwapwa na shule ya sekondari ya bweni ya Mpwapwa.

Kwa kuwa nyumba hizo hazijafanyiwa ukarabati muda mrefu:  Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati shule za sekondari za *Mpwapwa High School;* Shule ya Sekondari ya Dodoma; na Shule ya Sekondari ya Kilakala? Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia shule ya Sekondari ya Mpwapwa *(Mpwapwa High School)?*  Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu kupeleka gari jipya Wilayani *DEO* (Sekondari), *DED* (Elimu ya Msingi)?  Kwa nini asiwe *DEO* mmoja tu – Elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri  ya Muungano wa Tanzania kwa kuruhusu Chuo Kikuu kujengwa Dodoma. Ushauri wangu ni kwamba vyuo vikuu vyote vipewe vitendea kazi vya kutosha, magari, vifaa vya kufundishia, maabara za kutosha, majengo ya kutosha, wanachuo waongezewe posho ya chakula na vitabu ili kupunguza migogoro katika vyuo vikuu.

Je, madeni ya walimu ambao hawajalipwa kama vile likizo, matibabu, uhamisho na kadhalika Serikali ina mpango gani wa kulipa madeni hayo?

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba fedha za *MMES* zipitie katika Halmashauri za Wilaya kama ilivyokuwa *MMEM* badala ya kupitia moja kwa moja kwenye shule ya sekondari na hasa sekondari za kata ili udhibiti wa fedha hizo ufanyike vizuri?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya walimu kwa kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu na walimu wakuu walipwe posho ya madaraka.

Je, ni sababu gani zinazofanya mtihani wa darasa la saba kuvuja mara kwa mara?

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote kwa hotuba nzuri na kueleweka. Nina mchango katika maeneo mawili katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika mpango wa *MMEM* na *MMES* tatizo ambalo linaelekea kukua kwa kasi ni *"drop outs"* kwa wanafunzi kutokana na wasichana kupata mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya yangu ya Kilombero hili limekuwa tatizo ambalo utatuzi wake ni mgumu kutokana na wazazi wa watoto wa kike kuwa na mahusiano na wenye kufanya makosa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kutokana na ukuaji wa teknologia itumike njia ya kisasa kwa kuwapima, wanaohusika kutumia kipimo cha *DNA* bila kujali mahusiano ya mkosaji na wazazi wa msichana husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya kawaida, ni vigumu kumtia hatiani mkosaji kwa kutumia ushahidi wa kawaida wa Kimahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchakavu wa Majengo ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Ifakara:- (Shule za Wacuba), Wilaya yangu inayo shule ya Wasichana ambayo hapo awali ilikuwa ya mchepuo wa kilimo ambayo ilijengwa kwa msaada wa Serikali ya Wacuba. Niliitembelea shule hiyo mwezi Aprili na kuona uchakavu wa majengo, madirisha kubomoka na kuwa na matundu machache ya vyoo ukilinganisha na idadi ya wanafunzi. ni kweli kama hatua za haraka hazitachukuliwa wanafunzi hao watakuwa wanaishi kwenye mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia eneo la shule limechimbwa vifusi kiasi cha kuacha mashimo ambayo wakati wa masika huwa yanajaa maji. Kwa vile shule iko karibu na Mto Lumemo ambao una mambo wengi, kunaweza kuwa hatari kwa maisha ya wanafunzi kama mamba hao wataingia kwenye mabwawa hayo. Ni vizuri Wizara ikashirikiana na Wizara ya Miundombinu ili mashimo hayo angalau yasawazishwe baada ya kumaliza kazi yao *(TANROADS).*

**MHE. DR. WILBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:- Kwa kuwa walimu wengi waliopangwa kwa mara ya kwanza, maeneo mbalimbali nchi nzima walipotoka tu vyuoni wamepata matatizo makubwa sana.

Wamepelekwa Wilayani bila Halmashauri husika kupewa taarifa na hivyo walipofika kukataliwa na Wakurugenzi na kulazimika kurudi makwao wakati hawana fedha. Serikali haikuwapa fedha za kutosha kwa nauli na kujikimu ikizingatiwa wengi ni

vijana wadogo sana ambao wanaathirika kisaikolojia na kijamii. Naomba ufafanuzi wa kina na Serikali imechukua hatua gani kurekebisha hali hii na pia kuhakikisha hali hii isitokee tena.

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa kumekuwa na tatizo kubwa la utoaji wa fedha za *capitalization*; kuficha chanzo kilichofutwa cha *UPE*. Je, kwa miaka tangu 2005 hadi 2008 Mei, zimetolewa kwa kila kichwa cha mtoto kiasi gani kwa kila mwaka? Iwapo kiasi cha dola10 iliyoahidiwa haitimii, Serikali inasema nini kuhusu hali hiyo? Sera ya dola10 kwa kila kichwa cha mtoto imefutwa? Kama ndiyo, mbona haikutangazwa rasmi?

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu uliojitokeza unafidiwa vipi? Kazi zilizotegemewa kufanywa na fedha hizo zinafanywa na mafungu gani? Athari ya hali hii inadhibitiwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameitikia sana wito wa kujenga shule za sekondari za Kata: Serikali inafahamu kuwa Kata nyingi ni kubwa sana kiasi cha kuwa ni vigumu watoto kutembea kwenda shule asubuhi na kurudi jioni, jambo linaloathiri ufanisi wa elimu, kwa vile wanafunzi wanachoka kutembea kutokuwa na chakula cha hakika mchana, jambo linalowaathiri afya za miwili na akili, na hata kuwafanya kuingia kwenye vishawishi mbali mbali ambayo matokeo yake ni mimba kwa wasichana na madawa ya kulevya kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kuzungumzia takwimu ambazo ni dhahiri zimeongezeka, tunachukua hatua gani za makusudi kudhibiti madhara haya? Kwani matokeo mengine ya athari hizi yanachukua muda kuonekana. Mathalan, kwa nini isiwe sera rasmi ya lazima, kila shule kuwa n a bweni au hosteli kwa watoto wa jinsia zote kunusuru Taifa letu?

Kwa vile gharama ya elimu inazidi kuongeza na hasa ya elimu ya juu, kiasi kwamba familia nyingi za kawaida dhahir sasa hazitaweza kupeleka tena watoto wao chuo kikuu. Utaratibu wa *means testing* umeonyesha dosari kubwa katika tathmini ya uwezo wa wazazi/walezi. Je, Serikali itatazama upya lini sera yake ya kuchangia gharama ya elimu na kushirikisha wadau wote ili kutafuta mbinu mpya ya kugharimia elimu bila kujenga matabaka yasiyo ya lazima katika nchi yetu?

Serikali haioni umuhimu wa kutazama upya muundo wa Bodi ya mfuko wa elimu, mfumo mzima wa utoaji mikopo na urejeshwaji wake? Serikali haioni kuwa mfuko huo unaweza kuendeshwa *effectively* na chombo kinachopatikana kwa *tender* kuliko ilivyo sasa, utaratibu ambao utaondoa Serikali katika mgogoro wa mara kwa mara na wakati huo huo mfuko kuendeshwa *effectively* na *Efficiently* jambo litakaloondoa ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha, upendeleo wa mara kwa mara na hata kuondoa hisia za upendeleo wa kisiasa katika jambo lisilohitaji itikadi wala siasa! Tukicheza na elimu tutatumbukiza nchi yetu pabaya sana.

Matatizo ya mabadiliko ya mara kwa mara ya mitaala yameathiri sana elimu yetu. Tutaacha lini *Experimental Approach* katika mfumo wetu wa elimu? Kwa sasa karibu

kila Waziri mpya anapoingia anakuja na mfumo wake. Serikali lazima itoe kauli iliyo wazi katika jambo hili kwamba mabadiliko ya mara kwa mara ya mitaala au maamuzi ambayo hayajafanyiwa utafiiti wa kina, kama tulivyofuta michezo mashuleni, kuondoa baadhi ya masomo kama kilimo, biashara na ufundi imegharimu sana Taifa na wakati huo huo kujenga hisia za ubadhirifu. Mathalan wakati ufundi ulipofutwa, nini kilitokea kwa vifaa vya ufundi vilivyokuwa bandarini wakati ule na vingine vilivyokuwa njiani? Katika hili, nataka maelezo ya kina, vinginevyo sitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea majibu ya kina katika maeneo haya, vinginevyo sitaunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. PETER MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yeka nzuri. Kwa kutambua ongezeko kubwa la wahitimu wa Kidato cha Sita na hasa ifikapo mwaka 2010; Je, Wizara ina mkakati gani wa kukabiliana na tatizo hilo? Hili halijitokezi vizuri katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu wake, Wakamishna, Wakuu wa Taasisi na Idara kwa hotuba iliyoandaliwa kitaalamu, yenye takwimu na malengo ya kuboresha elimu ngazi zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba hii kwa kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kabla ya kutenganisha Wizara ya Elimu na Mafunzo na Wizara ya Sayansi na Elimu ya Juu, Wizara hizi mbili ziliongozwa na sera mbili. Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 na Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1996 wakati elimu ya ufundi ya mwaka 1996.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kwamba ni wakati muafaka Serikali kuainisha sera hizi kwa kuzipitia kwa makini ili kuleta uwiano unaokidhi matarajio na kiu ya elimu nchini. Kamati teule iliyoundwa kupita sera, ifanye kazi yake mikoa na Wilaya ishiriki kikamilifu kwa ajili ya kupata maoni ya wadau wengi. Nashauri baadhi ya wajumbe watembelee baadhi ya nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Madola kwa lengo la kuboresha sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya elimu ya mafunzo ya mwaka 1995 iliweka msisitizo kuwa elimu ya awali ni msingi wa elimu ya msingi, hivyo elimu ya awali ipewe kipaumbele katika mfumo wa elimu rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba mpango mkakati wa ujenzi na upanuaji wa shule/madarasa ya elimu ya awali uandaliwe kitaifa na utekelezwe sambamba na mipango ya Serikali ya kuboresha elimu ya msingi, sekondari, *VETA* na

Elimu ya Juu.  Nchi zilizopata mafanikio makubwa katika nyanja ya elimu zilwekea katika elimu ya awali.

Tusiachie jukumu hili kwa sekta binafsi bali sekta binafsi itaongezea nguvu tu. Kama Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilivyoelekeza, Serikali kuongeza kasi ya upanuzi wa elimu ya awali sasa Wizara iandae mpango mkakati wa muda mfupi, muda wa kati na mrefu wa kujenga madarasa, kuwaandaa walimu mtaala wa vitendea kazi kwa kila shule ya awali katika kila kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri katika sekta ya Elimu ya Ufundi (*VETA)*:  Ninashauri kuwa, tamko la (ahadi) ya Serikali ya mwaka 2005/2006 kuhusu ujenzi wa vyuo vya ufundi *VETA* kwa kila Kata nchini itekelezwe kwa kuwa elimu ya ufundi *VETA* imewekwa chini ya Wizara ya Elimu.  Mpango na ujenzi wa vyuo hivyo utolewe kwa wananchi  ili waweze kushiriki kama walivyoshiriki katika kutekeleza mpango wa elimu ya msingi na sekondari. Wakati wa kutekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi n Sekondari.  Wakati wa kutekeleza mpango  huu uanze sasa, katika wilaya ya Rorya madhehebu ya kidini, Roman Katholiki, Anglikan na Memmoninte wamekubali kujenga vyuo vitatu vya ufundi. Tatizo ni kupata kibali kutoka *VETA* Kanda.

Mhshimiwa Naibu Spika, naomba  Wizara itoe kibali ili vyuo hivyo vijengwe.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni nilikuwa nikiangalia *Star TV* katika kipindi cha jarida maridhawa na nikaona wakieleza kuwa huko Mwanza kuna darasa lina wanafunzi 120 wakiwa katika darasa moja pamoja.  Je, suala hili ni kweli? Naomba jibu. Kama ni kweli, kwa nini basi wanafunzi hao wanakaa wengi kiasi hicho? Katika siku hiyo hiyo niliona wakisema kuwa katika shule hiyo wanafunzi wanakaa darasa moja na walimu.  Huku mwalimu anasomesha na walimu wengine wamo darasani wanafanya kazi zao.  Je, hili nalo ni kweli au hakuna ukweli?  Naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kuongelea kuhusu suala la walimu wanawake walio na waume, yaani walioolewa, na waume zao nao wanafanyakazi sehemu nyingine au mume huyo akapata uhamisho kwenda sehemu nyingine, kwa kuwa mwanamke ndiye anayetakiwa amfuate mume wake:  Je, kwa nini Serikali inakataa kuwaruhusu wanawake hao kuwafuata waume zao?  Je, Serikali haioni kutowaruhusu wanawake hao kufuata waume zao wanasababisha usumbufu kwa familia hizi kuzitengenisha na wanaweza wakawaingiza kwenye matatizo ya ndoa za watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kuliongelea ni kuhusu shule za sekondari. Ninayo taarifa kuwa shule hizo zimejengwa kwa wingi, lakini nasikia hazina walimu wa kutosha, nyingine zina walimu wawili au watatu na nyingine zinao walimu, lakini walimu hao hawana taaluma ya kutosha.  Je, Serikali inasema nini kuhusu hili?  Je, Serikali haioni kuwa kujenga shule nyingi lakini hazina walimu, vifaa

vya kusomeshea kuwa elimu bora haipatikani isipokuwa tunaona kuwa na shule nyingi lakini hakuna elimu bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, isingekuwa busara kujenga shule za sekondari kidogo kidogo kutokana na mahitaji yanapohitajika tofauti na sasa kuwa kila Kata ijenge shule japo haina mahitaji?

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Wizara hii, kwanza niwapongeze kwa kazi ngumu kwenye Wizara hii. Je, ni lini Serikali itapanga vizuri kuhusu malipo ya walimu wao walinavyopangwa mikoa na mawilaya mbalimbali kuliko kuwamaliza nguvu wanapofika kwenye vituo vyenyewe wawe wameishafikishiwa pesa zao? Kama Serikali inavyojua, mashule yapo mengi, hayana nyumba za walimu na nyumba za kupanga ni za matatizo. Nawapongeza wananchi kwa kuchangia ujenzi wa masekondari pamoja na umaskini wao walionao. Naomba Serikali isiwakatishe tamaa.

Ni lini Serikali itaboresha kituo cha watoto wenye ulemavu, viziwina vipofu? Bajeti zinatolewa mara kwa mara kwa kila mwaka: Je, Serikali mkoani Kagera vipi? Mara kwa mara nachangia Wizara hii, sijaona unafuu wa Mkoa wa Kagera. Naomba Serikali iweke nguvu kuhusu elimu pamoja na malipo ya walimu waridhike ndipo watakuwa na nguvu ya kufundisha bila kuwa na mawazo yoyote ndipo watatoa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ufundi kwa wanafunzi, nashauri Wizara iweze kueneza kipindi cha ufundi pamoja na walemavu kuwapa vifaa vinavyoendana na ulemavu hasa kwenye vituo hivyo na mara kwa mara Serikali iwe inawahusisha kwenye michezo ya aina zote hasa kama watoto wanaigiza. ni watoto wanaosahaulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watoto yatima, natoa rai Serikali itenge pesa za kupeleka watoto hao, lakini hazifiki kwa watoto, wanafukuzwa kila siku, wanazuiwa kufanya mitihani, watoto wanazungushwa inafika mahali wanakata tamaa, wanakuwa watoto wa Mitaani. Serikali ifanye mikakati ya kuwa inawasilisha malipo hayo shuleni kwenye akaunti ya shule ndipo watoto watasoma na sisi wabunge tutapata nafuu ya usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *VETA* kuboresha vituo hivyo ili watoto wengi waweze kujiunga, wengi wanapenda kujiunga lakini hakuna vifaa. Shida ya vituo vya watu binafsi inakuwa gharama kubwa wazazi hawawezi kuhimili lakini Serikalini itakuwa na unafuu. Chuo cha Kagera naomba, najua ni kwa nini Serikali mbona imekitupa. Je Serikali inasemaje kituo hiki kuwa ni magofu. Serikali basi itoe uamuzi yakarabatiwe au?

Mikopo kwa wanafunzi hasa wa Mkoa wangu wanaoleta malalamiko wenyewe kupata mikopo inakuwa vigumu kupata mikopo. Naomba mikopo hiyo itolewe sawa. Yangu ni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nachangia kuhusu mirathi ya wajane wa walimu waliokufa. Mjane pamoja na yatima Serikali ifanye mikakati kuwapelekea miradhi yao ili kuwasaidia kuliko mama huyo kuzungushwa. Utamkuta mama anatembea analia njiani!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe (Mb), amewasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake kwa ufasaha mkubwa. Anastahili pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonyesha wazi kabisa ongezeko kubwa la wanafunzi wa elimu ya awali, wanafunzi wa elimu ya msingi, wanafunzi wa Sekondari, wanafunzi wa vyuo na ongezeko kubwa la idadi ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu nchini. Naipongeza sana Serikali kwa maendeleo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, ongezeko hili la idadi halijaendana na ubora wa elimu inayotolewa. Ni ukweli usiopingaka kuwa elimu yetu toka msingi hadi vyuo vikuu imeshuka kutokana na sababu nyingi. Uhaba wa walimu, uhaba wa madarasa na madawati, ukosefu wa maabara, maktaba na nyumba za walimu, uhaba wa vitabu vya rejea na tatizo la ubora wa walimu, maandalizi yao na mazingira yasiyoridhisha ya kufanyia kazi. Hivyo, ni vyema kwa Serikali kubadili mwelekeo wa nchi kutoka kwenye msisitizo wa idadi na kuelekea kwenye ubora.

Nimefarijika sana kwa taarifa kwamba shule zao za msingi zitapatiwa vifaa vya *TEHAMA*, vyuo 32 vya walimu, vitaunganishwa na mtandao wa *TEHAMA* na kwamba maandalizi ya uanzishwaji wa *TEHAMA* kama chombo muhimu cha kufundishia yatafanyika mwaka huu wa fedha. Uamuzi huu ni mzuri sana utakaosaidia kuziba pengo la uhaba wa walimu na kurekebisha kasoro za uelewa na za ufundishaji na baaadhi ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu sio mpya. Ulikuwepo siku za nyuma ambapo shule zote, vijijini na mijini, zilikuwa zinafaidi mafunzo ya Kiswahili, Kiingereza, Jiografia na Sayansi kupitia vipindi vya Redio Tanzania. Hivyo *TEHAMA*, yenye ubora zaidi kuliko redio, itakuwa na matokeo mazuri sana.

Aidha, Serikali iweke bajeti maalum ya kuvuta umeme wa gridi au kuweka umeme wa haya au upepo kwenye shule za vijijini ili nazo zifaidike na *TEHAMA*. Ni vyema hilo likawa jukumu la msingi la *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza ubora wa elimu yetu, Serikali yenyewe ibebe jukumu la kujenga maabara na maktaba za shule zote ili uwepo uwiano wa viwango. Vile vile ili uwiano wa walimu uwepo kati ya vijiji na mijini, Serikali itengeneze *special package* kwa walimu wanaoamua kufundisha shule za vijijini. Halmashauri zinaweza kuongezea vivutio zaidi.

Suala hili ni muhimu kulifanyia kazi: mwalimu anayefundisha vijijini atakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

(a) Kuchelewa kupata mishahara;

(b) Huduma za lazima kama vile hospitali, posta na benki kuwa mbali;

(c) Ukosefu wa miundombinu bora na vyombo vya usafiri pale ambapo mwalimu anataka kusafiri;

(d) Ukosefu wa fursa za kujiendeleza kimasomo; na

(e) Mazingira magumu ya kufanyia kazi: ukosefu wa nyumba nzuri kwa walimu, ukosefu wa huduma muhimu kama maji ya bomba, umeme na kadhalika. Sehemu nyingine zina mapori yenye wanyama wakali, mito mikubwa yenye mamba wengi kama mito ya Kyela na kadhalika. Hali hii inahitaji kutambuliwa kimaslahi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda hadi siku ya leo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii. Naomba nizungumzie yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza jitihada ambazo zinafanywa kupitia mpango wa *MMEM* na *MMES*, kwani watoto wengi wameandikishwa, majengo mengi yamejengwa. Naomba Serikali itupie macho katika suala la ubora wa elimu. Moja ya sababu ya kutokuwa na ubora wa elimu ni pamoja na upungufu wa walimu. Mfano Kata ya Nyasato na Mbogwe Wilayani Bukombe ina shule za Msingi 15, mahitaji ya walimu 168, waliopo 87, upungufu 81, hii ni hatari sana kwa elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bima ya Taifa *(NIC)*, naomba Serikali iwasaidie walimu kupata mafao yao hasa muda wao unapotimia. Tatizo lililopo, wateja huombwa kupeleka *salary slip* tangu walipofunga mkataba na mwisho wao. Huu ni usumbufu, kwani ni jukumu la Taasisi husika/Serikali kutunza kumbukumbu za wateja wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaoandikishwa kupitia *MMEM and MMES,* nashauri Serikali iweke *teaching allowance*. Kada nyingine zinapata *overtime*, kwa nini walimu wasitengewe *teaching allowance* ili wapate changamoto katika kazi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Bayport Financial Institution (BFI)* imeingia mkataba na walimu kuwakopesha. Hata hivyo, inalalamikiwa sana nchi nzima.

Kwa nini Wizara ililitumia kampuni hili kwenye Halmashauri kulitambulisha lifanye kazi hii wakati hawana ukweli ndani yake? Naomba Serikali iingilie kati suala hilo ama ivunje mkataba huo mara moja au ufanyike marekebisho haraka iwezekanavyo. Kama Serikali haiingilii kati suala hili, inanipa masikitiko sana, kwani walimu wanaumia na mkataba mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina orodha ya baadhi ya walimu toka Bukombe wenye matatizo ambao wameandika barua zao. Mfano:-

| **S/No** | **Jina la Mwl.** | **Kiasi alicho-omba** | **Maku-baliano Makato** | **Kiasi alicho-pewa** | **Makato anayo-katwa** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | R. K. Benjamini | 800,000/= | 27,000/= | 710,000/= | 66,085.52 |
| 2. | Frank Shango | 2,000,000/= | 72,000/= | 800,000/= | 81,070.00 |

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni machache tu, hawakati kulingana na makubaliano wala hawapewi nakala ya mkataba. Nataka majibu ya suala hili la unyanyasaji ama kusitisha mkataba au kurekebisha makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upandishaji madaraja halina ukweli ama kwenye Halmashauri na ngazi ya juu. Naomba Serikali ilifanyie kazi. Pengine kutokuwepo mtalaam wa *TSD* katika Wilaya, naomba Afisa wa *TSD* Bukombe apelekwe ili kupunguza matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iwapatie semina walimu kila mitaala inapobadilika. Mafunzo haya yataongeza kiwango cha utaalamu wa walimu katika maeneo wanayofundisha. Nashauri Serikali isifanye mabadiliko ya mitaala mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi, ni lini tawi la Kizumbi Shinyanga litaanza kupokea wanachuo? Eneo lao ni kubwa, majengo yapo, nini kinafanya chuo hiki kisifanye kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa kuiweka Bukonde katika Wilaya 25 zitakazojengwa *VETA*. Nawahakikishia eneo lipo, tumetenga zaidi ya hekta 100. Naishukuru Wizara kuzipatia vijana waliomaliza form four kujiunga na ualimu *Grade IIIA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba walimu hawa warejeshwe Bukombe, itasaidia kwa sababu ni wazoefu wa maeneo. Mfano, waliohitumu mwaka huu, nilileta barua yangu kwa Katibu Mkuu na orodha ya majina ili warejeshwe Bukombe, hakuna hata mmoja aliyerejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika**,** nawapongeza Waziri, Manaibu wote na watumishi wa Wizara hiyo kwa hotuba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watoto wanaosomeshwa na Halimashauri, hasa Halmashauri ya Kigoma – (Vijijini) ambao ni yatima na wale wasiojiweza wanasomeshwa sekondari, watoto wale hawatolewi ada hiyo ya Sh. 20,000/= kwa mwaka. Vile vile huwa shuleni wanaambiwa wanunue *uniform*, kiti na meza, madaftari, vitabu na jembe, ndoo na *ream* ya karatasi. Kwa kuwa hao watoto ni yatima: Je, hayo yote watayapata wapi? Vile vile watoto hao husimamishwa mitihani kwa kuwa hawajalipiwa karo. Je, hiyo karo ya hao watoto inakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali itoe majibu. Baada ya hapo ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtoto ambaye anasoma *Mazungwe Secondary School* Kigoma vijijini ambaye ni Kulwa Husein yuko *form one*. Baada ya kwenda ziara katika kijiji cha Kazwamimba, nilitembelea shule hiyo ya Mazungwe nikapata taarifa ya huyo mtoto kuwa hasemi hasikii na anasoma Kidato cha kwanza. Nilichukua jukumu la kwenda kumwona Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Ufundi akaniambia nipeleke Jina hilo kitengo cha Elimu Maalum, baada ya hapo nikamwona Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, baada ya hapo mwezi Mei, 2008 barua ilipelekwa kwa *Head Master Mazungwe Secondary School* ili apelekwe Tabora alikokuwa amechaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barua hiyo ya kutoka Wizarani ni ya kujisomesha mwenyewe wakati mama yake hana mbele wala nyuma, chakula cha jioni bila mtoto wake kuuza maharage na miwa stesheni, huo mlo mmoja wa usiku, hali yeye na mama yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali haikuchukua fursa ya kumsomesha mtoto huyo? Hivi Serikali imemsaidia au inamdidimiza mlemavu huyo wakati alikuwa anayapenda masomo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iweze kumsomesha mtoto huyo mlemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja nikitegemea Serikali imesikia. Ahsante.

**MHE. PROF. RAPHAEL MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ludewa imekamilisha (ikishirikiana na *VETA* – Nyanda za Juu) mahitaji ya ujenzi wa chuo cha ufundi Wilayani ili kwenda sambamba na uwekezaji unaotarajiwa kuanza mwaka huu (2008) katika chuma cha Liganga na makaa ya mawe mchuchuma na kuwasilisha maombi kwako Mheshimiwa Waziri tukiwa hapa Bungeni. Je, Serikali inasemaje kuhusu kusaidia ujenzi wa chuo hicho mara moja?

Kwa kuwa muundo wa Bodi za Shule za Sekondari za Kata hauzingatii uwakilishi wa jamii zilizojenga shule hizo na kanuni zinazotumika zinampa madaraka makubwa sana Mwalimu Mkuu katika kuchagua Wakurugenzi wa Bodi za Shule na kwa kuwa shule hizo sasa zinasimamiwa na Halmashauri za Wilaya: Je, kwa nini muundo huo wa Bodi na kanuni hizo zisihuishwe ili kuboresha zaidi usimamizi wa shule hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika changamoto zilizoainishwa katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 94 ni pamoja na mazingira katika shule nyingi na kusababisha watumishi kutopenda kufanya kazi katika maeneo hayo hasa pembezoni mwa nchi pamoja na Ludewa. Serikali ina mchango gani katika kushughulikia changamoto hii badala ya kutaka wananchi peke yao watafute ufumbuzi wa suala hili?

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wote wa Wizara kwa kazi kubwa inayowakabili. Wizara hii imeunganishwa na Wizara mbili baada ya kuunda Baraza jipya la Mawaziri mwezi Machi, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unahusu jambo moja tu ambalo limekuwa kero kubwa sana kwa wanafunzi wa shule ya sekondari ya Geita ambayo ilikuwa chini ya Bodi ya Pamba ya Mkoa na kuomba ichukuliwe na Wizara ya Elimu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu shule hii ichukuliwe na Serikali, huduma ya chakula katika shule hii imekuwa duni sana. Uongozi wa shule wanajitahidi sana hasa walimu wa shule hii kuwashawishi wazabuni kulisha shule kwa kutoa huduma mbalimbali. Lakini imefikia mahali wazabuni hawa wameshindwa kabisa kuendelea kutumia fedha zao bila Serikali kuwalipa kwa huduma wanayotoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono kama Serikali itanitamkia ni lini watalipwa malimbikizo ya madai yao ya nyuma, hasa kwa waliotoa huduma kwenye shule ya Sekondari ya Geita.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wataalam wao wote waliohusika katika maandalizi ya bajeti hii. Hata hivyo, nina mambo kadhaa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa sahihi nilizonazo zinaonyesha kwamba bado wizara haijalipa malimbikizo ya madi ya walimu kwa nchi nzima. Malimbikizo hayo yapo kwenye maeneo yafuatayo:- kutolipa mishahara kwa wakati, malimbikizo ya mishahara *(salary arrears)*, madai ya likizo, matibabu, gharama za uhamisho na masomo. Hadi sasa madai halisi kwa walimu wa shule za msingi yanafikia shilingi bilioni 12.3 na madai ya walimu, vyuo na ukaguzi yanafikia shilingi bilioni 4.2. Madai haya ni mengi na napenda niishauri Wizara ihakikishe kwamba madai yote ya walimu yanalipwa kwa wakati. Aidha, naomba Wizara itoe taarifa ndani ya Bunge hili, ina mpango gani wa kulipa madeni hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tusisubiri walimu wengine ndipo Serikali iwalipe kama ilivyotokea mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika,nimepata malalamiko katika chama cha walimu *(CWT)* wilayani Mbozi kuhusu mikopo inayotolewa na taasisi ya *"Bayport Financial Services"*. Kwanza mikopo hiyo ilianza kutolewa kwa hila kwani walimu waliingia kwenye mkataba bila kujua masharti mengi kwenye mikataba hiyo. Pili na mbaya zaidi, pamoja na kwamba mikataba ni makubaliano ya pande mbili, lakini ni jambo la hatari sana kwa Serikali kuruhusu Taasisi kadhaa za fedha kuwakopesha walimu bila ya kujiridhisha na masharti ya mikopo yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo inayotolewa na Taasisi hiyo, kwanza ni ya kitapeli na naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kuridhisha. Taasisi hii hutoza riba kubwa sana kwenye mikopo. Kwa mfano mkopo wa Sh. 650,000/= humlazimisha mkopaji kurejesha zaidi ya milion tatu. Huu kama sio wizi, ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi sana kutoka kwa walimu kuondolewa kwenye *payroll*. Hali hii imesababisha usumbufu mkubwa kwa walimu nchini. Hali hii inawakatisha walimu tamaa na hivyo kuzorotesha utendaji kazi kwa walimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama walimu ambao waliomba ruhusa na kumbukumbu kwa maandishi, lakini wakaondolewa kwenye *payroll.* Hili pia ni jambo baya sana na namwomba Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, upandishwaji wa vyeo na urekebishaji wa madaraja kwa walimu ni jambao zuri sana. Hata hivyo, zoezi hilo ambalo lilifanyika sana katika kipindi cha mwaka 2006 na 2007, halikufanyika vizuri. Dosari zifuatazo zilijitokeza:-

(i) Baadhi ya walimu waliostahili hawakuorodheshwa;

(ii) Baadhi ya walimu hupewa madaraja ya chini au ya juu kulinganisha na sifa zao;

(iii) Waliopandishwa, wengi wao hawajapewa barua;

(iv) Baadhi yao hawajalipwa malimbikizo ya mishahara;

(v) Baadhi yao wamerekebishiwa vidato *(increament)* badala ya madaraja *(salary scales);* na

(vi) Walimu (baadhi) wenye sifa zinazofanana kabisa kupewa madaraja tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaonyesha udhaifu mkubwa uliopo Wizarani. Namwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo, kwa nini hali hiyo inajitokeza? Lakini pia achukue hatua za kurekebisha mapungufu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanafanya kazi ngumu sana na katika mazingira magumu sana. Siku za nyuma Wizara ilikuwa inalipa posho hizo kwa walimu. Hata hivyo, katika mazingira yasiyoeleweka, posho hizo ziliondolewe. Mimi naamini kwamba sababu zilizotolewa na Tume ya Rais ya Elimu ya mwaka 1981 juu ya kuwepo kwa posho hizo bado zipo. Aidha, walimu wanafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum, wanastahili pia wapate posho maalum, kwani wanafanya kazi maalum yenye taaluma ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini, kumejitokeza matatizo mengi sana kwa mfano migomo isiyokwisha vyuoni, wanafunzi wamekuwa wakieleza kutoridhishwa kwao na viwango vidogo vya pesa wanazopewa kwa chakula, kwa vitabu na hata kwenye mafunzo ya vitendo. Viwango vya sasa vipo chini kwa mfano mwanafunzi anakwenda kwenye mafunzo hulipwa Sh. 6,000/= kwa siku. Hivi nani anaweza kuishi kwa fedha hizo kwa siku kuanzia chai, *lunch,'dinner* hadi malazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni kuzuiliwa kwa matokeo. Nimesikitika sana kupata habari kwamba zaidi ya wanafunzi 1,540 wa Chuo Kikuu cha Ardhi matokeo yao yamezuiliwa na hao wote ndio wenye udhamini wa Serikali. Ni wanafunzi 60 tu ambao hawadaiwi. Hii ni hatari sana. Nashauri utafutwe utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa elimu unajulikana na hauna mjadala na sio suala la kuchezea. Inasikitisha kuona elimu inafanyiwa majaribio. Yawezekanaje katika dunia hii ya utandawazi na ushindani tufute mitihani ya darasa la nne? Iwapo tunafuta mitihani kwa mitindo wa mafunzo rekebishi, basi afadhali Serikali isiingie gharama za mitihani bure. Lazima tufuate misingi, la sivyo misingi itatugeuka.

Pamoja na matatizo mengi ya elimu, ni lazima Serikali iwekeze katika elimu. Lakini kuwekeza kusiwe tu kujenga madarasa tu, la hasha. Tunahitaji walimu na vitendea kazi. Sasa hivi tatizo kubwa ni ukosefu wa walimu ambao ndio msingi wa ubora wa elimu. Wanafunzi waliweza kufundishwa hata chini ya miti. Hivyo ni vyema Serikali iwekeze katika ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo yaliyovutia watoto mashuleni ni chakula hasa ikizingatiwa kuwa familia nyingi zinaishi chini ya dola moja. Hivyo chakula mashuleni kiliwavutia sana watoto, kwani chakula kimeongeza sana mdondoko na naamini hilo la kwamba wanadondoka kwa hofu ya mtihani sio kweli. Lingine ni

michezo, *brass band* mashuleni ambapo siku hizi hakuna. Wizara lazima iweke vivutio mashuleni.

Elimu ya Sekondari, pamoja na juhudi za Serikali ya kujenga shule za Kata, bado tatizo la ubora liko pale pale na hii itazua mtafaruku mkubwa hasa la usawa, lakini kukosa utaifa, kwa kuwa eneo lile lile alilozaliwa, hivyo kutojua kama kuna makabila mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula ni vema kipatikana na chenye staha na sio cha Sh. 450/=. Mtihani wa *form two* ni lazima uwepo kama kigezo cha uelewa, lakini pia kutamfanya mtoto afanye jitihada zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa Wizara hii unaonyesha dhahiri kuwa elimu ya juu haijatendewa haki, kwani imetengewa asilimia 21 tu huku elimu ya msingi ikipewa asilimia 67 huku tukijua wazi mahitaji (gharama) ya elimu ya juu ikiwa juu sana. Mfano mwanafunzi mmoja ni zaidi ya Sh.1,500,000/= na msingi ni sh.20,000/=. Hii ni hatari wakati tunajua wazi elimu ya juu pekee ndio itakayopeleka nchi yetu katika ushindani kiuchumi, kisayansi na kadhalika.

Tatizo kubwa la elimu ya juu sasa ni mikopo kwa wanafunzi. Sasa hivi wanafunzi wengi wamezuiwa matokeo yao kwa kuwa hawana fedha za kulipia. Lakini baya ni kuwa hata wale waliomaliza *(finalists)* wamezuiwa na hivyo hawataweza hata kupata ajira ili walipe madeni yao huku ni kukiuka katiba ya kwamba kila Mtanzania ana haki ya kuajiriwa. Tukizingatia kuwa Watanzania wengi wanaishi chini ya dola moja. Hivyo wanafunzi hawa wangepewa vyeti wangeweza kufanya kazi na hivyo kujilipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Means testing*, naamini kuna tatizo kubwa sana la kipimo hiki kwani mikopo hiyo hutolewa kuendana na jinsi mwanafunzi alivyojaza fomu. Lakini ikumbukwe wanafunzi wengi hawakuelimishwa kuhusu ujazaji, hivyo kudhani ukiandika una uwezo mkubwa ndio utaingia chuo. Kuna haja ya Wizara kutembelea shule za *"A" level* kuwapa elimu. Pia kila chuo kiwe na ofisi ya mkopo ili wanafunzi waweze kwenda kueleza matatizo yao, hivyo kupunguza maandamano ya wanafunzi kwenye Bodi.

Nashauri *means testing* iangaliwe upya na ikibidi *cost sharing policy* iwe *reviewed* na iletwe hapa Bungeni. Mimi naamini bado tunaweza kuwasomesha watoto wetu bure kama alivyotuwekea misingi mizuri baba wa Taifa Mwl. Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ni watu muhimu sana katika uboreshaji wa elimu. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la kutowapa mishahara kwa wakati na vile vile masuala ya fedha za likizo zao. Serikali imewafanya walimu kama makarai yatumikavyo katika ujenzi. Ni kwa nini wanajeshi au Taasisi nyingine wanalipwa *overtime* lakini walimu wameachwa tu huku tukijua bila walimu hakuna elimu? Mnyonge mnyongeni, haki yake mpatieni!

**MHE. DR. CHARLE MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Pongezi nyingi kwa kazi nzuri zinazofanywa na Wizara ndani ya Uongozi wa Mheshimiwa Waziri.

Hoja ya uhaba wa wahadhiri vyuo vikuu. Pamoja na mikakati ya kuajiri wataalamu wapya katika ajira ya kudumu na pamoja na ajira za mikataba kwa wastaafu wanaopenda, napendekeza kuwa:

(a) Kama ilivyo nchi nyingi duniani, vyuo vikuu vya umma vianzishe mpango wa kuwatumia wataalam wengine wenye sifa, lakini wako nje ya vyuo, Watanzania wenye nafasi/wanaopenda watumike kufundisha masomo husika kwa wakati uliopangwa *(visiting lectures)* bila ya kuwa na ajira za kudumu chuo husika. Wataalamu hao pia watumike kusimamia wanafunzi wa shahada za juu *(Postgraduate supervision),* kwa mfano, mimi nimekuwa msimamizi *(lockl supervision)* kwa mwanafunzi Mtanzania *Andalusia University (Spain)* mwaka 2006, (MSc); kwa Mtanzania katika Chuo kikuu *Trondheim (Norway) PHd* mpaka Machi, 2008. Huu ni mfano tu.

(b) Serikali iruhusu kwa uwazi, uwepo wa mpango huu katika vyuo vikuu ili uwe rasmi. Kila Silaha *(Human Resosurce)* iliyopo nchini itumike bila gharama kubwa. Lakini kwa manufaa makubwa ya Taifa.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Maghembe na Manaibu wake wote wawili wanastahili sifa maana kazi wanaiweza. Hongereni kwa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipendekeza shule tano ambazo zinakidhi haja ya kupandishwa kuwa *high schools*. Shule hizi ni St. *Pouls' Secondary School* – Liuli; *Hagati Secondary School; Makita Secondary School; Luanda Secondary School;* na *Lundo Secondary School.*

Wizara ilimtuma Mkaguzi ili azikague Shule hizo, lakini Mkaguzi huyo alifanya uzembe wa hali ya juu. Yeye alifika Mjini Mbinga na kukagua Shule ya Makita tu na kuipandisha, hakwenda kwenye Shule nyingine zilizotajwa. Wilaya tulipendekeza *St. Pouls' Secondary School, Makita Secondary School*, pamoja na *Luanda Secondary School.* Je, ni haki Wilaya yenye Majimbo mawili kupata Shule moja tu ya *High School?* Naomba nipatiwe maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ionyeshe moyo wa huruma kwa kuzisaidia Shule Binafsi hasa mishahara ya walimu, kwani mchango wa kielimu kwa Shule hizo ni mkubwa sana kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni cha zamani sana hapa nchini na kimetoa mchango mkubwa sana kitaaluma. Kwa sasa chuo hicho kina zaidi ya wanachuo 20,000, wakati

miundombinu ni ile ile iliyojengwa miaka ya 1970. Walimu ni wachache sana na wanafundisha madarasa makubwa sana zaidi ya wanafunzi 200, bila motisha kwa walimu hao, yaani mishahara midogo, pensheni duni na ndiyo maana wanahama nchi.

Bajeti hii haizungumziii matatizo haya, naomba Mheshimiwa Waziri, anipatie maelezo kuhusu msimamo wa Wizara katika hili.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Vyuo Vikuu, Walimu Wakuu, Walimu na Watendaji wote katika Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwaelimisha watoto wetu. Bunge na Jamii kwa ujumla, tunalo deni kubwa sana kwenu. Natambua kwamba, mishahara na mazingira ya kufanyia kazi haviridhishi. Kweli dhamana yenu ni wito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa wazo jema la kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma. Hasa hasa Mheshimiwa Rais, anastahili kuungwa mkono na Bunge letu Tukufu, kwa kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hata kumpa moyo akope popote ili azma ya kupokea wanachuo elfu arobaini na zaidi itimie haraka iwezekanavyo. Ujenzi unaoendelea sasa hivi unatia moyo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali itafute Walimu au Wahadhiri wa Vyuo Vikuu kutoka popote nje ya nchi, kwa gharama muafaka na wahadhiri hao, Serikali ikope fedha kutoka taasisi za fedha kugharimia mishahara, posho, vitabu na vifaa vyote muhimu katika kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa busara kuruhusu Sekondari za Kata kujengwa na Wananchi ili Serikali ichangie kuleta walimu, vifaa na kadhalika. Naishauri Serikali isisitishe zoezi hili kwa sababu itatafsiriwa kuwa kitendo cha ubaguzi uamuzi huo ukitolewa sasa. Haki ya elimu kwa watoto wa Taifa hili ni haki ya Kikatiba. Tukumbuke usemi wa hekima “Elimu Haina Mwisho” ni wajibu wetu wote Jamii na Watanzania kujenga majengo, kupata vifaa na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya walimu na pensheni zao ni muhimu viboreshwe ili kuvutia vijana wetu wengi kujiunga na taaluma hii. Mke wangu ni mwalimu, lakini ukweli na uzito wa hoja yangu haudhoofishwi na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ifikirie upya uamuzi wa kuwa na Maofisa Elimu wa Wilaya wawili kila Wilaya. Kwa kuzingatia ukweli kwamba, tuna upungufu mkubwa wa Walimu wa Sekondari, ni ufujaji wa rasilimali watu kuweka walimu wazuri wawili ofisini kufanya kazi ya utawala! Ofisa mmoja anatosha na sio lazima awe mwalimu kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuwapongeza Walimu wa Jimbo la Muleba Kusini na wanafunzi wao kwa bidii yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili; Mheshimiwa Mahiza na Mheshimiwa Kabaka, hongereni kwa kuandaa bajeti vizuri na kuiwasilisha vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu wa mwaka jana, niliiomba Serikali ione uwezekano wa kupeleka majukumu ya ulipwaji *Bills* mbalimbali katika Hazina Ndogo Mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala ni muhimu sana ili kuepusha adha zinazopatikana katika malipo kama ya umeme, maji, simu na kwa *suppliers* wa vyakula au waendesha kantini za Mashule ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kuchelewa kulipa waleta vyakula ghafi na waendesha kantini, limekuwa kubwa hadi kupelekea wanafunzi kurudishwa nyumbani kabla ya muhula kwisha. Hii inasababishwa na ya kukosekana chakula baada ya aliyepewa mkataba wa kuleta chakula kushindwa kuendelea kuleta chakula sababu ya kuchelewa kulipwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ione utaratibu mpya nilioupendekeza wa ku-*decentralize* malipo toka Wizarani na yawe *controlled* na Hazina Ndogo za Mikoani ili kuweza kuboresha huduma hii na kuepuka kuathiri wanafunzi kisaikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kazi nzuri wanazofanya katika dhana nzima ya kuleta mabadiliko ya kuboresha Elimu siku hadi siku. Walimu wanakabiliwa na matatizo kadhaa, ambayo ninaishauri Serikali iyafanyie kazi kama ifuatavyo:-

(i) Kuboresha nyumba za walimu ili walimu watakapopangiwa kufanya kazi wasipate usumbufu, tusijaribu kuwapatia walimu nyumba zinazoshusha hadhi yao.

(ii) Ni vyema tukaboresha maslahi ya walimu kadiri itakavyowezekana, kwani kazi hii ni ngumu kwa kila hali na ugumu pia unaonekana kwenye tafsiri ya neo lenyewe la UALIMU kwa maana ifuatayo:-

U - Usumbufu (kazi hii ni ya usumbufu, unajituma muda wote).
A - Adha (Kazi ya ualimu ni ya kuhangaika kupata ukweli darasani).
L - Lawama (Kazi ya ualimu ni ya lawama kwa Wizara husika, wazazi na watoto).
I - Inda (mwalimu huigwa kwa mwendo wake au sauti anapofundisha; au nguo anazopenda kuvaa na kupewa jina).
M - Mahangaiko (kazi ya ualimu ni ya mahangaiko).
U - Uvumilivu (walimu ni wavumilia kazi kwenye mazingira magumu).

Hivyo kazi hii ni ngumu na walimu ni lazima wapate maslahi yao kikamilifu.

Ninashauri Serikali iandae Sera Maalumu ya kuhakikisha Shule za Sekondari na Vyuo vinapata usafiri wa kudumu kuondoa tatizo la usafiri.

Ninaishauri Serikali ihakikishe wanawaenzi na kuwatunza walimu wastaafu, kwani hali zao za maisha siyo nzuri. Tusisubiri mpaka wafe, tukawatunze kwa risala za majonzi wakati walipokuwa hai wastaafu hawa walitelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Mimba za wanafunzi Mashuleni linatisha, hali hii itaendelea sana ikiachwa bila Mkakati Maalum wa kurekebisha adhabu kwa tatizo hili. Ninashauri Serikali iandae adhabu zitakazotolewa kwa wanafunzi watakaopata mimba ili waogope na iwe fundisho kwa wengine na kutoa adhabu pekee kwa aliyempa mimba mwanafunzi, pia ni vyema adhabu ya aliyempa mimba mwanafunzi iwe ni kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali itilie mkazo zaidi masomo ya Sayansi Mashuleni, kwani wanafunzi wamebainika kupenda zaidi masomo ya sanaa *(arts).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuandaa mazingira mazuri ya kuboresha maabara za kutosha mashuleni, ambazo zitakuwa na vifaa kamili vya masomo yote ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upandishwaji vyeo na urekebishaji wa madaraja yao ni tatizo, hasa tatizo la Alfabeti na tatizo la kurundikwa katika cheo kimoja. Ninaishauri Serikali irekebishe tatizo hili kwa kuweka madaraja tofauti na kupatiwa barua zao; na warekebishiwe mishahara yao baada ya kupandishwa madaraja hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho za kufundisha na posho za mazingira magumu ziboreshwe zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu na maafisa wote Wizarani na katika Taasisi mbalimbali, kwa matayarisho mazuri ya Hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara kubwa na yenye umuhimu wa kipekee kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, wametoa michango mingi ya mawazo kwa dhamira ya kuboresha shughuli za Wizara hii. Kwa mfano, Mheshimiwa Makwetta, ametoa rai kuhusu upelekaji wa madaraka Mikoani na Wilayani. Ninaafikiana na hoja ya Mheshimiwa Makwetta; twende taratibu tena kwa Mipango na Mikakati yenye uhakika ili tusiathiri vibaya ubora wa Elimu tunayoitoa.

Masuala ya upungufu wa walimu, nyumba za walimu na vitendea kazi ni budi yafanyiwe kazi na kurekebishwa haraka. Aidha, malipo ya Mishahara, posho mbalimbali za walimu pamoja na Wazabuni wa vyakula yalipwe kwa wakati ili kuepuka madhara makubwa yatakanayo na ucheleweshwaji wa malipo kama haya. Kwa mfano, wazabuni wa Shule za Sekondari za Tabora walilazimika kusimamisha huduma zao na hivyo kulazimisha Shule hizo kufungwa kwa upungufu wa vyakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Karne ya Sayansi na Teknolojia. Hivyo, maendeleo ya haraka ya nchi yetu yatategemea sana uwepo/upatikanaji wa wanasayansi wengi hapa nchini katika fani mbalimbali kama vile Wahandisi, Madaktari, Watafiti mbalimbali na kadhalika. Ili nchi iweze kuwa na wanasayansi wengi (wanaume kwa wanawake), Serikali haina budi kuwa na Mkakati Maalum wa kuhakikisha kwamba, wanafunzi wengi zaidi wanachukua masomo ya sayansi. Aidha, Serikali haina budi kuondoa karo kwa wanafunzi wote wanaochukua masomo ya sayansi kuanzia Kidato cha Tano na Sita mpaka Vyuo Vikuu. Ujenzi wa Maabara, ni lazima ili kuwawezesha wanafunzi wa sayansi kujifunza kwa vitendo.

Serikali iboreshe mishahara ya walimu, pamoja na marupurupu ili kuwavutia walimu wazuri kubakia katika ajira na kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Hivi sasa kuna malalamiko mengi kuhusu ucheleweshaji wa malipo mbalimbali ya walimu.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusoma na kuchunguza katika kitabu cha Bajeti ya mwaka 2008/09, ukurasa wa 103 kielelezo Na. 3, ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya 25. Nimechunguza na kubaini kuwa, Wilaya za zamani zinasahaulika kama zina kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Geita ina wakazi sasa zaidi ya milioni moja, ukichukulia ongezeko la asilimia 3.4 kutoka idadi ya watu 712,000 mwaka 2002 wakati wa sensa. Vijana walioko Shuleni kwa mwaka ni wengi sana, hakuna Wilaya ambayo imezidi kutoa wanafunzi wengi ukilinganisha na Wilaya nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia ya Serikali kusahau Wilaya za zamani na kupeleka maendeleo kwa Wilaya mpya, kwa kudhani kuwa Wilaya za zamani zinajitosheleza kwa kuwa na mahitaji yote. Nafikiri hata Wizara ninapoandika hivi itashangaa kuona Wilaya ya Geita haina chuo cha Ufundi Stadi kwa ajili ya vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kigezo kipi kilichotumika kuchagua Wilaya hizi? Nashangaa kuona Wilaya ya Temeke ina Chuo cha *VETA* lakini bado inaongezewa chuo kingine; huu ni upendeleo wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika umri huu ni aibu kuwa tunalalamika, tunaitaka Serikali ijenge Chuo cha Ufundi Stadi Geita haraka iwezekanavyo. Tunachoka kukaa kila siku tunaomba omba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi. Nawapongeza sana Waziri, Manaibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa inayowakabili na wanayoitenda kwa juhudi kubwa.

Kero yangu kubwa ni takwimu zinazopanda za wasichana wanaopata mimba Shuleni. Mwaka jana, wakati Wabunge wakichangia hoja ya Wizara hii, kilikuwa kilio cha Wabunge wengi, tukitegemea takwimu zitashuka, lakini ndiyo kwanza zinazidi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kimekuwa kilio kwa wazazi kulikoni? Shule zimegeuka kilio kwa wazazi wa watoto wa kike. Wasichana wengi sana huharibikiwa maisha yao na kukosa elimu. Hii imechangiwa sana na hizi Sekondari za Kata zilizojengwa bila hosteli za wasichana, pamoja na mazingira mabaya ya shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe makini zaidi katika kutekeleza Sera ya Elimu nchini. Hii ni kutokuwa na *proper forward planning* kuanzia sasa, naomba Waziri aweke bayana kabisa, ataweka mikakati gani kutatua tatizo hili kubwa katika jamii na kwa sekondari zinazoendelea ambazo hazina hosteli za wasichana? Kila mwaka watu wanalia na kulipigia kelele hili, lakini tatizo linashika kasi na watoto wanaangamia.

Pili, kwa shule zitakazojengwa, Waziri atueleze wazi kuwa ujenzi wa madarasa utaenda sambamba na ujenzi wa hosteli ya wasichana. Bila mikakati madhubuti na ya makusudi, mwakani tatarudi hapa na takwimu za wasichana wanaopata mimba shuleni zitakuwa mara mbili au tatu.

Kero ya Pili ni shule nyingi zilizoanzishwa kukosa walimu. Wananchi wamechangisha fedha nyingi sana za ujenzi wa shule na shule nyingi zimefurika watoto. Kinachosikitisha ni shule kutokuwa na waalimu. Wananchi wanajiuliza; kwa nini wanachangia fedha zao nyingi kwa ajili ya watoto kupatiwa elimu duni namna hii? Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 100. Hali hii inasikitisha (mifano hii hai ipo Mkoani Manyara); kwa nini wananchi wachangie elimu hatarishi (watoto kurudi nyumbani na mimba) na elimu duni?

Mheshimiwa Waziri, aweke bayana kuwa kuanzia sasa kila darasa moja linalojengwa na nyumba moja ya mwalimu ijengwe. Vilevile ili walimu wakubali kubakia kwenye Shule za Sekondari za Kata, wapewe *hardship allowance.* Hii iwe lazima, kwa sababu utakuta eneo hilo hakuna maji, umeme, nyumba ya kupanga, simu, zahanati wala hakuna soko na kadhaika. Siyo rahisi kumlaumu mwalimu anayekataa kuishi eneo kama hilo, lakini akiwekewa *hardship allowance* kwenye mshahara wake, atapata motisha na atavumilia.

Tatizo la tatu, shule nyingi hazina vitabu kabisa, walimu wengine wanafundisha tu kwa kutumia uzoefu. *NGOs* zimefanya utafiti na imebainika hivyo baadhi ya shule za msingi huko Babati Vijijini. Wanafunzi wa aina hiyo wanawekewa misingi ipi ya elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia uwezo wa Halmashauri zetu kukabili uzito wa majukumu waliyopewa. Mimi sikubaliani kabisa kwa nini kila Idara ipitishe fedha Halmashauri. Si kwa kuwa hawawezi, bali watazidiwa na majukumu na matokeo yake mambo yatakapoharibika tutashindwa kulaumu. Sasa hivi kuna Halmashauri zina akaunti za benki mpaka 800. Hapa kuna tatizo kubwa! Kuna hatari kubwa ya kupoteza fedha bila kujua.

Serikali itafute mfumo bora na hili limeonekana ni tatizo siku nyingi, lakini Serikali inalifumbia macho. Fedha za Elimu zitafutiwe mfumo tofauti kwa ufanisi zaidi, bila kujali Sera au Sheria inasemaje ili kuokoa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kujenga Shule yajumuishe maeneo ya kulima mashamba au bustani kama shule za zamani. Kazi za mikono zinasaidia kupunguza utoro shuleni na pia kuwapatia watoto chakula. Hii hali itaboresha elimu za watoto; kiakili na kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaunga mkono hoja hii mpaka Mheshimiwa Waziri atakapoweka bayana, Mikakati mipya ya Wizara ya Elimu ya kupunguza mimba mashuleni, ili takwimu zitashuke badala ya kupanda. Mikakati ya sasa inaelekea haifanyi kazi.

Tupunguze kilio cha wazazi, tunusuru maisha ya watoto wa kike.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, pamoja na Viongozi wengine wa Wizara hii, kwa kuandaa bajeti vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia bajeti hii na kuisaidia Wizara katika kuboresha vipaumbele vyake katika utekelezaji wa bajeti hii, ambayo ninaiunga mkono, kuna mambo kadhaa yafuatayo ambayo naomba kuyachangia:-

Kwanza, tatizo la uhaba wa Walimu wa Sekondari, hasa Mkoa wetu wa Shinyanga ni mkubwa sana. Shule nyingi sana zimejengwa toka 2006, lakini walimu hakuna kabisa. Katika Jimbo la Msalala, Wilayani Kahama, wingi wa walimu katika shule ni kati ya 2 hadi 8! Shule nyingi zilizojengwa kwa nguvu za wananchi, kama vile Baloha, Ngogwa, Ntobo, Lunguya, Bulige, Mwalugulu, Jaana, Nyikoboko, Kinaga na Ngaya, zote zina walimu chini ya wanne kila moja! Jambo hili limelalamikiwa sana na wazazi kuwa watoto wanaenda kupoteza muda. Naiomba sana Serikali, iuangalie Mkoa wa Shinyanga, hasa Kahama. Pamoja na jitihada ambazo Serikali inafanya, naomba Mkoa wa Shinyanga uangaliwe zaidi, kwani hata msingi wa wanafunzi hawa nao si mzuri, hivyo uwezo wao hata wa kujisomea pasipo walimu ni mdogo.

Pili, ni tatizo la ukubwa, utaratibu na usimamizi wa michango ya Sekondari. Jambo hili limekuwa kero kubwa sana. Michango inafikia hadi Sh.50,000 kwa kaya kwa maeneo fulani! Huu ni mchango wa sekondari pekee, bado miradi mingine nayo pia inahitaji ushiriki wa wananchi! Kwa sasa miradi mingine kama ya *TASAF* inasuasua

kutokana na ushiriki mdogo wa wananchi, inavyoonekana wananchi wapo *overstretched!* Aidha, usimamizi wa michango hii nao ni mbovu. Watendaji wa Kata hawana taaluma ya uhasibu hivyo, wanashindwa kabisa kusimamia. Maeneo mengi fedha za wananchi zimepotea (kuna sehemu zimeliwa na Watendaji, lakini kuna sehemu, hata Watendaji wenyewe hawajui nini kimetokea kutokana na elimu yao kwenye eneo hilo kuwa ndogo). Naishauri sana Wizara, iangalie upya utaratibu mzima wa uchangiaji na usimamizi wa fedha za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika Elimu ya Sekondari ni Mkakati wa Upanuzi wa Shule za Sekondari za kutwa kuwa za bweni na hatimaye ziwe za *A level.* Hivi sasa Serikali imeelekeza kila Wilaya iwe na mpango wa Shule mbilikuwa za *A level.* Jambo hili linavyoonekana limeachiwa Wilaya zijitegemee. Naomba Wizara iliratibu ki-Wizara, viwango vya elimu nchini haviko sawa. Kuna mikoa ambayo tayari ilikuwa na Shule za *A level* na bweni za Kitaifa na mingine haikuwa nazo. Hivyo, si sawa Mikoa/Wilaya isiyo na *A level* (kama Kahama), kuiacha ihangaike yenyewe, huku ikihangaika kupanua shule za kawaida za *O level!* Mzigo unakuwa mkubwa mno kwa Wilaya. Naiomba Serikali ichukue jukumu la kuweka uwiano Kitaifa kwamba, shule kadhaa za *O level* ziwe na *A level.* Wizara yenyewe ihusike moja kwa moja katika hili. Hii ndiyo maana ya Serikali na ndiyo maana ya kutokuwa na Serikali za Majimbo! Kabla ya mwaka 2000, ikiwa na watu zaidi ya 500,000, Kahama haikuwa na Sekondari ya Serikali hata moja; hata hii leo haina sekondari ya bweni hata moja na haina Sekondari ya *A level* hata moja hata leo hii.

Je, ni sawa kuitaka Wilaya hii ishindane na Ilemela, Hai, Marangu na hata Korogwe zilizokuwa na Sekondari za bweni zaidi ya mbili toka miaka ya 1980? Naiomba Serikali, isaidie jitihada za Wananchi wa Kahama ambao tayari wanahangaikia Shule za Mwalimu Nyerere, Mpera, Busangi, Mwendakulima na Bugarama ili ziwe na bweni na baadaya zipate *A level.*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lenye matatizo ni utaratibu wa chakula mashuleni. Jambo hili linalalamikiwa sana na wananchi. Inavyoonekana, utaratibu huu kwa sasa unatumika kusaidia maeneo ambayo kuna viongozi wenye nguvu Serikalini. Wananchi wa Msalala, hasa Kata ya Isaka, Jaana, Isagehe, Mwalugulu na Kinaga, wamekuwa wakilalamikia uwepo wa *WFP depot* Isaka na shirika hilo la *UN* kutoa chakula cha mashuleni kwa shule za mikoa mingine huku wao wakishinda na njaa mashuleni. Mara kadhaa, wameniomba niwasiliane na *WFP* na nimefanya hivyo lakini kila mara *WFP* wanatoa jibu kuwa Wizara ndiyo inayopendekeza shule za kuingizwa kwenye mpango huo.

Naiomba sana Wizara, ishirikiane na *WFP*, ambao kimahusiano na ujirani mwema, wapo tayari kuiingiza Wilaya ya Kahama kwenye mpango huo. Ilimradi Wizara imeridhia na kuwaelekeza hivyo. Naomba sana hizi *sentiments* za wananchi kuwa hawasaidiwi labda kwa kuwa hawana kiongozi mwenye nguvu Serikalini, tuzikanushe kwa vitendo. Kutokana na ukubwa wa umaskini na utoro mashuleni, naomba Serikali iingize Mpango huu kwenye bajeti yake, badala ya kuwaachia wafadhili na wazazi. Bora Serikali iongeze au irejeshe ada *Primary Schools* ili iweze kugharimia Mpango huu

badala ya kuuachia wafadhili. Lazima tukubali kuwa nchi yetu hailingani kimaendeleo na umaskini toka mkoa mmoja hadi mwingine. Serikali/Wizara iwajibike kuleta usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni uhaba wa vifaa vya kujifunza na kufundishia mashuleni pamoja na vifaa vya michezo. Kwa kuwa Serikali imekubali kurejesha michezo mashuleni, ni vizuri sasa ikawajibika kuhakikisha uwepo wa vifaa vya michezo na viwanja vya michezo mashuleni. Itenge fungu la vifaa vya michezo, hata mipira walau minne kwa shule kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba kusisitiza Wizara itoe majibu kwa hoja zangu zote. Kwa kuwa siwezi kuchangia kwa maandishi (si lazima leo), lakini nipate majibu nitakayokwenda nayo, ambayo kwa msingi wa *collective responsibility*, nitawajibika kwenda kuwaeleza/kuwajibu wananchi wangu, ambao ndio hasa wanahitaji majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa ushauri ufuatao:-

(a) Upungufu wa walimu umalizwe haraka hasa Shule za Sekondari. Tusione aibu kuwatafuta nje kujaza mapengo yaliyopo. Twende nchi jirani za Asia, Amerika na Ulaya kupata walimu, mfano *volunteers* vijana na wazee kama tulivyofanya mara baada ya Uhuru. Hivi sasa wazazi na wanafunzi wanalalamikia ukosefu wa walimu hata kusita kuchangia zaidi ujenzi, wanasema Serikali "inalangua elimu" imedanganya. Sote tunafahamu madhara ya *little education.*

(b) Tusibomoe *syllabus* zetu. *Syllabus* ya Tanzania ni nzuri sana. Tatizo haina walimu wa kufundishia inavyotarajiwa. Ushahidi ni Watanzania kushindana kibingwa waendapo kusoma vyuo vya nje baada ya Sekondari.

(c) Serikali iige Zanzibar kuhusu ujenzi wa maabara kwenye Sekondari, hata kwa kukopa

(d) Tuangalie tena *(review)* maana ya Elimu ya Ufundi. Tunaweza kusema kwa dhati na kwa ushahidi kwamba, tuna *value for money spent on VETA?* Tunahitaji kuwa na tafsiri mpya ya nini Ufundi; ni huo unaotolewa sasa; ni viwango na vifaa vya sasa? Leo mashine ni *computerised, digital; VETA* wanafundishia *outmoded equipments*, tena kijuu juu *that means low quality output.* Aidha ni vyema *VETA* ikatoa vijana kuendana na mahitaji ya uchumi ambao unakua kisekta. Ingekuwa vizuri kupata maoni ya waajiri kwamba, wanahitaji mafundi wa viwango gani. Yapo malalamiko yao kuwa *there is no taxation without representation*, kwani wanakatwa kodi *(training levy)* bila kufaidika na wanaohitimu humo. *VETA* inasema nini juu ya wanaohitimu Sekondari za Kata? Hawa si malighafi yao? Hawa ni kufundisha ufundi wa kawaida kama wa Darasa la VII au ufundi wa aina gani na kwa viwango vipi?

(e) Lipo tatizo la wanafunzi yatima na wanaotoka familia fukara au wenye mzazi mmoja asiye na uwezo; ni wengi sana. Tunashukuru upo mpango wa kuwasaidia lakini hautoshelezi. Kuna haja ya kubuni mpango wa kujibu tatizo vizuri zaidi.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwaka 2006, Jimbo la Songwe lilikuwa na Shule moja tu ya Sekondari ya Serikali. Hivi sasa Jimbo hilo lina shule saba na nyingine tatu zinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, matatizo ni upungufu wa walimu, baadhi ya shule zina walimu watatu tu.

Pili, ukosefu wa mabweni hasa ya wasichana, Serikali iunge mkono kwa kuweka au kuanzisha Mfuko wa Ujenzi wa Mabweni.

Tatu, Mwaka 2003/04 baadhi ya Shule za Sekondari zilifutiwa Matokeo ya Mtihani wa *Form IV* kutokana na Shule hizo kuvujisha mitihani. Katika baadhi ya Shule hizo, Watumishi wake walijifanya walimu wakati hawakuwa na sifa za ualimu. Wengine walipatikana na vyeti vya ualimu vya kugushi. Kutokana na hilo, Serikali ilitangaza kuwa itawachukulia hatua za kisheria wale watumishi waliopatikana na tuhuma za makosa ya kijinai. Je, kwa nini Serikali haikutekeleza hatua au dhamira yake?

Kuna mtindo ulioanzishwa miaka ya hivi karibuni ya kutolewa elimu ya twisheni nje ya madarasa. Je, Serikali haifikirii kuanzisha tuisheni kunawashawishi walimu waelekeze uwezo wao kwenye tuisheni?

Wapo baadhi ya walimu wamejiingiza katika kazi ya utendaji wa siasa, yaani wamegombea nafasi za uongozi kwenye vyama vya siasi na wamechaguliwa katika nafasi hizo. Nia ya walimu waliofanya hivyo ni baadaye kugombea nafasi ya Ubunge kwenye maeneo walipo. Je, lile agizo kupitia Waraka Maalum unaowatahadharisha walimu wasijiingize kwenye siasa umefutwa?

Baadhi ya walimu katika Shule za msingi wamekaa shemu moja kwa muda mrefu. Matokeo yake walimu hao hujiingiza kwenye biashara na mambo mengine kama vile kwenye siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeniwezesha kuamka na kufika hapa Bungeni bila ya kukamatwa mkono. Pia nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa staili yako ya kuliongoza Bunge. Kabla sijaendelea na mchango wangu ni vyema niipongeze Wizara hii kwa nia yake ya kufuta ujinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa niruhusu nitoe mchango wangu kwa kuanzia niipongeze Serikali kwa umahiri wake wa kufanikisha

madarasa mengi nchini. Suala hili ni zuri sana. Pamoja na uzuri huu, ipo haja sasa Wizara ichukue hatua za kutuondolea tatizo sugu la ukosefu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa walimu mashuleni utachangia kwa kasi kuwa na kizazi maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za walimu, pamoja na ukosefu wa walimu, hili linachangiwa sana na ukosefu wa walimu, kwani mwalimu ni mtu anayehitaji kuwezeshwa. Kukosekana kwa nyumba za walimu, kunachangia kwa kiasi kikubwa. Hivyo, Serikali iwe tayati kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mitihani kwa wanafunzi; mitihani ni kipimo kwa wanafunzi si kitu kingine. Ni kitu gani kinachopelekea kuvuja kwa mitihani? Dosari hii inawadhoofisha wale wote ambao hawakuhusika. Naiomba Serikali ichukue tahadhari ili kulitatua tatizo hili

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bajeti, Wizara ya Elimu imekabiliwa na mzigo mkubwa kutokana na ufinyu wa bajeti. Nahisi Serikali ilisahau mzigo wa Wizara. Kwa mfano, kuna uhaba wa chakula katika Shule za Sekondari. Ni vyema Serikali iitupie jicho la rehema ili kuinusuru Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nasema *Inshaallah.*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote, Makamishna na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuinua Elimu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati wa Bajeti, Waziri hapa aliahidi hapa hapa Bungeni kwamba, atatoa fedha za kujenga hosteli Shule ya Sekondari Mwamgeza, ambayo itatumiwa na wanafunzi wa Ki-Hadzabe ambao mpaka sasa tunajitahidi sana waendelee kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kushirikiana na wananchi kwa kujenga madarasa, nyumba za walimu, maabara na vyoo. Kwangu kila Kata imeshakamilisha ujenzi wa shule, tatizo bado maabara, hosteli na nyumba za walimu. Naomba sana, kwa sasa jitihada zote zielekezwe kwenye kuhawilisha mambo niliyotaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namwomba sana Waziri na wenzake wajikite kwenye kutafuta walimu wa kutosha. Sasa hivi shule nyingi hazina walimu. Naomba sana shule za msingi zianze kupata chakula cha mchana shuleni. Kwa kusaidiana na *WFP* na Halmashauri zetu, hili linawezekana kabisa. Kwenye shule ambazo *WFP* inatoa chakula; maendeleo na mahudhurio ni mazuri sana, pia wanafunzi wengi wanafaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Hata hivyo, madai ya walimu yalipwe haraka.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja upande wa walimu. Bila ya walimu hapana elimu, tunaweza kuwa na mabanda mengi na wanafunzi wengi lakini bila walimu hapana elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye nidhamu kwa wanafunzi; Serikali ilitilie maanani sana suala la nidhamu kwa wanafunzi, pamoja na walimu mashuleni. Bila nidhamu mashuleni hatutapata wataalam, wafanyakazi na viongozi bora kwa taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Elimu Bora. Elimu Bora ni ile inayotolewa kwa vitendo zaidi. Kwa hiyo basi, Serikali yetu kama inataka nchi yetu ipige hatua nzuri ya maendeleo na kupunguza umaskini kupitia Elimu, basi lazima shule zetu kuanzia msingi zifundishwe zaidi kwa vitendo halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira kwa walimu. Serikali ihakikishe kwamba, ili walimu waweze kutoa elimu vizuri kwa wanafunzi, basi wawe na maslahi na mazingira mazuri ya kiualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eimu ya msingi ndio msingi wa elimu ya juu. Kwa hiyo, ikipatikana elimu nzuri ya msingi, bila shaka tutapata watu tunaowahitaji katika taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ya ualimu na mafunzo kwa ajili ya wanafunzi, kama vile semina na vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaunga mkono hoja, napenda nipate maelezo ya kina ni sababu zipi zimeifanya Wilaya ya Geita isipatiwe Chuo cha Ufundi Stadi?

Geita ina zaidi ya watu milioni moja. Imekusanya watu kwenye migodi na mialo pamoja na vijiji vikubwa. Kuna watoto wengi sana wanamaliza masomo ya Msingi/Sekondari, hawana pa kwenda. Matokeo yake wanajihusisha na ujambazi na umalaya. Serikali halioni hili? Naomba Wilaya ya Geita ipatiwe Chuo cha Ufundi Stadi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ujambazi katika Mkoa wa Mwanza hususan katika Wilaya ya Geita, walimu wanaishi bila amani kutokana na kuenea kwa ujambazi ambao wamekuwa wakifanyiwa hususan watokapo kupokea mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara/Waziri katika majumuisho atoe tamko juu ya usalama wa walimu hawa wa msingi vijijini pamoja na mali zao.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Watumishi wa Wizara yako kwa kufanikisha maendeleo katika nchi yetu. Napenda kutumia fursa hii kuzungumzia hoja mbalimbali. Pamoja na kuwepo na mafanikio, pia kuna matatizo yanayoikabili Wizara hii kwa mfano:-

- Matatizo ya walimu wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu hasa vijijini, walimu hao hawana nyumba za kuishi. Nauli kwenda vijijini na bei mbaya na huduma za kijamii hazipatikani.

- Walimu walioko vijijini hawarekebishiwi madaraja yao. Tatizo hili limeleta tofauti ya walimu walioko daraja moja kutofautiana, huku wengine wakipandishwa na wengine kubaki.

- Walimu kutorekebishiwa mishahara yao na kubaki kwenye ngazi moja ya mshahara huku wengine wakiwa wamerekebishiwa.

- Upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya kutosha na kwa wakati. Kulipa madeni ya shule za bweni kuhusu madeni ya chakula ili kuboresha mpango wa upatikanaji wa huduma ya chakula mashuleni.

- Kuhusu *VETA*, kwenye swali langu mwezi wa nne kuhusu Shule ya *VETA*, kujengwa Longido. Naibu Waziri alisema, nanukuu: “Ujenzi wa *VETA* Wilayani Longido, Wizara itajenga chuo hicho ifikapo mwezi Desemba, 2008 itakuwa imeanza.”

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi kwani Chuo hicho cha *VETA* hakipo kwenye mpango, hata kwenye jedwali ukurasa wa 103 (kielelezo Na. 3), Wilaya ya Longido haimo kabisa. Wananchi walimsikiliza sana Naibu Waziri alipoeleza kwamba, *VETA* ni muhimu sana Wilayani Longido ili kupunguza kasi ya vijana wanaokosa kazi za kufanya na kwenda mijini kulinda nyumba za watu kwa sababu hawana kazi mbadala. Naomba Mheshimiwa Waziri, *VETA* ijengwe kwenye Wilaya ya Longido.

Mwisho, naomba walimu wanaoishi kwenye mazingira magumu, wapewe kipaumbele ili waweze kudumu na hali iliyoko kwenye maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi hawakujenga maeneo au majengo ya maabara, baada ya aliyekuwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Joseph Mungai, kueleza kwenye Bunge kwamba, Serikali ijenge maabara kwenye Sekondari zote ndipo wananchi hawakuhangaika tena kwenye ujenzi huo. Kwa hiyo, naomba sasa kazi hii ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule yetu ya Sekondari Longido haina walimu wa Kidato cha Tano na Sita na kwa bahati mbaya wana walimu wanne tu. Ahsante.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake yenye mwelekeo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, napenda kuwapongeza Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, kwa ushirikiano wao na kazi nzuri wanayomsaidia Mheshimiwa Waziri. Pamoja nao, nawapongeza Watendaji nikianzia Katibu Mkuu na wengine, kwa kazi nzuri yenye mshikamano mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo yote, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia yafuatayo: Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; ni vyema Serikali iifuatilie kwa karibu Bodi ya Mikopo kwa madhumuni ya kuifanya Bodi ifanye kazi zake kwa uaminifu mkubwa na si kwa upendeleo kwa wanafunzi wachache. Ikiwa kama mwanafunzi ameomba mkopo, basi mkopo huo utolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia ya wanafunzi kupata mimba kwa sasa si kitu cha ajabu. Kitu ambacho kinakiuka maadili yetu. Kwa hiyo, napendekeza wanafunzi wakiume au wanaume hasa walimu, endapo itathibitika kuhusika na mimba za wanafunzi basi hatua kali zichukuliwe kwa kufunguliwa mashtaka na ikithibitika wapewe adhabu kati kuliko adhabu iliyopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza wanafunzi wanaohitimu *VETA* wapatiwe misaada ama mikopo ya fedha na vifaa vya ufundi, kwa ajili ya kuwafanya vijana hao waweze kujiajiri wenyewe na kuajiri wenzao na kujipatia maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali pia iwasiliane na kumsaidia Waziri wa Elimu, Serikali ya Zanzibar ili Zanzibar waanzishe Vyuo vya *VETA* ili na wao waweze kujikomboa na kujipatia kipato kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ianzishe maktaba nyingi na zilizo bora wilayani na hasa vijijini, kwa sababu bila maktaba za kisasa basi wanafunzi hawawezi kufanikiwa vizuri katika masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila maabara za kisasa, wanafunzi hawawezi kufanya mitihani yao ya masomo ya sayansi. Kwa hiyo, nashauri Serikali kwa zile shule zisizo na maabara, basi wawekewe maabara, kwa kuwa bila maabara za kisasa wanafunzi hawataweza kufanya mitihani kwa *practical* na bila *practical* basi hakuna kufanikiwa vizuri kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya yote hayo, napenda kuunga mkono hoja tena kwa asilimia mia moja.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja. Naomba nianze kwa masikitiko makubwa sana, kwa kuona kuwa kuna uonevu mkubwa katika ugawaji wa rasilimali wa wa nchi hii. Ukurasa wa 103 imechagua Wilaya 25 ambazo hazina Vyuo vya *VETA* (Ufundi Stadi), sielewi ni kigezo gani kimetumika, Geita haina chuo chochote.

Geita ina takriban watu zaidi ya 900,000, hakuna chuo chochote ni Wilaya ya zamani. Wilaya mlizopendelea zote ni Wilaya mpya na changa. Geita imekosa nini au mna maana gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sielewi unatumia utaratibu gani? Naomba nielezwe Wilaya kati ya zilizopewa vyuo zinazozidi idadi ya watu Geita, uzalishaji na idadi ya wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba na Sekondari ukiondoa Kindononi, Ilala na Temeke; je, *VETA* zilizoko Dar es Salaam zipo Wilaya gain? Huu ni upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili siungi mkono hoja.

Ni lini chombo cha walimu kitakuwa kimoja; walimu kuwa chini ya mwajiri mmoja?

*UNESCO* itafanyaje kazi kwa kiasi kidogo ilichopewa? Tafadhali iangaliwe upya.

Kwa nini Elimu ya Watu Wazima inachukuliwa kama kitengo, wakati inategemewa kwa kukamilisha upungufu katika ngazi zote za elimu?

Madeni ya walimu yatalipwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba michezo izidi kuimarishwa ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ituelewe, Chuo cha Ufundi Stadi hatuna wala Chuo cha Udereva tu hakuna. Je, Geita inaadhibiwa kwa kuwa haichangii Mapato ya Serikali? Geita haina chuo hata cha *U-sister*, idadi ya wanafunzi wa Geita ni sawa na wananchi wote wa Mkoa wa Lindi; kwa nini tusipewe chuo? Geita imekuwepo tangu Ukoloni; ina Kosa gain?

**MHE. MUDHIHIR MOHAMED MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Shule ya Sekondari ya Nanyanje ndani ya Jimbo la Mchinga, ambayo kuhamishiwa kwake kupelekwa Kijiji cha Chikonji kulitokana na sababu za kitaalam, sasa suala hili limekuwa mtaji wa kisiasa kwa *CUF* dhidi ya CCM.

Mimi bado naamini kuwa, kwa vile Shule hii haijafutiwa usajili, kuanzishwa kwa Sekondari ya Chikonji hakuhalalishi kufutiwa usajili Sekondari ya Nanyanje. Yapo madarasa ya kutosha Nanyanje. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, ameahidi kuwa,

Shule hii haijafutwa. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, ameahidi Bungeni kuwa, Serikali itaziunga mkono Sekondari zote mbili.

Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, awahakikishe watu wa Nanyanje, Jangwani na Namatiwi kuwa *Selection Board* mwaka huu wa 2008 itateua wanafunzi wa Kidato cha Kwanza (2009) Nanyanje, tutapangiwa walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini ahadi ya Serikali kuhusu Sekondari ya Nanyanje ni ahadi ya vitendo na siyo maneno ya Antonio na Ottavio kuhusu Lepido katika igizo la Julias Kaizari sehemu ya IV onyesho la I:

> ‘Tungempa mtu huyu utukufu wote huu,
> Ili kujipunguzia mzigo wa malawama,
> Taubeba kama punda anavyobeba dhahabu,
> Kilalama na kutoka jasho kwa uzito wake,
> Kiongozwa na kuswagwa vile tutavyomonyesha,
> Na mara afikishapo amana tupapendapo,
> Tutamtua mzigo wake na kumwachilia,
> Sawa na punda mtupu, atikise masikio,
> Ajiendee mbugani, akale majani yake’.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa Kamati ya Matumizi nitahiari kuwa punda wa Antonio kwa sababu ya Sekondari ya Nanyanje, nitakuwa mnyama niutie ulimi puani. Sitotikisa masikio kama Punda wa Antonio wala sitoenda mbugani kula majani bali nitabakia CCM kuitetea Ilani yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili linahusiana na Chuo cha *VETA* Mkoani Lindi, umekuwa ni wimbo wa “Alfu Leila Uleila” hakuna kinachoendelea. Hatusemi kuwa tunadanganywa, bali hapana shaka pia kuwa hatuambiwi ukweli. Ahadi hii ya Chuo cha *VETA* Mkoani Lindi inafanana na maneno ya Buruto wa William Shakespeare, Sehemu ya II, Onyesho la I:

> ‘Lakini ni wazi kwamba, unyenyekevu ni ngazi ya kila mtaka cheo, Ambayo anayepanda hutazama kwa juu, bali akishakanyaga kile kipago cha mwisho, mara huipa kisogo ngazi aliyopandia, akatazama mawingu na kudharau vya chini.’

Mheshimiwa Naibu Spika, nataraji Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, atatueleza watu wa Lindi ni lini chuo hiki kitaanza kuengwa na lini kitakamilika. Wakati wa Kamati ya Matumizi nitakataa kwa niaba ya Mkoa wa Lindi kuwa ngazi ya Buruto, watu watukanyage wakivuka kwenda zao na sisi tupo palepale. Ahsante.

**MHE. EPHAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuanda hotuba nzuri.

Ongezeko la wanafunzi wanaotakiwa kuingia Kidato cha Tano na Sita ni suala la kufa na kupona. Kwa Mikoa/Wilaya zilizo *marginalized* kielimu (Dodoma ikiwa mojawapo), upendeleo maalumu ufanywe wa kuanzisha Shule za *A level* na kuwaongezea fursa vijana hao, vinginevyo, watabakia kuwa wafagizi kwenye Vyuo Vikuu ambavyo vinajengwa kwenye maeneo yao.

Ujenzi wa Mabweni *(Hostels)* kwa ajili ya Shule za Kata utiliwe mkazo, hasa kwa ajili ya wasichana.

Nashauri kasi ya kuwasomesha walimu iongezwe ili kuboresha Elimu ya Sekondari

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Maabara uende sambamba na ujenzi wa Madarasa.

Serikali/*TANESCO* iache tabia ya kudai gharama zisizo halali wakati Shule hizi mpya zinapoomba kuunganishiwa umeme. Malipo yanayostahili ni yale ya *service line* pamoja na mita na si vinginevyo. Wizara ilifikishe suala hili kwa wanaohusika *TANESCO*, kwani mipango yao ya kuhimiza elimu ya sayansi ndiyo inaathirika sana. Katika Jimbo la Uchaguzi la Dodoma Mjini, ipo Shule ya Makutupora ambayo inashindwa kuunganisha umeme kutokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, yenye mwelekeo wa kuboresha taasisi zote ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, sasa naanza kuchangia kama ifuatavyo:-

(a) Serikali isaidie ujenzi wa nyumba, madarasa na hosteli katika Shule za Sekondari. Napenda nitumie nafasi ya awali, kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya kujenga Shule za Sekondari kwa kushirikisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali, naiomba Serikali ikumbuke kauli yake wakati walipojibu swali langu hapa Bungeni kuwa itatoa kipaumbele kusaidia umaliziaji wa ujenzi wa hosteli, nyumba na madarasa na pale watakapoona wananchi wamekamilisha maboma ya majengo haya, itamalizia kwa kutoa bati na mbao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mkoa wa Singida, umejenga maboma mengi ya hosteli hivyo Serikali imalize kama walivyonijibu swali langu. Mfano wa Shule ambazo zimekamilisha maboma nilimpa Mheshimiwa Mahiza, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Mkoani Singida mwaka huu.

Mheshimiwa naibu Spika, pamoja na ombi hili, pia naishauri Serikali inapogawa fedha kwa ujenzi wa nyumba za walimu, pamoja na hosteli, itoe kipaumbele kwenye shule ambazo ziko vijiji vya mbali na hakuna hata nyumba za kupanga kwa walimu hata wanafunzi; mfano Shule ya Mgungira Singida Vijijini, Mwamagembe Manyoni Magharibi, Sanza Manyoni Mashariki, Tulya Sekondari Iramba na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, natambua juhudi za Serikali katika kulipa madai mbalimbali ya walimu wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali, bado malimbikizo ya madai ya walimu yanazidi kuwa makubwa zaidi; mfano, 2007/08 madai yalikuwa shilingi bilioni 9.5, Serikali ilijitahidi kulipa shilingi bilioni 7.1. Sasa madai ya walimu wa shule za msingi tu shilingi bilioni 12.2, madai ya sekondari na vyuo ni shilingi bilioni 4.2; jumla yote shilingi bilioni 16.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali inatisha sana; ni njia ya kuwakatisha tamaa walimu wa kuwapa vishawishi kupokea rushwa, kutumia vibaya fedha za shule na mali zake. Napenda kusikia Serikali inayo mipango gani ya haraka kuondoa madeni haya na kuanza ukurasa mpya wa kutokudaiwa na walimu tena kwani walimu ni sawa na taasisi nyingine za Serikali ambazo hazikopwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanadai fedha za matibabu, likizo, uhamisho, gharama za masomo pia hawalipwi mishahara kwa wakati kama ilivyokuwa mwaka 2006/07; huko benki kumetokea nini tena?

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, najua inajulikana wazi kuwa, migogoro ya wanafunzi katika Shule za Sekondari sasa ni mingi sana. Shule nyingi ukifuatilia vyanzo vya migogoro utakuta ni walimu. Napenda kutoa mifano miwili tu ya shule zilizokumbwa na migogoro; Shule ya Kifaru Wilaya ya Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro, mwalimu aliwalazimisha wanafunzi kushika kinyesi cha binadamu kwa mikono, jambo ambalo ni baya sana la kudhalilisha utu wa binadamu. Mwalimu huyu amechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Shule ya Sekondari ya Shelui Wilaya ya Iramba Mkoa wa Singida, chanzo cha mgogoro ni walimu kukiuka makubaliano mfano chakula, pia kutumia fedha za wanafunzi, walimu kutembea na wanafunzi wa kike na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wakuu wa Shule kutokukaa kwenye vituo vyao vya kazi, cha kusikitisha adhabu zinazotolewa zinakuwa kwa wanafunzi na sio walimu tena. Naiomba Serikali, itoe ufafanuzi katika hoja hii ili Watanzania wajenge imani na Serikali yao.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa utaratibu mzuri wa Serikali wa kukutana mara moja kila baada ya miezi mitatu, kutatua matatizo ya walimu. Bado hoja zao nyingi za msingi hazijapata ufumbuzi mfano posho ya kufundishia na posho za mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwaelewe walimu kuwa wanafanya kazi ngumu na hata nje ya muda wa kazi. Mfano, mwalimu anafundisha darasa lenye wanafunzi 120. Pamoja na jitihada za ujenzi wa madarasa, Tanzania ina baraka ya uzazi tunazaa sana. Idadi hii ni sawa na madarasa matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata baada ya kutoka kazini, anaondoka na madaftari ya wanafunzi ya masomo matano au zaidi kwenda kusahihisha usiku ili kesho aweze kuendelea na somo/masomo mengine. Vilevile mwalimu huyu huyu, baada ya kusahihisha lazima kabla ya kulala ajiandae kwa masomo ya siku inayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbe Tume ya Rais ya Mwaka 1981 iliainisha wazi uzito wa kazi ya mwalimu. Naiomba Serikali ikubali kutoa posho kwa walimu wa mazingira magumu na posho ya kufundishia. Hii itawapa moyo sana walimu kufanya kazi yenye tija na kuachana na biashara saa za kazi na dhuluma kwa wanafunzi/wazazi.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na orodha iliyotolewa ya mwaka 2006 hadi Oktoba, 2007 ya walimu waliostahili kurekebishiwa madaraja yao, bado kuna upungufu mwingi unajitokeza kama nitakavyoorodhesha hapa chini:-

(i) Baadhi ya walimu wamepata madaraja ya juu tofauti na stahili zao;

(ii) Walimu baadhi waliorekebishwa mishahara yao hawajalipwa malimbikizo yao;

(iii) Baadhi ya walimu wenye sifa za kufanana wana madaraja tofauti;

(iv) Baadhi ya walimu hawapo kwenye orodha ya wanaostahili kurekebishiwa; na

(v) Baadhi ya walimu wamerekebishiwa vidato badala ya madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sasa Serikali ihakikishe inaondoa kero hizi za walimu ili kuzuia migogoro ya walimu na Serikali yao.

(f) Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe walimu wanawajibika karibu Wizara tatu au zaidi; Wizara ya Elimu, Wizara ya Utumishi na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naishauri Serikali itoe uamuzi juu ya tatizo hili, ili walimu wabaki na chombo kimoja cha ajira kwani Wizara tatu zinawapa milolongo mirefu sana katika kupata huduma au haki zao.

(g) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara imekuwa na utaratibu wa kuunganisha masomo ya mitaala hubadilika sielewi ni kwa nini walimu hawapati kozi au semina fupi ili waweze kupata uelewa kwa kufundisha mitaala hii mipya. Ninapata wasiwasi kuwa walimu wanafundisha kwa kufuata vitabu tu sio kwamba wana uelewa wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vilevile Serikali inataka kutoa taaluma ipasavyo ni vyema walimu wawe wanapata nafasi ya kupandishwa daraja na vidato, pia mfano walimu wa Daraja la IIIA angalau robo wapate kozi ya *diploma* na walimu wa *diploma* angalau robo kupata digrii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia kupata walimu wenye viwango vya juu na uelewa mkubwa wa kutoa taaluma sambamba na wakati tulionao sasa.

(h) Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuitambua kada hii kuwa ina jukumu kubwa katika kusimamia utoaji wa taaluma katika shule zote za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuijulisha Serikali kitengo hiki ukaguzi hakijapata huduma ya Serikali ipasavyo, kwani fedha wanazopata ni ndogo sana, bado suala la vifaa ni tatizo kubwa sana hasa usafiri na kadhalika. Naiomba sana Serikali ione uwezekano wa kuongeza bajeti ya Kitengo cha Ukaguzi na ipewe vifaa hasa usafiri. Hii itasaidia kusimamia taaluma inayotolewa mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mkuu wa Mkoa na Sekretarieti yake ya Mkoa, pamoja na Watendaji wote mikoani, bila kuwasahau Wanasiasa, Madiwani na Wabunge wa Mkoa wa Singida, kwani wanafanya kazi kubwa ya ujenzi wa Shule za Sekondari nyingi na kufanya Shule za Sekondari Singida kuwa 120.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa mkoa unajenga Shule za Elimu ya Juu kila Tarafa na Tarafa zipo 21; hivyo basi, naiomba Serikali ipeleke maabara angalau moja kwa kila Tarafa ili azma ya mkoa izae matunda. Bila maabara, shule hizi zitakuwa ni bure kwani taaluma ya sayansi, haitatolewa vilivyo, vilevile hata Shule za Sekondari za kawaida watatumia maabara hiyo moja hadi pale Serikali itakapopata uwezo wa kupeleka kila shule maabara yake. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Serikali inatambua uhaba wa walimu kwa Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Naishauri Serikali iongeze Vyuo vya Ualimu Daraja la III A na *Diploma* ili iweze kusomesha walimu wa kutosha ambao watawatua mzigo walimu ambao wanafundisha vipindi vingi kuliko kawaida, ama darasa lenye wanafunzi wengi kuliko kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Waziri atoe ufafanuzi wakati wa majumuisho yake ili tujue msimamo wa Serikali kupitia hoja za Wabunge kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mabadiliko yaliyofanyika ya kuwa na Muundo Mpya wa Elimu hadi ngazi za Halmashauri. Jambo ambalo litasaidia kufikisha huduma kwa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta ufanisi bora, nashauri awepo *Chief Education Officer (CEO)*, mwenye taaluma ya kutosha ya elimu akisaidiana na Waratibu wawili; mmoja wa Shule ya Msingi mwingine wa Shule ya Sekondari. Hii itarahisisha usimamizi kikamilifu; kimadaraka na kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanzishwa Shule za Sekondari za Kata, walimu wengi wa Shule za Msingi waliojiendeleza kielimu kwa gharama zao na kufikia ngazi ya *diploma* wamehamishiwa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamisho huu unafanyika bila kuzingatia taratibu za ajira zinazoambatana na haki stahili za walimu hao kiutumishi mfano, malipo ya uhamisho, kuhamisha utumishi na kadhalika; naishauri Serikali uwepo uratatibu unaoeleweka kuhusiana na suala hili, kuwatendea haki walimu na kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nimalizie kwa kusema kuwa, naunga mkono hoja nikitegemea Serikali itanipa majibu ya hoja zangu Waziri atakapotoa majumuisho. Nawaombea Mungu awape afya ili watekeleze azma yao vyema.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja. Natoa pongezi kwa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu wa Wizara na Wataalamu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kama ufuatao:-

Wizara ikishatayarisha mitaala mipya, iwakusanye Maafisa Elimu wa Mkoa na Wilaya ili wapewe semina na kuhakikisha wameielewa hiyo mitaala mipya ili wakirudi na mitaala hiyo kabla hawajasambaza mashuleni, wawaite Walimu Wakuu wa Shule husika waelimishwe, baada ya hapo ndipo utekelezaji uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara isisitize sana Elimu ya Ufundi katika Shule zote za Sekondari ili ufundi huo uwasaidie wanafunzi ambao hawawezi kuendelea na elimu ya juu. Kuhusu Shule za Ufundi *VETA*, tunaomba wanafunzi wakifaulu wapewe vitendea kazi ya fani waliyojifunza kama ruzuku au mkopo kwa masharti ili wakirudi majumbani waweze kuanzisha miradi ya kujitegemea kuliko ilivyo hivi sasa hawapewi msaada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaitikia sana suala la ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata. Ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii, suala la madawati na vitendea kazi, mzigo huu ubebwe na Serikali, la sivyo kuendelea kuchangisha wananchi; wananchi watachoka na kuichukia Serikali yao na wamejitolea shughuli nyingi kama vile ujenzi wa zahanati na Vituo vya Afya. Kama hatuwezi kukamilisha vitendea kazi bora kwenye

Shule zetu za Serikali, tusitegemee watoto wetu kupata elimu bora. Wizara ihakikishe usafiri upo kwenye Shule za Sekondari.

Suala la shule za walemavu, kama wa aina ya viziwi, vipofu na walemavu wa viungo limezungumzwa sana humu Bungeni kwa muda mrefu, lakini vitendo vyetu na usimamizi wa kauli zetu na utekelezaji ni tatizo. Kwa mfano, Shule ya Bwigiri (vipofu), Shule ya Viziwi Tabora ambayo haina mwenyewe, kwa kuwa Shule hiyo huishi kama chombo cha misaada kwa watu/wananchi ili wapate pesa ya kuwapatia chakula na kama wakishindwa kupata huamua kufunga shule. Je, isingekuwa busara kuichukua shule hiyo ya Viziwi Tabora iwe mikononi mwa Serikali na iwe ya Kitaifa, kwani ina majengo mazuri yaliyofadhiliwa na wahisani wa dini ambao wameikabidhi?

Malipo kwa walimu wastaafu ambao wamefundisha kwa mkataba, wapo baadhi Tabora ambao tangu Novemba, 2007 mpaka sasa hawajalipwa madai yao.

Serikali isisitize michezo mbalimbali kwa wanafunzi wa msingi na sekondari, ili kukuza vipaji vyao. Serikali iangalie pia kudumisha utamaduni wa maeneo husika au mkoa husika ili wanafunzi wajue utamaduni wao wa asili.

Walimu wa Shule za awali wanakatishwa tamaa kutokana na malipo ya mishahara yao kama posho. Mazingira ya kufundishia hayaridhishi kwani madarasa yaliyopo hayatoshelezi wao kuwa ndani ya madarasa badala yake hufundishia chini ya miti. Je, wakati wa masika inakuwa vipi? Serikali iangalie upya.

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mheshimiwa Mantumu Mahiza, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Shule ya Sekondari Kizaga; niliwahi kuelezea katika Bunge la mwaka 2006, juu ya ubadhirifu wa fedha za Mradi wa Ujenzi wa Hosteli, fedha zilizotolewa na wahisani. Walimu wawili walihusika na tuhuma hizo, kinachoshangaza hakuna chochote kilichofanyika mbali ya Wizara kuchukua hatua za kuwahamisha mwalimu *(Head Master)* huyo kupelekwa mkoa mwingine huku yule *Second Head Master* akibaki pale pale Kizega Sekondari. Katika kufanya hilo, hiyo hosteli hadi leo toka 2006 imesimama ilihali ikiendelea kuchakaa bila ya kujua nani ataiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya shule hizi za sekondari ni ya wananchi lakini tumefurahi sana tunapopata wafadhili kusaidia katika kuboresha ujenzi katika Sekta hii ya Elimu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa naelewa suala hili wanalifahamu vizuri, basi wachukue fursa ya kwenda kukamilisha ujenzi wa hosteli hiyo. Nasema hivyo kwa kuwa wananchi hawapo tayari tena kwa kuwa wamefahamu fika fedha iliyotolewa imeibiwa na mtu mmoja na bado Wizara ikamwekea kifua kwa kumhamisha kwenda mkoa mwingine ili ubadhirifu huo ufichike. Hilo sikubaliani nalo na Waziri naomba anipe maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba mwaka huu Wilaya ya Iramba haimo katika Mpango wa Ujenzi wa *VETA* Wilaya, lakini ningeomba Mheshimiwa Waziri akubali yale majengo yaliyoachwa na Kampuni ya Ujenzi wa Barabara ya CHICO. Majengo hayo tayari yamekabidhiwa kwa *WDC* ya Ulemo na tumeona haja juu ya eneo hilo kuwa Chuo cha *VETA* kijengwe mahali hapo na hasa kwa kutumia majengo hayo yaliyoachwa na Kampuni ya CHICO. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, aiingize Wilaya ya Iramba kwani hakutakuwa na gharama ya aina yoyote kuhusiana na majengo mbali na kutuletea walimu na vifaa vingine vya kufundishia na kadhalika.

Mwaka ujao wa 2009, tunategemea kuwa na *High School*s mbili; ile ya Iguguno na Lulumba. Namwomba Waziri, pindi shule hizi zitakapoanza, naomba ziwe zimekamilika kwa kila kitu, wakimwemo walimu, vifaa vya maabara na zana nyingine za kufundishia. Katika kufanya hivyo, kutakuwa ni katika kuanza na kuziimarisha shule hizi.

Walimu walioomba kufanya kazi kwa mkataba baada ya kustaafu, tafadhali maombi yao yashughulikiwe. Walimu hawa tunawahitaji Wilayani Iramba ili wasaidie upungufu uliopo nao ni Mwalimu Geofrey Pyunze; Mwalimu Nesphero Mathayo; Mwalimu Shani; na Mwalimu Kassihu Maksudi.

Mwisho, tuna matatizo ya walimu wa mchepuo wa sayansi kwenye Shule zetu za Sekondari. Tumeomba tupewe walimu, pamoja na idadi ya upungufu kwa ujumla.

**MHE. SIGIFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Shida yangu sasa ni miaka mitatu kule Ruangwa kuna Shule ya Sekondari ya Nkowe, ipo Tarafa ya Mnacho, Kata ya Nkowe, haina umeme ingawa ni 0.9 km tu kwenye nguzo pale Mpumbe. *TANESCO* wanataka walipwe Sh. 25 milioni; je, hamuwezi kuwalipa hizo hela ili umeme upatikane pale? *Headmaster* wangu, Mwalimu Nchimbi, tunalia ili tatizo hili limalizike safari hii.

Ruangwa hakuna benki, walimu hapanda malori yanayokuja Ruangwa kubeba korosho, ufuta, nyanya, vitunguu, mahindi na mazao mengine ili kwenda *NMB* Nachingwea. Hivi hatuwezi kupata angalau *landrover* ya kuwabeba hawa walimu kuwapeleka benki Nachingwea? Tafadhali sana.

Walimu waliopo Ruangwa kwani hainogi kuwapeleka kozi mbalimbali za kuwa-*promote standards* zao? Tafadhali sana.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri na Wataalam wake, kwa hotuba nzuri waliyoiandaa na kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 27 Juni, 2008 wakati wa kupitisha bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa vifungu, niliomba ufafanuzi wa Waziri juu ya uhalali wa kuhamishwa kwa Shule ya Sekondari ya Nanyanje kwenda Chikonji. Shule iliyojengwa kwa jasho kwa makubaliano ya Kata zote za Nanyanje, pamoja na Diwani wao wa CCM. Pamoja na kueleza dosari kadhaa za kuwepo Shule ya Sekondari Nanyanje na kwa ajili ya kuheshimu uamuzi wa wananchi, alitoa kauli kuwa Shule ya Nanyanje itabaki pale pale na haitahamishiwa tena Chikonji. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kutoa kauli hiyo ya msimamo.

Wananchi wa Nanyanje waliokuwa wanafuatilia majadiliano ya Bunge walifurahi sana na kuupongeza uamuzi huo wa Serikali. Pamoja na uamuzi huo mzuri, yapo maswali ambayo bado hayajapata majibu na tungependa Mheshimiwa Waziri, atupatie majibu kwa niaba ya Wanakijiji wa Nanyanje.

Shule ya Nanyanje iliingiziwa shilingi milioni 45; shilingi 7,000,000 kwa ajili ya darasa; shilingi 18,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba; na shilingi 20,000,000 kwa ajili ya maabara. Kwa nini pesa hizo zipelekwe Chikonji wakati ni za Nanyanje? Tunaomba pesa zirudishwe Nanyanje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia Bodi ya Mikopo, inatoa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwa asilimia 60, 40 na 20. Suala hili linapingwa na Watanzania wengi kwa sababu mbili kubwa; Kipato cha Mtanzania kwa mujibu wa *Tanzania Economic Survey 2006* ni kidogo sana; asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima wa jembe la mkono ambao kilimo chao hakina tija; na wanafunzi wanaosoma kwa mikopo ambayo wanapaswa kuilipia baadae wanakuwa hawana upendo wa kweli kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vyetu vinakumbwa na migomo ya mara kwa mara kutokana na hali halisi ya vyuo. Mara nyingine kwa ukosefu wa maji, ubora wa chakula na kadhalika. Cha kusikitisha, mara nyingi wanafunzi wanapogoma Serikali inawafukuza Shule, lakini baadae chuo kinakaa na kuwarudisha kuendelea na masomo. Kuwafukuza wanafunzi sio suluhisho, kwa nini Wakuu wa Vyuo wasikae na wanafunzi wakasikiliza malalamiko yao na kuyatatua badala ya kuwafukuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mikopo inalalamikiwa kwa kutoa mikopo kwa wasiohusika na kuwanyima mikopo wanaostahili. Wanafunzi wa Chuo cha Ardhi, wanaopata mkopo wa asilimia 100, wanadai kuwa mkopo wa shilingi 5,099,000 wanazopewa ni shilingi 3,185,00; ndizo zinazotolewa na Serikali kwa uhakika, zilizobaki huwa wanachangia wanafunzi wenyewe (Sh. 1,914,000), ikiwa wanaopata mkopo wa asilimia mia moja kumbe kwa uhalisia shilingi 1,914,000 ni za wanafunzi wenyewe; je, wale wanaopewa mkopo wa asilimia 20 au 40 hali iko vipi?

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya na kuweza kushiriki kikao cha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, lakini pia elimu ni ufunguo wa kila sekta katika utendaji ulio bora na wenye ufanisi katika maisha ya mwanadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuwe na Madaktari bora, Wanasheria, Mainjinia na wengineo ni lazima tuwe na elimu iliyo bora. Elimu bora inapatikana kwa kuwa na walimu bora, ambao wamekuwa *committed* katika kazi ya ualimu. Walimu bora wanapatikana kwa kuandaliwa wao wenyewe, pamoja na kuandaliwa mazingira bora ya utendaji kazi, ikiwa ni pamoja na vitendea kazi bora, kuwa na maslahi bora, motisha, makazi bora na huduma nyingine muhimu. Pia ni mihimu wapatikane walimu wa kutosha kuanzia Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na madarasa ya kutosha ni sehemu moja, lakini sehemu ya pili na muhimu zaidi ni kuwa na walimu bora wa kutosha, pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu kipya cha Dodoma kina vyuo vingine vitatu ndani yake. Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba, nyenzo muhimu za kujifunza kwa wanafunzi hao zinapatikana kwa ukamilifu na kwa uhakika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la migomo na maandamano yanayofanywa na baadhi ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu, kutokana na mikopo au kushindwa kulipia ada mbalimbali. Je, Serikali imejiandaa vipi ili kuondoa kero hii na wanafunzi waweze kusoma bila ya usumbufu wa aina yoyote, hususan wale ambao wazazi wao ni wa kipato cha chini?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa kazi ya ualimu ni kazi ya wito, lakini jambo la walimu kuwabebesha mimba wanafunzi wao ni la aibu na fedheha kubwa. Naomba hatua kali za kisheria, zichukuliwe dhidi ya walimu wanaowabebesha mimba wanafunzi mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia ya sasa ni ya utandawazi, sayansi na teknolojia. Hivyo, huu ni wakati ambao wanafunzi wanapaswa kuhamasishwa kujifunza masomo ya sanyansi kwa wingi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Wanafunzi wa kike wanapaswa kupewa kipaumbele ili waendane na wakati wa sasa, sambamba na wanafunzi wa kiume.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Sekta ya Elimu nikitaka kuuelezea nitakuwa narudia tu maelezo ya Waheshimiwa Wabunge wengi sana na wadau mbalimbali wa Sekta hii. Elimu imekuwa ni Sekta iliyo katika mjadala mpana na wa kina. Masikitiko makubwa niliyonayo ni kwamba, maneneo yamekuwa ni mengi sana kuliko vitendo katika kuchambua changamoto za Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linaloniumiza kichwa kila siku ni mwelekeo wa Taifa. Elimu ndiyo inayoelekeza ni wapi Taifa linakwenda na ni nini ajenda za Taifa. Kwa mfano, mnano miaka ya 1970 na 1980, ajenda ya Taifa ilikuwa ni kujitegemea na ukombozi. Hivyo, tulitangaza kaulimbiu zilizokuwa zinaongoza misingi ya elimu yetu;

*education for self reliance;* na *education for liberation.* Kauli mbiu hizi zilikuwa na maana kubwa sana katika kuiweka sawa jamii na matokeo yake, hivi sasa tuna Taifa moja imara na lenye upeo mkubwa wa kisiasa. Hali haitakuwa hivi katika siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu siku za nyuma, Shule za Sekondari za Serikali ndizo zilikuwa vituo vya ubora *(Centres of Excellency)*, ukitaka kupata walimu wazuri, shule zenye vitabu vya kutosha, shule zenye maabara na maktaba nzuri, unakwenda katika Shule za Sekondari za Serikali. Hivi sasa ni kinyume chake, Shule za Serikali ndio zimekuwa mbaya na hazina walimu. Walimu wa Shule za Serikali wamekata tamaa na hawafundishi vizuri wanafunzi. Mazingira ya shule yamebadilika na kuwa mabaya sana. Sehemu kubwa ya shule hizi sasa tunaziita Shule za Kata.

Kinyume na Shule za Serikali, Shule Binafsi ambazo wanasoma matajiri ni nzuri na zina walimu na mazingira bora ya kufundishia. Shule hizi zinaitwa *Academies.* Tunajenga Mataifa mawili ndani ya nchi moja; la waliosoma vizuri (matajiri) na waliosoma vibaya (maskini). Mfumo wa Elimu wa aina hii ni hatari kwa Taifa na unaligawa Taifa. Ni vyema kurekebisha hali hii kwa kuweka mazingira bora ya kusoma kwa Shule zote za Sekondari za Serikali zikiwemo Shule za Kata.

Kwa changamoto za sasa zinazolikabili Taifa letu hasa zama hizi za ushindani mkubwa ni vyema kutazama upya mfumo wa elimu. Ni vyema sasa elimu ya msingi *(universal and compulsory education)* iwe mpaka kidato cha pili. Wakati huo huo kuwe na darasa la nane, ambalo litajikita kufundisha vijana Lugha; Hesabu; na Huduma kwa Taifa *(National Service through community work and skills development).*

Hebu tujifunze mfumo wa elimu wa Ujerumani ambao ni *dual system*, kwa kuwa na shule za ufundi kama *parallel to the normal schooling* ili wale vijana wenye vipaji vya ufundi wachukue mkondo huo daima.

Kuna haja ya kuzingatia sana Taarifa ya Shirika la Hakielimu kuhusu ubora wa elimu. Serikali ikae na wadau kama Hakielimu ili kuangalia uwezekano wa kuwa na mjadala mpana kuhusu ubora wa elimu ili tuweke vigezo vya Kitaifa kuhusu *what is quality education?* Ripoti hii ya Hakielimu ya Mei, 2008 ni muhimu sana ipewe kipaumbele katika mjadala huu. Ripoti hii ina mambo mengi sana mazuri.

Napenda kujua Mamlaka ya Elimu katika Mkoa wa Kigoma imefanya nini katika miundombinu ya elimu? Ninaomba angalau wajenge bweni moja katika Shule ya Sekondari Bitale kwa ajili ya wasichana. Ninaomba sana suala hili.

Walimu wa Shule ya Msingi Bitale, Jimboni Kigoma Kaskazini, hawajapandishwa madaraja kwa muda mrefu sana. Tafadhali ninaomba mfuatilie suala hili la Walimu wa Shule Sekondari Bitale ili wapate haki yao ya kupanda madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka nikiwa Kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi nimekuwa nikijihusisha na suala la mikopo ya wanafunzi. Suala la nani anapata mkopo

ni tete sana. Napenda kufahamu hivi suala la *means testing* linashughulikiwa namna gani?

Mimi ninashauri kuwa, fomu za mikopo wawe wanapewa vijana wakiwa muhula wa pili wa Kidato cha Tano na waende nazo nyumbani wakati wa likizo ili wajaze huko na kurejesha wanaporudi muhula wa kwanza wa Kidato cha Sita. Hii itatoa muda mkubwa sana kwa Bodi kuchambua fomu na mikopo na *verification* kufanyika.

Bodi itumie *PR Companies* ili kutumia *popular means* za kufikia vijana ili waelewe suala la mikopo na taratibu zake. Nipo tayari kutoa ushauri katika hili kwani nina uzoefu wa kutosha kabisa katika eneo hili.

Nimefuatilia kwa kina sana Hotoba ya Wizara ya Elimu na kulinganisha malengo ya nchi ambayo yanaongozwa na MKUKUTA kama sehemu ya utekelezaji wa Dira 2025.

Nimelinganisha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Taarifa ya Umaskini na Maendeleo 2007, kwa masikitiko makubwa sana, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri haina ulinganisho wowote na Taarifa ya MKUKUTA. *MKUKUTA cluster II: Improvement of Quality of Life and Social well-being* ni fungu muhimu sana kwa Wizara ya Elimu kwani lengo la kufikia viashiria vya kielimu limeainishwa. Hata hivyo, taarifa hii muhimu inayotolewa na Serikali na inayotufanya kujipima kama tunafikia malengo, haionekani kuhusishwa katika Hotuba ya Waziri wa Elimu. Hivi ni lini Serikali itakuwa makini na kuwa na uratibu bora wa masuala yake? Inawezekanaje Hotuba ya Bajeti ya Elimu isizingatie taarifa ya MKUKUTA? Sasa tukifika miaka mitano ya MKUKUTA tutasemaje kuwa tumezingatia changamoto zinazoainishwa na Ripoti hii ya kila miaka miwili?

Kwa mfano, Ripoti ya Umaskini 2007 inatahadharisha tofauti kubwa iliyopo miongoni mwa mikoa, kuhusiana na *enrollment* ya watoto kwa Shule za Vidudu *(Nursery)*; is it right language? Kwa mfano, *NERs ranges from 5% to over 40%;* ina maana Dar es Salaam (5.6%), Mtwara (43.8%), Mwanza (39.5%). Hii tofauti ya kijinsia ni suala la kuangaliwa sana.

Kuna tatizo la vitabu – wingi na ugawanyaji wa vitabu hivyo. Watoto walipoulizwa katika utafiti wanasema kuwa wanachangia kitabu kimoja watoto 20. Hali hii haiwezi kuboresha elimu. Serikali inabidi kuzingatia takwimu hizi katika hotuba zake Bungeni ili Watanzania wajue, wazazi wajue na wachape vitabu wajue. Ninashauri kuwa, Serikali ijenge utamaduni wa kuzingatia Taarifa muhimu kama taarifa hii ya *PHDR* 2007 na kutoa kauli za Serikali ili kuwe na mwelekeo mmoja katika nchi. Kama tumeamua kwa DIRA 2025 na MKUKUTA ndio *instruments* za maendeleo ya nchi ni bora basi Hotuba za Mawaziri zijibu changamoto zinazotolewa na utekelezaji wa mikakati hii.

Nimesikitishwa sana na Wizara ya Elimu kutozingatia taarifa niliyoitaja *extensively* katika mchango wangu huu. Ninaomba Serikali itoe majibu kuhusiana na changamoto tatu ambazo zimetolewa na *PHDR 2007* ukurasa wa 51 ili tuanzie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la kheri.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sitaunga mkono hoja hadi niambiwe ni lini Wizara yako itapeleka Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Sumve. Suala la Mkuu wa Sekondari ya Sumve, aliyekuwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Margaret Sitta analifahamu, pamoja na ahadi hewa za kunipatia mwalimu, lakini pia suala hilo Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza analifahamu vizuri, ahadi nyingi nimeahidiwa bila utekelezaji.

Mheshimiwa Maghembe naye nimeshamweleza tatizo la Mkuu wa Sekondari ya Sumve kutokuwepo kwa zaidi ya miaka, naye aliniahidi kulitafutia ufumbuzi lakini hadi leo Shule ile ya *A level* haina Mkuu wa Sekondari, mbali na upungufu mkubwa wa walimu waliopo. Je, nini tatizo? Je, shule ile ni ya Serikali? Naomba nipate maelezo ya lini mwalimu atapatikana na jina lake nilijue leo, vinginevyo kwenye vifungu nitang'ang'ania shilingi ya Waziri.

Katika Shule za Sekondari za Wananchi za Mwagi, Bungulwa, Ngulle na Mantare nazo hazina Walimu Wakuu. Naomba nipate maelezo ya kina ni lini Serikali itapeleka walimu katika maeneo hayo?

Kama nilivyosema, nitaunga mkono pale tu nitakapoambiwa jina la mwalimu na ataenda lini *Sumve Girls.* Vinginevyo, nilisema nitasimamia kwenye vifungu, sina kawaida, ninamheshimu sana Mheshimiwa Profesa Maghembe, lakini kwenye hili naomba anielewe.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia juu ya Elimu ya Watu Wazima, hasa juu ya MUKEJA.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo wananchi wengi wanaoujua Mpango huu wa MUKEJA. Wanaufahamu Mpango huu ni Watendaji wa Elimu tu. Inaonekana hata Wataalam wasiokuwa Idara ya Elimu wengi hawaujui Mpango huu. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha, afafanue juu ya Mpango huu wa MUKEJA. Ninaamini Mpango unapojulikana unapata ushiriki mzuri wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mpango huu wa MUKEJA unaohusu wa kusoma madarasa ya Sekondari, Mipango ambao inahusu kusoma *Form I* na *II* mwaka mmoja, *Form III* na *Form IV* mwaka mmoja na *Form V* na *VI* mwaka mmoja. Inafahamika wengi wa wananchi waliokuwa hawajaendelea shule hawakufeli bali Shule za Serikali zenye *school fees* ya chini zilikuwa hazitoshi. Kwa hiyo, wanafunzi hawa waliachwa kwenda shule. Kwa bahati mbaya walishindwa kwenda shule za *private* kwa kuwa wazazi wao walikuwa maskini, hawakuwa na uwezo wa kulipia Mpango huu wa MUKEJA. Mpango huu ni mzuri, ulikuwa unatoa matumaini kwa wanaotaka kuendelea, lakini kwa mbaya *school fees* ni kubwa sana. Idara ya Elimu ya Watu Wazima Makao

Makuu, wanatoza Sh. 235,000 mwaka wa kwanza na Sh. 245,000 mwaka wa pili. Ada kubwa imewafanya vijana/watu niliowataja hapo juu, kushindwa kuendelea leo MUKEJA, ambayo ndiyo tumaini lako la kuwaendeleza, imekuwa kikwazo kwa matumaini yao kwa kuwa *school fees* ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atuambie; je, ana utaratibu gani wa kupunguza *school fees* ili wananchi hawa wasikate tamaa. Naomba Waziri atupatie majibu.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni nataka kujua kwa namna gani elimu ya juu, ambayo ni eneo la Muungano, limefinyangwa pamoja na Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Elimu ya Ufundi, kwani nashindwa kuelewa ni vipi Wizara moja ikawa inashughulikia elimu ya Muungano na pia mambo yasiyohusu Muungano?

Serikali imeanzisha Mpango wa MMEM na MMES kupanua nafasi za elimu kwa vijana wetu. MMEM imefanikiwa na vijana wengi sasa wanamaliza Shule ya msingi. Hivyo, wengi sasa wanaanza Shule za Sekondari. Baada ya miaka mitatu au minne kutakuwa na wimbi kubwa la vijana wanaomaliza masomo ya sekondari. Je, tumejiandaa vipi kukabili wimbi hili la wanafunzi katika Vyuo Vikuu tulivyonavyo? Kupanua miundombinu ya Vyuo Vikuu vilivyopo kuna kikomo. Chuo Kikuu pekee kinachoweza kudahili wanafunzi wengi ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hivi sasa Chuo hicho tayari kimedahili wanafunzi 41,000. Ili kukiwezesha Chuo Kikuu Huria kudahili wanafunzi wengi zaidi ni lazima kukiwezesha katika maeneo mawili:-

Eneo la kwanza ni uwezo wa kuwalipa *part time Lecturers* kwa uhakika na kwa wakati. Walimu hawa ambao wapo wengi chuoni, ndio wanaotunga na kusahihisha mitihani na kazi nyingine za kuelimisha wanafunzi. Kila mtu anataka kulipwa kwa kazi yake. Hivyo, ikiwa walimu hewa hawana uhakika wa malipo ya jasho lao au kama hawalipwi kwa wakati ni dhahiri watavunjika moyo wa kujituma katika kazi yao. Jambo hili ni muhimu wakati huu tukiwa tunangoja wimbi kubwa la wanafunzi watakaomaliza *Form Six* wakisukumwa na mafanikio ya MMES na kwa kweli walimu hawa wanahitajika kwa wingi zaidi kwa ajili hii.

Namna bora ya kuwalipa *part time lecturers* ni kwa kuweka malipo yao katika kasma ya misharaha *(PE)* na sio kwenye matumizi mengine ya uendeshaji *(OC).* Vyuo vyote vya nje, mfano, *University of South Africa, Zimbabwe Open university* na *Open University (UK),* wanalipa wahadhiri wao kama hawa kupitia *PE.*

Mpango tulionao hivi sasa wa kuwalipa *part time lecturers* kupitia *OC* umeletea madai ya wahadhiri hawa kwa kipindi cha miaka mitano ya Sh. 320,256,474, namna hii itasababisha kukimbiwa na wahadhari hao ambao tunawahitaji sana.

Eneo la pili la kukiwezesha Chuo Kikuu Huria kudahili wanafunzi zaidi ni kupanua vituo vya mikoa ili viweze kutoa huduma huko huko mikoani. Huduma hizo ni

pamoja na maktaba, maabara za kompyuta, kambi za kufanyia mitihani, ofisi za walimu na wafanyakazi wengine.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Manaibu Waziri wote wawili pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwanza kwa kazi ngumu, nyeti na muhimu inayofanyika na pili kwa hotuba nzuri iliyosilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa kuiomba Wizara iwe makini kuangalia maslahi ya Walimu ambayo ni mishahara na posho mbalimbali na walipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia chakula cha watoto kiangaliwe ili wapate chakula bora na cha kutosha ili kiwawezeshe kufuatilia masomo. Wapo watoto ambao wazazi wao wana uwezo wa kifedha wanaweza kujinunulia chakula cha ziada, lakini wapo wazazi ambao hawajiwezi, naomba bajeti ya chakula iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *tuition*, ni nzuri lakini mazingira yake ni mabaya kwa sababu mtu yeyote anaweza kuanzisha na kuendesha masomo hata kama hana taaluma. Nashauri Wizara iliangalie suala hili ili kama *tuition* ni lazima basi zifanyike mashuleni na viwango vya malipo vieleweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Walimu, mtu anajiuliza ni kwa nini matatizo yao hayashughulikiwi katika muda mfupi, mishahara, posho, gharama za matibabu, yote haya Mwalimu hayapati kwa wakati. Athari zake ni kubwa maana Mwalimu anapoteza muda wa kufundisha kwa kufuatilia au kunung'unikia maslahi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi huu utaratibu wa Walimu kutokuwa na chombo kimoja cha kuwahudumia, Serikali haioni kwamba kuwa ndicho chanzo cha matatizo? Kuna Wizara ya Elimu, TAMISEMI, Halmashauri za Wilaya, Chama cha Walimu, vyote hivi vinahudumia Walimu. Walimu ndilo kundi kubwa katika makundi yote ya watumishi, ni vema wakaundiwa utaratibu wa pekee wa kuwahudumia usio na mzunguko wala urasimu usio na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya awali, ni muhimu sana lakini isipotolewa kwa utaratibu na maadili yanayotakiwa, inaweza kuleta madhara. Wizara ifundishe Walimu Maalum wa kutosha kwa ajili ya shule hizo na kila Shule ya Msingi iwe na madarasa ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango yote iliyoelezwa katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii, ni mizuri sana na tunajua Waziri na Manaibu wake ni watu makini nikiamini pia kuwa hata Watendaji wote ni makini katika kazi zao, basi niwatakie kila la kheri katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii, kuipongeza Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii kwa bajeti nzuri ambayo inakidhi haja na yenye matumaini lakini pia nipongeze ni bajeti ambayo inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na jitihada ya Chuo hiki na majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja mbalimbali katika kutimiza malengo ya Serikali, Chuo hiki kilisaini Mkataba wa Ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi/Bahari sehemu ya Buyu huko Zanzibar ambapo ujenzi huo unaendelea kwa kusuasua na kwa kasi ndogo kiasi ambacho baadaye inaweza kuleta matatizo kutoka kwa Mkandarasi wa ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho anieleze kupitia Bunge hili ni kwa nini Serikali ilikataa kutoa dhamana ya mkopo wa fedha kutoka *CRDB Bank* kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo?

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi, pia naipongeza bodi hii ya mikopo kwa jinsi inavyofanya kazi zake katika mazingira magumu ya kuwapatia wanafunzi mikopo kwa fedha ambazo wahitaji ni wengi kuliko uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kumalizia na naunga mkono hoja.

**MHE. MTUTURU A. MTUTURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, zifuatazo ni kero kubwa Jimboni kwangu.

- Kuna upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu. Mahitaji ni nyumba 1,719 na zilizopo ni 476 nakisi ni nyumba 1,243. Mwaka uliopita hatukupewa fedha za ujenzi wa nyumba za Walimu.

- Upungufu wa madarasa ni mkubwa. Mahitaji ni 1,660, yaliyopo ni 885 na nakisi ni madarasa 775.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali itupatie ruzuku ili tuwahamasishe wananchi kuchangia nguvu za ujenzi wa nyumba na madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tunasisitiza ombi letu la awali, wanafunzi Walimu tuliowapeleka vyuoni wamalizapo masomo warudishwe Tunduru kwani wanayamudu mazingira ya nyumbani kwako tofauti na Walimu kutoka maeneo mengine ambao huwa waharipoti kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kwa kuwa mazingira ya Tunduru bado ni magumu, tunaiomba Serikali iendelee kutoa kipaumbele kwa wananchi wa Tunduru ili kazi ya kuondoa ujinga iwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawapongeza kwa kazi nzuri ambayo ni ngumu sana. Nawaombea kwa Mungu awape ujasiri na nguvu za kuhimili vishindo vya ugumu wa kazi mliyopewa kwa niaba ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, shule za sekondari zimeongezeka sana lakini masomo ya sayansi na hisabati hayafundishwi inavyostahili, Walimu wengi hufundisha kwa nadharia tu. *Practical* zinafanyika baada ya shule kupata *advance instruction* kutoka Baraza la Mitihani wanajadili maswali na hayo tu ndiyo yanayofundishwa kwa *practical*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wengi hata kama vifaa vipo hawawezi kufundisha, kwa sababu nao walipitia mfumo huu. Hawakufanya *practical* shuleni na mtihani waliofanya ni *alternative to practical*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza yafuatayo:-

- Kila Shule iwe na maabara;

- Wizara wapeleke fedha za vifaa vya maabara mashuleni;

- Walimu waliohitimu hivi karibuni katika kipindi cha miaka 10 wapewe *In-service Training;* na

- Mtihani wa *alternative to practical* uondolewe. Hakuna kitu kama hiki kwenye sayansi, tufundishe sayansi kama vile inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chakula cha wanafunzi. Naomba nielezwe, kwa bajeti hii ni kiasi gani kimetengwa kwa kila mwanafunzi kwa siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya Wizara, naomba Wizara iwe wazi kama Wizara ya Miundombinu, mtueleze kiasi (kwa ujumla) cha madeni. Wizara ya Miundombinu katika bajeti hii, wameeleza madeni ya Wakandarasi, wakatenga kiasi kikubwa cha bajeti walipe madeni hayo. Wizara ya elimu itueleze wana madeni kiasi gani ili sisi tuwasemee, Serikali ifike mahali wapange bajeti kubwa zaidi. Je, Wizara ina madeni kiasi gani na je yatalipwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mihula ya *O – Level* na *A- Level,* inagongana. Walimu wanaofundisha *O –level* na *A- Level*, hawaweze kupata likizo kwani hawa wakifunga hawa wanakuwa bado wanaendelea kusoma. Wakuu wa Shule ndio kabisa hawapati likizo. Naomba nielezwe ni lini mihula hii itahuishwa ili kuondoa matatizo haya yaliyo ndani ya uwezo wenu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa elimu, je, hakuna mfumo wa elimu endelevu? Kila awamu ya Serikali inakuja na mfumo wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi katika wingi huu wa Shule za Sekondari hadi 3, 7 kuna uwezekano tena wa Walimu mmoja mmoja kuendelea kuwasiliana na Wizara moja kwa moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, katika mfumo huu wa elimu, nini nafasi ya kazi ya *REO* kwa elimu ya sekondari? Mbona anaonekana hana kazi labda:-

- kutatua migogoro ya wanafunzi waliofukuzwa;

- kuteua wajumbe wa Bodi za Shule za Sekondari; na

- Ni *agent* wa Baraza la Mitihani katika Mitihani ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mpango gani na nafasi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu anaitwa Mratibu wa Elimu ya Sekondari, Ofisi yake iko kwa *DAS*, fedha zake zinapitia kwenye Shule za Sekondari iliyo karibu, hivi huyu anafanya kazi yake akishirikiana na nani, DC au Mkurugenzi wa Halmashauri? Anaratibu namna gani wakati hata baiskeli hana? Hivi hii nafasi ni ya lazima? Mimi naona inaongeza tu matumizi kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maswali yangu yajibiwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI A. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni, Serikali iliamua kuhuisha muundo wa utumishi wa Walimu kwa kupunguza ngazi katika muundo huo na kuweka mfumo wa Alfabeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mfumo huo upandishaji vyeo Walimu na urekebishaji wa madaraja yao, umekuwa tatizo sugu. Kadhalika hali hii imesababisha kero kubwa kwa Walimu wenye uzoefu tofauti kurudikwa katika cheo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alito agizo kwamba zoezi la urekebishaji wa madaraja ya Walimu lifanyike. Nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwamba baada ya kipindi cha mwaka mmoja, orodha za Walimu wanaostahili kurekebishiwa madaraja imetolewa lakini pamoja na kwamba hatua zimeanza kuchukuliwa bado kuna dosari kadhaa ambazo zimejitokeza. Miongoni mwa dosari hizo ni kwamba baadhi ya Walimu wanaostahili kurekebishiwa hawajaorodheshwa.

Aidha, kuna baadhi ya Walimu wamerekebishwa vidato badala ya madaraja. Pia pamejitokeza tatizo la Walimu wenye uzoefu na sifa zinazofanana wapewa madaraja

tofauti.  Kadhalika Walimu wengi walipandishwa madaraja hawajapewa barua zao na kadhalika. Nashauri Serikali kuchukua hatua za dhati na za haraka kuondoa dosari hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua kubwa ya kuongeza madarasa kupitia mpango wa MMEM na MMES.  Hii ni hatua ya kupongezwa.  Lakini kila jambo zuri lina kasoro zake.  Ujenzi huu wa madarasa haukuzingatia ujenzi wa nyumba za Walimu.  Matokeo ya kasoro hii, imefanya baadhi ya shule zinakuwa na Walimu wachache mno na hilo hupelekea ubora wa elimu kushuka. Naishauri Serikali kuchukua juhudi za makusudi kuongeza nyumba za Walimu ili tuwe na Walimu wa kutosha kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zetu zina uhaba mkubwa wa Walimu.  Tatizo hili linaongezeka siku hadi siku kadri shule zinavyoendelea kujengwa bila kuzingatia uwiano wa Walimu na Wanafunzi. Hali hii, inaifanya kazi ya kufundisha kuwa ngumo mno.

Ni lazima Serikali ichukue jitihada za makusudi na madhubuti kufundisha Walimu wapya na wa viwango vinavyostahili kukidhi mahitaji ya Walimu nchini. Aidha maslahi ya Walimu yaboreshwe ili kuvutia wasomi wengi kupenda kazi ya Ualimu lakini pia wale waliopo kazini waendelee kufanya kazi hiyo kwa moyo mkunjufu.

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa watumishi hususan Walimu inaleta balaa/kasheshe badala ya unafuu wa maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabenki, taasisi rasmi za fedha na taasisi zisizo rasmi za fedha/za MIKOBA nyingi zimejitokeza kuwakopesha Walimu kwa riba mpaka 50%. Taasisi hizi zimewaingiza Walimu na watumishi wengine "mjini" kwa kushirikiana na waajiri wao kuingia kwenye mikataba mibaya ya mikopo.  Wanakopa kwa kurubuniwa na kujikuta wanakopa kila taasisi ya fedha. Matokeo yake ni kwamba hawana kitu kwenye *payroll*.  Walimu wanapokwenda benki mwisho wa mwezi wanakuta hawana kitu kwa sababu mshahara wote umekwatwa kulipia ku-*service* mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zisizo rasmi za fedha zimeshirikiana na waajiri kuwakomoa Walimu na watumishi wengine, zimewahadaa.  Mikopo inatolewa ndani ya masaa 24 na mikataba ya haraka haraka! SACCOS nazo! Walimu hawapewi mafunzo ya *"cash management"* matokeo yake wame- *mismanage* mikopo hiyo.  Matokeo yake:-

1. Walimu wamelemewa na mzigo wa madeni ya taasisi za fedha na SACCOS;

2. Wameshindwa kupata ahueni ya maisha;

3. Muda mwingi hawafundishi wanazunguka kujitafutia riziki kwa njia zingine, hawana uhakika wa maisha, wamekuwa kama kuku wa kienyeji katika kujitafutia riziki;

4. Muda mwingi pia hutumia kujificha kuwakwepa wale wadai/waliowakopesha ili kuepuka kufilisiwa vifaa vyao/mali zao na pia hukwepa hufikishwa Mahakamani; na

5. Kwa sababu hiyo, waathirika wakubwa ni wanafunzi wao ambao muda mwingi hawafundishwi ipasavyo, hivyo hakuna elimu bora hapo. Hatutakuwa na wanafunzi walioandaliwa vema kwenda *Standard V* wala *STD.VII* na *Form II* wala *Form IV* pia *Form VI* na Chuo Kikuu. Hii ni *vision cycle.* Elimu yetu inakuwa duni tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

1. Naiomba Serikali inunue mikopo/madeni yote ya Walimu ili wafutiwe mikopo hiyo waanze upya kwenye *payroll* zao. Si jambo geni kwa Serikali kufuta madeni ya Mashirika/Taasisi za Umma pale yaliposhindwa kulipia gharama za uendeshaji au yalipofilisika. Serikali izilipe taasisi hizo za fedha zilizokopesha Walimu;

2. Mikopo waliyokopa Walimu, mingi wametumia kujinunuliwa vifaa muhimu *TV, Fridge, Cookers,* Baiskeli na kadhalika, vifaa hivi si anasa ni vifaa muhimu kwa maisha bora. Mikopo hiyo ifutwe Walimu wapewe motisha;

3. Walimu hawa wasipofutiwa madeni yatawachukua hadi miaka mitatu wakikatwa, itafika mpaka mwaka 2010 wakati wa uchaguzi na ndiyo wengi watakuwa wasimamizi wa kura. Hasira zao zitaelekezwa kwa Serikali zaidi kwa kuwaandalia mikataba mibovu ya mikopo; na

4. Serikali iwaandae upya Walimu wakati wa kuwapa mikopo na kuwafundisha *"cash management"*. Taasisi *bogus* za fedha zifungiwe, zisikopeshe.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara wakiwemo Wahadhiri, Walimu na Wanazuoni mbalimbali. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

(1) Serikali iwapeleke watoto Maalbino walioko Kanda ya Ziwa wanaouwawa ovyo kwenye Shule za Msingi au Sekondari za *boarding* vinginevyo watakwisha;

(2) Ujenzi wa Shule zote zizingatie mahitaji ya walemavu;

(3) Msingi wa elimu yoyote ni elimu ya awali. Sasa hivi ni asilimia 8.3% tu ya wanafunzi hupitia shule za awali, asilimia hii iongezwe haraka;

(4) Malengo ya elimu hayaendani na fedha inayotengwa kibajeti na Serikali. "Ukitaka kula nguruwe chagua aliyenona". Maadamu tumejiwekea malengo, basi

tuyatengee fedha ya kutosha vinginevyo tuyapunguze malengo hayo ili yaendane na hali halisi ya fedha/bajeti;

(5) Wanafunzi wanaofaulu kwenda *high schools* lakini wanakosa nafasi, waundiwe utaratibu maalum wa mpito wa kwenda moja kwa moja Chuo Kikuu lakini waongezewe muda wa mwaka mmoja zaidi kuliko wale wanaomaliza *form six;*

(6) Upanuzi mkubwa na wa haraka wa elimu ya juu nchini, umesababisha changamoto kubwa ya upungufu wa Wahadhiri, mishahara iongezwe kwa kiwango cha kutosha ili ku-*attract Recturers* walio nje ya uhadhiri, ndani na nje ya nchi waweze kuwa *re-attracted back into lecturing* badala ya kuajiri *expatriates*.

(7) Ujenzi wa maabara kwenye Sekondari za Kata, iwe kipaumbele na namba 1 katika bajeti mbili zijazo. Masomo ya sanyansi bila *pacticals* ni "bora elimu"

(8) Serikali ihamasishe sekta binafsi kwa kutoa motisha *say* kupunguza ushuru kwa vifaa vya ujenzi kwa wananchi watakaojenga *hostels* na nyumba za kuishi Walimu katika maeneo maalum yatakayobainishwa na Serikali *(Local Government or Central Government)* yaliyo karibu na Shule zetu, hasa za Kata nchini kote, Serikali haiwezi kufanya kila kitu yenyewe. Wizara (Serikali) iangalie haraka uwezekano wa *Private – Public partnership*. Kama ambavyo NSSF (private sekta), inavyojenga mabweni katika Vyuo Vikuu, watu binafsi pia (NSSF binafsi) wahamasishwe kujenga mabweni kwenye Sekondari zetu ili Walimu wanaopangiwa kwenda huko wahamasike kukaa huko.

(9) Nawapongeza Wizara kwa chapisho zuri sana la "*Basic Education Statistics in Tanzania (BEST)", keep this up* na liunganishe *(include)* sasa elimu ya juu.

(10) Uhakiki wa vyeti feki, hasa degree *(1st ,2nd 3rd degree)*, umefikia wapi? Kuna *free riders* wengi sana nchini wanaoneemeka na vyeti feki, tujifunze toka Uganda (Bunge la Uganda) ambako wamechukua hatua madhubuti, kwa nini Serikali ina kigugumizi kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa, nianze kwa kumpongeza Waziri, Manaibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizarani kwa hotuba mliyotusomea leo licha ya changamoto nyingi zinazowakabili, hongereni sana na Mwenyezi Mungu awaongoze vema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hotuba kuwa na yale yote tunayotarajia au ya vipaumbele hapa nitachangia katika maeneo machache tu. Nianze kwa maswali ambayo nitahitaji majibu yake wakati wa kuhitimisha hotuba hii.

(i) Je, zile dola kumi ($10) kwa mtoto wa shule ya msingi bado zipo? Kama zipo kuna haja ya kutolewa ufafanuzi wake kwani kuna malalamiko mengi juu yake; na

(ii) Ni kwa nini ule utaratibu wa kupeleka vitabu kwenye shule mbalimbali umevurugika sana kiasi kwamba sasa kuna kila aina ya *publishement* na utaratibu mzima wa ununuzi wa vitabu sio mzuri, unalalamikiwa sana. Ninaomba maelekezo yatolewe na kusisitiza utaratibu ufutatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo au ushauri.

(i) Ninapendekeza Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kizidi kuwekewe msisitizo kwani hivi sasa idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika ni kubwa sana;

(ii) Ninashauri ufanyike utaratibu wa kukusanya watoto wote walioko mitaani ili waweze kupatiwa elimu kwa kuwa idadi yao inaongezeka sana ambapo ni matatizo makubwa sana hapo baadaye;

(iii) Msisitizo mkubwa sana kwenye masomo ya sayansi ni muhimu sasa kuanzia Shule za Msingi hadi Vyuoni pasipo kusahau Elimu ya Ufundi *(Technical Schools)* pia wale wanafunzi watakaoonyesha nia ya kuendelea na masomo ya Sayansi, ni vema wakasaidiwa zaidi hususan wasichana; na

(iv) Kuwepo na chombo kimoja tu cha kuwahudumia Walimu badala ya utaratibu uliopo hivi sasa ambapo ni mvurugano mtupu! Je, uanzishwaji wa hiki chombo umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu na Katibu Mkuu, kwa kuwasilisha taarifa hii na hoja hii muhimu kwa umakini wa hali ya juu na kuwa wazi katika kuonyesha hali halisi ya elimu na matatizo yake na njia muafaka ya jinsi ya kuyatekeleza mambo yenye utata. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza, nashauri kuwa Wizara hii kwa ujumla isimamiwe kwa kila hali na Wizara yenyewe moja kwa moja. Suala la kuziachia Halmashauri bila ya mkono wa Wizara na utaalamu wake, kuna hatari tukadhani elimu inaboreka wakati inaporomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya ya utangulizi, napenda sasa nieleze yanayotusibu Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni tatizo la kukosa Walimu katika Mkoa kwa kisingizio cha mazingira ya umbali wa Mkoa wetu. Jitihada za Mkoa kutoa motisha kwa kutumia nguvu zetu wenyewe na kuwachangisha wananchi, Wabunge na wakulima ili kutoa motisha, imeanza kuwa ni kero. Wangependa kujua maelekezo ya Rais kutaka Mikoa ya pembezoni ipewe kila aina ya msaada ikiwa ni pamoja na kuwapa motisha ili wazifanye kazi zao vizuri, yameishia wapi? Hivi nini kimetokea kwa Wizara kushindwa

kuunga mkono jitihada za Mkoa katika suala hili? Hivi Wizara inataka tuje na hoja binafsi kuitaka Wizara mbalimbali zisimamie vizuri maagizo ya Rais? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwa na Chuo cha Ufundi Makao Makuu ya Mkoa hatuwezi kulikwepa. Tunashukuru kwa Chuo cha Ufundi – Mpanda ambacho kinatarajia kuifanya kazi hii, lakini mlundikano wa vijana ambao wangefaidika ikiwa ni pamoja na mafunzo ya jioni, ni kuimarisha chuo kilichopo mjini Sumbawanga ambacho kinaendeshwa na Wamisionari wa Katoliki – Katandala. Wakipewa misaada ya kupanua hosteli yao, vifaa vya ufundi na Walimu, wangeweza kuifanya kazi vizuri wakati Serikali inaendelea kujenga vyuo hivi kwa kila Wilaya, kama Ilani inavyoagiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu hii ya pili ya kuendeleza ujenzi wa Shule za Sekondari, nashauri kuanzia sasa mkazo uwe ni kujenga maabara na maktaba ili lengo la nchi yetu kwenda sambamba na azma ya kuingia katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia itimie. Hivyo Walimu wa Sayansi waandaliwe wengi ili waweze kukidhi malengo ya mellenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine namwomba Mheshimiwa Waziri afafanue juu ya matatizo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu juu ya haya yafuatayo:-

1. Wanafunzi wanaonyimwa vyeti vya kuhitimu kwa kushindwa kumaliza madai yao. Kwa nini kusiwe na mikataba kwa wale wasio na uwezo ili wazilipe baada ya kupata ajira?

2. Pili wanafunzi wanaendelea na masomo lakini wanalazimika wasirudi chuoni mpaka walipe madeni yao je, kwa nini ufuatiliaji wa ukweli wa madai haya usifanywe ili kubaini wanaodanganya hawana uwezo wakati wazazi au ndugu wa karibu wanajiweza?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi nini mwisho wa migogoro hii ya wanafunzi wa vyuo vyetu na migogoro ya hata shule zetu za sekondari? Kero hizi tusikubali kuzilea. Tuzidhibiti mapema ili tupunguze madhara ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napongeza jitihada zinazofanywa na Bodi ya Mikopo kwa jinsi wanavyopambana na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matatizo ya uendelezaji wa mfuko huu muhimu kwa maendeleo ya elimu kwa vijana wetu

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2005 – 2010, sehemu (a), ukurasa 64, Serikali imelenga kuimarisha mipango ya elimu ya watu wazima yenye manufaa pamoja na mafunzo ya fani mbalimbali za stadi za kazi mijini na vijijini katika maeneo ya kilimo, biashara, ufugaji, utunzaji wa vitabu n.k. Serikali imeazimia kufanya na kuongoza shughuli hizi za kutoa elimu na maarifa ya kazi kwa wananchi kwa kushirikiana na

mashirika yasiyo ya kiserikali chini ya Sera ya Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Je, ni kwa kiasi gani azma hii imetekelezwa na Serikali na maeneo gani yaliyofanikiwa zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Jimbo letu la Kigamboni, tuna matatizo ya upungufu wa Walimu wa Shule za Sekondari. Naomba Wizara ifuatilie tatizo hili na kulimaliza.

Vilevile kutokana na ufinyu wa fedha katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, pia tunakabiliwa na tatizo la uwezo wa kujenga nyumba za Walimu. Jambo hili ni muhimu sana hasa ukizingatia mazingira ya eneo lenyewe. Wizara haina budi kusaidia Halmashauri kukamilisha ujenzi wa nyumba za Walimu na maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, elimu ya Ualimu, naelewa kwamba hili ni jambo muhimu kwa Wizara ili kuinua vipaji vya Walimu. Je, mafunzo haya Wizara imeyapa kipaumbele kwa upana gain?

Aidha Kiswahili hivi sasa kinakua sana kwa maana ya kusambaa sehemu nyingi nje ya nchi na kutumika katika Taasisi muhimu duniani. Ni zipi juhudi za Wizara zinachochukuliwa katika kukuza Kiswahili Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hatua za kuona kwamba Vyuo Vikuu Vishiriki viwili vya elimu vya Mkwawa, na Changombe kuanzishwa zimechukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, idadi ya Walimu Tarajali wa lugha ya Kiswahili imeongezwa kwa kiasi gani kwa lengo la kukidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma na kasi yake ya maendeleo ya chuo hicho imeonekana. Nashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kwenda sambamba na ujenzi wa nyumba za Walimu wa chuo hicho kwani gharama za ujenzi zinapanda sana na pia ni suala muhimu kumwezesha Mkufunzi kufanya kazi kwa utulivu. Angalieni njia ya kupata mfadhili wa kusaidia hili, tuhangaike zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Jimbo la Kigamboni, ni mji mpya wa Jiji la Dar es Salaam. Muda mfupi ujao kutokana na mipango ya Serikali juu ya uendelezaji wa mji mpya wa Kigamboni, idadi ya watu inazidi sana. Hivyo, kwa umuhimu sana, naiomba Wizara ya Eimu kuweka mkakati wa kujenga Chuo cha ziada kutoa elimu ya mafunzo ya ufundi Stadi na VETA kuuwezesha uma huo kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAIDI AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashawishika kuamini kwamba elimu katika nchi yetu inakwenda mrama. Pia nashawishika kusema kwamba ni lazima sasa tuwe na mjadala wa kitaifa kuhusu suala la ubora wa elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nashawishika kuamini, ni pale wasomi wa nchi hii walipolalamika, nilisikia kipindi katika luninga ambacho kilijadili suala hili la elimu akiwemo Profesa Shivji na wenzake, walinigusa sana hasa pale walipojadili ubora wa elimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na upungufu uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati chuo kinajengwa kilikuwa iimeandaliwa kwa idadi maalumu ya wanachuo kwa mfano maktaba ni kwa ajili ya wanachuo 3,000 leo wapo wanachuo zaidi ya 12,000. *Seminar rooms* zilizopo ziliandaliwa kwa ajili ya wanachuo 20/25 leo wanatumia wanachuo 70 hadi 100. Kuanzishwa kwa Vyuo \vikuu vingi kwa wakati mmoja ikama ya wakufunzi haitimiliki katika kila chuo kwa maana ya uwiano wa Mkufunzi na Wanachuo. Hawa ndio wasomo wanavyoona na mashaka waliyonayo kuhusu ubora wa elimu na kushauri uwepo mjadala wa kitaifa, mimi naamini ipo haja hiyo ya kuwepo mjadala huo kwa mustakabali wa nchi yetu na kizazi chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya mipango mibovu ya elimu na utoaji wa Walimu isiyokidhi viwango na ubora, hauwezi kuziona athari zake mara moja au wakati ule ule lakini athari zake ni kwa baadaye ambazo zinaweza kuliangamiza Taifa kwa kutokuwa na wasomi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo pia matatizo katika Vyuo vya Ardhi na Tumaini Iringa kutokana na Bodi ya Mikopo kutopeleka fedha katika vyuo hivyo kwa wanafunzi waliopata sifa za kupata mikopo hiyo na wanaoadhibiwa sasa ni wanachuo. Bodi na Serikali hamjawatendea haki wanachuo hao kwa kuwaadhibu kwa namna yoyote ile maadamu tayari maombi yao ya kupata mikopo yalikuwa yamekubaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vyuo hivyo hivyo ya elimu ya juu, Chuo Kikuu Huria *(OUT),* kinafanya kazi vizuri, kimejitangaza, watu wamekuwa na ari ya kujiendeleza na idadi ya waliojiunga na masomo mabalimbali imeongezeka pia. Lakini yapo malalamiko katika Kitivo cha Sanaa za Jamii *(Faculty of Art and Social Sciences)* ya kutopata/kutoonekana matokeo ya mitihani au kazi za majaribio *(assignment)* na kuwapa usumbufu watahiniwa na kuwaongezea gharama. Kama ni upungufu katika utunzaji wa nyaraka au uchache wa Wakufunzi na idadi ya Watahiniwa, naomba tatizo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni sehemu tu ya matatizo ya elimu ya juu, huku chini kwa maana ya sekondari na elimu ya msingi, ndio hayasemeki. Lakini yanafanana kama ya elimu ya juu, idadi ya wanafunzi imeongezeka mara dufu pamoja na jitihada zinazofanywa za kupunguza tatizo la upungufu wa Walimu katika shule za msingi na Sekondari lakini bado tatizo lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo ni namna gani tunaweza kupata Walimu bora na siyo bora Walimu? Kupunguza muda wa mafunzo ya Ualimu ili kuondoa tatizo la Walimu, ni kujihadaa na kupunguza ubora wa elimu. Elimu bora itapatikana tu pale tutakapokuwa na Walimu ambao wamepata mafunzo timilifu na ya muda mrefu kama ilivyokuwa kwa wale Walimu ambao wamefundisha viongozi wa leo waliopo madarakani ni kwa sababu Walimu waliowafundisha walipata mafunzo stahiki. Haiwezekani kumpata Mwalimu wa siku 22 kwa maana ya mafunzo ya mwezi mmoja,

siku nane za mapumziko na kama itakuwepo sikukuu ya Taifa maana yake siku za kumuandaa Mwalimu zinapungua. Hakuna njia ya mkato ya kumpata Mwalimu bora kwa mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo Mwalimu anaandaliwa katika mazingira gain wakati vyuo vyetu takriban vyote vipo katika hali mbaya? Mazingira, vitendea kazi, vifaa, chakula, mafao ya Wakufunzi, idadi ya Wakufunzi, ni dosari kubwa. Kama Wizara haitawekeza katika Vyuo vya Ualimu na kuondoa dosari zilizopo, hatua zinazochukuliwa za kuongeza idadi ya wanafunzi bila ya kuwepo ongezeko la Walimu bora, ubora ya elimu yetu itakuwa mashakani, pia ni lazima sasa wanachuo walipwe ipasavyo na hasa wakati wakiwa mafunzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpata Mwalimu bora, zipo nyumba za kutosha kwa Walimu? Je, Walimu wanalipwa vizuri na kwa wakati bila usumbufu na mafao mengineyo yanalipwa kama inavyostahiki na bila usumbufu?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, motisha kwa Walimu wa vijijini na maeneo ya pembezoni na mazingira magumu wanalipwa kama Serikali ilivyoahidi kuwapa motisha Walimu hao ambao wanafanyakazi kwa upendo na matumaini? Je, mgawanyo wa Walimu unazingatia mahitaji halisi ya kila shule nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzingatia haya, sasa tunapima vipi ufundishaji wa Walimu hao ni kwa kuwepo na mitihani *(tests/examinations)* kwa maana majaribio na mitihani ndio njia ya kupima uelewa wa wanafunzi na kutimiza wajibu kwa Walimu kufundisha kwa maana kama ufaulu ni mzuri basi Walimu wanatimiza wajibu wao, kama ufaulu mbaya basi lipo tatizo na tupate ufumbuzi wa tatizo hilo. Hivyo basi, suala la mitihani kama ni kipimo lazima iendelee ili kuweza kuchuja, tuachane na maamuzi ya kisasa yasiyo na utafiti, baada tu ya kuambiwa mdondoko wa wanafunzi *(dropouts)* ni kwa ajili ya mitihani basi unaamua kufuta mitihani. Haiwezekani! *Dropouts* zina sababu zake nyingi, tujitazame, tujisahihishe badala ya kufanya maamuzi ya pupa na kufurahisha viongozi wanaotoa maagizo. Wapeni taarifa sahihi viongozi ili watoe maamuzi sahihi, msiwadanyange.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza wananchi wote nchini kwa jinsi walivyojitoa kwa kujenga shule za msingi na Serikali ambapo ulikuwa ni wajibu wa Serikali kujenga shule hizo. Hivyo basi, Serikali sasa ni lazima isaidie jitihada hizi za wananchi kwa kukamilisha na kujenga nyumba za Walimu na maabara na kupeleka Walimu wa kutosha katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo pekee hayatoshi pia kuwepo vitabu vya kutosha vya kujifunzia na kufundishia na ziada. Pia vifaa vya maabara kwa shule za sekondari zote nchini. Ugawaji wa upendeleo usio na usawa ni hatari kwa Taifa letu maana baadhi ya watoto katika maeneo fulani nchini wanapata mafunzo kwa nadharia na vitendo na wengine hawapati, huu ni ubaguzi katika utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila ninapochangia Wizara hii, narudia na kurudia kuiomba Serikali, mzigo kwa wananchi hawa maskini ambao kila mwaka wanapewa agizo la kuchangia mradi mpya uliobuniwa na Serikali, wameelemewa na kushindwa kukamilisha miradi ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa MMEM, kabla haujakamilika tukaanza MMES, nasikia sasa upo mpango wa MMAM (Kujenga Zahanati/vituo vya Afya). Sasa zipo shule za msingi ambazo hadi sasa hazijakamilika na zina upungufu wa madarasa, madawati na msongamano wa wanafunzi. Naiomba Serikali isaidie juhudi hizi na kuzifanya shule hizi kuwa shule kwa ukamilifu ili watoto wanaosoma katika shule hizi wapate haki sawa na wenzao ambao shule zao zina madarasa ya kutosha, madawati vitabu na Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kupongeza juhudi za Wizara kwa kuona tatizo la uhaba wa Walimu wa Sekondari na kuajiri Walimu wa mkataba. Lakini tatizo la upungufu wa Walimu wa Sekondari pia lipo kwa shule za msingi, kwa nini Wizara haichukui hatua hii kwa shule za msingi pia? Wapo Walimu wazuri waliopata mafunzo timilifu na uwezo wa kufundisha bado wanao, tuwatumie. Naiomba sana Wizara kulitafakari suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba tena Wizara na taasisi zake pia Hazina kuharakisha kuwalipa mafao yao Walimu wanaostaafu na malipo ya mirathi kwa warithi wa Walimu ambao wamefariki ni usumbufu na adha kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yenu yote, kwa hotuba safi na fasaha na pia kwa kazi nzuri ya kuleta mageuzi ya elimu hasa ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mafanikio yoyote hayakosi matatizo. Tatizo kubwa mojawapo ni upungufu wa Walimu, vifaa na hata maabara na mabweni hasa nikizingatia kwamba bajeti hi ndogo sana ukilinganishana mahitaji yanayoendelea kupanuka.

Wizara imeeleza changamoto mbalimbali na malengo juu ya namna ya kukabiliana nazo. Hata hivyo, ninachoweza kufanya chini ya utaratibu tuliojiwekea, ni kuunga mkono kile kidogo kilichopatikana na inategemewa kwamba pengine mwakani hali itaruhusu nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu pamoja na hayo, yapo matatizo *local* ambayo ninaomba Wizara iyashughulikie:-

(a) Hadi tarehe 30/6/2008, Wazabuni wanaolisha Sekondari za Wilayani kwangu walikuwa wanadai Sh.320m/=. Nashauri jitihada zaidi zifanyike kabla hawajatugomea na kuleta matatizo zaidi;

(b) Nashauri fedha toka Wizarani ziwe zinapelekwa Halmashauri badala ya Wakuu wa Shule za Sekondari. Mfano Wizara ilipeleka Sh.14m/= Kalenga Sekondari toka Desemba na hazijatumika na hata usalama wake hatuujui;

(c) Nashauri kila Mkoa uwe na Wakaguzi wa Elimu na wale wa Ujenzi ili kusiwe na hali ya ovyo ya Mikoa mingine kama Iringa kuombaomba huduma hizo toka Mikoa mingine. Kwa hiyo, utaratibu uliopo wa kanda siyo mzuri;

(d) Mheshimiwa Waziri, nilikudokezea tatizo la uhafifi wa uongozi wa Sekondari ya Kalenga ambao unapelekea kushuka kwa taaluma na pia mlipuko wa fujo kila mara. Nashauri hatua zifaazo zichukuliwe; na

(e) Upungufu wa Walimu ngazi ya elimu ya msingi na wa sekondari unatisha. Lakini hili tatizo ni la nchi nzima. Niombe tu Wizara itusaidie Iringa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, baada ya kusema haya, naomba niunge mkono hoja hii, nakutakia kila la kheri, hoja ipite salama.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri, Manaibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa maandalizi mazuri ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za ufafanuzi na majibu. Katika ukurasa wa 68 wa Hotuba ya Waziri, unaelekeza Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), kuandaa rasimu ya mfumo wa Tuzo zitakazotambulika kitaifa *(National Qualification Framework).* Mfumo huu ni unazingatia mambo yafuatayo.

*Qualification,* kutambulika Kitaifa na Kimataifa yaani *Credibility*, *qualification* kulenga mahitaji ya nchi yaani Vision 2025 yaani *qualification relevance, qualification* kuweza au kumruhusu mhusika kuendelea na ngazi ya masomo inayofuata yaani *progression*, mfumo kuruhusu *flexibility, acces*, *legitimacy recognition of prior learning* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyotajwa hapo juu, yanadhihirisha umuhimu wa wadau wengi kushiriki kwenye maandalizi ya *N.Q.F.*

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali ni kama yafuatayo:-

(1) Waziri aeleze muundo wa Kamati inayoandaa *NQF* ili kujionea ni namna gani Kamati hii imeshirikisha sekta za ufundi, afya na kadhalika;

(2) Kwa nini kazi hii wamepewa *TCU* na wala sio NACTE?; na

(3) Kwa nini Elimu ya Ufundi haipewi Kipaumbele na Wizara? Mfano *enrollment* ya vyuo haiongezeki lakini mahitaji ya mafundi ni makubwa sana na maendeleo ya nchi yoyote yanategemea sana sekta hii ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 103, Jedwali la Vyuo vya Ufundi VETA, Wilaya ya Makete imeathirika sana na janga la UKIMWI, ina zaidi ya watoto yatima 13,000. Njia pekee ya kuwasaidia wananchi hawa ni kuwawezesha kielimu hasa vyuo vya Ufundi *(VETA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali ni kama yafuatayo:-

(1) Kwa nini Wizara haikutoa upendeleo kwa Makete kupewa Chuo cha *VETA*?;

(2) Kwa nini Serikali/Wizara inapeleka vyuo zaidi ya Kimoja Mkoa mmoja wakati mikoa mingine haina kabisa kama Iringa?; na

(3) Tunaomba jedwali lirekebishwe ili Makete ipate chuo cha *VETA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nawasilisha.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uangaliwe uwezekano wa kurudisha shuleni watoto wa kike waliopata mimba kuendelea na masomo baada ya kujifungua ili kuokoa wasichana wanaopoteza nafasi za kuendelea na masomo. Cha kusikitisha zaidi ni kwamba mara nyingi wanaopata mimba huwa wenye uwezo mkubwa darasani. Tuwaendeleze watoto wa kike kwa manufaa ya Taifa letu. Kumwendeleza mwanamke ni kuendeleza familia na Taifa kwa ujumla.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa afya na kunipa uwezo wa kuchangia hotuba hii kwa kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kuleta hotuba nzuri yenye uchambuzi mzuri na yenye kuleta matumaini mema na iliyojalia Ilani ya Uchaguzi wa CCM 2005 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri imejitosheleza, nina mchango mdogo unaohusu Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Katibu wa Baraza na timu yake nzima kwa kazi nzuri na ngumu wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwamba mitihani yote ya Kitaifa inaendeshwa kwa amani na utulivu bila ya uvujaji na pia kunapobainika matukio machache ya udanganyifu wa sheria na kanuni inachukua hatua kwa wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za kinidhamu zinazochukuliwa, ni pamoja na kumfutia matokeo Mtahiniwa na kumzuilia kutofanya mtihani kwa muda wa miaka miwili (2). Hii adhabu ya pili mimi kwa maoni yangu naomba iondoshwe. Kwani kufanya hivyo, ni kumdumaza mwanafunzi ambaye kwa namna moja imesababishwa na yule aliyempatia majibu ya mtihani huo. Kwa hiyo, adhabu kali apewe aliyemsababishia mwanafunzi huyo udanganyifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Baraza wawe makini na uchunguzi wao wa kubaini udanganyifu ili wasije wakawaonea wengine wasiohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninataka kujua ni njia gani wanatumia kufahamu waliofanya udanganyifu. Mheshimiwa Waziri angenielimisha wakati wa kujibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu mdogo, naunga mkono hoja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi kumshukuru Mungu kwa kuwa ametujalia uzima.

Pili nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu, Manaibu Waziri wote pamoja na wataalamu wote kwa ujumla kwa kuweza kuandaa hotuba hii nzuri ambayo imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Tunakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa sera zake madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la wanafunzi wa kike wanaopata mimba wakiwa shuleni. Tatizo hili limekuwa kubwa kiasi kwamba lisipotafutiwa ufumbuzi ni tutaweza kuja kuwa na idadi kubwa ya watoto wengi wa mtaani. Watoto wengi wanaopata mamba, ni wale ambao wazazi wao ni watu wa kawaida na wengine hawana kitu kabisa. Utakuta familia pale nyumbani, nina watu jumla ya 10, huyo naye anaongeza wa kumi na mmoja. Kwa kuwa kipato cha familia hiyo hakitoshi, ananyanyaswa na baadaye anaweza ukamkuta yule binti na mtoto wake mgongoni akiombaomba huko mitaani pia baada ya muda anapata mimba nyingine kwa hiyo maisha yake yote yanaishia mtaani mama ni wa mtaani na watoto pia ni wa mtaani. Kwa hiyo, Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa watoto wanapopata mimba hawarudishwi nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwepo na Shule Maalum (bweni), kwa wale wanafunzi wanaopata mimba shuleni wakishajifungua waendelee na masomo kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia wanafunzi chakula wakiwa shuleni. Tokea enzi za Mkoloni tulikuwa tunapewa uji mchana, tumehamasisha wananchi kujenga madarasa lakini ni wajibu wetu kuweka utaratibu wa watoto kupewa chakula wakiwa shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ubakaji kwa watoto kuanzia miaka 7 – 9, naomba Serikali iongeze adhabu kwa wale Walimu wanaowabaka wanafunzi. Tatizo hili limekithiri hasa Mkoa wa Manyara. Walimu wana tabia mbaya ya kuwadanganya wanafunzi kwa pipi na kuwapa madaftari kalamu na hatimaye huwafanyia watoto vitendo viovu hasa madarasa ya MEMKWA. Mwalimu huyo alikamatwa na kupelekwa kituo cha Polisi Mererani lakini baadaye aliachiliwa eti hakuna ushahidi. Watoto wenyewe waliofanywa vitendo hivyo ndio mashahidi/lakini eti hakuna ushahidi. Naomba Wizara ifuatilie kuona kwamba Walimu kama hawa wanachukuliwa hatua za kisheria na hatimaye kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nianze kuchangia hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya ili kutatua matatizo ya elimu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kwamba ni vema kurejesha ule mfumo wa mitihani katika darasa la nne, la saba na la kumi ili kutoa vijana ambao ni *"gualified"* kwani mtoto anapojua kwamba hakuna mtihani unaomkabili basi hachukui juhudi ya kusoma kwani anajua anakwenda mpaka kufikia *Form IV* matokeo yake tunapoajiri, tuaajiri watu ambao sio *"competent"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndio msingi wa maisha na kwa maana hiyo sekta zote, Wizara zote na shughuli zote zinategemea elimu hivyo lazima msingi wa elimu uwe mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tupate Taifa lililo bora kwa kila hali lazima tupate Walimu wenye uwezo, wanaowezeshwa vizuri ili wakidhi mahitaji yao ya kufanya kazi kwa kuipenda kazi yake. Mwalimu wa Tanzania anafanya kazi katika mazingira magumu. Hivyo, naomba tuhakikishe Serikali inawapatia Walimu nyumba za kuishi, mishahara inayoridhisha kulingana na ukali wa maisha na mishahara ipatikane kwa wakati unaostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa shule nyingi ni jambo la busara, lakini shule isiyokuwa na Walimu wa kutosha, vitabu vya kusomea, madawati na vitendea kazi vyote, bado hatujatatua tatizo la elimu Tanzania. Leo hii tunazungumzia kuungana na wenzetu ambao kiwango chao cha elimu kiko juu, je, Watanzania katika ushindani wa soko la ajira kwa elimu hii tunayotoa tutakuwa na nafasi gain?

Mheshimiwa Naibu Spika, sekondari zetu zina uhaba wa maabara, vifaa muhimu vya kufundishia, naomba sana mwaka wa fedha ujao bajeti ya Wizara hii iangaliwe upya

kwani hali ya elimu Tanzania ni mbaya sana, kuiboresha elimu ni kuboresha mfumo wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nimalizie kwa kusema tuwatunze Walimu kwani ndio wazalishaji wa watumishi wa Wizari zote. Tuwatunze hasa tukizingatia kwamba kazi hii ya Ualimu tafsiri yake ni hii ambayo nataka niitoe:-

U - Usumbufu (lazima Mwalimu ajitume muda wote).

A - Adha (lazima atafute ukweli wa analotaka kulifundisha).

L - Lawama (mwanafunzi akifeli, lawama kwake na wanaopata mimba pia lawama kwake).

I - Inda, Ikrani (Kila jina baya hupewa mwalimu au jina la Utani pengine kwa sauti yake, kivazi chake ama topic anayoifundisha tu).

M - Mahangaiko (Kuhangaika kutafuta vielelezo na kujiandaa kwa somo la kesho kila siku).

U - Umuhimu (uwe mvumilivu kwani kuwako watoto 50 na kuendelea kwa wakati mmoja ni kazi inayohitaji uvumilivu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ijipange upya.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Profesa J. Maghembe, Waziri wa Elimu, Manaibu wake Mheshimiwa G. Kabaka na Mheshimiwa M. Mahiza, Katibu mkuu, Naibu katibu Mkuu, Wakurugenzi, Makamu wa Wakuu wa Vyuo Vikuu, Walimu na Maafisa wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya ingawa katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, nachangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuhusu madaraja ya Walimu ingawa mchakato wa kurekebisha madaraja haya ulianza 2006, lakini mpaka leo hivi marekebisho hayo yana utata. Walimu wengine wenye sifa sawa wanapewa madaraja tofauti, Walimu wengine wala bado hawajaorodheshwa, Walimu wengine wamepewa madaraja ya juu kuliko stahili yao. Sasa hali hii itaendelea mpaka lini? Yafaa kero hizo zifikie kikomo mapema kwa vile Walimu wataendelea kuvunjika moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa posho ya mazingira magumu kwa Walimu wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu/mahitaji maalum kwa vile baadhi wa Walimu inawabidi kwenda kuwachukua hao watoto majumbani kwao asubuhi na

kuwarudisha mchana baada ya masomo. Kwa msingi huu ambapo wajibu wa Mwalimu unaongezeka lakini wala hana motisha wala kutambuliwa vizuri. Hivyo Walimu hawa nashauri wapewe posho ya kazi ngumu ya ziada wanayoifanya kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya Walimu ni wimbo tuupendao mwaka hadi mwaka kwa vile muda wote Walimu wa ngazi zote hawalipwi madai yao ya marekebisho ya mishahara baada ya kupanda madaraja, posho za uhamisho, usafiri, masomo na kadhalika. Kwa hili, hebu Serikali ihakikishe inatenga fedha za kulipa malimbikizo hayo ili kuanza ukurasa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhaba wa Walimu wa Sekondari nchini, kumejitokeza utaratibu wa Walimu wa Diploma katika Shule za Msingi kuhamishiwa katika Shule za Sekondari. Ni jambo jema lakini kuna utaratibu gani wa wazi uliowekwa ili kuwatendea haki wahusika na kuepuka migongano ambayo inaweza kutokea baadaye.

Mheshimiwa naibu Spika, chombo cha ajira na huduma za Mwalimu. Nakubaliana na ushauri uliotolewa katika taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii Bungeni, suala hili mchakato wake ulianza tangu 2002 hivi, lakini cha kusikitisha mchakato huo haumaliziki. Walimu kwa sasa wako chini ya Wizara Tatu (3) tofauti, hivi tatizo ni lipi hasa? Utafiti ulikwishafanyika, ulipitiwa na Baraza la Ushauri la Elimu, je, sasa kuna nini? Naomba nipatiwe majibu/ufafanuzi unaoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kusikia kuwa Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima, sasa itakuwa Idara kamili, haya ni maendeleo. Cha msingi, Idara iongezewe uwezo ili isimamie kupunguza idadi ya wasiojua kusoma ambayo kwa sasa inaongezeka hapa nchini. Pamoja na faraja hii, napenda kuliarifu Wizara kuwa kuna kituo cha aina yake pekee nchini cha Elimu ya Watu Wazima kwenye Shule ya Msingi Mwere - Morogoro ambacho wanafunzi wake wote ni wazee wasioona. Wazee hawa wamemudu kuandika na kusoma kwa kutumia "*Braille Machine*' moja ambayo wanayo kwa sasa. Kwa msingi huo, naiomba Wizara uwapelekee vifaa husika ili wasikate tama ya kuhduria masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa mwaka 2007/2008 ilinunua vifaa vya kujifunzia kwa shule na vitengo vya Viziwi, Wasioona lakini kwa aina nyingine za ulemavu hapakuwa na vifaa vilivyonunuliwa. Hivyo nataka ufafanuzi zimetengwa kiasi gani cha fedha kwa mwaka 2008/2009 kwa ajili ya vifaa hivyo? Zaidi napendekeza badala ya kununua *wheel chairs* zinunuliwe *try circles* kwa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitishwa sana na ukosefu wa mazingira rafiki kwa watoto/wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Ieleweke kwamba hii ni moja ya sababu ya watoto hao kutoandikishwa kabisa au wachache tu. Ni miaka kadhaa sasa tangu *MMEM* ianze na kila nilipoulizia ramani muafaka za majengo rafiki napewa taarifa kuwa zipo katika Halmashauri zetu. Lakini mbona shule zinazojengwa hakuna chochote kinachorekebishwa.

Kwa vile suala hili nimelizungumzia kila Bajeti ya Wizara ya Elimu *unless* napewa majibu ya kuridhishwa kwa kweli itakuwa vigumu kuielewa Wizara kwani yaelekea Serikali haina dhamira ya kuondoa kero hii ambayo wala haihitaji nyongeza ya Bajeti.

Naishukuru Serikali kwa kuongeza asilimia ya kuwakopesha wanachuo wenye ulemavu ili waweze kumudu masomo yao. Hata hivyo, kwa vile ajira kwa wanachuo hawa baada ya masomo ni haba au hapati kabisa, nashauri wanafunzi hawa wasomeshwe bure na Serikali kwani wala sio wengi kiasi cha kuharibu Bajeti. Wazazi kwa upande wao wa huwalea kwa shida mno.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Manaibu wake kwa kunadaa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubora wa elimu, kwa kuwa azma ya Serikali ni kutoa elimu iliyo bora, ni lazima mipango yetu ya utekelezaji ionyeshe sura ya azma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Walimu, tunahitaji kuona shule zetu hapa nchini zinafundishwa na Walimu walio bora, wanaopewa maslahi yao muhimu ili waweze kufundisha vizuri.

Kuhusu maslahi ya Walimu, Serikali irekebishe makosa yake ya nyuma ili kulipa madai yote ya Walimu na Watendaji wote wa Elimu watekeleze wajibu wao ipasavyo.

Kuhusu mafunzo ya Walimu, Serikali isiingie katika mtego wa kuandaa Walimu kwa njia ya *crash programme*. Kufanya hivyo, ni kuua kabisa dhana ya elimu bora. Ukitaka kumwandaa Mwalimu ipasavyo, ni lazima umsomeshe si chini ya miaka miwili. Walimu walikaa vyuoni miezi sita, si Walimu ni watoto ambao wameenda kufundisha watoto wenzao na hao pia wanachangia sana katika kujiingiza katika kufanya mapenzi na wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu idadi ya mikondo, ni kweli tunayo haja ya kuhakikisha kuwa vijana wote wanaofaulu vizuri mitihani ya *Form IV* wanajiunga na masomo ya *Form V,* lakini msongamano madarasani hautoi elimu bora. Ushauri, Wizara iangalie upya uamuzi wake wa kuruhusu mikondo nane kwa darasa moja la *Form I* na kuendelea. Ukifanya hivyo, unaruhusu wanafunzi 1,280 katika mikondo 32. Si rahisi kumudu kutawala shule ya aina hiyo na si rahisi kupatikana elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufundishaji wa masomo ya sayansi, nimefurahi kuona Serikali imedhamiria kuhakikisha elimu ya sayansi inaimarishwa katika Shule za Sekondari na Vyuo Vikuu. Tatizo kubwa la ukosefu wa maabara katika Shule za Sekondari hasa kwa masomo ya *Form V* na *VI*, ni tatizo kubwa sana. Kujenga maabara moja tu katika Wilaya kwa mwaka hatuwezi kufika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya kifedha si nzuri, nashauri kuwa afadhali Serikali ikope kutoka kwa washirika wengine wa maendeleo ili kujenga maabara za kutosha na kuzipatia vifaa vyake wananchi waachiwe kujenga majengo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi katika *Form V* na *VI*, Wizara ijitahidi kuongeza ujenzi wa madarasa ya *Form V* na *VI*. Mwendo tunaokwenda nao, ni mdogo. Bado kuna wanafunzi wengi wanaofaulu vizuri mitihani ya *Form IV* lakini si wote wanaopata nafasi katika *Form V*, kwa mfano mwaka 2007, vijana 1,675 walikosa nafasi kati ya wanafunzi 4,500, waliobaki wanakwenda wapi? Kwa hiyo, katika azma hii, lazima Serikali iongeze mwendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ya *REO (Regional Edication Officer)*, anapewa jukumu la kuwasimamia *DEOs* wote Mkoani na kuratibu kazi za elimu Mkoani. Mshahara wa *REO* ni mdogo mara 3 – 4 chini ya *DEO*, wakati *DEO* analipwa Sh.1.2m kuanzia Januari 2008, *REO* analipwa mshahara wa Mwalimu wa kawaida, ambazo si zaidi ya Sh.400,000 na karibu wengi wana *Masters*, ni haki hiyo? Naomba Wizara iwatetee hawa watumishi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

**MHE. THOMAS A. MWANG’ONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Jumanne Maghembe na Naibu wake, Mheshimiwa Mantumu Mahiza kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inakabiliwa na kero nyingi. Hata hivyo, kwa muhtasari tu, naomba nijadili baadhi ya kero hizo kama ifautavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wamekuwa wakikabiliwa na kero na matatizo mengi ambayo yaawaathiri katika kutenda kazi zao. Kero hizi ni pamoja na kutolipwa haki zao kwa wakati hasa pale ambapo wamekwishatimiza wajibu wao, hivyo kupelekea malimbikizo ya madai ya fedha zao kwa muda mrefu.

Malimbikizo haya yanatokana na madai ya:-

(a) Mishahara isiyolipwa kwa wakati;

(b) Marekebisho ya mishahara baada ya kupewa vyeo vipya; na

(c) Fedha za matibabu, likizo, gharama za masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyingine kubwa ipo katika suala la madaraja ya Walimu. Upandishwaji vyeo Walimu na urekebishwaji wa madaraja yao imekuwa tatizo sugu tangu pale Serikali ilipoamua kuhuisha muundo wa utumishi wa Walimu kwa kupunguza ngazi katika muundo huo na kuweka katika mfumo wa alfabeti. Hivyo

kumekuwa na kero kubwa ya Walimu wenye uzoefu tofauti kurundikwa katika cheo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni posho ya kufundishia na posho ya mazingira magumu. Muda wa Mwalimu wa kufundishia unajumuisha masaa ya kazi yaliyoainishwa katika masharti ya utumishi. Inajumisha saa zilizowekwa kisheria, ambapo zimekusudiwa katika hali halisi ya ufundishaji kama uandaaji masomo, kusahihisha, mafunzo kazini, mikutano ya wafanyakazi na kuwasaidia wanafunzi shughuli nyingine za kitaaluma. Hivyo Mwalimu ana kazi nyingi za ziada ambazo angestahili kulipwa posho ya saa za ziada.

Aidha Walimu wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu, wanastahili pia kupata posho maalum. Hii ni kwa sababu wanayo taaluma za ziada na hufanya kazi kwa muda mrefu wakiwapatia wanafunzi elimu maalum kulingana na mahitaji yao.

Pia baadhi ya Walimu hulazimika kuwafuata wanafunzi nyumbani kwao wakati wa asubuhi na kuwarudisha baada ya masomo yao. Upo ushahidi unaoonyesha kwamba baadhi ya Walimu wamelazimika kwenda kufundisha shule za kawaida baada ya kuona kwamba hakuna motisha yoyote wanayopata kwa kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero ya Walimu kuondolewa katika “*payroll*”. Ni kweli lipo tatizo la Walimu hewa. Aidha, pamoja na kuwepo kwa tatizo hili, pia limesababisha tatizo la baadhi ya Walimu kuwaondolewa katika “*payroll*” wakati wakiendelea kuwapo katika ajira. Hii inatokana na baadhi yao kuwekwa katika kundi la “watumishi hewa” wakati wakiwa masomoni na wengine wakiwa katika vituo vya kazi. Kuondolewa kwa Walimu katika “*payroll*” na kuwasabishia kuishi bila mishahara, ni kero kubwa inazorotesha utendaji wao wa kazi na hatma yake ni kuwa na malimbikizo ya madai ya stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero hizo tajwa hapo juu, ni baadhi tu ya kero nyingi zinazoikabili Wizara hii. Ombi langu kuu ni hebu Wizara iyapitie upya kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha yanatatuliwa. Baada ya kujadili kero hizo, natamka rasmi kuwa naunga mkono hoja iliyo mbele yetu.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaupongeza uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuunganisha Wizara ya Elimu pamoja na uteuzi wa Mheshimiwa Profesa Maghembe na Manaibu Mawaziri wote wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri na ninaipongeza timu yake yote kwa maandalizi mazuri ya hotuba na majedwali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kuhusu gharama za elimu kwenye shule za *private*. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kufungua milango kwa shule za binafsi, ahule hizo zimekuwa zikitoza gharama kubwa sana hususani zile zinazoitwa *Academy* na

zile za *International* bila kusahau zile zinazotumia majina ya *"Saint"* ambazo sio *seminary* za Kiislamu au za Kikristo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa Serikali kuweka kiwango cha ada kama ilivyo kwenye Vyuo Vikuu? Jambo la kusikitisha ni kuwa ada hizo zinafikia kwenye mamilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na shule hizo kudai ada kubwa, zinamudu pia kulipa mishahara mikubwa, hivyo kufanya Walimu wengi kukimbilia kufundisha kwenye shule hizo za *private* na kusababisha upungufu wa Walimu kwenye shule zetu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Walimu ni muhimu sana katika jamii, ninapendekeza mishahara yao iangaliwe upya kama walivyofanya jirani zetu Kenya kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, nawajibika kuchangia kwa njia ya kuuliza maswali machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, elimu ya juu ni suala la Muungano, kinachonishangaza ni kwamba hotuba yako kwa sekta hii ya Elimu ya Juu, haikuonyesha hata kidogo utashi wa Katiba au kuonyesha dalili kama Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ina chochote ambacho kinaweza kikaelezwa kama inahusika. Mfano ulipoelezea Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Mheshimiwa Waziri hakuona kama ipo haja ya Watanzania kupitia Bunge hili kujua muundo wake? Kwa kuwa Elimu ya Juu, ni suala la Muungano, kuna haja ya kuelewa ukweli huo na kuonyesha jinsi sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano inavyoshiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa umevitaja Vyuo Vikuu mbalimbali vya Tanzania, jambo ambalo linatoa uelewa kwa Watanzania na yeyote atakayesoma kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, je, kama pana maelewano mazuri, sio jambo la busara kutamka kama katika Tanzania hii kuna vyuo vikuu huko Zanzibar ambavyo vinakidhi haja ya kutoa elimu nchini Tanzania?

Nasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri amevitaja Vyuo Vikuu ambayo sio vya Serikali Kuu. Hii inaonyesha kuna kasoro na inawezekana havikutajwa kwa sababu havitambuliwi ingawa vinathibitishwa hapa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri anibainishie maana ya elimu ya juu inaanzia wapi? Makubaliano mapya ya Mfuko wa Elimu ya Juu kati ya Zanzibar na mamlaka ya Elimu ya Tanzania yanasemaje?

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali watu ndio msingi wa elimu ya awali, sekondari na elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iweke mkazo katika maslahi ya Walimu. Madai yao yalipwe, vyeo wapandishwe kwa wakati na nyumba za kuishi Walimu zijengwe na kutunzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi uwepo na kuhakikisha kuwa Idara ya Ukaguzi inafanya kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wagawiwe katika shule bila upendeleo ili kukwepa shida ya baadhi ya shule kuwa na Walimu wengi na nyingine haina Walimu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za bweni ziongezewe bajeti kwa mahitaji ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, ianze mchakato wa kujenga Chuo cha Ufundi Kiteto ili kuweza kuwachukua vijana wanoamaliza elimu ya msingi na ambao hawapati nafasi kuendelea na elimu ya juu.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuwapongeza, Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa juhudi wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mbinga ambalo ni pamoja na mji wa Mbinga, kuna Sekondari 36 *(operational)* kuondoa shule kongwe ya Kigonsera. Hakuna Sekondari ya Kidato cha Tano hakuna Sekondari yoyote katika Jimbo hili iliyosaidiwa na Serikali (Wizara) ujenzi wa Kidato cha 5/6 na wala maabara au maktaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo liliainisha sekondari zifuatazo ziwe High Schools nazo ni Ruanda, Makita na Hagati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuharakisha azma hiyo, Serikali itusaidie fedha kama iliyotajwa katika ukurasa wa 17. Hii itahakikisha kuwa na *high school* kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Mbinga day secondary* ilikuwa Chuo cha Ualimu na kubadilishwa kuwa sekondari. Ombi letu, eneo letu linafaa kwa Chuo cha Ualimu, hivyo shule hiyo ibadiliwe na kuwa Chuo cha Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Ufundi *(VETA)*, Wilaya ya Mbinga, inazo sekondari nyingi zaidi Kimkoa na ni wanafunzi wengi zaidi. Sielewi kwa nini haikufikiriwa kujengewa Chuo cha Ufundi. Wizara imeondoa Chuo cha Ualimu na nafasi hii ya ujenzi wa Chuo cha *VETA,* ilipelekea pia Mbinga haikufikiriwa, naomba tupewe nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Vyuo Vikuu, ili kuleta uwiano wa Vyuo Vikuu, napendekeza pia Mkoa wa Ruvuma upewe Chuo Kikuu kama ilivyo Iringa. Chuo cha Ualimu Songea kinawweza kuanza mara moja shughuli za Chuo cha Ualimu kuhamishiwa Mbinga, Halmashauri ipo tayari kutoa eneo. Kama ni kuanza upya basi eneo la mwambao wa Ziwa Nyasa litafaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma wa Walimu, uzoefu wangu unaonyesha kwamba Walimu katika vijiji hufika Wilayani na pia hawa wa Wilayani wanapofika Wizarani huduma katika ofisi zinazohusika haziwi nzuri sana, ni vizuri mahasiano yaboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni ufunguo wa maisha ya binadamu hivyo basi elimu kupewa kipaumbele namba moja, ni sawa na haki. Hivyo, ili kutimiza lengo la Serikali, ni dhahiri kipaumbele hiki kiendelezwe kwa muda mrefu na sio kuishia katika bajeti hii 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na elimu bora, ni lazima kuwa na vitendea kazi bora, kama Walimu waliohitimu katika fani zao, madarasa yaliyo bora yatakayomfanya mwanafunzi kusoma bila kuchoka, maktaba zilizosheheni vifaa ambavyo vitamfanya mwanafunzi kupenda kusoma kwa vitendo, vitabu vya rejea vitakavyomfanya mwanafunzi kurejea kile alichokisoma na mtihani wa kupima ufaulu wa wanafunzi kwa kile ambacho wamekisoma. Hivyo basi, ni wajibu wa Wizara kuyatenda hayo ili kupata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoro ni tatizo ambalo linaikabili sana jamii ya wanafunzi, pamoja na mambo mengi, jambo hili bado halijapatiwa muafaka, sijui kama haya yanatokea kutokana na hali ya maisha au ni tabia na hulka za jamii tu. Ni budi sasa Wizara ikalishughulikia jambo hili kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wanayo matatizo mengi ya msingi lakini tatizo la nyumba za kuishi bado halijapatiwa ufumbuzi. Pamoja na nia ya Wizara kujenga nyumba kwa kupitia mpango wake wa MMEM na MMES, bado lengo halijafanikiwa. Hivyo, Wizara ifikirie mpango ambao Walimu watapata nyumba zilizo bora za kuishi ili waweze kufanya kazi zao kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri ya Wizara kulipa madeni ya Walimu pamoja na wazabuni lakini bado madeni yanaendelea kuwepo hivyo Wizara itafute mpango mwingine wa kuyatatua malimbikizo ya madeni ili Wizara iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri pamoja na Manaibu Waziri kwa bajeti yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimesoma hotuba, naona Serikali inatoa fedha za vyumba vya madarasa 200 ya Kidato cha 5 na 6 na vyumba 230 vya maabara kidato cha 5 na 6, je, ina maana Serikali haikutenga fedha za kidato cha 1 hadi cha 4 kwa ajili ya baabara na vyumba vya madarasa?

Pili, ninapenda kufahamu shule za msingi ambazo Walimu wapo lakini wengi ni wagonjwa hivyo kusababisha upungufu wa Walimu, Serikali ina mpango gani wa kuwastaafisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo watumishi wengi wa shule hasa za sekondari, wapishi na watumishi wengine, je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa mishahara kuliko kulipwa kama vibarua?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kufahamu mikakati ya Serikali kuondoa tatizo la chakula shuleni ili zisiwe zinafungwa na vile vile madai ya Walimu yatapataje ufumbuzi wa kudumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mikakati ya kuendeleza Kiswahili kama lugha ya Taifa, bado lugha ya Kiingereza haiwezi kukwepeka maana ni lugha pekee ya kutusaidia katika dunia ya ushindani wa ajira na kibiashara. Nashauri katika nchi yetu, Kiingereza kisipuuzwe kabisa.

**MHE. MCHUNGAJI DR. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwapongeze kwa pamoja Waziri, Manaibu Waziri na timu yote kwa Hotuba nzuri iliyokidhi matarajio ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na ulipaji wa Kodi za Majengo na *Skills Levy* kwa shule zisizo za Serikali. Shule zisizo za Serikali zinatoa elimu kwa watoto wa Kitanzania kama shule za Serikali! Shule zisizo za Serikali, zisamehewe kodi kwa sababu shule ni huduma na sio biashara. Shule hizo zimeleta changamoto ya kuboresha shule zetu, zimesaidia kuinua kiwango cha elimu, zimesaidia kurudisha watoto waliokuwa wanasoma nchi jirani kwa kutafuta elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba shule hizo zisaidiwe na Serikali ama kwa kupewa vitabu, vifaa vya maabara na Walimu walipwe na Serikali au ruzuku maana zote ni Shule za Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Walimu kutoka nje ya nchi, sheria mpya inataka Walimu kutoka nje ya nchi wachukuliwe wenye Digrii na sio chini ya hapa lakini Walimu waliopo hawatoshi nchini. Walimu tunaowahitaji ni wa chekechea na wa shule za msingi. Walimu wa kiwango cha chekechea na msingi ni Walimu wa ngazi ya Cheti tu. Tunaomba utaratibu wa mwanzo uendelee wa kusajili Walimu kutoka nje ya nchi wenye ngazi ya vyeti kwa ajili ya shule zetu za awali na msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *English* isisitizwe maana hakikwepeki kwenye shule zetu.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yake ambayo ameiwasilisha, inaleta matumaini makubwa katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Manaibu Mawaziri wa Elimu wanavyoshirikiana katika kufanikisha kazi zao pamoja na wataalam wote katika kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kujitahidi sana na kuweka mikakati kutatua matatizo yaliyomo ndani ya sekta hii, zipo changamoto ambazo zinaikabili Wizara katika kuwaondolea mzigo wananchi, wazazi, Walimu pamoja na wanafunzi na Watendaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu kuwa Serikali katika mwaka wa fedha 2007/08 na huu wa 2008/2009, imejitahidi kuongeza fedha katika sekta hii kwa madhumuni ya kutatua matatizo mengi ambayo yanaikabili. Ni vema Serikali ikawa na udhibiti mzuri wa kushirikiana na Wizara katika kutatua changamoto hizo.

- Michango inayotozwa kwa ajili ya madawati itumike vizuri na makusudio yaonekane na Wizara itenge fedha zitakazounganishwa na zile za michango ili kuondoa malalamiko ya kila siku kwa wazazi;

- Ajira za Walimu ziongezwe na iondoe usumbufu uliopo wa Mwalimu kutoka masafa ya mbali kwenda katika shule anayofundisha ni vema ajira ziangalie na ukaazi ikiwezekana;

- Kuondoa ubinafsi, rushwa na udhitibi katika kutoa ajira za Walimu;

- Kuwapandisha daraja Walimu waliofanya kazi kwa muda mrefu na kuwalipa stahili zao mapema;

- Michango ya ujenzi ikaguliwe kupitia kamati za shule;

- Familia zisizokuwa na uwezo ziangaliwe vizuri ambazo zimetoa wanafunzi wanaojiunga na sekondari, wale wangine wanaosita kuendelea na masomo ya sekondari;

- Madeni ya Walimu na Wazabuni yashughulikiwe kabla ya mwaka mwingine wa fedha;

- Serikali na Wizara itoe vipaumbele kwa Walimu wanajituma ili kuondoa tatizo la Walimu kwenda kufundisha zaidi madarasa ya kujiendeleza kwa kisingizio cha mshahara mdogo;

- Serikali ikamilishe suala la ujenzi wa nyumba za Walimu ili kuondoa visingizio kwa Walimu vilivyozoeleka;

- Hatua kali zichukuliwe kwa Walimu wanaohusika na masuala ya kuwapa mimba wanafunzi;

- Kudhibiti utoro uliokithiri shuleni;

- Kuweka usawa kwa wanafunzi wanaohitaji mikopo;

- Kuthibitishwa kazi watumishi wa sekta hii na kupandishwa vyeo wale waliotumikia kwa muda mrefu;

- Viwango vya mishahara kwa Walimu viangaliwe upya;

- Serikali kuendelea kutenga fedha za kutosha za kuboresha vitendea kazi katika Baraza la Mitihani;

- Watumishi, wanafunzi waendelee kupatiwa elimu ya compyuta ili kuongeza ujuzi kikazi na kimasomo;

- Kuendeleza majengo ya Vyuo vya Ufundi Stadi kwa wanafunzi wasiobahatika kuendelea na masomo ya sekondari; na

- Kuendeleza tabia ya kufanya mikutano ya mara kwa mara ya wazazi na wanafunzi ili kuweza kujua maendeleo ya watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia hotuba hii kwa kuishukuru Wizara na Kamati husika kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2008/2009. Nawashukuru sana na ninaamini mipango iliyoandaliwa itatekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Mtwara, una shule za sekondari 121 zikiwemo 113 za Serikali na nane za binafsi. Kati ya Shule 113 za Serikali sita ni za Bweni, shule hizo za bweni mbili zipo Mtwara Mikindani na tano ni za binafsi. Mtwara katika shule za kutwa hakuna hosteli kabisa. Tandahimba kuna hosteli mbili katika shule ya Tandahimba na Luagala. Newala kuna shule zenye hosteli tatu nazo ni Mnyambe, Mtangalanga, Kiuta. Masasi kuna Chungutwa na Lukuledi, Nanyumbu kuna shule yenye hosteli moja nayo ni Mangaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule hizi za sekondari 121 zilizoko Mkoa wa Mtwara, mahitaji ya Walimu 1565, waliopo 794, pungufu ni Walimu 771. Katika shule za msingi, kuna shule 603, mahitaji Walimu ni 6207, waliopo 4677, pungufu ni 1530. Katika shule za sekondari zenye maabara ni 16, shule zisizo na maabara 105.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika kutoa takwimu hizi ili Wizara iweze kupata hali halisi ya elimu katika Mkoa mzima wa Mtwara, kwani bado kielimu tuko nyuma, pamoja na matatizo yanayotukabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jamii yetu, Mkoa unajitahidi kuwa na mikakati ya kutatua matatizo hayo. Ukiangalia takwimu za taarifa yangu utaona upungufu mkubwa wa Walimu waliopo, upungufu wa maabara, upungufu wa hosteli za wasichana ni tatizo kubwa sana ambalo linachangia kushuka kwa elimu Mkoani Mtwara na matatizo hayo makubwa yapo nje ya jamii kwani yanahitaji nguvu za Wizara, je, Wizara itatusaidiaje kuhakikisha upungufu huu mkubwa wa Walimu unaisha? Je, Wizara haiwezi kutoa upendeleo wa kuongeza fedha za MMEM na MMES ili kutatua tatizo la hosteli na upungufu wa madarasa ambalo ni tatizo kubwa pia? Katika hali hii, kama hakutakuwa na jitihada za ziada kwa kweli elimu, Mkoa huu utaendelea kuwa chini, tunaomba sana hatua za utekelezaji zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, katika shule ya sekondari ya Mtapika, tunatarajia kuanzisha Kidato cha Tano na Sita, lakini shule haina hosteli na ina upungufu wa majengo. Kwa kuwa katika eneo hilo, kuna majengo ya shule ya wasioona ambayo kwa miaka mingi haina wanafunzi na majengo yanakaa bila matumizi yoyote na yanaharibika na Halmashauri ya Masasi iliomba majengo haya tukabidhiwe ili yawe sekondari na maombi yalienda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao ndio wamiliki na hawajapata jibu mpaka leo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri afanye mazungumzo na Wizara ya Afya, kutuombea majengo haya yamilikiwe na Halmashauri, kwani ni pesa za Serikali zilizotumika katika ujenzi, hivyo kupewa kwa kuyatumia kama sekondari si vibaya kwani wananchi ndio walipa kodi. Nasisitiza sana Mheshimiwa Waziri atusaidie upatikanaji wa majengo haya na maombi yote niliyoomba katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Elimu, Profesa Maghembe na Manaibu Waziri wake kwa kuingoza Wizara hii kubwa na nina matumaini makubwa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mengi yaliyozungumzwa na Wabunge wenzangu na pia naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, ninapenda kwa kifupi kuelezea malalamiko yangu kuhusu upatikanaji wa Walimu katika Mikoa ya Kusini. Mpaka leo, Wizara haijapata ufumbuzi katika suala la Walimu waliopangiwa Kusini kutoripoti katika vituo vyao. Naona suala hili Wizara inalifanyia mzaha kwani haielezeki kwa nini hawa

Walimu ambao ni waajiriwa wa Wizara hawaendi Kusini licha ya miundombinu waliyokuwa wanalalamikia kuboreshwa kwa kiasi kikubwa. Panahitajika dawa kali ili kuondoa tatizo hili, Wizara ikionekana inachukua hatua, bila shaka Walimu watakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu, kuna Shule za Sekondari za Kitaifa za Ndanda, Chidya, Masasi na *Mtwara Girls*, kuna shida maalumu katika Sekondari ya Ndanda ambapo kuna madeni makubwa ya mamilioni ya umeme maji na chakula. Shule inapata huduma nyingi toka kwa wamissionari wa Abbey Ndanda, ambao wanavumilia sana hali ya madeni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa sekondari ya Ndanda inakatiwa umeme na maji na matokeo yake ni wanafunzi kufanya fujo ya kuvunja majengo ya Parokia Ndanda na kuleta hasara kubwa. Hivi juzi wanafunzi wamefanya fujo kubwa Parokiani kwa ajili ya kukata umeme ama kupunguziwa masaa ya kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni mbaya, kwa hiyo ninamtaka Waziri anihakikishie ni lini atalipa madeni haya ya *Ndanda Secondary* la sivyo itabidi nitoe shilingi katika bajeti yake. Wizara inaonekana haijali kulipa madeni haya, nataka katika bajeti hii, anihakikishie kuwa atamaliza madeni yote katika shule hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwa mzima na kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Pia napenda kuwapongeza Waziri na Manaibu wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano wanaotupa tunapokuwa katika Kamati yetu ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu tatizo la mimba kwa wasichana hasa wa shule za msingi. Kipindi tunasoma katika shule ya msingi, mara kwa mara, wanafunzi wote wasichana walikuwa wakipimwa afya zao hususan ujauzito kutokana na zoezi hilo, wasichana walikuwa wakijitunza kuogopa wasije kuwa na mimba. Kwa vile wasichana wa sekondari, elimu ya kujikinga na kuzuia ujauzito kwa kiasi fulani wanayo, je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kuanzisha upimaji mamba wanafunzi wa shule za msingi ili kuwaweka katika hali ya tahadhari?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hizi *Teachers Resources Centres* (Vituo vya Walimu), napenda kumuulizia Mheshimiwa Waziri, hivi vituo vinatumika ipasavyo? Kwa mawazo yangu, vituo hivi vingekuwa ni vituo vya kuwakutanisha Walimu mara kwa mara kwa mambo kadhaa kwa mfano:-

a) Walimu ni watu wanaopenda kujiendeleza, kwa hiyo, vituo hivyo vingekuwa ni mahali pa kuwachochea Walimu wajiendeleze ili kukuza taaluma yao; na

b) Mara nyingi mabadiliko ya mitaala inachelewa kuwafikia baadhi ya Walimu hususani wale wanaofundisha shule zilizo mbali na ofisi za Wilaya;

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nizungumzie kuhusu suala zima la ukaguzi. Kwa uzoefu nilio nao, mara nyingi ukaguzi unafanyika katika shule zilizo karibu na Makao Makuu ya Wilaya au Shule zilizo katika maeneo ya mjini. Shule nyingine zile za vijijini ambazo ziko mbali zinaweza kukaa hata miaka mitatu bila ya kufanyiwa ukaguzi. Utakuta shule kama hizi zinakuwa ziko huru kufanya chochote. Badala ya masomo ya darasani, watoto hao hupelekwa kulima mashamba ya baadhi ya Walimu. Walimu hawajali kabisa suala zima la wanafunzi kuingia darasani na kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hizi Kamati zinazosimamia ujenzi wa madarasa iwe ya MMEM au MMES. Inaonekana wanaosimamia zoezi zima la ujenzi wa madarasa, ni wabadhirifu na uchunguzi uliofanywa kwa kina wasimamiaji hawa wa majengo wana tija wanayopata. Wengi wamejenga nyumba na wengine wamenunua vyombo vya usafiri. Wizara ihakikishe kuwa majengo yajengwayo yana ubora lakini pia Serikali iangalie jinsi gani itaongeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa au nyumba za Walimu hutokana na kupanda bei kwa vifaa vya ujenzi.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafahamu kuwa Halmashauri ya Mbulu kwa kushirikiana na TAMISEMI, inahudumia jamii ya Kihadzabe katika Kata ya Yayeda kwa upande wa elimu ya msingi *"pilot school's"* katika maeneo ya kuwinda na kurina asali na pia shule ya bweni ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi katika kutekeleza azma ya Serikali ya kila Kata kuwa na shule ya sekondari ya Wilaya ya bweni katika Kata ya Yayeda kwa ajili ya watoto wa Kihadzabe na jamii ya wafugaji. Jamiii hizi hazina uwezo wa kuchangia fedha au kufanya kazi ngumu za mikono. Tulileta ombi maalum Wizarani ili kusaidiana katika ujenzi wa Shule hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri Mahiza, alipotembelea eneo hilo, aliomba andiko rasmi ili Serikali ijenge shule hiyo, Wilaya tayari imewasilisha andiko hilo Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ichukue jukumu la pekee katika ujenzi wa shule ya sekondari kwa ajili ya jamii za Kihadzabe. Uamuzi wa Wizara, ni muhimu kwa sasa kwa vile suala hili litakuwa agenda ya Mheshimiwa Rais katika ziara yake Mkoani Manyara hivi karibuni.

**MHE. KHALIFA SULEIMAIN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mabadiliko yaliyofanywa katika Bajeti ambayo mimi nayapongeza. Hata hivyo nina ushauri kwa mambo yafuatayo. Kwanza ni madeni ya wale wanaolisha mashuleni kwa vyovyote jitahidini yalipwe tena kwa wakati. Hii itasaidia watoto wetu kupata shibe na hivyo wataweza kusoma.

Pili, tatizo la wanavyuo ambao hawajamaliza kulipia gharama, kufutiwa matokeo na kuzuiwa kuendelea kusoma, naomba suala hili liangaliwe upya na kwa kina!

Ukimfutia mtu matokeo maana yake hakusoma na hivyo haajiriwi!  Je, huo mkopo wa Serikali ataulipa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mishahara ya walimu na madeni yao, jitahidini yalipwe.  Ninyi nyote wakuu na sisi wengi wetu ni walimu, si vyema kusahau tulikotoka! Chinua Achebe alisema; *"When one finger gets oil, it swells to the others."The oil is on your fingers! Please! Please!*

Mheshimmiwa Naibu Spika, kila la heri, *Amin.*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya kwanza kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Profesa Juamnne Maghembe, Naibu wake, pamoja na wataalamu wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kupanga elimu kuwa kipaumbele cha Taifa na hivyo kupewa fedha zaidi ya Wizara nyingine. Kwa kutambua umuhimu wa elimu kwa Watanzania kuwa ndio mkombozi pekee wa kutusaidia kutoka hapa tulipo kupiga hatua mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika,   pamoja na Bajeti kubwa kupelekwa sekta ya elimu bado hali ya shule zetu za msingi na sekondari nyingi ni mbaya na haswa za vjijini.

Mheshimiwa Naibu Spika,  tunahitaji kuwapatia watoto wetu elimu bora na siyo bora elimu.  Serikali imejitahidi kuhamasisha wananchi wajenge shule na madarasa, wananchi wamejenga madarasa kwa nguvu zao zote. Madarasa hayo mengi hayana vifaa vya kufundishia, hayana madawati, hayana maabara na pia walimu ni wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika,  kuna shule ya msingi ina walimu wawili au watatu, shule ina madarasa saba na madarasa hayo yana mikondo miwili hadi mitatu, hivi kweli hapa watoto wanasoma?  Cha kusikitisha zipo shule ambazo zina walimu hadi ishirini, kwa nini Serikali inaruhusu hali hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana shule zetu zote za sekondari/zijengewe maabara.  Tunahitaji wataalam wa sayansi katika fani mbalimbli. Tunahitaji madaktari, injinia, wataalamu wa madini na kadhalika,  bila elimu kwa vitendo nadharia peke yake haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika,  nchi yetu maliasili zetu zinaporwa sana na wageni kutokana na kukosa wataalamu wa fani hizo.  Ili kunusuru nchi zetu ni lazima tuzalishe wataalamu wengi watakaosimamia nchi zetu kwa manufaa ya Taifa letu!

Mheshimiwa Naibu Spika,  Mkoa wa Tabora na *particularly* wilaya ya Urambo inaongoza kwa kuwa na walimu wachache shuleni, tunaiomba Serikali ihakikishe suala la walimu linatatuliwa ili tuwezeshe elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika,  kuna huu mpango wa kuwapatia *short courses* wanafunzi wa *Form VI (one month*) ili wakafundishe sekondari.  Hapa tuko makini kweli

Serikali? Walimu hawa shuleni wanaitwa *voda faster*. Cha kwanza kuwa hawatadumu katika kufundisha kwani hawana *methodology,* pili hawawezi kufundisha watoto wakapa-*form* vizuri. Ni vizuri Serikali ikaboresha sana mazingira na mishahara ya walimu ili kuvutia zaidi wanafunzi kusomea kazi hii ya wito. Maeneo mengi na nchi nyingine mwalimu analipwa mishahara mikubwa kuliko mtu yeyote kiasi bila mwalimu hakuna Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kina eneo kubwa sana ambalo liko wazi na ingeweza kujengwa hosteli kwa ajili ya walimu kwa wanafunzi ambao wengi wanaishi nje ya chuo na wengine mitaani kabisa uswahilini ambapo inachangia hata kushindwa ku-*perform* vizuri. Fedha zinazotumika kukodi nyumba za watu huko mitaani kwa ajili ya makazi kwa wanachuo ni nyingi sana kiasi ambapo zingetosha kabisa kujenga hosteli ili kuendelea kutumika miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu siyo endelevu na ni matumizi mabaya ya fedha za wananchi wa Tanzania na zaidi kila mwaka chuo kinaongeza wanafunzi na tatizo la makazi linaongezeka kila siku. Tutafute jinsi gani ya kupata suluhisho la kudumu la tatizo hili la uhaba wa malazi kwa kuwa wabunifu endelevu kwa vyuo vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarimu wa Serikali wa kutoa ufadhili wa nafasi za vyuo nchini wanafunzi waliofaulu kwa daraja la kwanza na pili kwa wanawake na daraja la kwanza kwa wavulana, huu ni ubaguzi wa aina yake ambao kwa awamu zote za Serikali haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa watu wakubwa wenye uwezo waliobahatika kusoma katika shule nzuri za mjini *(tuition)* ndio wanaofaulu kwa *division one* na *two.* Wale watoto wa walalahoi wa vijijini ambao shule haina walimu, hakuna maabara, hakuna vifaa, wanatembea umbali mrefu ndio wafike shule na wanakuwa wamechoka, hawawezi kufaulu vizuri. Sana sana wakifauli sana ni *division three* na *four IV,* ina maana hawa wasiende vyuoni? Ina maana aliye maskini aendelee kuwa maskini na tajiri aendelee kuwa tajiri? Hivi utafiti gani ulifanyika kabla ya kuanza kwa mpango huu kuona kama wanafunzi wote wa shule zote vijijini na mjini watatendewa haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba ufafanuzi na kwa nini kwenye Wilaya moja kunakuwepo michango ya shule inayotofautiana. Kata moja inachangisha shilingi 10,000/= kwa familia na kata nyingine wanachangisha shilingi 25,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini kina mama wanadhalilishwa kwa sababu ya michango ya shule? Kina mama wajawazito wamekuwa wanakurupushwa ovyo bila kujali hali zao za afya kwa sababu ya mchango. Tunaomba pia majibu kuhusiana na suala la mama mjamzito aliyejifungua *lock-up* kwa sababu ya kukosa/kushindwa kuchanga shilingi 25,000/= mchango wa sekondari huko Shinyanga Vijijini. Serikali itoe tamko leo hapa Bungeni kuhusiana na viongozi waliosababisha hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi pia wanachangishwa michango lakini hawasomewi mapato na matumizi ya fedha zao. Hili ni tatizo sehemu nyingi na mwananchi akihoji anakaripiwa na atabambikiwa kesi ili anyamazishwe.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakuu wa shule ili awe mwalimu mkuu wa shule ya msingi lazima awe na *diploma.* Mkuu wa shule ya sekondari yenye kidato cha kwanza hadi cha nne, lazima awe na angalau Digrii moja. Mkuu wa shule ya sekondari yenye kidato cha tano hadi cha sita lazima awe na angalau digrii ya uzamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakuu wa shule hawa ni wasomi kama wasomi wengine walio katika Taifa hili. Wakuu wa shule hawa ni wasimamizi wa wanafunzi (600 – 1,500) wanasimamia walimu (wengi tu 30 – 100), wahasibu, maboharia na kadhalika. Wakuu hawa ndiyo kiungo kati ya shule na jamii inayowazunguka, Halmashauri, Wilaya, Mkoa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza kwa nini wakuu wa shule wanapewa madaraka lakini hawapewi vyeo vya madaraka, vinavyokwenda sambamba na mshahara (kiwango fulani). Mbona Wizara nyingine wana vyeo vya madaraka *(substantive post).* Matokeo yake ni kuwa unakuta mkuu wa shule anawaongoza watu wanaomzidi mshahara. Hii ni kutomtenda haki huyu mkuu, anadhalilishwa. Je, akiishiwa aende kukopa kutoka kwa walimu walio chini yake? Zamani wakuu wa shule walikuwa wanalipwa *responsibility allowance,* lakini ikaondolewa mwaka jana wakati wa Bajeti nilichangia kuhusu suala hili hili na nilielezwa kuwa baada ya zoezi la marekebisho ya mishahara lililoamriwa na Rais, kukamilika basi na wakuu wa shule vyeo vyao vya madaraka vitafahamika. Je, ni lini vyeo vya madaraka ya wakuu wa shule vitatangazwa? Je, vianzio vya mishahara yao ni vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini utaratibu wa kuwalipa *responsibility allowance* utaanza? Naomba maswali yangu yajibiwe ili niunge hoja mkono.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wao wote kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia machache sana kwa nia ya kuboresha kama ifutavyo:-

Kwanza, ongezeko la shahada mpya kwenye baadhi ya vyuo vikuu kwa mfano Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kuongeza shahada mpya ya elimu. Tatizo langu ni uwepo wa miundombinu ya kutoa mafunzo haya pamoja na wahadhiri wenye utaalam wa *Education.* Hatua hii siyo kwenda nje ya *core speciality* ya chuo hiki?

Pili, vyuo kudahili wanafunzi wengi kuliko uwezo wao hususan uwepo wa miumdombinu ya kutosha pamoja na rasilimali watu yaani walimu wa kutosha. Napenda kushauri kwamba vyuo vitenge zaidi katika kutoa *quality training* na siyo *quantity* kwa

sababu vijana wetu wanahitaji kuwa na uwezo wa ushindani katika soko la ajira katika ulimwengu wa utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kwamba vyuo vikuu viangalie uwezekano wa kutoa huduma za ushauri nasaha kwa wanafunzi kwa utaalam zaidi kwani hali ilivyo sasa hairidhishi. Vijana wetu wanayo matatizo ya mbongo mtu kutokana na mahangaiko yanayotokana na ugumu wa maisha na kuhangaika kutafuta namna ya kusoma kwa amani kutokana na ukosefu wa miundombinu ya kutosha. Mfano, wanafunzi wanaishi zaidi ya wanne kwenye vyumba ambavyo vilijengwa kwa ajili ya watu wawili. Mwingine ana *TV,* mwingine muziki na kadhalika. *You can imagine the situation.* Hivyo mazingira yanakuwa siyo *very condusive for reading,* hata kupumzika. Hivyo uhitaji wa *psychological support* wa kitaalamu katika vyuo vyetu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninalia na ukarabati wa shule ya sekondari ya Ifakari. Shule hii ni ya wasichana na uwezo wake ni kuhudumia wanafunzi 500 tu. Lakini sasa inahudumia wanafunzi zaidi ya elfu moja, cha kusikitisha ni idadi ya matundu ya vyoo kulinganisha na idadi ya wanafunzi. Shule hii ina vyoo 20 tu. Vyoo vyote vya ndani vimefungwa kutokana na uchakavu na ukosefu wa maji. Majengo yote yanavuja vibaya sana kufikia hata kuathiri mfumo wa umeme.

Aidha, mazingira ya shule yameharibiwa sana na zoezi la *TANROAD* Morogoro la kuchimba kifusi katika eneo la shule. Kitendo hiki bado kinaendelea na kimesababisha uwepo wa mabwawa makubwa ambayo ni masalio ya mbu, achilia mbali kelele na mavumbi katika eneo la shule. Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kuingilia tatizo hilo ambalo ni hatari kubwa kwa shule hii.

Mwisho, naomba sana Wizara iwajengee walimu nyumba kwa sababu hakuna nyumba za kupanga karibu na shule hii. Walimu wengi wanaikimbia shule hii kwa sababu ya kukosa nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, nampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Naibu Mawaziri wake pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri ya Bajeti nzuri yenye ufanisi na kueleweka pamoja na mipango mizuri iliyoorodheshwa ikiwemo kuongezwa posho kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, ingawa halitoshi kwa mujibu wa hali ya maisha, lakini bora kupata kuliko kukosa na zaidi mipango kwa watoto wenye ulemavu naomba itiliwe mkazo, waongezewe kupata vifaa vya kujimudu na vya kujisomea, pia walimu wenye ujuzi wazidi kuongezwa na kupatiwa ujuzi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu katika shule na vyuo yaboreshwe ili kuwaondoshea usumbufu. Mwaka jana nilizungumzia hili suala kuwa kuwepo na maafisa wa elimu maalum ngazi za Wilaya na Mikoa, pia bado kuna ubaguzi kwa walimu wenye ulemavu hawapandishwi daraja wala hawapatiwi nafasi ya kujiendeleza, kwa hiyo, washughulikiwe na wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naitakia kila la kheri Wizara hii katika utendaji. Naunga mkono hoja.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Nawapongeza Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wake kwa hotuba nzuri. Nimechukua nakala za kutosha kugawa kwenye shule zangu zote za sekondari.

Tatizo langu kubwa ambalo nahitaji maelezo ni kuwa ujenzi wa shule za *A – Level* huko Wilayani ni mgumu sana kwa sababu, watoto wanaoingia katika shule hizo wanatoka nchi nzima.

Hivyo wananchi wanasita kujitolea kujenga shule hizo. Ushauri wangu ni kuwa ama Serikali yenyewe ijenge shule hizo na ilete watoto kutoka popote nchini. Utaratibu huu ni aghali sana kwa Serikali. Tabia za watoto wa shule hizo kawaida ni mbaya sana au shule hizo zichangiwe kwa kiasi fulani na wananchi halafu Serikali itoe bati, saruji, vioo na *furniture.* Watoto watakaoingia humo 60% iwe watoto wa eneo hilo na 40% watoke mahali pengine.

Kwa vyovyote vile suala hili liangaliwe kwa undani zaidi. Mifano ya kuyaacha majengo yaliyoanzishwa kwa ajili ya *A-level* ni kama vile shule ya Kifanya. Wamejenga madarasa mazuri manne lakini wameacha kuezeka sababu ya mfano walioona katika shule ya *A- level* mpya ya Uwemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu katika shule hizi za *A – level* hawapo, maabara hakuna, chakula kwa watoto hao hakipo. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee mchango wangu wa jana nilioutoa kwa maandishi. Naomba ufafanuzi kwa Serikali kuhusu vigezo vya kutoa mkopo kwa asilimia kwa sababu havifuatwi na kwa nini pesa ya mazoezi kwa vitendo inatolewa kwa asilimia isitolewe sawa kwa watu wote kama ilivyo kwa chakula?

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi huu utasaidia sana kupunguza malalamiko ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu, kwani wataelewa zaidi na itawasidia kufuatilia haki zao.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nami kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Katika mambo ambayo mimi yananiuhuzunisha katika walimu ambao ni walemavu wa viungo kutokuwa na vifaa vya kuwawezesha aidha, kwa kutembea au kufundishia. Hata katika Wizara ya Elimu, palipo majengo yao, ofisi ya kuwahudumia walemavu walimu hao iko ghorofa ya tatu, hawa ni walemavu na upandaji wao ni mgumu. Hivyo basi, naiomba Wizara kuangalia suala hilo na kuwatengea ofisi hiyo chini ili waweze kufika katika huduma zao kwa urahisi na kwa usalama kama tukifanya hivyo tutakuwa tumewatendea haki walemavu hao.

Pia napenda kuchangia suala la michango. Tunapoamua wananchi wachangie maendeleo ya ujenzi wa madarasa, basi tuwape pumzi ya kujipanga vizuri wazazi hawa, lakini katika shule zingine mzazi huyo amechangia mchango wa madarasa kwa shilingi 20,000/= na ndio mchango mzima alioambiwa, lakini anapotaka kumwandikisha mtoto shule, anachajiwa shilingi 10,000/= na kama hana, basi mtoto huyo haandikishwi shule na wala hapokelewi. Hii naona sio halali kwani kama mzazi ameshachangia jengo, lakini akileta mtoto mpaka atoe tena shilingi 10,000/=. Sasa basi naiomba Serikali itazame upya suala hili la michango. Sote tunajua wananchi wetu ni maskini na hawana kipato. Naishauri Serikali itoe tamko kali kwa wale wanaochangisha na kukataa kuandikisha watoto. Nina imani watoto wote watasoma hata kama mzazi hana uwezo. Ahsante.

**MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa hongera kwa Waziri, Naibu Mawaziri wake wote wawili, katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wizara nzima kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa kuwasilisha hotuba yao vizuri.

Pili, naomba kuchangia kuhusu elimu hasa masomo ya sayansi, kwa ujumla watoto wengi siku hizi hawapendi masomo ya sayansi. Wasiwasi wangu japo bado hatuna maabara ya kutosha kwa staili hii ya watoto kutopenda masomo ya sayansi, tutakuwa na wataalam ambao sio wanasayansi. Taifa bila wana sayansi ni matatizo.

Ombi langu na ushauri wangu kwa Wizara ni kubuni mikakati ya kuwashawishi watoto kupenda masomo haya ya sayansi hasa wanafunzi kuanzia *form one.* Jambo lingine ni kwamba walimu wanaofundisha masomo ya mchepuo wa *Arts* wanawashawishi na kuwadanganya wanafunzi kwa mbinu zozote zile kusudi wachukue masomo yao, hasa wale watoto wenye akili kwani baadhi ya shule, huwapatia zawadi walimu kufuatana na ushindi wa wanafunzi. Kwa mfano, mwalimu atapata zawadi nono ikiwa wanafunzi wake wamepata alama A kwenye somo lake kulinganisha na wakipata B,C,D na E.

Ushauri wangu ni kufanya mkutano na wakuu wa shule (kikanda) na kuwaeleza na kuwaagiza wawashawishi wanafunzi wao kuchukua masomo ya sayansi kama ilivyo kuwa miaka ya nyuma, kupita kwenye shule na kuwashawishi wanafunzi (hasa *form one)* kuchukua masomo ya sayansi, kutoa zawadi/motisha kwa wanafunzi watakaofaulu vizuri masomo ya sayansi, kuwatafutia *sponsorship (full)* wanafunzi watakaofaulu vizuri masomo ya sayansi na wanafunzi wote wanaochukua kozi/fani za sayansi kuwapatia kazi Serikalini au popote pale; wanapohitimu masomo yao vyuoni.

Mheshimiwa Niabu Spika, ni vizuri tujitahidi kuinua masomo ya sayansi. Bila sayansi hakuna maendeleo.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri katika vipengele vifuatavyo, kwanza, yapo malalamiko kutoka kwa walimu wa mkoa wa Kigoma kutokulipwa madai ya kwenda kusoma kwa maana ya kurudishiwa gharama ambazo walimu wanajigharamia wanapokwenda kusoma, wakati kibali cha kwenda kusoma kinatolewa na Wizara/ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili ni lazima litolewe maelezo kwa sababu madai ya walimu yamekuwa mengi kiasi cha kuona kwamba Wizara haisimamii kikamilifu kwa kupitia kwa maafisa elimu Mikoa/Wilaya.

Kuhusu malimbikizo ya madai ya walimu yamekuwa kero kubwa kwa sababu walimu wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mengi ambayo yanawaathiri katika utendaji wa kazi zao. Kero hizo za walimu ni pamoja na kutokulipwa haki zao kwa wakati hasa pale ambapo wamekwishatimiza wajibu wao, hivyo kupelekea malimbikizo ya madai ya fedha zao kwa muda mrefu. Hili limekuwa ni kero kubwa kwa maana ya kustahili kutolewa maelezo ya kutosha. Malalamiko hayo yanahusu vipengele vifuatavyo, mishahara isiyolipwa kwa wakati, marekebisho ya mishahara baada ya kupewa vyeo vipya *(Arrears)* na fedha za matibabu, likizo, gharama za masomo pamoja na uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, upandishwaji vyeo walimu na urekebishwaji wa madaraja yao umekuwa tatizo sugu, tangu pale Serikali ilipoamua kuhuisha muundo wa utumishi wa walimu kwa kupunguza ngazi katika muundo wa utumishi huo na kuweka katika mfumo wa *alphabet.* Kutokana na hali hiyo kumekuwa na kero kwao na hasa wale wenye uzoefu tofauti kurundikwa katika cheo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya walimu wanaostahili kurekebishiwa hawajaorodheshwa, baadhi ya walimu wamerekebishiwa vidato badala ya madaraja, baadhi ya walimu wenye uzoefu na sifa zinazofanana wamepewa sifa tofauti, walimu wengi wakipandishwa madaraja hawajapewa barua zao, baadhi ya walimu wamepewa madaraja ya juu kuliko wanayostahili na wale wachache waliorekebishiwa mishahara yao hawajalipwa malimbikizo ya mishahara ya kuanzia Julai, 2007. Hili naomba litolewe maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matukio ya walimu kushambuliwa shuleni na wakati mwingine kuuawa wakiwa katika vituo vyao vya kazi. Hiyo inatokana na jamii kutothamini umumhimu wa kazi ya mwalimu. Kaw mantiki hii ipo haja ya Serikali kuchukua hatua madhubuti ili kulinda usalama wa walimu na kukomesha suala hili. Mifano hai ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu walimu wamefanya kazi bila kupelekwa kuhudhuria mafunzo kazini. Jambo hili ni hatari kwa mustakabali wa elimu na walimu nchini. Kunatakiwa kuwepo utaratibu sahihi ulioandaliwa na Serikali ili walimu wahudhurie mafunzo kazini. Hiyo itaimarisha uwezo wao wa kukabiliana na mabadiliko ya mitaala lakini pia itaimarisha utendaji kazi. Serikali inatakiwa kujua ni walimu wangapi watakwenda masomoni kwa mwaka wa fedha husika na hivyo kuhifadhi kumbukumbu zao badala ya kuwaruhusu.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wake wote wawili, Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na yenye kuonyesha vyema tunakoelekea katika sekta hii muhimu. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi kwa maelezo zaidi katika maeneo kadhaa. Aidha, pamoja na shukrani na pongezi hizi nawapa pole kwa kazi kubwa waliyoionesha katika kuipanua sekta ya elimu katika ngazi zote mbili yaani elimu ya msingi (msingi na sekondari) na elimu ya juu. Kwa upande wa wingi wa vijana wanaoingia katika hatua mbalimbali ya elimu, kazi imekuwa kubwa sana.

Ombi langu kwao, wasikatishwe tamaa na kejeli za watu wanaosema kuwa kazi zote hizi ni bure. Ni kweli uwingi bila ubora siyo hoja, lakini mimi ninaamini ya kuwa kwa jinsi mlivyojipanga ubora ni kitu katika ajenda yetu. Ni vyema ijulikane ya kuwa si mara zote ongezeko la wingi *(quantity)* wa vijana na fursa zao kujiunga na masomo vikaendana sambamba na ubora hususan katika sekta pana kama hii ya elimu.

Aidha, wakati mwingine huwezi kuongelea ubora kwa kitu kisichokuwepo. Leo tu waongelea juu ya upungufu wa walimu na vijana shuleni kwa kuwa shule nyingi na wanafunzi wengi wapo. Hii sasa ni changamoto inayotutaka tuangalie upya vipaumbele yetu. Huwezi kuongelea kuongeza idadi ya shule kama huna shule hata chache. Hivyo kama ilivyo kawaida, kila hatua ya maendeleo inapofikiwa huwa inafuatia na changamoto zake.

Hivyo nawaomba mjielekeze katika changamoto zifuatazo, kupata walimu wa kutosha na wenye sifa kwa shule zetu hizi zilizopo zitakazozidi kupewa vibali vya kufunguliwa, kama wananchi na Waheshimiwa Wabunge wengi wanavyosema vifaa vikiwemo vitabu na vifaa vya maabara vipatikane vya kutosha shuleni ili vichangie katika kuboresha sekta hii na kutafuta njia muafaka kupunguza idadi ya wanafunzi wanaoshindwa kumaliza shule kwa kuangalia tiba ya mianya mbalimbali zinaozochangia katika midondoko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuiunganisha sekta ya elimu kuwa chini ya Wizara moja. Mimi nauona uamuzi huu ni uamuzi wa kimaendeleo. Aidha, uamuzi wa elimu ya msingi na sekondari kupelekwa TAMISEMI ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kuwa elimu ya kidato cha kwanza hadi kidato nne ndizo ziwe TAMISEMI na zote ziwe za kutwa isipokuwa mwenye shule wananchi au binafsi wanapoamua vinginevyo. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ibakie na kidato cha tano na sita *(boarding)* vyuo vya ufundi vya *VETA*, vyuo vya ualimu na vyuo vya elimu ya juu. Kuoanisha haraka mihula ya shule za *A level* ili viingiliane vyema na mihula ya vyuo vya ufundi vitakavyokuwa vikipokea vijana wahitimu wa Kidato cha sita.

Aidha, kuwe na kada ya vyuo vya ufundi vitakavyokuwa vikipokea vijana wahitimu wa kidato cha sita tu. Mihula ya vyuo hivi viwe sawa na ile ya vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia uamuzi wa kutangaza kuwa kidato cha nne ni elimu ya lazima kwa kila mwananchi. Ombi langu, nitaomba Mheshimiwa Waziri wakati

wa kuhitimisha aeleze uamuzi huu wa kuifanya elimu ya kidato cha nne kuwa ni ya lazima utafikiwa lini kizuizu kilichopo sasa ni kipi?

Kuhusu eneo la shule maalum, kwa muda mrefu sasa tumekuwa na utaratibu wa kuendesha shule hizi. Upungufu uliopo ni jengo lake halijulikani, hatuna utaratibu mzuri wa kuwafuatilia vijana wanaopitia katika shule hizo jambo linalopoteza umuhimu na maana ya kuwaweka wanafunzi katika shule hizi.

Maombi yangu ni kuwa wanafunzi hawa wasomeshwe bure na Serikali bila kujali kama mzazi wake anao uwezo au la, shule hizi ziundiwe utaratibu wa kuwa karibu na wanafunzi katika shule hizi utaratibu huu uwe mara kwa mara ukiwapima kama wanaendelea kuwa na sifa hizo. Vijana wanaopoteza sifa, utaratibu huo uwe wazi kuwaondoa katika shule hizo na kuwapeleka katika shule zingine za Kitaifa zisizo maalum.

Pia shule hizi ziwe ni taasisi za kuandaa viongozi wa nchi yetu. Hivyo hata mitaala ya elimu itakayokuwa ikitolewa katika shule na taasisi za aina hiyo iwe maalumu na shule hizi ziendeshwe mithili ya seminari zinazoandaa watu maalumu kwa nchi yetu wa kesho na baadaye. Ni vema uongozi uwe uliandaliwa tangu mapema kwa vijana kutoka katika jamii waanze kupata mionjo ya uongozi, kuanza kuiheshimu nchi, wananchi wake, utamaduni wake na maadali yake tangu wakiwa bado vijana. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeweka mahali pema maana na umuhimu na shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe, tuanze kuandaa vijana viongozi wa nchi yetu kupitia shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la michezo mashuleni, naipongeza sana Serikali kurudisha michezo katika shule. Kwa bahati mbaya nyaraka husika zinazoelekeza jinsi ya kuendesha michezo mashuleni, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa kutoa maelezo, je, kilichorudishwa shuleni ni kitu gani, michezo, mashindano ya michezo kati ya shule na shule au elimu ya ufundi wa michezo kwani kama ni michezo, iko mingi ni ipi au tumerudisha yote? Kama ni yote ichezwe kwa utaratibu upi bila kuwaathiri kielimu darasani. Ikumbukwe kuwa mtu akipewa kuchagua kati ya kitu kigumu na chepesi atachugua chepesi kisicho na changamoto nzito na nyingi michezo ni miepesi kwa sababu kwa sehemu kubwa inaenda na uhiari, elimu ya darasani kwa kuwa ni vitu vigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni mashindano gharama zake zitalipwa na nani na kwa utaratibu gani? Na yataendeshwa vipi? Kama ni elimu ya ufundi wa michezo kwangu mimi ndiyo muhimu kama ndiyo naomba kujulishwa muhtasari wa michezo ipi iliyo tayari na kama imesambazwa? Je, walimu wa kutosha wapo?

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa utaratibu mzuri wa kuanzisha shule za sekondari karibu kila kata, kote nchini. Hata hivyo nina machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upo upungufu mkubwa kwa baadhi ya walimu wa shule hizo za sekondari za kata hasa maeneo ya vijijini. Hali hii inatokana na baadhi ya walimu hao wakihitajika kwenye shule walizopangiwa wanakosa nyumba za kuishi, matokeo yake huamua kurudi alikotoka. Nashauri Serikali iwe inawalipa fedha za kuanzia maisha ili wanapokosa nyumba, waweze kuishi kwenye nyumba za kupanga na kwa walimu wanaopewa uhamisho wawe wanalipwa mapema fedha za uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo pia tatizo sugu la wanafunzi wa kike kupewa mimba na baadhi walimu na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya walimu hao kwa sababu ya udanganyifu unaofanywa kwa wazazi wa wanafunzi hao kwamba wasitajwe ila mtoto wao atatunzwa na hupewa fedha kidogo kisha hutelekezwa. Nashauri ipigwe marufuku kwa walimu wasiooa kuwatumikisha wanafunzi wa kike kwa kazi za nyumbani kwa walimu kama vile kuwapikia, kuwachotea maji na kadhalika. Kwa vile huwa nikishawishi kimojawapo cha kuwabaka na mwanafunzi huogopa kumtaja mwalimu.

Pia lipo tatizo la shule za sekondari za bweni kuwa na malimbikizo ya madeni kiasi cha shule kukosa chakula kwa wanafunzi. Mfano shule ya sekondari ya Iyunga mkoani Mbeya iliwahi kufungwa kabla ya wakati kutokana tu na kukosa chakula si Iyunga tu, hivi sasa ni shule nyingi zimefungwa. Naishauri Serikali ilitazame tatizo hili kwani linasababisha chuki kati ya wazazi, jamii na Serikali yao. Aidha, Wizara iwe inafuatilia kwa makini shule hizo ili fedha zinazotolewa kwa ajili ya chakula kama zinatumika ilivyokusudiwa, wapo baadhi ya viongozi wa shule hizo ambao siyo waaminifu, hivyo huchangia kiasi kikubwa kuwepo kwa upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja 100%.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara ya walimu wa vyuo vikuu, walimu wa vyuo vikuu mfano *Faculty of Law University of Dar es Salaam*, walimu wetu hawa wanalipwa mishahara midogo isiyokidhi mahitaji ya walimu wetu. Kutokana na hali hiyo walimu wa vyuo vyetu hulazimika kuingia mitaani na kufanya kazi zao binafsi yaani *consultanchy.*

Katika kufanya hivyo muda wa kuwafundisha vijana wetu unapotea na matokeo yake tunapata wanafunzi ambao hawakutayarishwa vizuri na kwa kuwa wanafunzi hawa tunawahitaji wawe wataalam kwenye sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya kutoa haki yaani sheria (mahakama na wawakili wa Serikali) ni dhahiri kuwa huduma itakayotolewa itakuwa siyo bora. Ni muhimu sana Serikali iwezekeze katika eneo hili ili tupate *output* yenye viwango kwa *future* ya nchi yetu. *Nothing comes out of nothing.* Tuwalipe walimu wetu wa vyuo vizuri kwani pia hii itatupunguzia walimu wetu kukimbilia nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee elimu ya vitendo shuleni. Elimu ya vitendo ni muhimu lakini kwa bahati mbaya sana shule nyingi hazina maabara wala umeme. Napendekeza Wizara ijitahidi kununua *science kits* angalau kwa kuanzia wakati tunajiandaa kujenga maabara ya kudumu. Pia Serikali iwekeze katika umeme unaotumia nguvu ya jua kwa kila shule kwa ajili ya mwanga na *practical.* Ni lazima Serikali iweze

sana katika maeneo haya vinginevyo Taifa letu litaendelea kukosa wanasayansi ambao ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa walimu wa sayansi na hisabati ni tatizo kubwa linaloikumba nchi yetu. Nashauri wanafunzi wanaosoma sayansi wapewe upendeleo wa kupatiwa mikopo tofauti na wengine.

Pia walimu wa sayansi na hisabati wapewe mishahara mizuri na marupurupu zaidi ili kuwatia moyo kuongezeka. Mwalimu anayetoa wanafunzi wenye alama za juu katika mitihani ya Taifa wapewe *bonus* kwa kila alama ya A katika *Physics, Chemistry,* au *Mathematics* apewe shilingi 10,000/= au zaidi. *Bonus* hii itawafanya walimu wajitume sana kufundisha masomo ya sayansi. Narudia kusema kuwa ni lazima Serikali iwekeze katika eneo hili. *Nothing comes out of nothing.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo kwa walimu, mikopo ya vifaa vya ujenzi, pikipiki, baiskeli hata magari. Walimu wetu wanashindwa kukopa fedha na vifaa vya kutosha kwa kuwa mishahara yao ni midogo hivyo mwalimu hawezi kukopa fedha yoyote ya maana itakayomsaidia. Napendekeza mishahara ya walimu kuanzia shule ya msingi, sekondari na vyuo iongezwe ili waweze kukopesheka kwenye mabenki ya biashara.

Kuhusu mafunzo, Serikali igharimie mafunzo ya walimu wanaotaka kujiendeleza. Baadhi ya walimu hawalipiwi fedha za masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya ualimu, kwa kuwa tunao uhaba wa walimu na kwa kuwa shule zetu za kata hazitaweza kupeleka watoto wote *High School* ni muhimu kuwa na vyuo vya ualimu japo viwili au vitatu kwa kila wilaya. Programu hii itasidia kutuondolea uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mimba kwa wanafunzi wa sekondari limekithiri. Pamoja na sababu nyingine mojawapo ni uhaba wa hosteli kwa wanafunzi wetu. Wanapewa mimba huko mitaani wanakolala wanakutana na wanaume wapuuzi wanawarubuni watoto wetu.

Kuhusu tatizo la uhaba wa walimu Karagwe, Wilaya ya Karagwe ni Wilaya ambayo iko pembezoni na mpakani mwa nchi za Uganda na Rwanda. Walimu wengi wanaopangwa Karagwe hukataa kwa kisingizio kuwa ni mbali. Lakini tatizo lingine linalochangia ni uhaba wa nyumba za walimu. Tunaomba nyumba za walimu na walimu wa kutosha. Pia walimu walio mpakani wapewe posho ya mazingira magumu. Pia wanakatishwa tamaa kwa kucheleweshewa mishahara yao. Ni lazima mshahara ulipwe ndani ya mwezi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chakula, uji, chai kwa wanafunzi, nashauri Serikali iwapatie watoto wetu wa shule za msingi chakula angalau uji basi ili kuwawezesha kusikiliza vizuri wanayofundishwa.

Kuhusu malipo ya walimu, walimu wetu warejeshewe fedha zao za matibabu, marekebisho ya mishahara *(arrears),* fedha za likizo na za uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitihani ya darasa la nne na kidato cha nne ndiyo kigezo pekee na kizuri cha kupima uwezo na uelewa wa wanafunzi. Pia mitihani hii itatoa msukumo wa watoto wasome.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzito ya kuelimisha Taifa. *Good job, keep it up.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Gaudentia Kabuka na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Katibu Mkuu wa Wizara, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa hotuba iyotayarishwa vizuri kwa kuainisha utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 na kueleza malengo yaliyopangwa kwa kutekelezwa kwa mwaka 2007/2008 na kutoa malengo ya mwaka wa fedha 2008/2009 vile vile imechanganua kila idara na vyuo vyote. Nawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina machache ya kuchangia madai ya walimu yaliyokaa kwa muda mrefu, malimbikizo ya mishahara, madeni ya matibabu, uhamisho na malipo ya likizo, walimu waliojisomesha bila kurejeshewa malipo, kwa nini yanaendelea kulimbikizwa? Na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake hajaeleza utaratibu gani utachukuliwa kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo na ushauri kama hayalipwi kwa sasa ni vizuri akajulishwa kuhusu stahili yao na kama hawastahili vile vile wajulishwe na kiasi gani wanastahili kulipwa.

Utaratibu wa kupanga walimu kwa uwiano wa wanafunzi 45/50 kwa mwalimu mmoja urekebishwe kwa sababu kuna shule zenye wanafunzi wachache na ina wanafunzi mpaka darasa la saba au mpaka kidato cha nne kuna uwezekano wa kuwa na walimu wawili tu au mmoja tu. Katika shule hiyo na wanafunzi wakakosa kupata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kuwa na sekondari mbili za kidato cha tano mpka sita kila Wilaya nampongeza sana, tatizo ni kigezo cha kuwa na mwalimu angalau mmoja mwenye shahada. Naomba Wizara iweke utaratibu wa haraka wa kuwapanga walimu kwenye Wilaya zote au kwa mfano Wilaya ya Mbarali nimekuwa nikiomba walimu wa aina hiyo kwani vigezo vyote tumetimiza na shule ya Madibira na Rujewa zilikwishateuliwa na ombi la walimu tumeliwasilisha ofisini kwako Waziri wa Elimu.

Kuhusu bodi ya mikopo, bado kuna tatizo kuhusu utoaji wa mikopo utaratibu wanaotumia umefanya wanafunzi wengine wakose, sijajua ni vigezo gani wanatumia tofauti na uamuzi wa Serikali.

Pia naomba kujua kwa nini pesa za mikopo kwa ajili ya mafunzo zinachelewa sana kutoka bodi ya mikopo kwenda vyuo husika. Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa walimu na vyuo kuhusu uwasilishaji wa pesa zinazotakiwa kulipwa kwa ajili ya wanafunzi wanaopelekwa kwenye vyuo hivyo.

Kuhusu hosteli za Chuo Kikuu cha Muhimbili zilizoko *Chole Road* ni lini zitakamilika ili wanafunzi wa chuo hicho wahamie huko ili kupunguza msongamano wa wanafunzi kulala chumba kimoja zaidi ya wanne? Mwaka huu nimepitia kwenye kitabu cha maendeleo sijaona pesa yoyote iliyopangwa kwa ajili ya ukamilisho wa hosteli hizo. Lakini kwenye malengo ya kazi za mpango wa kukamilisha lipo. Naomba kujua pia uendeshaji wa hosteli hiyo utakuwaje na utakamilika lini? Na nini mpango wa usafiri kwa wanafunzi wa chuo hicho ukizingatia wengi wanakaa hosteli za Mabibo na maeneo mengine na nauli na usafiri inabidi kujitegemea.

Kuhusu ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Muhimbili ni vizuri ukaendelea kufanyika sambamba na ujenzi wa vyuo vikuu vipya, kwa kweli hali ya majengo yote haya si nzuri sana hasa mabweni yote yana matatizo.

Naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma, na kasi kubwa inayoendelea kwa sasa ikiwa imezingatia mahitaji yote yanayotakiwa kwa Chuo Kikuu, nimetembelea hivi karibuni, napongeza sana! Ushauri sasa ni kuendelea kujitangaza ili wananchi wa ndani na majirani wajue kuna chuo hicho na kozi zinazotolewa na zitakazotolewa baada ya kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kujua vyuo vikuu tulivyonavyo nchini vimeshiriki vipi kuandaa wanafunzi wanaotegemea wajiunge katika vyuo hivyo wanapokuwa kwenye elimu ya msingi na sekondari. Ili kuondoa au kupunguza tatizo linaloonekana kujitokeza sasa, kuwa wanachuo wengi wanachagua kozi kwa lengo la urahisi na kupata kozi. Kwa hivyo, vyuo vikuu visipokuwa na kitengo cha kutoa elimu ya umuhimu wa kila masomo au kosi tunaweza tukajikuta tunakosa kabisa baadhi ya walimu au wataalam wa aina fulani ambao soko la kazi ni dogo sana kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la walimu wa hesabu kuanzia elimu ya msingi na sekondari ni kubwa sana. Hesabu ni somo muhimu sana naomba Wizara iangalie ni vipi itaongeza walimu hawa ili kila shule iwe na mwalimu mwenye uwezo wa hesabu na kiingereza.

Naunga mkono hoja na kumuomba Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake ajipange vizuri ili tuondoe kero hizi za muda mrefu za walimu tuanze upya ili tuwe na ajira mpya za walimu.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe kwa kufanya kazi zako kwa umahiri mkubwa na vile nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri pamoja na timu yake yote kwa kuiandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya uwalimu ni kazi ngumu sana inahitaji uvumilivu mkubwa. Walimu wanaishi maisha duni, hawana makazi, mshahara hautoshi, hawawezi kutoa ufanisi mzuri kwa sababu Wizara haitekelezi majukumu yao vizuri. Madeni yalipwe ili wanafunzi wapate huduma shuleni kama chakula na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zetu zina upungufu wa walimu na hata vitendea kazi na Serikali inahimiza somo la sayansi lisomeshwe kwa kasi zaidi, lakini la kusikitisha hizo shule hazina maabara wala vifaa vya kusomeshea hilo hupelekea wanafunzi wengi kutokufaulu masomo yao kwa hiyo, Serikali ifanye wajibu wake kwa kuboresha mapungufu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wapatiwe majengo mazuri ili wabakie vijijini badala ya kukimbilia mjini na wapate mishahara yao mapema, wasicheleweshewe au kupata usumbufu mishahara yao kupelekwa Wilaya nyingine. Vile vile matokeo ya mitihani ya wanafunzi yasicheleweshwe kwa sababu watoto wanabakia nyumbani muda mwingi kiasi ya miezi mitatu jambo ambao yanawarudisha nyumba kwenye masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watoto wengi wa kike wanabeba mamba, hii inarudisha nyuma maendeleo ya elimu kwa mtoto wa kike. Jumla ya watoto 18,000 toka mwaka 1905 hadi 2008 hii inasikitisha kwa hiyo, sasa hivi tunataka *fifty, fifty,* kweli tutafika?

Kwa hiyo, naiomba Serikali, kwa mtu yeyote atakaembaka mtoto au kumpa mimba hata ikiwa ni mwalimu wake achukuliwe hatua ama kifungo cha maisha na wahasiwe ili liwe funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kufanya kazi vizuri kwa kufuatilia matatizo katika shule lakini bado mnayo kazi ya kuhakikisha wanafunzi wanafaulu kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nawaombea kila la kheri.

**MHE. FATMA ABDALLA TAMIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuandika mchango wangu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri mwenyewe na Naibu Mawaiziri wake jinsi wanavyochukua jitihada kuiongoza hii Wizara usiku na

mchana kwa hali na mali mnaonyesha juhudi zenu hasa na kuonekana kuleta maendeleo makubwa katika sekta hii ya elimu nakupongezeni sana pamoja na watendaji wenu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana kwa Bajeti hii. Bajeti mama au ni roho katika mwili wa binadamu, ndio msingi wa maisha ya mwanadamu kutengewa fedha kidogo sana hazitoshi hata kidogo mahitaji ni mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iitizame Bajeti hii kwa jicho la pekee ili fedha ziongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar tulikuwa tuna mgao wetu maalum kuhusu elimu ya juu, tofauti na sasa hivi ule mgao haupo tena tunachanganyishwa na mikoa yote katika uombaji wa nafasi za elimu ya juu kwani iwe hivyo kwa sababu Zanzibar ni nchi na ina mamlaka yake kamili kama nchi nyingine zilivyo hii inasababisha au inachanga kuongeza katika kero za Muungano. Tunaomba kurudishwe utaratibu wa zamani wa kupewa nafasi zetu kwa sababu Zanzibar ni nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninahuzuni sana kutokana na asilimia nyingi ya wanafunzi wadogo kupata mimba mwaka hadi mwaka na kusababisha hata kupata ongezeko kubwa la UKIMWI kwa sababu ya kupata ujauzito wanafunzi kwa kufanya ngono isiyokuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu waombwe wazazi kushirikiana na walimu katika malazi ya watoto wetu kwa kila mara kufanya vikao baina ya wazazi na walimu na wazazi kufuatilia nyendo za watoto ili tusiwaachie walimu peke yao na kufuatilia maendeleo ya watoto wetu shuleni ili mtoto asijione yuko huru na kusababisha utoro shuleni na kufanya vitendo visivyo na maana ili tupate kulinda mila zetu, silka zetu na desturi ili kulinda mmomonyoko wa maadili yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, shule binafsi, nashukuru takwimu za Wizara hasa katika sekta hii binafsi kuhusu elimu, kwa taasisi, watu binafsi, mashirika ya dini na kadhalika. Katika kusaidia sana kuinua viwango vya elimu hasa kwa kuwa na ongezeko la shule na kujishughulisha kwa karibu katika sekta hii maarufu kama wadau wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tunakubali huduma wanayoitoa lakini naomba Wizara iwe karibu sana na shule hizi ili kuona ubora na viwango vya vitu mbalimbali vinavyotolewa ili kupata elimu bora *(Quality education),* kuangalia viwango vya ada na masuala ya kiutawala kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa maana kwamba inatisha pale tunapoona wamiliki wa shule binafsi kuwa na maamuzi yenye nia ya kukiuka misingi ya elimu. Inapaswa kueleweshwa juu ya umiliki wao *(owner)* lakini shule inabaki kuwa ya

wanafunzi (umma) ambao ndio wameshiriki kutumia shule hiyo na pia wazingatie wanapopewa cheti cha uendeshaji ulioridhiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha vitendo vilivyofanywa na mmiliki wa shule ya sekondari ya *Green Acres High School*, Julian Buyogo wa Dar es Salaam kwa kitendo alichokifanya hivi karibuni kwa kutumia nguvu nyingi katika kutuliza ghasia, zilizojitokeza shuleni hapo na yeye mwenyewe kufyatua risasi huku akiwa amelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo alichokifanya pamoja na kwamba vurugu zilitokea ni hatari kwani vipo vyombo vya kiusalama ambavyo ndivyo vilivyo na uwezo wa kutuliza ghasia. Naomba Waziri achukue hatua kali kwa mmiliki huyo na wengine wenye tabia zinazofanana na mmiliki wa shule hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, suala la mtihani wa darasa la nne na kidato cha pili ni muhimu sana kwa kuwa kunamfanya mwanafunzi kuweka juhudi, tangu awali kwa maana akijua asipofanya bidii basi hataendelea. Kufuta mitihani hii kutazorotesha juhudi za elimu. Ahsante.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo machache katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu katika hili tunapaswa kutambua umuhimu wa mwalimu katika maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Pamoja na umuhimu mkubwa wa mwalimu kwa maendeleo ya Taifa letu bado amekabiliwa na matatizo kadhaa katika kuleta ufanisi wa kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wetu wanafanya kazi nzito lakini Kipato chao hakiridhishi kabisa. Mishahara ya walimu ni midogo sana, haiwezi kukidhi haja ya maisha kwa wakati tulionao. Pamoja na ufinyu wa mishahara hiyo, hawaipati kwa wakati, upo ucheleweshwaji mkubwa wa mishahara hiyo. Aidha, walimu wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kwa kukosa nyumba bora za kuishi maeneo ya kazi, huduma nyingine muhimu kama usafiri, umeme, tiba za afya na kadhalika. Walimu wanao mzigo wa kufundisha idadi kubwa ya wanafunzi kwa darasa moja jambo ambalo linapunguza ufanisi wa kazi. Pamoja na matatizo hayo walimu pia wanapata usumbufu mkubwa wa fedha zao za likizo ama kwa kucheleweshwa au wakati mwingine kuzikosa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanafunzi, zipo changamoto mbalimbali zinazowakabili wanafunzi wetu na hivyo kutokufanya vizuri katika masomo yao au wakati mwingine kutoroka masomo. Michango ya mara kwa mara ni kero kubwa kwa wanafunzi wetu na wengi hawamudu. Ukosefu wa vitendea kazi shuleni kama madaftari na hata chaki, vitabu vya mazoezi, madawati ya kukalia na kadhalika vinarudisha nyuma ufanisi wa wanafunzi.

Kwa wanafunzi wahitimu wanakabiliwa na tatizo la kupata vyeti vyao au *result slip* za matokeo yao kwa urahisi. Hili linahitaji kupatiwa ufumbuzi lisiendelee kuwakatisha tamaa wahitimu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ni midogo sana na ina usumbufu mkubwa katika kupatikana kwake. Aidha, imedhihirika kwa wanafunzi wa tabaka la watu wa chini ambao wengi wao ni vigumu kupata daraja la kwanza na la pili utakuwa ni ndoto. Tatizo hili litapelekea kujengeka tabaka la walionacho kuendelea kupata elimu nzuri na tabaka la walio wengi kuishia na elimu na kujua kusoma na kuandika tu. Hivyo, basi ni vyema utaratibu wa mikopo ukaangaliwa upya, usiwatenge watoto wa Watanzania maskini walio wengi. Ahsante.

**MHE. MARGARET A. MKANGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda sasa nimekuwa nikihimiza Serikali kuimarisha kitengo cha elimu maalum pale makao makuu ya Wizara na mikoani si kwa kuongeza watendaji tu bali hata kimuundo wa kitengo. Naendelea kuishauri kuwa kitengo hiki wakati umefika kiwe kurugenzi kwa vile watoto wenye ulemavu wanaongezeka licha ya mauaji ya albino. Baadhi ya wazazi wameacha kuwaficha watoto wao, walimu husika wanajitolea kufanya kazi hata ya kuwafuatilia watoto wenye ulemavu kwenda shule na kuwarudisha baada ya masomo. Changamoto za watoto wenye ulemavu ni nyingi, hivyo kuhitaji nyongeza ya raslimali watu na fedha, nashauri wakati umefika sasa kitengo hicho kiwe kurugenzi kamili.

Pia katika kuimarisha kitengo kuwa kurugenzi, nashauri kuwa pawe na maafisa elimu wa elimu maalum katika ngazi ya wilaya kama ilivyo kwa afisa elimu vifaa, ufundi na kadhalika. Katika ngazi hii, hasa ikizingatiwa suala la ushushaji madaraka wilayani/halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu naunga mkono hoja kwa mategemeo kwamba nitapata majibu sahihi, yatakayoambatana na utekelezaji wa Wizara katika *issues* mbalimbali.

**MHE. BENSON M. MPESYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii, kwanza kumpongeza Mheshimiwa Profesa Juamnne Maghembe kwa hotuba yake nzuri yenye maandalizi ya kitaaluma. Pia napenda kuwapongeza Naibu Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, kwa kumsaidia vema Mheshimiwa Waziri katika kutuendelezea Wizara hii nyeti.

Pili, naomba nitumie nafasi hii pia kuwapongeza walimu wote wa jimbo la Mbeya Mjini kwa kufanya vizuri Kimkoa na Kitaifa, hasa upande wa shule za msingi. Nawapongeza walimu wote wa *St. Francis Girls Secondary School* kwa kufanya vema katika masomo ya Kidato nne kwa mwaka 2007 na kushika nafasi ya kwanza Kitaifa na kupelekea kuwa na wasichana wengi waliofanya vema kwenye masomo ya sayansi.

Tatu, naomba nieleze masikitiko yangu juu ya maendeleo ya shule ya sekondari Iyunga, hii ni shule kubwa na yenye hadhi yake na historia ya kipekee katika mkoa wa Mbeya na Kitaifa pia. Mpaka sasa hivi shule hii imefungwa toka tarehe 6 Mei, 2008, mpaka leo hii shule ya Iyunga haijafunguliwa. Hii si halali na inawanyima watoto haki ya kusoma na kupata misingi bora ya elimu. Sababu ya kufungwa kwa shule hii ni

madeni sugu, kama ifuatavyo, umeme shilingi 13,000,000/=, maji shilingi 19,000,000/= na chakula shilingi 570,000,000/= za wazabuni.

Pamoja na kuhakiki madeni yote kwa zaidi ya mara tatu bado tatizo hili halijapatiwa majibu, ningependa kujua ni lini deni hili litalipwa? Na ni lini shule itafunguliwa rasmi ili kuwapatia vijana hawa elimu na haki yao, takriban wanafunzi 1,380. Elimu ya sasa ni mashindano, itakuwaje kwa Iyunga sekondari?

Nne, ni juu ya suala zima la kukiimarisha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na chuo hiki na majukumu yaliyopo mbele yake, ni lazima matatizo ya kina yapatiwe ufumbuzi wa haraka ili wimbi la vijana wanaomaliza kidato cha sita, hasa wale wanaotokana na mpango wa *MMES* waweze kupata elimu na ujuzi bila matatizo.

Naomba nishauri, kama mjumbe wa *council* ya Chuo Kikuu Huria, tatizo kubwa ni kutumika kwa *OC.* Kama eneo la kulipia malipo ya walimu *(part timers).* Katika nchi zinazoendesha mfumo huu wa elimu huria, wana mfumo tofauti katika kuwalipa *(part-timers)* na hivyo kufanikiwa kufanya vizuri katika eneo hili la kutoa elimu huria. Nashauri malipo ya *part-timers* yawekwe ndani ya *personel emoluments' (PE).* Utafiti umeonyesha kuwa hii ndiyo njia sahihi ya kuwa na *part-timers* wanaoweza kufanya kazi vizuri na kutoa matokeo ya mtihani kwa wakati.

Tano, madeni ya walimu, naipongeza Serikali kwa kulipa malimbikizo ya madeni ya walimu takriban shilingi bilioni 7.1 kati ya shilingi bilioni 9.1 zilizokuwa zikidaiwa. Serikali itafute njia endelevu ya kuyalipa madeni haya. Mpaka sasa bado Serikali inadaiwa tena shilingi bilioni 12, deni hili isiachiwe Wizara tu, tunahitaji *intervention* ya Hazina katika tatizo hili.

Sita, hii ni mara yangu ya tano, naomba ombi lile lile, naomba shule ya sekondari Mbeya ipatiwe gari la usafiri, shule imekuwa kubwa na ni ya bweni wana gari chakavu la muda mrefu ST.61. Naomba safari hii ombi langu lipewe uzito unaostahili.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii nami nichangie katika hoja hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa juhudi zao kubwa wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hotuba hii kama ifuatavyo, kwanza ni kuhusu malimbikizo ya madai ya walimu. Ni lini Serikali itaacha kuwaonea walimu kwa kutokuwalipa mishahara yao kwa wakati? Kwani malimbikizo ya madai ya walimu ni makubwa sana. Ni sababu zipi zilizopelekea Wizara kuwalipa walimu madai yao pale tu walipotishia kugoma? Je, pesa hizo zilitoka wapi, kwa nini hazikulipwa mpaka watishie kugoma? Tafadhali naomba majibu. Fedha hizo ni mishahara, marekebisho ya kupewa vyeo, fedha za matibabu, likizo, uhamisho na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za walimu, madarasa na hosteli, inasikitisha kuona kuwa mzigo mzito wa kujenga nyumba za walimu ni wa wanafunzi na wananchi. Hivi kuna tofauti gani ya kufuta kodi ya kichwa na michango wanayosumbuliwa wananchi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, mara hosteli, jamani si bora kodi ya kichwa irudi? Maana wananchi wanasumbuliwa na hata wengine wanakimbia nyumba zao. Tafadhali naomba jibu, kwa nini Wizara isibebe mzigo wake?

Kuhusu mazingira mazuri ya walimu, hapa Bungeni mara kwa mara nimesikia Mawaziri wakijibu maswali juu ya walimu kutokwenda kuripoti walikopangiwa au wanaripoti tu na warudi kutokana na mazingira mabovu, jibu inakuwa ni kwamba Halmashauri au wenyeji wa eneo lile waweke mazingira mazuri kwa walimu wapya. Hivi Waziri anafahamu kuwa kuna Halmashauri zingine hazina uwezo kutokana na uchumi wa eneo lile. Pia hali halisi ya wananchi wa eneo husika wao wenyewe hawako katika mazingira mazuri kutokana na hali ya uchumi wa eneo husika, hawaoni kama wanaigawa nchi kwa kupata wasomi toka sehemu moja na nyingine kubaki duni? Kwani walionekana hawana uwezo watapata walimu tena wazuri. Jamani, Wizara ibebe mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wasomi wa nje ya nchi, naomba kumuuliza Waziri kuwa je, Serikali ina utaratibu gani juu ya kuwatambua wasomi wote walioko nje ya nchi? Je, inawatumiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la uhaba wa vitabu shuleni ambavyo ndio msingi mkubwa kati ya mwalimu na mwanafunzi, bila vitabu elimu hiyo ni batili.

Je, Wizara inatambua kuwa utaratibu wao wa sasa wa kusambaza vitabu ni mbovu? Kwa nini wasitumie mpango wao wa zamani wa kwenda kuvinunua moja kwa moja *publishers?* Kwani utaratibu wa sasa unaotumika ni wa kibabaishaji na unatoa mwanya mkubwa kwa wizi na udanganyifu. Wizara inaweza kulipa fedha ya vitabu 100, lakini vikapelekwa vitabu 10 tu. Je, Serikali pia Wizara inasemaje kuhusu vitabu ambavyo viko kwenye maghala hapa nchini? Je, inajua hilo? Kama halijui, je, Waziri atakuwa tayari kutembelea maghala yale, ajionee yalivyofurika na watoto wetu wanapata taabu, kitabu kimoja watoto kumi. Je, Waziri anasemaji?

Kuhusu Baraza la Mitihani, kuna tatizo kubwa sana limetokea Baraza la Mitihani, hili nitaomba Waziri anijibu kwa makini, kwani kuna mambo mengine inabidi yachukuliwe kidharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi waliojiandaa kufanya mitihani wanaojulikana kama *private candidate* wengi wamefutiwa usajili wa kufanya mtihani mwezi wa kumi na hali wakiwa wamelipia taratibu zote pamoja na *tuition fee.* Sababu walizotoa, eti ni majina kukosewa, jamani, tutafika kweli? Hivi ni utaratibu wa wapi? Kwa nini mambo haya yasirekebishwe? Mnataka hawa waende wapi? Mimi naomba Waziri anipe jibu na atoe tamko, hawa vijana wafanye mtihani. Muda bado upo na ni vizuri tu kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Mikopo, kwa kusema hayo, naomba nizungumzie juu ya Bodi ya Mikopo, kweli fedha zilizotengwa hazitoshi kabisa, ni vita nyingine tena, watu wa bodi wanapata shida kubwa kwani wanafunzi wapya na ongezeko kubwa, pia wale ambao wameshaaanza lazima waendelee. Hivi naiomba Serikali iongeze pesa kwenye bodi hii.

Mwisho, naomba kujua fedha zilizotengwa kwenye Wizara hii je, ndizo Wizara ilivyoomba na ndio Bajeti yao? Na kama sio je, mambo yataendaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema na kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, Naibu katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote ambao kwa namna moja au nyingine wametoa mchango wao katika kufanikisha utayarishaji wa hotubu hii. Baada ya pongezi hizo sasa niingie katika kuchangia hotuba hii mambo mawili/matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kutoa kipaumbele cha kwanza katika kupanga Bajeti yake kwa Wizara hii ya Elimu ili kuinua kiwango cha elimu nchini na kujiweka tayari katika ushindani wa Kimataifa kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaelewa kwamba hakuna Taifa lolote linaloendelea au lililoendelea bila ya kuwa na wasomi (wataalamu) waliopata elimu iliyo bora kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora haiwezi kupatikana na vyuo vikuu moja kwa moja bali lazima ianzie toka shule za awali, msingi, sekondari na baadae vyuo vikuu. Elimu bora sio tu kujiandaa kwa kujenga majengo mengi ya madarasa bali pamoja na hilo, pia pawepo na mikakati madhubuti kuhakikisha panakuwepo vitendea kazi vya kutosha, walimu wa kutosha na wenye ujuzi unaolingana na ngazi zao wanazofundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa vigumu sana kwa Serikali kufikia lengo la kupata elimu bora kama Wizara ya Elimu haitakuwa tayari kivitendo kutatua matatizo yanayowakabili hasa yale ya walimu kuanzia shule za msingi hadi wa vyuo vikuu kama vile kulipwa mishahara yao kwa wakati, (kuna taarifa Mheshimiwa Naibu Spika hadi kufikia tarehe 30/05/2008, mishahara ya mwezi Mei, 2008 ya walimu wote walio chini ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu ilikuwa haijalipwa).

Matatizo mengine ni kulipwa pesa za likizo ipasavyo, kujengewa nyumba hasa kwa walimu wanaofundisha vijijini na ikiwezekana basi sio vibaya kama ama Wizara au

Chama cha Walimu wakatafuta mikopo kutoka mashirika au mabenki ili kuwasaidia walimu waweze kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyefahamu ugumu wa kazi ya ualimu na hali duni ya kipato chao. Hivyo basi Wizara ikiweka mikakati mizuri ya kuwaondolea matatizo yao niliyoyataja hapo juu ni dhahiri itawafanya walimu wetu watulie na waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa na endapo walimu watapuuzwa kutatuliwa matatizo yao na kuwajali katika maslahi yao mbalimbali, tutawafanya wahangaike kujitafutia maslahi na hapo itakuwa vigumu ile dhana nzima ya elimu bora kufikiwa na badala yake kutabaki na ile dhana ya bora elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu tatizo sugu la madeni ya wazabuni. Lazima tukubali kwamba umefika wakati sasa kwa Wizara ya Elimu ikae na kujipanga upya na kuona haja ya kuyalipa madeni yote ya wazabuni ili watoto wetu walio katika shule za bweni waweze kupatiwa chakula kwa wakati na cha kuridhisha ili kuwajenga mwili na akili na waweze kusoma kwa utulivu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu mitihani ya darasa la nne na kidato cha pili. Mimi kwa mawazo yangu naona bado ipo haja ya kuendeleza kuwepo kwa mitihani hiyo ingawa baadhi ya watu wanaipinga kwa kisingizio tu eti inachangia mdondoko wa wanafunzi wale wasiofaulu mitihani hiyo na pale wanapotakiwa warudie mwaka. Hii sio sababu ya msingi, kwani kumuacha mwanafunzi aendelee kusoma tu toka mwanzo wa mwaka hadi mwisho na kutoka darasa la kwanza hadi la kumi bila kufanyiwa mitihani, kwa kweli hii ni kumdumaza mtoto na kumfanya asiwe na hofu juu ya masomo yake kwani anajua hatakuwa na kikwazo chochote kitakachomfanya ajiandae kwa mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitihani kwa kweli ni mizuri na ni vyema iwepo na kama dhana hiyo ya kusababisha mdondoko basi mimi ningeshauri mitihani iwepo lakini ya mchujo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na madai ya walimu. Kwa muda mrefu walimu wameilalamikia Serikali kuhusu mishahara yao kutolipwa kwa wakati unaopaswa. Aidha, wana madai yanayohusu marekebisho ya mishahara, baada ya kupandishwa vyeo. Madai haya kwa mwaka 2006/2007 yanafikia kiasi cha shilingi 12,266,697/=. Kutokana na takwimu za *VWT* katika mikoa 21 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali iliangalie upya suala la madai ya walimu ili kuepusha migogoro na migomo isiyo na misingi.

Kuhusu uhaba wa nyumba za walimu ni tatizo lingine ambalo linalalamikiwa sana na walimu nchi nzima. Pamoja na jitihada za wazi kuhusu jitihada za Serikali katika miradi ya *MMEM* na *MMES* ni vema Serikali ijitahidi kuongeza nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa walimu hasa katika shule za sekondari ni mkubwa sana. Hali hii inakuwa dhahiri kila mwaka kutokana na mafanikio ya *MMEM* ambayo imeandikisha watoto wengi kuliko uwezo wa Serikali kufundisha walimu wanaolingana na upanuzi wa shule za msingi kutokana na mradi wa *MMEM.* Serikali ingeshauriwa kupanua vyuo vya kufundisha walimu.

Aidha, Serikali ingejaribu kwa nguvu zote kuwaita na kuwaajiri walimu waliostaafu wafundishe kwa vipindi kwa mikataba.

Suala la Bima ya Afya *(NHIF)* walimu wengi (karibu wote) ni wadau na wanachama wa mfuko huu wa Bima ya Afya. Pamoja na jitihada na kazi nzuri ya mfuko huu, kumekuwa na malalamiko miongoni mwa walimu wafundishao vijijini kuwa huduma ya mfuko huu hairidhishi. Walimu wanashauri kuwa huduma za mfuko huu wa Bima ya Afya ingeboreshwa hasa usajili wa maduka ya dawa ambayo ni machache vijijini. Kwenye suala la Bima ya Taifa *(NIC)* ni eneo lingine linalololalamikiwa na walimu. Walimu wengi walikuwa wamechangia bima za maisha kwenye Shirika la Bima la Taifa *(NIC).* Baadhi ya bima zao zimeiva lakini hawajapata malipo yao. *NIC* ilitoa ahadi ya kuwalipa stahili zao tangu mwaka 2001, lakini hadi leo wanachma hawajapata mafao yao ya Bima. Ni vizuri Serikali sasa (ambayo ndio inamiliki Shirika la *NIC)* itoe tamko kuhusu haki za wanachama hawa

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu Mawaziri wote na watendaji wake wa Wizara kwa kufanikisha na kuwasilisha Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndio msingi wa maendeleo yote na tarajio la Serikali kumfikia kila mtu. Kwa hiyo naiomba Serikali ikipitishwa Bajeti hii kusimamia vizuri ili elimu ya mwanzo ya msingi, sekondari na ya juu na elimu nyingine ipatikane zaidi ya ilivyo sasa na tuweze kujitegemea kwa wataalamu wa mambo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaofundishwa Tanzania kwa gharama zote watumike ndani ya Tanzania wasiruhusiwe kwenda kufanya kazi nje kuancha uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mitihani au Baraza la Mtihani kwa nini hadi leo au mwaka huu bado hawako makini juu ya mtihani kupenya na hawa wanaopenyesha ni kina nani? Na Serikali kwa sasa watachukua udhibiti gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu kwa kweli wanahitaji kuenziwa kwa hali zote. Naomba sasa Serikali iwafikirie. Kwa niaba ya wananchi wa Magogomeni na mimi mwenyewe naunga mkono hoja ipitishwe.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu wa maandishi.

Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na Naibu Mawaziri kwa maandalizi mazuri ya hotuba. Kwa namna ya pekee kabisa naipongeza Wizara kwa kutenga Bajeti ya kugharamia elimu ya sekondari, wanafunzi 51,000 wanaotoka katika familia duni na yatima. Hatua hii itaondoa hali ya watoto hawa kujisikia kutokuthaminiwa na kutengwa kwani wapo wengi waliofaulu kujiunga na sekondari lakini hawakuweza kusoma kutokana na kukosa ada pamoja na mahitaji mengine.

Napenda kuishauri Serikali iwasaidie pia wale ambao wangetaka kujiunga na vyuo vya ufundi kama *VETA* lakini hawana uwezo. Vile vile wapo wale wanaopoteza wazazi au walezi katikati ya masomo. Ni vema Serikali ikatenga fungu kwa ajili ya watoto wa aina hii.

Pia kuna tatizo la watoto waliofanya mtihani wa kidato cha pili bila kulipia ada ya mtihani, hawa huchelewa kuanza masomo ya kidato cha tatu au kuacha shule kabisa kwani huwa hawapewi matokeo ya mitihani mpaka hapo watakapolipia deni la ada ya mtihani. Kwa kweli huu ni uonevu mkubwa na kuwakosesha haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Suala la kuchangia ujenzi wa shule halifanyiki kwa uwazi katika maeneo mengi. Utawala bora unahimiza kata zote ziwe na mbao za matangazo. Napenda kuishauri Serikali ifuatilie kuhakikisha kuwa gharama zote zinazohitajika kwa ujenzi, pesa zinazotolewa na halmashauri kiasi kilichochangiwa na kila mwananchi pamoja na majina yao viwekwe wazi kwenye mbao hizi za matangazo kila mwezi. Kufanya hivi kutapunguza malalamiko na kuwawezesha wananchi kuchangia elimu kwa imani chanya.

Katika changamoto zilizopo katika kitabu cha hotuba ya Bajeti, ukurasa 94 kipengele cha (e), naishauri Wizara ishirikianie na mikoa kutambua maeneo yenye mazingira magumu pamoja na huduma zinazohitajika, kama ni maji, barabara, umeme, Wizara ya Elimu ijadiliane na Wizara husika ili kuyapa maeneo hayo kipaumbele katika kutoa huduma ili walimu/watumishi waweze kukubali kufanya kazi katika maeneo yote ya nchi yetu.

Ninao pia ushauri kuhusu utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi. Usahihishaji wa mitihani ufanyike kwa umakini na wanafunzi warudishiwe karatasi zao za mitihani kabla ya kwenda likizo ili waweze kufanya masahihisho na kujisomea. Walimu katika shule nyingi hawarudishi karatasi za mitihani kabla ya wanafunzi kwenda likizo wakihofia malalamiko ya upunjwaji wa alama katika usahihishaji. Tatizo hili husababisha

wanafunzi kutofuatilia vizuri yale yaliyofundishwa wakihisi kuwa kuna upendeleo na vile vile hukata tamaa kutokana na upunjwaji wa alama.

Suala la mishahara na maslahi bora kwa walimu ni la msingi sana kwa kuwa mishahara ya walimu ni midogo na hucheleweshwa, ni vyema Serikali ikawajumuisha walimu katika mpango wa mikopo ya JK (ya wajasiriamali wadogo) ili nao waweze kuanzisha na kuendeleza biashara zao ndogo ndogo. Walimu wakiwezeshwa kwa kupewa mitaji wataweza kupunguza ukali wa maisha.

Kuhusu walimu wajane na wale waishio na virusi vya UKIMWI wafikiriwe kwa kipaumbele cha kwanza kwa kupewa mikopo ili huduma yao iwe endelevu, wasikatishe huduma kwa sababu ya maradhi au vifo. Vile vile walimu hawa watakuwa na maisha marefu hivyo kuweza kuwaleta na kuwatunza watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano wa wasichana kwa kadri ya takwimu unaonekana kupungua kutoka shule za sekondari kwenda kidato cha tano na unapungua zaidi kutoka kidato cha sita kwenda elimu ya juu. Sera inaonyesha haja ya kuhamasisha wanafunzi wa kike wengi zaidi kuchukua masomo ya sayansi, lakini katika malengo ya mwaka 2008/2009 hakuna maelezo ya utekelezaji wa haja hii. Nashauri zawadi zitolewe kwa watoto wa kike wanaofaulu masomo ya sayansi tangu shule za msingi kwa madarasa yote hadi sekondari kuanzia kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa vyuo vikuu watumike vizuri kufanya tafiti mbalimbali na matokeo ya tafiti hizo yafanyiwe kazi katika kila sekta. Nashangaa ni kwa nini tunataegemea zaidi tafiti zinazofanywa na raia wa nchi za nje na hali Watanzania tunayo rasilimali watu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ahsante.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo yanayorudisha nyuma jitihada za wananchi kuendelea kujitolea kujenga shule za sekondari za kata ni ukosefu wa walimu katika shule hizo, vifaa vya kitaaluma na mara nyingine hata madawati. Ningependa kufahamu ni jitihada gani ambazo Serikali inachukua kukabiliana na matatizo hayo? Nafahamu wapo vijana wengi ambao wapo vyuo vya ualimu lakini kuna uhakika gani kuwa wakimaliza vyuo watakwenda kufundisha sekondari za kata wakati mishahara ni midogo kulinganisha na sekondari za binafsi *(private)* na mbaya zaidi huko anakopangiwa hata nyumba za kuishi walimu hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu Serikali ikaongeza nguvu katika ujenzi wa nyumba za walimu pamoja na mishahara inayokidhi haja. Kuhusu shule za msingi naiomba sana Wizara/Serikali kupitia halmashauri zetu kuhakikisha shule za msingi zinakuwa na madawati ya kutosha.

Kuhusu elimu ya juu, ningependa kupata maelezo ya kwa nini wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ardhi wamezuiliwa kupewa vyeti vyao vya kumaliza chuo? Inawezekana kuna madeni wanayodaiwa, lakini ni vyema wangepewa vyeti hivyo ili waweze kutafutia ajira na baadae waweze kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya kina kuhusu tatizo hilo la Chuo Kikuu cha Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Kwanza niipongeze sana taasisi hii kwa kazi nzuri sana wanayofanya ya kutoa elimu bora kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanaosoma katika taasisi hii wengi wao ni vijana ambao ama wamemaliza darasa la saba au kidato cha nne na kadhalika na wanaojiendeleza katika fani mbalimbali za ama cheti au stashahada. Lakini hili neno elimu ya watu wazima linakwaza sana na ukionyesha cheti cha taasisi hiyo kuna kama dharau kwamba umesoma ngumbalu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kubadili jina la taasisi hii hasa neno elimu ya watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Nawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri wake akiwa mama makini, Katibu Mkuu na manaibu wake, wakurugenzi na watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja za ufafanuzi, kwanza ni kuhusu fidia ya wazabuni waliohudumia (Songea) chakula Shule ya Sekondari Lekumba, shule hii ilipata misukosuko mingi ya kiuendeshaji kwa kuwa ilikuwa shule ya wazazi. Serikali kupitia Mawaziri wawili TAMISEMI kipindi kile cha Mheshimiwa Mizengo Pinda wakati Wizara ya Elimu alikuwa Mheshimiwa Margaret Sitta. Walishauri wananchi waridhie shule hiyo kuchukuliwa na Serikali na kwa kweli tukakubaliana hivyo. Kwa kuwa sasa shule hiyo iko katika uendeshaji wa kufuata sera ya elimu imerithi madeni na hasa deni la chakula la nyuma, shilingi milioni 50 halmashauri haina uwezo wa kulipa deni hilo. Nimemkabidhi Mheshimiwa Waziri barua maalumu ya kuomba Serikali isaidie tatizo hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Serikali kwa mwaka wa fedha uliopita shule zetu mbili za Serikali zimepanda daraja na kuwa zitatoa sasa elimu ya kidato cha tano na sita. Kwa muda mrefu shughuli nyingi za ujenzi wa shule hizi umefanywa kwa nguvu za wananchi halmashauri na Serikali kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kuwa tatizo kubwa ni la mabweni ili huduma hiyo ya elimu ya kati itolewe vizuri shule hizi zinahitaji kusaidiwa sana katika ujenzi huo wa hosteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Elimu ya Walimu Chekechea Wino, kwa kuwa msingi wa elimu bora kwa elimu ni kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano ambao kwa mujibu wa wanasayansi mtoto mdogo kutoka mwaka 0 – 5 ubongo wake unakuwa umeshaongezeka kwa asilimia 80 hivyo umuhimu wa kuwalea watoto hao kielimu ni muhimu sana, ni lini Serikali itaanza kuwaajiri walimu hao na hasa wale wanaomaliza chuo cha masista Wino ili wasaidie makuzi ya kielimu ya watoto hao na ni lini Serikali itazingatia umuhimu wa kuwa tena na shule za elimu ya awali kwa watoto *under five (5) years?*

Kuhusu mafao ya malimbikizo ya walimu,tatizo la malimbikizo ya mishahara na posho ya walimu limekuwa tatizo kubwa sana. Badala ya kupungua limekuwa likiongezeka. Uko umuhimu sasa wa Serikali kuangalia njia bora na muafaka ya kupunguza madeni hayo na kuendelea kutafuta namna yasiendelee kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watoto wa kike wanaopata mimba shuleni, kwa kuwa ipo mitazamo tofauti ambayo inapelekea kuonesha tatizo hili la mimba shuleni kutokuwa kubwa, naomba Serikali ichukulie suala hili kama ajali ambayo haitabiriki itatokeaje na athari yake haiwezi kutabiriwa, sisemi maana ya kupata mimba ni ajali ila mwenendo mzima wa tatizo hilo. Kama hivi ndivyo ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi kupitisha maamuzi ya kuhakikisha kuwa wasichana wanaopata mimba wanarudi shuleni ili kuendelea kupata elimu iliyokusudiwa katika kuwaletea maendeleo yao endelevu! Matokeo ya mama asiyeelimika ni kuendelea kuwa na Taifa la watoto wajinga.

Kuhusu Serikali kuongeza fedha za kasma ya chakula cha watoto shuleni, Wizara imepewa kipaumbele katika suala zima la elimu. Ni kwa nini mgao wa kutunza afya za watoto shuleni kwa maana ya kuongeza kasma ya chakula ni tatizo? Watoto wanapata taabu shuleni, tunaomba kama wazazi tuone umuhimu wa lishe kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa walimu. Mpaka sasa tatizo la walimu na hasa katika shule zetu za sekondari ni tatizo, mgao hauzingatii uwiano mzuri, uhamishaji usio na tija unaozifanya shule nyingine ziwe na matatizo. Mfano shule zetu ni muhimu ziwe na walimu mchanganyiko kwa maana ya kuwa na umuhimu mkubwa sana walimu wa kike nao wapelekwe shuleni. Zipo shule nyingi katika eneo langu zina upungufu mkubwa wa walimu wa kike na hivyo kuwafanya watoto wa kike wakose mwalimu wa kuwaongoza.

Kuhusu ujenzi wa maabara za sekondari, kwa takribani Bajeti mbili za kusaidia ujenzi wa maabara na mabweni katika mkoa wa Ruvuma zililenga Wilaya na mahitaji maalum, tunategemea sasa mwaka huu huduma hii itapelekwa katika halmashauri ya wilalya ya Songea katika shule ya sekondari Mpitimbi, Madaba na kadhalika. Zinahitaji huduma hizo na shule nyingine pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja pamoja na maoni yafuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu uanzishwaji wa vyuo vya ufundi *VETA* katika kila wilaya. Katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 Serikali ilitoa ahadi kwamba iko katika mchakato wa kuhakikisha kwamba kila wilaya inapata chuo cha ufundi cha *VETA* ili kuwasaidia vijana wanaomaliza darasa la saba. Wilaya ya Kishapu ina vijana wengi wanaomaliza darasa la saba hivyo inatakiwa kupewa kipaumbele katika ujenzi wa chuo cha *VETA*.

Mwaka 2007, Wizara ilituma watalaam wake wilaya ya Kishapu walikwenda kuangalia eneo ambalo litafaa kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha ufundi. Halmashauri ya wilaya ya Kishapu ilionyesha maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa chuo cha *VETA*. Ningependa kupata ufafanuzi je, Serikali imefikia hatua gani baada ya kuonyeshwa eneo linafaa?

Kampuni ya *Williamson Diamond Limited* ya Mwadui Wilaya ya Kishapu inayo majengo mazuri ambayo hayatumiki kwa kiwango cha kuridhisha. Kuna majengo yaliyokuwa yakitumika kwa ajili ya shule ya msingi, nusu tu ya majengo yanatumika. Kuna majengo yanayofaa kuanzisha mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa shule za sekondari zilizokaribu au kwa wanafunzi wa kike, pia kuna majengo yaliyoko kwenye ustawi wa jamii ambayo yanafaa kuanzisha shule ya sekondari ya kutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo majengo yanayofaa kwa kuanzisha chuo cha ufundi *VETA.*Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuyatumia majengo hayo kwa kuanzisha shule ya sekondari chuo cha ufundi *VETA* kama fedha za kuanzisha chuo kipya hazijapatikana na kuanzisha mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe ufafanuzi imetoa msukumo gani hadi sasa?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa hotuba na utekelezaji wa Wizara hii katika agizo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya msingi, tatizo kubwa linaloikumba elimu katika ngazi hii ni ukosefu mkubwa wa madawati. Je, hivi Serikali haiwezi kuweka mkakati wa makusudi kutoa vibali vya uvunaji wa misitu? Nia ni kupata magogo ambayo yangetengenezwa madawati awamu kwa awamu na hatimaye kupunguza tatizo hili la wanafunzi kukaa chini. Elimu ya msingi ikiwa mbovu, hata elimu ya kati na ya juu haitakuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za walimu wa sekondari, naipongeza Wizara ya Elimu kwa jitihada za ujenzi wa shule za sekondari kwa kila kata. Tatizo

kubwa ni shule hizo hujengwa kwenye maeneo yasiyofaa kabisa na mbali na huduma zote kwa mfano, barabara, maji, afya, umeme na kadhalika, hivyo husababisha walimu kukataa kufundisha Serikalini na kujiunga na shule za sekondari za watu binafsi.

Pia mwalimu anapochaguliwa kupelekwa huko bila nyumba na hata kama ipo sio bora, vinginevyo huambiwa akapange kwenye nyumba ya mtu binafsi, lakini kwenye mshahara wake hana nyongeza ya malipo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya walemavu, elimu katika sekta hii ni sawa na hakuna. Sijaona ni wapi mlemavu mwanafunzi wanamjali kwa asilimia mia moja kutokana na ulemavu wake. Kwa mfano, mwanafunzi akiwa mlemavu wa miguu, Serikali inapaswa imfae kwa mahitaji yote kwa mfano, *wheel chair* ili afike na kusoma vizuri shuleni badala yake mzazi ndiye anabeba uzito wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zihamasishwe kutenga fungu maalum la pesa kwa ajili ya walemavu wanafunzi waliomo ndani ya halmashauri hizo. Hii itapunguza malalamiko ya kusema kuwa walemavu wanabaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukirudi saa 11.00 jioni itabidi tuwaruhusu Manaibu Waziri waanze kujibu hoja na Waziri mtoa hoja kwa kawaida ana saa moja ya kujibu. Sasa ukijumlisha dakika 15 za Naibu Waziri na 15 za Naibu mwingine wanakuwa na nusu saa pamoja na Waziri ni dakika 60 wanazo za kujibu. Hizo zinatupeleka mpaka saa 12.30, ikifika saa 12.30 tutakuwa na dakika 75 tu za Kamati ya Matumizi, nami najua maana yake nini.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nasikitika sana kwamba Waheshimiwa Wabunge 14 hawakuweza kufikiwa, waliozungumza mara moja ni Wabunge watano ambao hawakufikiwa, waliozungumza zaidi ya mara mbili ni Wabunge tisa ambao hawakufikiwa. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali halisi. Sina matangazo mengine. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotoa taarifa kabla ya kusitisha shughuli za Bunge mchana ni kwamba sasa tutaanza na Waheshimiwa Manaibu Waziri kujaribu kutoa ufafanuzi kwa hoja mbalimbali mlizozitoa. Manaibu Mawaziri kwa kawaida wao kama Waheshimiwa Wabunge wana dakika zao 15 na Waziri mtoa hoja huwa anakuwa na muda wa saa moja. Kwa hiyo, wameamua kujumlisha saa zao zote zikapatikana dakika 90 za kujibu hoja zenu. Kwa hiyo, Waziri amegawa kwamba

kila Naibu Waziri atakuwa na dakika 20 na yeye mwenyewe atabakiwa na dakika 50. Kwa hiyo, namkaribisha Naibu Waziri wa kwanza, Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nitumie sekunde chache ili niweze kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wafanyakazi wenzangu viongozi Wakuu wa Chama na Serikali, ndugu, jamaa na marafiki wote kwa upendo na huruma zao kwetu na michango yao ya hali na mali wakati wa msiba mzito wa mama yetu Binti Zubeir, aliyefariki huko Tanga. Kwa niaba ya familia yangu, tunawashukuru mno, nasi tunawaombeeni heri katika maisha yenu. Kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, tunawaombea wazazi wetu rehema na amani katika maisha yao mapya. *Inna lillah wa inna ilaih rajiuna*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili namshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii kwa mara nyingine. Naamini imani yake kwangu ni kubwa, nami kwa uwezo Mwenyezi Mungu nimuahidi utumishi bora na kwamba nitashirikiana na wenzangu kuiletea nchi yetu maendeleo ya haraka katika elimu. Mwenyezi Mungu nakuomba uniwezeshe kumudu majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Profesa Maghembe - Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mama Gaudentia Kabaka kwa ushauri na ushirikiano wao mkubwa kwangu. Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu - Profesa Dihenga na Naibu wake Bw. Muhaiki, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizarani kwa ushirikiano wao ambao umewezesha kazi yangu kuwa nyepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, wananchi na watendaji wote katika Halmashauri mbalimbali kwa namna ya pekee walivyowezesha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 61 - ujenzi wa shule za sekondari kwa kila Kata kufanikiwa kwa zaidi ya asilimia 100. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa penye nia pana njia. Chama cha Mapinduzi kimeonyesha njia kwa kuwa na mipango thabiti inayowezesha jamii yake kujikomboa kiuchumi, kielimu na kijamii. Mengi yanasemwa kuhusu shule hizi, mazuri yenye kutia moyo, mabaya yenye kukatisha tamaa, kejeli na dharau za kila aina. Hata hivyo ukweli utasimama pale pale kwamba shule hizi ni mkombozi kwa walio wengi. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inajua inachokifanya, inayo dhamira ya kweli ya kuwaletea wananchi wake mabadiliko ya dhati katika elimu. Hivyo basi, nawasihi wananchi wote wasikate tamaa, kukatishwa tamaa na kejeli za wasioitakia mema nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inazitambua changamoto mbalimbali za kielimu zilizojitokeza na imeziandalia mpango mkakati na imara ya namna nzuri ya

kupambana nazo mfano, uhaba wa walimu, maabara, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, nyumba za walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe, hakuna masika yasiyokuwa na mbu na kwamba hakuna maendeleo yasiyoleta changamoto mpya. Nimalizie utangulizi wangu kwa kusema kama mgaagaa na upwa hali wali mkavu. Je, atakayeshinda shuleni wiki moja, mwezi mmoja na miaka minne atakuwa zuzu au bwege? Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Madiwani tushikamane kwa dhati ili kuwashawishi wananchi tuendelee kukamilisha ujenzi wa madarasa. Aidha, ninawaomba walimu wenzangu, wafundishe kwa uhodari kwani kero zao tunazitambua na tunazifanyia kazi. Wanafunzi nao wasome kwa umakini na juhudi kubwa. Namwomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kutimiza azma hii njema kwa kizazi chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba nitajihidi kwa kadri nitakavyojaliwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na zitakazosalia Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ataendelea kuzijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea hoja nyingi na nitazijibu kama ifuatavyo: kumekuwa na hoja ya utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi au utoro kwa ujumla ambayo hoja hii imezungumzwa na imetolewa michango mingi. Naomba niseme kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa pamoja tutafuatilia suala hili ili kuhakikisha suala la utoro linafikia mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kukawa na mikakati iliyowekwa kwa ajili ya wanafunzi walemavu. Kwa ujumla walemavu wamezungumzwa kwa kauli nzito sana naomba niseme Wizara yangu iko katika mkakati wa kuona namna itakavyoweza kwa haraka kupata angalau idara itakayojitegemea pamoja na kwamba masuala ya miundombinu, vifaa vya kufundishia, pamoja na hifadhi zao vitapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la adhabu za viboko. Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o amezungumza na kwa maandishi, lakini pia amezungumza mara nyingi hata katika michango yake mbalimbali. Suala la viboko limewekwa kwa mujibu wa kanuni tuliyotoa, waraka wa elimu wa namba 24 wa mwaka 2002. Bado tunasimama hapo hapo kwamba mwalimu anayestahili kutoa adhabu ya viboko ni Mkuu wa Shule au mwalimu Mkuu au aliyepangwa na Mkuu wa Shule tena kwa maandishi. Hivyo kwa kupitia Bunge lako Tukufu, niwasihi walimu wote wanaosikiliza sasa hivi tafadhalini, viboko acheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madawa ya kulevya suala hili linaongezeka kasi siku hadi siku na kwamba Wizara yetu inakabiliwa sasa na mzigo mkubwa kwani baadhi ya wanaoshiriki zaidi ni wanafunzi ama shule za msingi au za sekondari. Naomba niseme suala hili, tunalifanyia kazi. Lakini pia ni vyema tukaomba ushirikiano wa jamii kwa sababu dawa hizi ama zinauzwa mitaani au majumbani ambako sisi wananchi wote kwa ujumla tupo. Tunaomba tushirikiane, suala hili si zuri na matokeo yake sio mema kwa kizazi chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wanafunzi kupata mimba limezungumzwa sana. Naomba niseme tumelipokea, tunasubiri taarifa ya kamati maalum ambayo ilipita, tutaifanyia kazi na pamoja na hayo, tunaomba kuwakaribisha wadau wote kutoa maoni yao katika hoja inayoendelea hivi sasa ya kuboresha sera ya elimu kwa sababu hatuwezi kusema warudi shuleni kabla hatujaibadilisha sera. Kwa hiyo, kwanza tupate maoni kwenye sera ili tutengeneze sheria baada ya hapo kwenye sheria ndiyo tutasema wakishapewa ujauzito waje. Lakini pia itabidi na wenzetu wa afya waanzishe vitengo vya *MSCH* mashuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu itoe mafunzo ya ufundi, kipaumbele katika elimu masafa. Naomba niseme kwamba ili kutimiza azma hiyo, Wizara inasomesha wakufunzi 13 elimu maalum katika Chuo Kikuu huko Uganda, vile vile inapitia moduli mbalimbali kutoka kwenye Chuo cha Uganda na Kenya kwa ajili ya walimu elimu maalum ili na wao waweze kutoa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumzia pia kwamba Wizara ianzishe kozi maalum kwa ajili ya fani ya *otizim*, viziwi, wasioona, uoni hafifu na ulemavu wa viungo. Wizara yangu kwa kushirikiana na vyuo vya elimu maalum vya Kenya na Uganda inaandaa utaratibu wa kuandaa mafunzo hayo katika Chuo cha Elimu Maalum Patandi. Aidha, maandalizi ya kupanua Chuo cha Patandi yako tayari na fedha zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na hoja mchanganyiko juu ya shule ya Nanyanje Mkoani Lindi. Naomba niseme kwamba shule ya Nanyanje ambayo ilisajiliwa mwaka 2007 na kupewa namba ya usajili, Wizara imepokea taarifa kutoka kwa wakaguzi kwa lengo la kuisajili shule ya Sekondari Chikanji, maombi ambayo yanashughulikiwa. Hata hivyo, naomba niseme, Mheshimiwa Mbunge, Mudhihir alishaleta maombi yake na mapendekezo yake ofisini kabla hajapata ajali na kwamba tunaifanyia kazi tutampatia majibu, shule zote bado zinatambuliwa na hakuna iliyofutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeombwa pia tuitambue shule ya walemavu viziwi iliyopo Tabora ambayo inatakiwa tuchukue sisi. Shule ya watoto viziwi Tabora inamilikiwa na kuendeshwa kwa ushirikiano baina ya Jimbo Kuu la Kanisa Katoliki Tabora na Halmashauri ya Manispaa. Wizara haina taarifa kuwa Jimbo Kuu la Kanisa Katoliki Tabora limekabidhi majengo ya shule hiyo kwa Serikali. Namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora kwa maelezo ya uhakika ili kujua kama shule hiyo imeshakabidhiwa Serikalini au la. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa mabweni ya wasichana. Tumepokea ushauri mwingi wa namna ya kuwanuru watoto wasichana, lakini pia hata wavulana ambao wanatoka mbali kwenda kwenye shule zao. Naomba niseme, tumepokea ushauri, tutajadiliana na kuona namna gani kwa sababu hali ya hosteli kwa sasa fungu ni dogo, lakini tutaona namna ambavyo tunaweza kutoa hata ushauri wa kitalaam namna ambavyo Mikoa, Wilaya au Halmashauri zinavyoweza kujijengea mabweni yao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kunakuja hoja pia ya walimu wanaoshughulika na wanafunzi wa mahitaji maalum wapatiwe vyombo vya usafiri. Shule nyingi za bweni ni kweli hazina usafiri na hivyo wanafunzi wanapopata matatizo inakuwa vigumu. Wizara inazishauri Halmashauri za Wilaya wanakotoka watoto hawa wenye ulemavu zifanye utaratibu wa kuwasafirisha watoto hao nyakati za likizo. Aidha, wale ambao wako katika Serikali Kuu nako pia watafanyiwa utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la kwamba Serikali imeweka mkakati gani kuhakikisha kwamba wanafunzi wengi zaidi wanachukua masomo ya sayansi? Serikali inatambua umuhimu wa masomo ya sayansi na teknolojia ili kuharakisha maendeleo ya nchi yetu. Ili kufanikisha azma hiyo, Wizara imeweka mikakati ifuatayo: kutoa mafunzo kazini, kujenga maabara, kutoa ruzuku ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ionyeshe moyo kwa huruma kuwapatia mishahara walimu kwenye shule binafsi. Wizara inatoa ruzuku kwa shule zisizo za Serikali zilizotimiza masharti kama ilivyo kwa kanuni ya *GN 291* ya mwaka 2002.

Masharti hayo ni pamoja na shule kuwa imesajiliwa, kutoza ada iliyowekwa na Serikali na kufuata mtaala ulioidhinishwa na Kamishina wa Elimu. Ruzuku hiyo ni kama vitabu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na fedha kwa ajili ya mishahara ya wakuu wa shule au walimu walioko katika shule hiyo. Hata hivyo kutokana na uwezo mdogo wa Serikali ni shule chache zinatimiza masharti na kupatiwa ruzuku hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa za elimu kwa wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu wapewe fursa na mazingira maalum katika kupata elimu. Tumezingatia ushauri uliotolewa, tunajihidi kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira rafiki kwa shule na vyuo na pia kuongeza nafasi za kuandikishwa wanafunzi wenye ulemavu kwa kuanzisha shule au vitengo zaidi ya kuandikisha wanafunzi katika mfumo wa elimu jumuishi ili wasome katika shule iliyo karibu na wanafunzi wanapoishi, kununua na kusambaza vifaa na visaidizi vya aina mbalimbali kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu, kuzifanyia marekebisho na miundombinu shule za sekondari pamoja na za msingi ikiwa ni pamoja na miundombinu kwenye vioo.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya mazingira magumu, walimu wanaofundisha wenye ulemavu. Suala la posho kwa ajili ya walimu wanaofundisha katika mazingira magumu wakiwemo walimu wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu, bado linafanyiwa kazi na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Waziri mwenye dhamana ya utumishi akiwa tayari atatuletea taarifa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala kwamba pawe na Afisa Elimu kila Wilaya kwa ajili ya wenye ulemavu. Kwa kutambua umuhimu wa usimamizi wa elimu maalum, Wizara yangu imetoa maagizo kwa kila Halmashauri kuteua mtaalam mmoja wa elimu maalum aweze kuratibu utoaji wa elimu maalum katika Halmashauri husika. Agizo hili limeshaanza kutekelezwa, Halmashauri 22 tayari zina waratibu wa elimu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu watoto wenye ulemavu wasome bure ngazi zote. Wizara yangu ilishatoa maelekezo kwa kila Halmashauri nchini kugharamia elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari kwa barua C/BA308/495 ya tarehe 24/9/1999. Maelezo hayo yalitokana na agizo la Rais wa Awamu ya Tatu kwa barua yake Kumb. Namba hiyo iliyohusu msamaha wa malipo ya karo kwa wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushauri kwamba Wizara itoe elimu zaidi kwa jamii kuhusu Maalbino, kwa kutambua umuhimu wa kuelimisha jamii kuhusu wenye ulemavu wakiwemo Maalbino. Wizara yangu inatekeleza mipango ifuatayo:-Kipindi cha elimu maalum kupitia redio kwa kushirikiana na shirika la Utangazaji Tanzania *TBC*, kipindi hicho kinarushwa *TBC* kila siku ya Jumamosi saa 7.30 hadi saa 8.00 mchana na kurudiwa siku ya Jumanne saa 11.30 hadi saa 12.00 jioni. Mpango wa elimu kwa jamii kupitia kipindi cha kipimajoto kinachorushwa na kituo cha television *ITV* siku za Ijumaa, mpango mkakati wa elimu kuhusu haki za binadamu katika kanda ya ziwa, kushirikiana na *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, wameomba michezo iimarishwe. Napenda kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba michezo tangu awali haikufutwa. Yaliyokuwa yamefutwa ni mashindano. Hivyo, naomba niseme mwaka huu mashindano yatarudi rasmi kituo cha shule za msingi kitakuwa Morogoro kwa shule za sekondari kitakuwa Kibaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya shule ya Sekondari Kizaga mwalimu ambaye alituhumiwa kufanya ubadhilifu, Wizara ilituma watalaam kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa mahesabu ya kwamba mwalimu huyo katika ukaguzi uliofanyika katika ujenzi ule ilionekana kwamba dosari zilizoonekana ni chache. Hata hivyo, Waziri mwenye dhamana ameshaelekeza timu ya watalaam wa majengo watakwenda Sekondari ya Kizaga kukagua na kuona hali ilivyo na baadaye atatoa maelezo kwa kumalizia ujenzi uliokuwa umesalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwalimu aliyesababisha vurugu kwa kuwashikisha wanafunzi kinyesi, Wizara yangu imemsimamisha kazi mwalimu huyo na kumtumia hati ya mashtaka na pia kuhakikisha kwamba anapimwa akili baada ya hapo tume ya utumishi wa walimu itatoa hatma yake ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaguzi shule za msingi, Wizara imejiwekea utaratibu wa kulipa madai ya ukaguzi bila ucheleshwaji na kwamba kadri fedha zitakavyokuwa zinapatika watalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtaala wa elimu uliboreshwa mwaka 2005 na kuwa na masomo tisa ambayo ni maarifa ya jamii, sayansi, hisabati, Kiswahili, *English*, Haiba na Michezo, *TEHAMA* stadi za kazi na kadhalika. Hata hivyo Serikali inaona ni vyema kujenga misingi bora kwa wanafunzi katika maeneo ya elimu na historia, uraia na jiografia ili kukidhi malengo ya elimu nchini. Hivyo Wizara iliamua kufanya mabadiliko kwa kuanzisha masomo ya historia, uraia na jiografia badala ya somo la maarifa ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalo lilitokana na hoja nyingi zilizokuwa zinawasilishwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ndani kwa ajili ya kuona kwamba uraia ulikuwa umeminywa, ndio maana tukarudisha tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya mabadiliko ya mitaala mara kwa mara. Kitaalamu mitaala inaweza kuboreshwa baada ya kipindi cha mzunguko wa ngazi ya elimu kukamilika. Mfano, kipindi kisichopungua miaka saba kwa ngazi ya Elimu ya Msingi na miaka sita kwa ngazi ya Elimu ya Sekondari. Mtaala wa Elimu ya Msingi uliboreshwa mwaka 1996 na mwaka 2006, yaani baada ya miaka 10. Lengo ilikuwa ni kuboresha na kuifanya elimu itolewayo nchini iendane na mabadiliko ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masomo Rekebishi kwa wanafunzi walioshindwa katika alama ndogo. Madhumuni ya Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Pili, ni kupima maarifa na ujuzi alioupata mwanafunzi kutokana na mafunzo aliyojifunza katika Kidato cha Kwanza na kidato cha pili, na kuhamasisha walimu na wanafunzi wajitahidi ili kukamilisha mada zote za kidato cha kwanza na kidato cha pili kwa kuinua maendeleo katika masomo.

Aidha, ufundishaji wa masomo rekebishi kwa wanafunzi husika utapangwa na shule na utafuatiliwa na Wakaguzi wa shule, Maafisa Elimu, Waratibu Elimu na Wakuu wa Shule wenyewe. Hata hivyo, mawasiliano yatafanywa na TAMISEMI kuona ni jinsi gani walimu watakaofundisha masomo rekebishi watalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wengi wa Shule za Msingi kukaa muda mrefu katika kituo kimoja. Ni kweli kuwa mtumishi akikaa sehemu moja kwa muda mrefu huweza kuathiri utendaji wa kazi. Hata hivyo, uhamisho wa watumishi huhitaji fedha ili kuondoa mazoea na uwezekano wa kuathiri utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa maelezo yako. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa pili Mheshimiwa Gaudentia Kabaka.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa ili nichangie hoja iliyowasilishwa jana na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Profesa Jumanne Maghembe - Mbunge wa Mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kwa kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa majadiliano tangu jana hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kabla sijafanya hivyo, naomba nitumie nafasi hii adimu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua katika mabadiliko yalitokea mwezi Februari, mwaka huu kuwa Naibu Waziri wa

Wizara ya hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ambayo niliitumikia kwa zaidi ya miaka 30 kama mwalimu kabla sijaamua kuwa mwanasiasa. Naendelea kumuahidi Mheshimiwa Rais uaminifu, uadilifu wangu katika nafasi hii aliyonitunukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kwa jinsi anavyonishirikisha kikamilifu katika shughuli za Wizara kwa manufaa ya Taifa letu. Namshukuru pia Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, mwanafunzi wangu wa ualimu kwa ushirikiano mkubwa anayonipatia yeye akiwa kama mwenyeji wangu ndani ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana wataalam na watendaji wote wa Wizara chini ya uongozi wa Katibu Mkuu - Profesa Hamisi Dihenga na Naibu Katibu Mkuu Bwana Oliver Mhaiki kwa ushirikiano wanaonipa katika Wizara hii. Pamoja na hao, ninaomba niwashukuru sana Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu wananipatia ushirikiano wa dhati katika majukumu yangu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda niwashukuru sana wanawake na wananchi wote wa Mkoa wa Mara ninaaowawakilisha kupitia nafasi hii ya Viti Maalum kwa upendo, ushauri na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kazi zangu za kuwatumikia na ninawaahidi kwamba nipo pamoja nao katika maendeleo ya Mkoa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na siyo kwa umuhimu, ninaomba kuishukuru kipekee familia yangu ambayo ni pamoja na mume wangu John Kabaka, binti yetu Patiricia na mumewe Joel, wadogo zangu Modesta, Venerada, Alibinus na wifi yetu Agnes. Ninawashukuru sana kwa uvumilivu, upendo na ushirikiano mkubwa wanaonipa hasa katika kumtunza mama yetu mpendwa Christina Nyakimori ambaye kwa miaka miwili sasa amelazwa katika Taasisi ya Mifupa Moi. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninalo deni kubwa sana kwa Madaktari, Wauguzi na wahudumu wa Moi kwa *nursing care* kwa huduma nzuri wanayompatia mama yangu kadri anavyohitaji. Nawaomba wasichoke kufanya hivyo na mimi nitaendelea kuwaombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ambayo nilifikiri ni muhimu niyaseme, naomba sasa nijibu baadhi ya hoja kama nilivyosema hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni hoja inayohusu masuala ya *VETA*, imezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge 14 na kwa ajili ya muda, naomba nisiwataje kwa sababu hao wote watatajwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza mpango wa utekelezaji wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya, Wizara yangu iliweka vigezo vifuatavyo:- Kwanza, ujenzi uanze katika Wilaya ambazo hazina Chuo cha Ufundi Stadi cha aina yoyote na pili, Wilaya ambazo tayari zimeanzisha Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya, lakini Vyuo

hivyo vinahitaji kupanuliwa na kukarabatiwa ili kukidhi mahitaji ya Wilaya vifanyiwe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia vigezo hivyo, ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya vinatekelezwa kwa awamu kwa kuanzia Wilaya 25 ambazo hazina Chuo cha Ufundi Stadi cha aina yoyote pamoja na Wilaya tatu ambazo zina Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya, lakini vinahitaji kupanuliwa na kukarabatiwa.

Mafunzo katika Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya yanatolewa kulingana na mahitaji stadi zinazotakiwa katika Wilaya husika. Uchambuzi wa mahitaji ya stadi umefanywa katika Wilaya 74 nchini na Wilaya zilizobaki uchambuzi utafanywa kwa mwaka 2008/2009 ili kubaini mahitaji halisi ya Wilaya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inaangalia uwezekano wa kuvipanua na kuviimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze kuchangia zaidi katika kutoa mafunzo ya ufundi stadi Wilayani bila ya kuathiri malengo na mafunzo yanayotolewa na vyuo hivyo hivi sasa.

Aidha, Wizara yangu inakamilisha taratibu ili kuweza kupata fedha za nje kwa ajili ya kuharakisha utekelezaji wa azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, aidha, itaendelea kufuatilia Wilaya ambazo hazina Vyuo vya Ufundi Stadi, lakini havikuwekwa katika orodha ya Wilaya 25 au Wilaya zenye miradi maalum. Wilaya hizo ni pamoja na Geita, Makete na Ludewa. Kwa hiyo, Wilaya hizo zitafikiriwa pia katika Wilaya hizo 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Korea inajenga Vyuo vya *VETA* katika Mikoa mitatu iliyosalia ambayo ni Lindi, Pwani na Manyara. Mkandarasi amepatikana na Mkataba wa ujenzi utasainiwa tarehe 21 Julai, 2008 yaani Jumatatu ijayo. Ujenzi unatarajia kuanzia mwezi Agosti, 2008 na jiwe la msingi la Chuo cha Lindi litaweka mwezi Novemba, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine zilizojitokeza ni zile ambazo zimetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Omar Kwaangw’ ambaye alisema Serikali itoe *grant* kwa wanafunzi wanaochukua masomo wa sayansi kwa Vyuo Vikuu na hoja hii pia imetolewa na Mheshimiwa Suzan Lyimo Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 iliainisha utaratibu wa uchangiaji wa Elimu ya Juu ambapo kila mnufaika wa elimu hiyo anatakiwa kuchangia upatikanaji wake. Wanafunzi ni miongoni mwa wanufaika wa elimu wanayoipata na Sera inawataka wachangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuwasomesha wanasayansi wengi kadri inavyowezekana ili waweze kuchangia ujenzi wa Taifa.

Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti, jitihada za Serikali zina kikomo chake. Utaratibu wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu ndiyo njia inayotumika kuharakisha wanafunzi kuwagharamia masomo yao. Wanafunzi wa taaluma za sayansi kama vile Udaktari, Kilimo, Uhandisi na Usanifu majengo hupewe kipaumbele katika kupata mikopo hiyo badala ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele na itaendelea kufanya hivyo kwa wanafunzi wanaosomea taaluma ya sayansi. Kwa mfano, katika kutoa mikopo ya wanafunzi, jinsia pia imekuwa ikipewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeteremsha kigezo cha kupata udahili katika Vyuo Vikuu kutoka alama 4.5 hadi 2.0 kwa wanafunzi hao wa Kata.

Vile vile mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambao utaanza hivi karibuni unalenga katika kuimarisha miundombinu ya ufundishaji na kujifunzia kuimarisha mafunzo ya walimu wa sayansi, kuweka vifaa vya maabara, kuimarisha maktaba kwa kuingiza matumizi ya *TEHAMA* kwa wanafunzi wa sayansi. Lingine lililojitokeza pia katika hotuba ya Mheshimiwa Omar Kwaangw' ni kuhusu makazi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo yamechakaa na ni hatari kwa wanafunzi na anaomba ukarabati ufanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati za Huduma ya Jamii kwamba kuna uchakavu, ubovu na upungufu wa miundombinu takriban vyuo vikuu vyote vya elimu nchini. Vyuo hivyo vimejengwa zaidi ya miaka 30 iliyopita. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimejengwa zaidi ya miaka 45 sasa. Kwa hiyo, hivi karibuni Serikali imefanya upembuzi yakinifu kugundua gharama zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika Vyuo Vikuu vya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji mwingine ambaye alizungumza na kwa uchungu mkubwa sana kuhusu upungufu wa wafanyakazi katika sekta ya afya ambayo inatokana na Wizara yangu ni Mheshimiwa Dr. Ali Taarab Ali, ambaye tunasema ni kweli kuna upungufu wa madaktari nchini. Kukabili hali hii Serikali inachukua hatua zifuatazo, moja ni kuboresha miundombinu kulingana na uwezo tulionao katika Chuo Kikuu cha Tiba cha Muhimbili ili kuongeza udahili wa wanafunzi, kuongeza ajira na kutoa nafasi za ajira endelezi kwa walimu. Vile vile kuboresha mazingira ya kufundishia ikiwa ni pamoja na kuwapatia chuo eneo la Muroganzila ili kuongeza nafasi ya kupanua shughuli za elimu hiyo ya udaktari. *(Makofi)*

Katika Bajeti ya mwaka huu Serikali imetenga fedha za kuanzia uendelezwaji wa eneo hili. Aidha, Serikali imekipatia chuo *flats* zilizopo eneo la *Chole Road*, Oysterbay kuwa malazi ya wanafunzi. Pili, ni kuidhinisha uanzishwaji wa Vyuo Vikuu binafsi vinavyofundisha Madaktari kwa mfano *KCMC* ambayo ni sehemu ya Tumaini, *Bugando*

*University,* Herbert Kairuki na *IMTU,* Serikali inatambua mchango wa vyuo hivi binafsi katika juhudi za kuongeza udahili wa wanafunzi wa udaktari na fani nyingine za afya kama ifuatavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumpe nafasi Waziri aweze kujibu maana yake wengine naona mnazungumza mno. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Muhimbili 200, *KCMC* 25, Bugando 25 na *Herbert Kairuki University* 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji mwingine Mheshimiwa Estherina Kilasi, alitaka kujua hosteli za *MUHAS* zilizoko *Chole Road*, Oysterbay zinakamilika lini kwani pesa za kukamilisha ukarabati hazionekani kwenye Bajeti. Pia anasema uendeshaji wa hosteli hizo utakuwaje na usafiri wa wanafunzi utakuwaje?

Naomba nimjibu kama ifuatavyo, ukarabati wa hosteli hizo umeshakamilika kilichosalia ni ukosefu wa miundombinu ya huduma muhimu kama jiko na sehemu ya kulia chakula, sehemu ya kufulia nguo, nyumba za wasimamizi wa wanafunzi, uzio wa kuhakikisha usalama. Fedha zimetengwa katika Bajeti ya mwaka huu ili kukamilisha kuwepo kwa miundombinu hiyo.

Aidha, zabuni ambazo zimelenga kuwawezesha kuwepo kwa miundombinu hiyo zimeshatangazwa. Chuo kimelenga kukamilisha haya mapema iwezekanavyo baada ya upatikanaji wa fedha zilizotengwa. Pia utaratibu wa sasa wa chuo ni kuwa hosteli zote zinasimamiwa na kuendeshwa na chuo chenyewe. Utaratibu uliopo wa usafiri ni kuwa wanafunzi wanafanya mipango yao ya usafiri ikiwa ni pamoja na kukodi mabasi, ni matarajio yangu kuwa wanafunzi watakaokaa hosteli ya *Chole Road* watafanya mipango yao ya usafiri kama wenzao wanaoishi nje ya chuo wanavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji Mheshimiwa Al –Shymaa John Kwegyir, alichangia kwa uchungu sana kuhusiana na suala la maalbino na wote tunakubaliana naye na anasema maalbino wapatiwe nafasi za kujifunza katika vyuo vya *VETA* ili waweze kujitegemea kwa sababu vyuo vya *VETA* vina mazingira mazuri ya kujifunzia ukizingatia matatizo ya ngozi ya maalbino.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema vyuo vya ufundi vilivyomilikiwa na Serikali vinaandikisha wanafunzi wa aina zote wakiwemo maalbino kwa lengo la kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kujitegemea. Wizara inamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wanafunzi maalbino wenye sifa wataendelea kupatiwa nafasi za kusoma katika vyuo hivyo, aidha, Wizara inawahamasisha maalbino wenye sifa za kujiunga na vyuo hivyo waombe nafasi kusoma katika vyuo vya *VETA* vilivyopo karibu nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine liliulizwa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, ambaye alisema walimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni wachache wanafundisha madarasa makubwa sana zaidi ya wanafunzi 200 bila ya motisha,

mishahara midogo, operesheni duni na ndiyo maana wanahama nchi. Sisi tunasema Wizara inatambua tatizo hili na inafanya jitihada kulitatua. Jitihada hizo ni pamoja na kutumia *TEHAMA* katika kufundisha madarasa yenye wanafunzi wengi na kuongeza mishahara ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeunda Kamati maalum ambayo inaliangalia kwa undani suala la pensheni za wanataaluma kwa lengo la kuboresha. Ni matumaini ya Wizara kwamba baada ya kupata ufumbuzi wa mishahara ya pensheni hali ya wahadhiri kukimbilia maslahi bora zaidi nje ya nchi itapungua. Lakini hili ni suala ambalo liko katika nchi zote za *SADC* kwa wanataaluma kuondoka nchini mwao kwenda kutafuta maslahi mazuri zaidi nchi nyingine za *SADC* au penginepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Wilson Masilingi yeye anashauri kwamba Serikali itafute walimu au wahadhiri wa Vyuo Vikuu kutoka popote nje ya nchi kwa gharama muafaka na wahadhiri hao Serikali ikope fedha kutoka Taasisi za Fedha kugharamia mishahara, posho, vitabu na vifaa vyote muhimu katika kufundisha. Serikali imepokea ushauri kuhusu kutafuta walimu nje ya nchi, aidha, Chuo Kikuu cha Dodoma kimekwishaanza kutekeleza ushauri huo kwa kutafuta walimu wa fani mbalimbali nje ya nchi. Vyuo Vikuu vingine pia hupata walimu kutoka nchi za nje kwa taratibu za kubadilishana, kuazimana na kufanya tafiti za pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, walizungumzia kuhusu kuzuiliwa kwa matokeo ya mitihani kwa wanafunzi wa elimu ya juu walioshindwa kulipa ada za Chuo Kikuu cha Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuzuia matokeo ya mtihani au vyeti vya kuhitimu kwa wanafunzi ambao hawajakamilisha kulipa ada zao ni utaratibu unaotumika katika Vyuo Vikuu hapa nchini na kwingineko. Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Ardhi hali halisi ni kama ifuatavyo. Kwanza suala hili linawahusu wanafunzi wa shahada za kwanza, pili, idadi ya wanafunzi hao ni 1,324 na ukubwa wa deni ni shilingi 359,285, 000,000/=. Deni hili lina sehemu mbili yaani ada ya chuo na ada ya tiba. *(Makofi)*

Tatu, jumla ya wanafunzi 87 wamekamilisha kulipa ada zote yaani 58 wa mwaka wa kwanza na wa pili 29 na wa mwaka wa tatu hadi wa tano. Asilimia 53.4 ya wanafunzi wadaiwa wa Chuo Kikuu cha Ardhi wanadaiwa chini ya shilingi laki mbili kila mmoja. Ni asilimia 18.7 tu ya wanafunzi wetu wote ambao wanadaiwa zaidi ya shilingi laki tano kila mmoja. Wanafunzi ambao bado wanadaiwa walipewa muda wa mwaka mmoja wa masomo kukamilisha malipo yao kwa kulipa kidogo kidogo. Hitimisho Chuo hutumia ada hizo pamoja na mambo mengine kugharamia sehemu muhimu za mafunzo yao. Hivyo malipo yake hayawezi kuahirishwa aidha, viwango vinavyodaiwa wanafunzi wetu vinalipika kwa sababu viwango hivyo ni matokeo ya *meaning testing* iliyofanywa na Bodi ya Mikopo. Hivyo hakuna utaratibu mwingine wa kutumika bali kwa wahusika kukamilisha malipo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie uhalali wa *TCU* kuratibu mfumo wa Taifa wa tuzo za elimu (*National Qualifying Framework*) suala ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge. Tanzania haikuwa na mfumo wa tuzo za elimu unaosimamia na kuratibu hadhi na tuzo zinazotolewa baada ya kuhitimu ngazi ya elimu na mafunzo mbalimbali. Mamlaka ya Ufundi Stadi *VETA* na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* vilianzisha mifumo ya kuratibu tuzo hizo kwa mafunzo yatolewayo na vyuo vilivyo chini ya mamlaka zake yaani *National Vocational Award* na *National Technical Award*. Kwa kuwa Vyuo Vikuu bado havijawa na mfumo huo kwa ajili ya mafunzo ya ngazi ya shahada Serikali iliipa *TCU* jukumu la kuandaa mfumo wa tuzo za Vyuo Vikuu na pia kuratibu mfumo wa Taifa wa tuzo za elimu kwa kushirikisha mamlaka za Taasisi zikiwemo *NACTE, VETA, TIE* na *NECTA. (Makofi)*

Katika kutekeleza hilo, *TCU* imeunda kikosi kazi chenye wataalamu kutoka Taasisi husika na mapendekezo ya mfumo huu yatafikishwa kwa wadau wengine mwezi Agosti. Kwa hiyo, *NQF* sio mali ya *TCU* ila *TCU* ni waratibu na pendekezo hili linafanyiwa kazi katika sera ambayo inahuishwa hivi sasa. *(Makofi)*

Hoja nyingine ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa ni kuhusu wadau kushirikishwa katika kuanzishwa fomu moja ya kujiunga na Vyuo Vikuu nchini. Baada ya kujitokeza matatizo mengi katika mfumo uliopo sasa wa kudahili wanafunzi katika Vyuo Vikuu nchini Naibu Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu (Taaluma) wote nchini walikutana kwenye mkutano wao mapema mwaka huu uliojadili matatizo hayo, waliiomba *TCU* kuweka mfumo mmoja wa udahili wa wanafunzi ambao utatumika kwa Vyuo Vikuu vyote nchini. Katika mpango huo wanafunzi wanaotaka kujiunga na Chuo chochote cha umma au binafsi nchini watajaza fomu moja na mfumo mzima utasimamiwa na *TCU*. *TCU* imekwishabuni mfumo huo na ulijadiliwa na kukubaliwa na Vyuo Vikuu vyote. *(Makofi)*

Pia Serikali kupitia mradi wa Benki umetenga fedha za kununulia baadhi ya vifaa vya Mfumo wa Habari na Mawasiliano *(TEHAMA)* utakaowezesha kutekeleza mfumo huo. Kwa utaratibu huo wanafunzi watalazimika kuchangia ada ya udahili ya shilingi 20,000/= tu ambazo zitatumika kugharamia shughuli zote za udahili ikiwa ni pamoja na kusambaza fomu ya kujiunga na vyuo katika shule zote zenye Kidato cha sita na kuviwezesha vyuo vishiriki kwenye zoezi la pamoja la udahili. Gharama ya shilingi 20,000/= anayopaswa kulipa mwombaji anayejiunga na Chuo Kikuu ni nafuu kwake kwa sababu analipa mara moja kuliko ilivyo sasa ambapo hulazimika kulipa ada kwa kila chuo anachojaribu kuomba. Hata hivyo mfumo bado unajadiliwa na Vyuo Vikuu na wadai wengine na maamuzi kamili ya kiutendaji ni miongoni mwa majadiliano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda unakwenda lakini naomba tu nigusie pia suala aliloongea Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, kwamba Serikali haioni umuhimu wa kutazama upya umuhimu wa muundo wa Bodi ya Mikopo, utoaji na urudishwaji wake. Mojawapo ya matatizo ambayo yanafanywa kwa sasa utekelezaji wa mapendekezo ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kuwa magumu ni pamoja na vyombo vya fedha kutoa masharti magumu ya ukopeshaji ambayo wanafunzi wengi hasa toka familia ya maskini

hawezi kuyamudu. Masharti hayo ni pamoja na kuwa na dhamana zisizohamishika na gharama kubwa za uendeshaji ambazo zinapendekezwa na Mabenki ili kuendesha utoaji wa mikopo wakati taasisi za fedha zinapendekeza kutoa kati ya asilimia 10 na 15 kama gharama za uendeshaji. Gharama hizo ni asilimia 4.5 tu za fedha zilizokopeshwa kwa kutumia Bodi ya Mikopo. Mheshimiwa Dr. Slaa alitaka kuendeshwa kwa ufanisi zaidi kwa kutumia *tender open* na kuepuka migogoro ya mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ijitahidi kukusanya madeni yaliyokopeshwa kwa kutumia mawakala ambao watakuwa waaminifu na makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitaomba mtoa hoja aweze kuwasilisha maelezo yake, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii kutoa maelezo ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na kuhitimisha hoja yangu niliyoitoa jana asubuhi ili nipate fursa sasa na kuliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Wabunge wengi sana walitoa mawazo yao na walizungumza kwa uchungu kweli kweli na wale ambao waliandika, waliandika kwa *spirit* hiyo hiyo inayoonyesha ni jinsi gani Waheshimiwa Wabunge wamejihusisha kikamilifu katika maendeleo ya elimu katika majimbo yao na kwa ujumla katika nchi yetu. *(Makofi)*

Napenda niwashukuru sana na napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kupitia Wizara yangu tutayachukua mawazo yote ambayo yametolewa katika Bunge hili Tukufu na kuyafanyia kazi na hasa kuyajumuisha katika mjadala unaofanyika hivi sasa juu ya sera ya elimu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi walichangia hoja hii na wale ambao walichangia kwa kuzungumza hapa ndani ya Bunge naomba niwaorodheshe na kuwataja majina yao kwa kuwashukuru kama ifuatavyo.

Kwanza, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Susan Lyimo, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Mercye Emmanuel, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo waliotoa michango yao na michango mizuri sana ilikuja kwa maandishi yanatoka kwa Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Josephine Genzabuke**,** Mheshimiwa Lucy

Owenya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Mheshimiwa Martha Umbulla. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameleta maandishi zaidi ya mara moja ni Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Fatma Abdallah Tamim, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Mgeni Kadika, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Martha Mlatta, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Mtutura Mtutura, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Zulekha Yunis Haji, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare na Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengine 76 walichangia Wizara hii wakati wanachangia katika hotuba ya Wizara ya Fedha na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nao ni Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Abdi Mshangama, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dustan Mkapa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Mariam Kassembe, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Mercye Emmanuel na Mheshimiwa James Musalika. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Zabein Muhita, Mheshimiwa Brig. Jeneral Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Al-Shymaar Kweigry, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Bernedeta Mushashu, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Lucy Nkya, Mheshimiwa Zainab Vulu, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame na Mheshimiwa James Musalika ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mlivyoona hii orodha ni ndefu kweli kweli na kwa hiyo, maswali yaliyoulizwa ni mengi na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, tutajaribu kuyajibu kwa kadri muda utakavyoruhusu. Lakini nawaomba sana mkubali kwamba yale ambayo hatutaweza kuyajibu kwa sababu ya muda tulionao basi tuyalete kwa njia ya maandishi wakati tukiwa hapa Bungeni kabla hatujamaliza kikao hiki cha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja moja ambayo imetolewa kwa nguvu sana katika mjadala huu ni hisia kwamba labda ubora wa elimu unashuka na kwamba niseme Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumzia juu ya hoja hii na imetolewa kwa

nguvu sana nikaona ni vema nikachukua muda kidogo nikaielezea hoja hii na tuondoke hapa Bungeni wote tukiwa na uelewa mmoja juu ya dhana ya ubora wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa elimu ni dhana pana sana, inaweza kufasiliwa kwa vifaa ambavyo vipo ambavyo wanafunzi wanavitumia katika elimu ya msingi, katika elimu ya sekondari vinaweza kufasiliwa kwa walimu ambao wapo wale ambao wana sifa za kutosha. Lakini pia inaweza kufasiliwa kwa uwezo wa wanafunzi kumudu vile vipimo katika zile hatua ambazo ni muhimu za kupima elimu na katika nchi yetu hatua ya kwanza ni darasa la saba. Tunapima kwa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi. *(Makofi)*

Hatua ya pili ni ngazi ya sekondari ya kawaida au *O Level* wanapomaliza Kidato cha nne pale tunapima tuone uwezo wa wale wanafunzi ukilinganisha na wenzao kwa sababu mitihani ile pia inakuwa na *moderators* wanatoka kwenye mabaraza mengine ya mitihani ya nje ya nchi yetu. Halafu kwenye elimu ya juu ubora wa elimu unapimwa hasa pale ubora wa wahitimu unapopimwa kwa aina ya Maprofessa na walimu walioko katika chuo, lakini ubora wa utafiti unaofanywa katika vyuo vile na ubora wa huduma au *service* inayotoka kwenye vyuo vile na kupelekwa kwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la msingi vitu muhimu ambavyo viko shuleni. Katika mwaka 2002 tulikuwa na walimu wanaofundisha kwenye shule za msingi 109,000. Jana nilipokuwa nawaeleza idadi ya walimu hawa imeongezeka na kufikia 150,895. Vifaa katika shule labda nichague vitabu vimeongezeka kutoka kitabu kimoja kwa wanafunzi 20, kufikia sasa kitabu kimoja kwa wanafunzi watano. Tumejaribu kufanya mafunzo ya walimu kazini na katika Bajeti hii ya mwaka huu mtaona tumetenga fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza azma hiyo. Ukaguzi wa shule umeongezeka na kama tulivyoeleza katika hotuba ya Bajeti ukaguzi umefanywa kwa makini zaidi na Wakaguzi wameendelea kupewa mahitaji muhimu ili waweze kutekeleza kazi yao na mahitaji haya yataongezwa kadri ambavyo bajeti inaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine muhimu ni kiwango cha kufaulu na katika hili labda ni vizuri tueleze kwamba katika sera ya elimu wanafunzi wanakwenda kidato cha kwanza kwa kutegemea kufaulu na nitumie sehemu ya wanafunzi ambao wamefaulu na kuweza kwenda kidato cha kwanza kama moja ya vigezo muhimu vya kuonyesha kwamba elimu inaongezeka ubora. Katika mwaka 2004 vijana waliomaliza darasa la saba kujiunga na kidato cha kwanza walikuwa ni asilimia 30, mwaka 2005 walikuwa asilimia 36, mwaka 2006 walifikia asilimia 49 na mwaka 2007 walifikia 67.5 na mwaka 2008 ilishuka ikafika asilimia 51.2. Ukiangalia idadi ya wanafunzi ambao wapo shuleni utaona idadi hii imeongezeka lakini pia na ile asilimia imeongezeka. Kinachokuonyesha kwamba idadi ya wanafunzi wanaoongezeka kila wakati kutokana na elimu kuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu ya juu napenda kutoa rai kwamba wanafunzi wetu wengi sana ambao wanamaliza elimu ya vyuo vikuu na kwenda katika vyuo vikuu vya nje Marekani, Ulaya, Urusi na kwingineko wanafanya vizuri sana na wakati mwingine vyuo vile vinawaajiri kuwa wanataaluma au watafiti katika vyuo vyao.

Pamoja na hilo mtakuwa mnakumbuka kwamba mwaka 2007 mmoja wa Maprofesa wetu ambaye ni Mkurugenzi sasa wa *Institute of Resource Assessment* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alipata nishani ya *Nobel Peace Prize* kwa ajili ya utafiti wake. Sasa hii ndiyo *prize* unayoweza kupata kama msomi wa hali ya juu kupita zote na kama anatoka kwetu huwezi kurudi ukasema elimu hiyo imeshuka, itapanda ifike wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Chuo chetu cha Kilimo cha Sokoine, watafiti katika chuo kile wamegundua vitu vinne muhimu ambavyo vimepewa *patent* ya *research* katika dunia. Hili ni jambo muhimu sana ambalo ni lazima tuwapongeze watafiti wetu na tukipongeze chuo chetu hiki kwa ubora wa elimu. Katika mapitio ya vyuo vikuu vya kwetu ambayo yamefanywa na wataalam wa Kimataifa wakipitia vyuo vikuu vyote duniani. Katika vyuo vikuu vya Afrika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeshika nafasi ya tatu katika vyuo vikuu vyote vya Afrika Kaskazini ya Mto Limpopo na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kimeshika nafasi ya 84. Kwa hiyo, napenda niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kwamba hizi ni dalili nzuri na hofu zenu pia ni dalili nzuri kwamba mnataka maendeleo haya yaongezeke na sisi tutafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba tunafikisha hapo mnapotaka elimu ifike tutaipeleka kwa ushirikiano na Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limeongelewa hapa ndani ya Bunge kwa nguvu kabisa, kwa uchungu kabisa ni juu ya matatizo ya walimu. Utumishi wa walimu wetu hapa nchini ndiyo wametufikisha katika ubora huo niliokuwa nausema hapa na mimi napenda sana niwapongeze walimu wetu wote popote walipo hapa Tanzania kwa utumishi uliotukuka. Isingekuwa kazi kubwa kweli ya walimu wanayofanya tusingefika hapa tulipofika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napenda nichukue fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu niwashukuru sana walimu wa Tanzania pamoja na chama chao cha CWT kwa kazi nzuri sana ambayo wanafanya katika kulijenga Taifa letu. Aidha, kutokana na mazingira yalivyotofauti katika kufanya kazi hapa nchini, katika hotuba yetu ya Bajeti tumeeleza kwamba tutaunda *task force* ambayo itapitia upya *scheme of service* ya walimu wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ili kuangalia ni jinsi gani tunaweza kuboresha *scheme of service* ya walimu wale na kuwapa motisha huko wanakofanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaliangalia suala la wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo magumu na lipo njiani kutolewa maamuzi. Katika hili napenda niongeze neno lingine. Ni kweli kwamba walimu wana madai mengi sana kwa Serikali. Awamu ya kwanza ya madai haya yalifanyiwa uhakiki na zaidi ya shilingi bilioni tisa zililipwa kwa walimu katika mikoa mbalimbali wa shule za msingi na walimu wa sekondari. Kama tulivyoeleza pale awali Serikali haikulipa wale walimu ambao nyaraka zao zilikuja hazikuwa kamilifu. Tumetoa rai kwamba walimu wote ambao hawakupewa malipo yao na ambao wanadhani kwamba wamepunjwa walete nyaraka zao zote za madai hayo na Serikali itaendelea kuyahakiki madai hayo na itaendelea kuyalipa hata kama ni awamu kwa awamu. Lakini nitoe azma ya Serikali ya kumaliza madeni yote ya walimu ambayo wanaidai Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yapo madai ya wazabuni ambayo yamekuwa yanasumbua kweli kweli. Tuliwaita walimu wote wa shule za Sekondari wakaleta madai ambayo wazabuni wanatudai katika Mikoa mbalimbali na katika hatua ya kwanza Serikali imelipa shilingi 6.3 bilioni ili kushughulikia madeni haya na yale ambayo hayakulipwa ambayo yanakadiliwa kuwa karibu shilingi bilioni nne yataendelea kuhakikiwa maana yake mengi yalikuwa hayana nyaraka timilifu na uhakiki ukikamilika na wakileta nyaraka timilifu nataka niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba wazabuni hawa tutawalipa na tatizo hili la kudaiwa kila siku mimi nakubaliana na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba si vizuri katika utaratibu wa *cash budget* kuwa na *back log* ya madeni ambayo hayalipiki. Tutafanya juhudi zote kuhakikisha kwamba tatizo hili linamalizika.

Waheshimiwa Wabunge waliongea kwa nguvu sana kuhusu upungufu wa vifaa katika shule za sekondari hasa maabara ya kujifunzia sayansi na *TEHAMA*, tumechukua hatua thabiti kabisa. Kwanza ya kufanya *study concrete* ya kujua tatizo lenyewe kubwa kiasi gani. Tumeangalia tuka-*separate* yale ambayo ni ya kukarabati na vifaa vya kutengeneza tu yaendelee vizuri. Yale ambayo ni ya kuongezea vifaa na yenyewe yapo na yale ambayo hayana kabisa. Tumeangalia mahitaji ya maabara katika shule za sekondari ya kawaida kwa maana ya *O-level* na tumeangalia yale mahitaji ya *A-level* na tumetengeneza andiko zuri kabisa ambalo tunajadiliana na shirika letu la maendeleo na mimi nina uhakika kwamba kabla ya siku nyingi tutakuwa na la kuripoti kwenye Bunge lako Tukufu kuhusu ni hatua gani tuchukue kujenga maabara katika shule zetu za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wametoa mawazo mengi kuhusu suala hili. Nichague moja tu la Mheshimiwa Jackson Makwetta kwamba labda kutokana na tatizo lilivyokubwa tuchague shule fulani tuzipe maabara na nyingine tusizipe maabara. Lakini katika shule tukishaamua kwamba tunajenga shule ya sekondari ni kama kuamua kujenga barabara ya lami. Hatuwezi kuamua kwamba tukifika njiani pale kwa sababu hakuna mafuriko sana turuke tuweke lami mbele kule. Kwa hiyo, tumeamua kwamba hizi shule tutaziwekea maabara kulingana na kiwango cha elimu kinachotolewa katika shule zote ili tuwape fursa wanafunzi wote, wapate fursa ya kujifunza sayansi na wale ambao vipaji vyao vipo kwenye sayansi wasiwe wamebaguliwa katika utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yalitolewa pia malalamiko makubwa kabisa kuhusu wanafunzi wanaojiandikisha kama *private candidate* wengine kunyimwa kufanya mtihani huo. Nimeona hili vizuri nilieleze kidogo na Mheshimiwa Martha Mlata, alisimama kidete pale akasema hili lazima lielezwe ama hapatakalika hapa. Basi naona nilieleze vizuri ili tuweze kukaa wote humu ndani na tuwe na imani ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kipindi cha usajili, watahiniwa hupewa maelezo kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia pamoja na sifa wanazopaswa kuwa nazo ili waweze kusajiliwa kwa ajili ya kufanya mtihani. Aidha, fomu ya maombi ya usajili wa mitihani inaonyesha kuwa mtahiniwa anatakiwa kujaza taarifa kwa

mwandiko wake yeye mwenyewe na kuhakikisha amejaza kwa usahihi na kwa ukamilifu. Hata hivyo baadhi ya watahiniwa huandika majina na yale yaliyo kwenye kumbukumbu za Baraza la Mitihani. Pia baadhi ya watahiniwa kuandikia namba za mitihani ambazo hazioani na majina yao kwenye mitihani waliyofanya kipindi cha nyuma. Baraza la Mitihani lilikuwa na utaratibu wa kuwataka watahiniwa wanapowasilisha taarifa zisizo sahihi kufanya marekebisho ili hatimaye waweze kuruhusiwa kufanya mtihani. Changamoto iliyojitokeza ni kwamba baadhi ya watahiniwa wamekuwa hawawasilishi taarifa hizo hadi wakati wa mtihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma Baraza la Mitihani likikuwa likiwaruhusu kufanya mtihani kwa masharti kuwa matokeo yao yatazuiliwa hadi hapo watakapowasilisha taarifa sahihi. Utaratibu huo ulikuwa unaleta usumbufu katika Baraza la Mitahani kuendelea kufuatilia sifa sahihi za watahiniwa ambao tayari wamekwishafanya mtihani. Baadhi ya watahiniwa hao wamekuwa wakibainika kuwa hawakuwa na sifa na hivyo Baraza la Mitihani limekuwa likilazimika kufuta matokeo yao kwani kimsingi hawakustahili kufanya mtihani huo. Kwa mfano, mwaka 2005 Baraza la Mitihani lilifuta matokeo ya watahiniwa 137 wa mtihani wa ualimu daraja la “A” kutokana na sababu mbili zifuatazo. Sababu ya kwanza kuwasilisha taarifa za kughushi. Wote mnajua kwamba pale Dar es Salaam na miji mingine kuna vituo kule vina *print certificates* utadhani ni *certificate* kweli. Kumbe watu wamekwenda mjini wanatumia bongo wametafuta cheti cha bandia.

Pili, kutokuwepo hawa waombaji kwenye kumbukumbu za *NECTA.* Katika mtihani wa ualimu daraja la “A” uliofanyika mwezi Mei, 2008 imebainika kuwa wapo watahiniwa waliofanya mtihani bila kuwa na sifa. Uchunguzi unaoendelea kufanyika umebaini kuwa jumla ya watahiniwa 112 walifanya mtihani huo kwa kutumia vyeti vya watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa nimeleta watahiniwa wa namna hiyo. Mtahiniwa amekuja, amepigwa picha na Baraza imeiomba shule anakosema alisoma huyo mwanafunzi na cheti alicholeta walete picha ya mtahiniwa huyo. Wakati Baraza likipata picha hizo unaweza ukaona hapa, mtu ambaye ana ulemavu wa macho kipofu cheti chake kimechukuliwa na mtu ambaye anaona tena mzee na hapa msichana cheti chake kimechukuliwa na mvulana na hapa mtoto mdogo cheti chake kimechukuliwa na mtu mzee. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna udanganyifu mkubwa kweli kweli; na kwa sababu hiyo ni muhimu sana taasisi hii kukagua kwa uangalifu na kwa makini sana ili kuhakikisha kwamba watu hawatumii vyeti bandia na uhakiki huu tutauendeleza si kwenye vyeti vya shule za sekondari peke yake lakini hata Shahada, Stashahada, Shahada za Uzamili na hata Shahada za Udaktari. Kwa sababu kuna udanganyifu mkubwa sana ambao umebainika katika mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Richard Ndassa, alisema atatoa shilingi kwenye Kamati ya Bunge Zima kwa sababu mwalimu aliyemtaka katika Shule ya Wasichana Sumve hajateuliwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mwalimu

Joyce Mtafungwa kutoka shule ya sekondari Sengerema ameteuliwa tarehe 9 Juni kuwa Mkuu wa Shule hiyo ya Sumve. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nimalizie pale alipoishia Mheshimiwa Naibu Waziri, tumesikia *very loud and clear*, kilio cha Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa James Musalika kuhusu *VETA* ya Wilaya ya Geita. Nilipozungumza na wataalam wangu leo wameniambia kwamba suala hilo lilikuwa limeshashughulikiwa baada ya mawasilisho ya Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba katika Kamati ya Huduma za Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi pia tulipata maombi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu kutoa tamko juu ya michango mingi sana ambayo inatozwa na walimu wa shule ya sekondari kwa wanafunzi ambao wanajiunga na shule za sekondari. Suala hili liliongelewa jana na Mheshimiwa Nuru Bafadhil na liliongelewa hapa tena na Mheshimiwa Meryce Emmanuel na Waheshimiwa Wabunge wengi wameliongelea suala hili. Upo waraka wa Serikali ambao unazielekeza shule ni vitu gani ambavyo vinaweza kuchajiwa kwa wanafunzi. Ada shilingi 20,000, *caution money*, fedha ya kupiga picha kwa ajili ya kitambulisho cha shule, *uniform* na kadhalika na vitu hivi viko *very specific* kwa wanafunzi wa kutwa na kwa wanafunzi wa bweni. *(Makofi)*

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu itatoa maelekezo haya upya ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka. Aidha, katika waraka ule wa Serikali kama shule zina mahitaji maalum kuna maelekezo kama mahitaji yao yanahitaji mchango ambao hauzidi shilingi 25,000/= bodi ya shule inaweza kuamua juu ya mchango wa namna hiyo. Mchango unapofikia shilingi 25,000/= lazima Mkaguzi Mkuu wa Kanda lazima atoe kibali chake na shule hairuhusiwi kutoza zaidi ya shilingi 25,000 kama haina kibali cha Afisa Elimu Kiongozi. Kwa hiyo, tatizo hili tutalishughulikia kikamilifu na kuhakikisha kwamba walimu wakuu wanafuata utaratibu ambao wamepewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii wakati alipokuwa anatoa maelezo hapa alieleza kwa undani suala la ufinyu wa Bajeti na ni kweli na katika maeneo fulani fulani ambayo yako *very critical* ni kweli kwamba Bajeti tuliyonayo ni kidogo. Lakini nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba kwenye Bajeti ya Mamlaka ya Elimu Tanzania tutaangalia kwa jinsi ambavyo tumepewa Bajeti na jinsi ambavyo Bajeti tumeigawanya na kuona kama kwa kadri itakavyowezekana kuwaongezea Bajeti ili waweze kushughulikia miundombinu ya vyuo na shule ambazo wamekuwa wanazihudumia vizuri sana. *(Makofi)*

Napenda nichukue fursa hii, wakati tunaongea juu ya taasisi hii kujaribu kujibu sehemu ya swali alilouliza Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu maeneo gani ambayo Wizara yangu inashirikiana kwa karibu na Wizara ya Elimu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Moja ya maeneo hayo ni katika taasisi hii ya Mamlaka ya Elimu Tanzania. Katika mwaka mmoja, miwili iliyopita taasisi hii ilitoa jumla ya takribani shilingi milioni 296 kusaidia Chuo Kikuu cha Zanzibar katika *staff development*, taasisi iliwapatia shilingi milioni 50 katika kujenga uwezo wao wa *ICT*

wamewapatia kompyuta zenye thamani ya shilingi milioni 28.8 na katika *pre-entry training* ya wanachuo, taasisi imewapatia shilingi milioni 84 na kuwanunulia vifaa vya maabara vya thamani ya shilingi milioni 18.6. Kule *Karume College*, Taasisi hii imetoa shilingi milioni 115 kwa hiyo jumla ni shilingi milioni 296.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliulizwa pia upo uhusiano gani kati ya *TCU* na Chuo Kikuu cha Zanzibar. Chuo Kikuu cha Zanzibar kimeanzishwa kwa Sheria ya Chuo Kikuu cha Zanzibar iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar mwaka 1999. Sheria ile inatumika mpaka sasa. Baada ya kutungwa kwa Sheria ya Vyuo Vikuu, Sheria ile ilipelekwa kwenye Chuo, Baraza la Chuo likaiangalia sheria ile na moja ya mahitaji ya sheria ile ni chuo kutengeneza idhini yake ya kufundisha na kutoa *awards*. Chuo kimefikiria hilo, kimetengeneza *charter* yake kikaipeleka Wizara ya Elimu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Wizara ya Elimu kama inavyohitajika imeipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ametoa mawazo yake na yale mawazo yamerudishwa kwa Waziri wa Elimu na hivi leo mchana nimetaarifiwa kwamba hatua iliyobaki ni kupeleka kwa Mkuu wa Chuo ili apitie na kuridhia *charter* ile na baada ya hapo sasa sheria ile itawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi ili ile sheria iliyoanzisha Chuo iwe *repealed* na Chuo kipewe *charter* kwa ajili ya ku-*operate* kama vyuo vingine vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nieleze kwamba yapo mashirikiano mengi sana katika elimu kati ya Wizara yangu na Wizara ya Elimu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Maeneo hayo yako katika Kamati ambazo zimeanzishwa na zinafanya kazi na kukutana zaidi ya mara nne kwa mwaka. Zinaangalia mitaala, michezo na shughuli mbalimbali ambazo zinatuunganisha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliulizwa pia maswali kuhusu tathimini ya uwezo wa mwombaji wa mkopo wa Elimu ya Juu na Baraza la Mikopo ya Wanafunzi na kwamba Baraza lile linatumia kompyuta *almost exclusively* ili kufanya tathimini hiyo. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba pamoja na kufanya *scanning* na kuzisoma zile fomu na kumpanga sasa mwombaji katika ngazi ya uombaji fomu zile pia zinapitiwa sasa mkono kwa mkono kuangaliwa kwamba hivi ni kweli au namna gani. Hiyo ni hatua ya kwanza. Lakini hatua ya pili ni ya mwombaji mwenyewe akishapata yale matokeo ambayo yametolewa na yeye akiona kwamba hayalingani na vile mwenyewe ambavyo alivyo ana nafasi ya kuomba rufaa kwenye Bodi na hata kama Bodi ikishikilia uamuzi bado ana nafasi ya kuomba rufaa tena kwa Waziri mwenye dhamana ya elimu. Kwa hiyo hili linafanywa kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kitu kikubwa tulichonacho, tushirikiane kutafuta fedha zaidi, rasilimali zaidi katika mfuko ule ili wanafunzi wengi zaidi waweze kufaidika. Lakini wakati tunazo fedha ambazo hazitoshi kumpa kila mmoja akapata mkopo, ni muhimu sana tutafute njia ya kuweza kuwachambua wale ambao hawana uwezo wapewe kipaumbele, wale wenye uwezo mdogo, wachangie kama ile *policy* ya elimu inavyosema na wale ambao wana uwezo mkubwa waweze kujilipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niangalie maeneo mengine ambayo bado yamebaki. Eneo moja ambalo nataka nilisemee kidogo ni juu ya mtihani wa darasa la nne, juu ya mtihani wa darasa la kumi au *form two*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitihani hii haijafutwa! Hatufuti mtihani wa darasa la nne, hatufuti mtihani wa *form two*, maana pamoja na kusema sana juu ya suala hili, naona linarudiwa, linarudiwa, linarudiwa. Jamani, hatufuti mtihani wa darasa la nne, hatufuti mtihani wa *form two*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo sera ya elimu ambayo inatueleza elimu ya msingi ni kitu gani. Inasema; "elimu ya msingi itakuwa kwa wote na ya lazima kwa watoto wote wenye umri wa miaka saba hadi wamalize ngazi hii ya elimu." Na ngazi hii ya elimu ni ya miaka saba na kwamba Serikali itatoa kipaumbele kuhakikisha kila mtoto wa Tanzania anasoma na kupata elimu ya miaka saba. Sasa katika hili, ningependa kutoa takwimu kidogo tu; katika mwaka 2006, watoto 1,391,000 waliandikishwa kufanya mtihani wa darasa la nne. Lakini wakati wa kufanya mtihani, watoto 1,195,000 ndio waliofanya mtihani, jumla ya watoto 200,417 waliogopa kufanya mtihani huo, wakaondoka shuleni. Halafu walipofanya mtihani huo, watoto walioshindwa mtihani huo ni watoto 239,300 na waliokariri walipofeli ni 134,000. Kwa hiyo, katika mwaka huo peke yake kwa ajili ya huu mtihani wa darasa la nne, watoto 300,000 wamekwenda nyumbani mwaka 2006 na ukiangalia katika Mikoa, karibu asilimia 20 wanaondoka shuleni kwa sababu ya huu mtihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kurudia darasa maana yake ni kurudi kusoma, bila utaratibu unarudia tu, unajiunga na wale wadogo zako bila kuangalia saikolojia ya kurudia kusoma na wadogo waliokufuata nyuma na kukaa hapo mwaka mzima, utegemee basi utapita. Tunachosema, kama ambavyo tulipanga *MEMKWA*, tutawatambua hawa watoto ambao wanafeli, tutengeneze utaratibu wa kuwapa mafunzo ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tunaanza majaribio katika shule 200 ya *TEHAMA*, kuwafundisha kwa njia za kompyuta kuona kwamba hiki kitu inaweza kufanyika kwa namna gani. Kwa hiyo, jamani nawaomba sana, mtoto wa darasa la nne bado anacheza, bado ni mdogo na bado ana nafasi ya kujifunza. Hebu tuwape nafasi watoto wasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi yoyote hapa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika ambayo ina mtihani wa katikati ya shule za msingi, hakuna! Huu ni mtihani wa kizamani sana! Hakuna nchi ya namna hiyo, Kenya hawafanyi, Uganda hawafanyi, Rwanda hawafanyi, Malawi hawafanyi, hakuna mahali wanafanya kitu hiki. Kila mahali wana njia ya kuwajua watoto maana shule zote zinatoa mtihani wa *term*, zinawaangalia watoto wanafanya namna gani, zinatoa mtihani wa mwisho wa mwaka, watoto wanafanya namna gani na wanafanya hivyo darasa la kwanza, la pili, la tatu, hujamjua mtoto bado kwamba hajui kusoma na kuandika, unafanya nini hapo shule! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ndiyo lengo letu na tunafanya hili kwa nia njema kabisa badala ya kumrudisha mtoto awe hana mwenyewe, ameshindwa mtihani wa darasa la nne, hana mwenyewe, hamna mtu wa kumwangalia. Sasa tunataka tuwaweke chini ya uangalizi kamili, waweze kupata *remedial teaching* ili waweze kupita katika *huddle* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa elimu, ngoja niangalie kama kuna lingine. Mtihani wa *form two* uko hivyo hivyo, ni mtihani ambao hakuna nchi ambayo inafanya kitu cha namna hiyo, hakuna! Lakini mitihani hii hatutaifuta, tutaendelea kuitoa na tutaendelea kutoa motisha kwa wanafunzi wenyewe, kwa walimu wanaowafundisha na kwa shule ambazo zitafanya vizuri tutazipa motisha ili kuwe na ushindani huu na matokeo ya mtihani ule yatakuwa sehemu ya *continous assessment* ya mtoto anayemaliza *form four*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba ziko hoja nyingi ambazo hatujazijibu. Lakini kama nilivyokueleza hapo awali, tutahakikisha kwamba majibu yote tutayatoa kwa maandishi kwa Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaondoka hapa Dodoma wakati wa kikao hiki cha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki! *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kifungu 1001 – *Administration and General* ……………..Sh. 8,733,239,300/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Mikidadi unaanza!

Ngoja kwanza tufanye utaratibu, maana hapa mko 38! Sasa mara tano, mara kumi kwa sababu Waziri naye ana muda, maana yake ni dakika 300 na gawa kwa 60. Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tukubaliane utaratibu, hatuna namna, hii ndiyo hali halisi. Tukisema twende kwa kanuni zetu kabisa kabisa tutaishia watu 10 tu. Kwa hiyo, nashauri kabisa kwamba atakayesimama, mjipange vizuri, najua mna hoja nyingi sana. Tafuta hoja unayofikiria lazima ujibiwe. Tukifanya hivyo, wote mtafikiwa, tutaangalia mbele tunaishia wapi. Lakini naamini wote mtafikiwa. Kwa hiyo, jamani tuheshimiane kwa hili na uamuzi wangu uko katika Kanuni ya 71. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa muulizaji wa kwanza. Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 170…

**MWENYEKITI:** Naomba, wote ni mshahara wa Waziri tu, kwa hiyo, msitumie mshahara wa Waziri, muendelee tu kusema ili tuokoe muda.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** *Vote 46,* mshahara wa Waziri!

**MWENYEKITI:** Endelea, endelea, endelea!

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujibiwa maswali mbalimbali, kulitokea na maswali ya *VETA*, ujenzi wa shule za ufundi za *VETA* kwamba Sera ya Taifa inasema kwamba kila Mkoa kuwe na *VETA.* Sasa mshahara huu, pesa hizi zilizotengwa hapa ni pamoja na *VETA* ya Mkoa wa Lindi kwa sababu nimeona tu kwamba *VETA* za Wilaya zimeanza, je, Mkoani Lindi ni pamoja na pesa hizi?

**MWENYEKITI:** Zipi, za mshahara wa Waziri? Wewe sema Lindi kuna *VETA?* Lakini kusema mshahara huu kwa ajili ya *VETA* siyo! Au umeulizaje swali lako?

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa! Ahsante sana kwa kunisaidia! *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu msishike mshahara wangu ni mdogo sana! Ukishakatwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu tu, hiyo ni *concept* tu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iko *VETA* kwa ajili ya Mkoa wa Lindi. Mkataba kwa ajili ya *VETA* hiyo utasainiwa Jumatatu ijayo na jiwe la msingi litawekwa mwezi Novemba, 2008.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa hadi leo kuna shule nyingi ambazo bado zimefungwa na hata leo wakuu wa shule za sekondari wa Mkoa wa Kagera wameshinda kwa Mkuu wa Mkoa, hawajui wafanye nini na watoto kwa sababu hawana chakula; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa majibu mazuri kwamba anategemea kulipa, tunaomba kujua ni lini kusudi hawa watoto waache kuhangaika na ni kiasi gani sasa watapewa kusudi waweze kula vizuri hata kuliko wafungwa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza maofisa wa Wizara wako kwenye Ukanda wa Ziwa wanaendelea kuwalipa wazabuni. Kwa hiyo, labda leo siku imeshakwisha, lakini kesho wataendelea na kazi hiyo na ni matumaini yangu kwamba katika wiki hii hao wazabuni ambao hawajalipwa watakuwa wamelipwa.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza kwamba karibuni tutapata wimbi kubwa la wanafunzi waliomaliza *form six* na Chuo pekee ambacho kinaweza kudahili wanafunzi wengi zaidi ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania *(Open University).* Lakini sasa hivi kina matatizo ya malipo ya walimu wao *(Part-time Lecturers)* ambao kwa kweli tunawahitaji wengi zaidi kwa vile sasa hivi tunataka tutarajie wanafunzi wengi kuja. Malipo yao hayana uhakika na yanachelewa sana kuja kwa sababu yanaletwa katika *OC*. Kwa nini tusiyatie katika *Personal Emoluments (PE)* ili mishahara hiyo ije, wapate kwa uhakika na kwa wakati ili kazi ziende sawa sawa, *otherwise* watatukimbia walimu hawa *(Part-time Lecturers)* huku tukiwa tunataraji wanafunzi wengi kuingia *Open University* baadaye. La pili....

**MWENYEKITI:** Moja tu ndugu yangu! Wako watu 40! Mheshimiwa Waziri, wasaidizi wako pia wanaweza kukusaidia, siyo lazima uwe peke yako.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko, ni kweli kuhusu mishahara ya walimu wa Vyuo Vikuu kupitia *OC*. Tumewasilisha matatizo hayo kwenye Serikali na si muda mrefu yatapata ufumbuzi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, nimshukuru Naibu Waziri kwa kulithibitishia Bunge hili kama alivyofanya Mheshimiwa Waziri tarehe 27 Juni, 2008 wakati wa kuhitimisha hotuba ya Waziri Mkuu kwamba shule za Nanyanje na Chikonji hazitafutwa. Lakini nafikiri kwa sasa hivi siyo muhimu kwa Naibu Waziri kusema kwamba nani alikuwa wa mwanzo kuleta hoja hii hapa Bungeni, muhimu ilikuwa, hoja imeletwa, imeeleweka na suluhisho limepatikana, *finish!* Kabla ya kutaka ufafanuzi, nina mambo mawili ya kueleza. Kwanza, shule iliyoandikishwa ni Nanyanje, siyo Chikonji. Pili, pesa shilingi milioni 45 ambazo zimeletwa ni za shule ya Nanyanje kwa ajili ya kujenga madarasa, maabara na nyumba. Tatu, jana shule zilipofunguliwa, wanafunzi wa Nanyanje walikwenda Chikonji na walimu wao. Sasa ningependa kujua, Waziri aseme ni lini wanafunzi wa Nanyanje watarudi katika shule yao? (b)….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, aah ah!

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Ndiyo hilo hilo moja (a) na (b)!

**MWENYEKITI:** Tumemaliza. Mheshimiwa Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba niseme kwamba suala hilo liliwasilishwa na Mheshimiwa Mbunge Mudhihir Mudhihir na Kamati yake ilifika ofisini kwangu mimi kuniona juu ya matatizo ya shule hiyo; na kwa kuwa waliyaleta kwa maandishi, tulianza

kuyafanyia kazi. Matatizo yale ni ya kimsingi, tumepeleka wakaguzi kule, tumepokea ushauri wa kitaalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba hatutaharibu majengo ambayo yalijengwa. Lakini kutokana na hali ya kijiografia, tunaomba wanafunzi waendelee Chikonji na tutaendelea tena baada ya kuboresha miundombinu ile shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limezungumzwa pia katika *RCC* ya Mkoa wa Lindi na kwa kuwa Bunge hili hatuwezi kuingilia maamuzi ya Mkoa wa Lindi, naomba Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi walichukue hili wakalitolee maamuzi kwao. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu katika hotuba ya Waziri Mkuu, nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kuna walimu ambao wanafundisha kwenye shule lakini wanahamishwa kutoka shule, wanapelekwa Wizarani kufanya kazi za *administration*. Ningependa kujua ni nini tamko la Waziri kama atawarudisha walimu warudi kwenye *field* kwa sababu sasa hivi tuna matatizo makubwa sana ya walimu hasa wa sayansi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu ni watumishi kama watumishi wengine na kupangiwa kazi inategemeana pale ambapo watafanyakazi nzuri zaidi na kule Makao Makuu kuna kazi za kutengeneza mitaala, kutayarisha vitabu na kazi mbalimbali ambazo zinafanywa. Kama wale walimu ndio wataalam wazuri kupita hao, wataendelea kufanya hizo kazi na kule ambako wamechukuliwa tutapeleka walimu wengine. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Mimi katika mchango wangu wa maandishi niliomba Serikali itoe ufafanuzi kuhusiana na suala la michango ya ujenzi wa sekondari za Kata. *Rate* hazieleweki katika maeneo tofauti na imekuwa ikichangwa kwa kuwa-*harass* wananchi. Akinamama wengi utakuta wanarushwa kichura chura kwa sababu wameshindwa kuchangia na maeneo mengine, kwa mfano kwa Singida, nimefanya *research* ndiyo maana nasema. Kwa mfano Singida, kitongoji cha Kasisida, mke na mume wanatakiwa watoe shilingi 66,000/=, Sepukwa, Puma na maeneo ya Ikungi, maeneo mengine, mwanamke na mume wanatakiwa watoe shilingi 20,000/=. Lakini, ukiwa na ng’ombe, unatoa elfu moja moja kwa kila ng’ombe ulienaye, ukiwa na mbuzi, shilingi 500/=, ukiwa na kondoo shilingi 500/= kulingana na idadi na kama una punda vile vile unamlipia shilingi 1,000/=. Mbaya zaidi, Mkuu wa Wilaya aliandika barua ikasambazwa maeneo yote, ilikwenda kwa wananchi wakaambiwa wabandike vijijini. Inamtaka kila mwananchi alipe, lazima, asipotii amri hiyo afungwe miaka miwili.

Sasa naomba kujua, Serikali inasemaje na inatoa tamko gani kuhusu suala hili kwa sababu imekuwa ni kero sana kwa wananchi na wengi wana umaskini wa kipato, mtu mwingine hata uwezo wa kula hana, anaenda kufungwa kwa sababu ameshindwa kuchangia shule. Ahsante! *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za Kata zinajengwa kwa ushirikiano wa Seriikali Kuu na wananchi na Halmashauri za Wilaya na wananchi na msimamizi mkuu katika Wilaya kule ni Mkuu wa Wilaya. Lakini wakati wa kujenga, wananchi wanaunda kamati ya ujenzi, kamati ya ujenzi inapanga utaratibu wa michango utakavyokuwa. Utaratibu huu unapelekwa kwenye *Ward DC. Ward DC* inapokea na kurekebisha pale ambapo inaona siyo pazuri na kuweka utaratibu ambao wanaujua kule kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu hiyo, kwa kweli Wizara yangu haina taarifa ya watu kuruka kichura chura kwa ajili ya kuchangia shule na kadhalika. Tungemuomba Mheshimiwa Mbunge atuletee nyaraka hizo ambazo zinasema Mkuu wa Wilaya ameamuru mtu afungwe miaka miwili ili tuweze kuifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi swali langu ni la kisera. *(Makofi)*

Sisi wote tumelalamika kuona namna gani masomo ya sayansi hayapendwi. Lakini katika mchango wangu ni kwamba sababu kwa ujumla tunaifahamu ni kwa *nature* ya masomo yenyewe ya sayansi kulinganisha na masomo mengine, halafu ni suala la muda wa masomo ya sayansi. Lakini mwanafunzi au mtu anaye-*graduate* katika masomo ya sayansi akija kwenye *system*, ni mtu ambaye aidha, katika mshahara au katika mambo mengine ni chini kabisa. Je, Wizara na Serikali kwa ujumla, iko tayari sasa kubadilisha au kutangaza kivutio kwa wanafunzi wa sayansi na kufanya muundo wa masomo ya sayansi ambayo ndiyo yana upeo mkubwa katika kuendesha nchi ili wanafunzi sasa wavutike, waweze kupenda wenyewe masomo ya sayansi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufindi, napenda kutoa ufafanuzi wa masuala ambayo ameuliza Mheshimiwa Mohamed Mnyaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba wanaomaliza masomo ya sayansi wanapoenda kuanza kazi kwamba wao wanaanza katika kima cha chini kabisa cha mishahara. Wanaomaliza shahada za sheria za uhandisi na sayansi kwa ujumla wanaanza na mshahara *TGS E* wakati wanaomaliza kada nyingine wanaanza na *TGS D*. Kwa hiyo, wanaomaliza sayansi wanaanza na mshahara wa juu zaidi ukilinganisha na ambao wamemaliza katika kada nyingine. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimeshitushwa sana kauli za Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala la mitihani ya darasa la nne na darasa la kumi. Na nimeshitushwa zaidi na sababu anazozitoa za kwa nini kwamba mitihani hiyo inaendelea, lakini wanafunzi wataendelea. Kwa kweli sababu zake hazijengi mantiki na imejengeka imani ya kwamba mitihani hii ni ya zamani sana. Mheshimiwa Mwenyekiti, mitihani hii siyo ya zamani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipofanya mtihani wa darasa la nne mwaka 1987, ilikuwa *intake* ya pili ya kufanya mtihani wa darasa la nne. Mitihani hii ilianzishwa wakati Mheshimiwa Makwetta akiwa Waziri wa Elimu. Kwa hiyo, siyo ya zamani kama jinsi ambavyo Waziri na baadhi ya Wabunge wanavyotaka kutuaminisha na Waziri anasema kwamba, mitihani hii watafanya *test* kwenye baadhi ya shule ili baadaye ndiyo waweze kuona ni jinsi gani ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali hivi sasa isiweke huo mfumo wa kuwasaidia hao wanaofeli ili waweze kujiendeleza watakapokaa tena kwenye mtihani badala ya kuwaachia tu watu wapite kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba; ni vipi Waziri anaitafsiri Sera hii ya Elimu kwa kutoa *sweeping statement* kuhusiana na mitihani ya darasa la nne na *form two?* Waziri akumbuke kwamba, mwaka jana alipokuwa Waziri wa Maliasili, alitutangazia bei mpya hapa za vitalu na baadaye bei zile hazikutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, naomba uzamie katika hili tu. (*Kicheko*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie ndiyo hilo hilo, kwa sababu ni suala la *credibility*. Ninasema kwamba, kama kuna maamuzi ambayo yalitolewa hayakutekelezwa leo maamuzi ya mitihani yanapotolewa kwa nini tusiamini kwamba hayataheshimiwa pia?

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ijaribu kuangalia upya uamuzi wake kuhusiana na suala la mitihani ya darasa la nne na suala la mitihani ya darasa la kumi. Hii ni kwa sababu, naamini kabisa kwamba, maamuzi ambayo Serikali inayachukua leo, yatakuwa ni gharama kubwa sana kwa watoto wa Tanzania miaka michache ijayo.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri, uwe *very brief.*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nimekieleza kipo kwenye Hotuba ya Bajeti kwamba, mtihani huu unapima mafanikio na maendeleo ya mwanafunzi ili kuona iwapo malengo ya ufundishaji na kujifunza yamefikiwa na kwa sababu hiyo, hauwezi kufutwa, kwa kuwa unalenga kupima uwezo wa kusoma, kuandika, kuhesabu na kubaini kasoro zilizopo ili kuweza kufanya marekebisho na pia kuboresha njia na mbinu za kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kutoa fursa ya kubaini kama wanafunzi ama watoto wote wenye matatizo, sasa wanaweza kulengwa *personally* na kusaidiwa, badala ya

kurudia na kujiunga tu kwenye kundi. Sera inaeleza wazi juu ya utaratibu huu wa elimu ya msingi. Nilichojaribu kueleza pale ni kwamba, lazima tubadilishe namna ya kuwapa watoto elimu, kuwamotisha na si kutumia tu *system* ya kuwafanya waogope. Tuwafundishe watoto wapende shule na hakuna nchi ambayo ina mitihani katikati ya shule ya msingi ambayo inamfanya mtoto arudie darasa au akimbie shule. Takwimu tulizonazo zinaonyesha mdondoko mkubwa kutokana na mtihani huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri hivi sasa tuna mjadala unaoendelea kwa wananchi kuhusu Sera ya Elimu hii ambayo nimeishika na ningependa Waheshimiwa Wabunge, muisome ili muone malengo ya Sera hasa katika Shule za Msingi. Majadiliano haya, yatatuwezesha kufikia mahali ambapo kwa pamoja tutaamua kwamba, tufanye nini juu ya suala hili.

**MWENYEKITI:** Unajua, Mheshimiwa Waziri unasema kwamba, mitihani ya darasa la nne na *form two* itaendelea, sasa unapoendeleza na maneno mengine watu hawaelewi; umesema inaendelea ama itafutwa? Ungekuwa umesema mengine ni *internal affairs* katika Wizara yenu, namna mtafanya ni ya kwenu wenyewe kule. Sasa ukituambia hayo unatuchanganya; mtihani utafanyika ama hautafanyika?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtihani wa darasa la nne haukufutwa unaendelea na mtihani wa darasa la kumi unaendelea haukufutwa.

**MWENYEKITI:** Basi nashukuru.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza, ningeomba kwa ruhusa yako nifanye sahihisho; Waziri alipokuwa anaelezea juu ya Vyuo vya Zanzibar alisema wamevisaidia. Ninavyofahamu, kwa mujibu wa Katiba yetu, suala la elimu ya juu ni la Muungano; kwa hiyo, si kwamba wamesaidia bali ni wajibu wao. Ningeomba kusahihisha hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika mchango wangu nilizungumzia suala la wanafunzi ambao wanasoma Sayansi na *Arts*, wanapopewa mikopo chukua *category* moja ya D; wanafunzi wa Sayansi wanalipa kama shilingi milioni moja na wanafunzi wa *Arts* wanalipa shilingi laki tano, bahati mbaya sikuweza kupata ufafanuzi wowote kwa Waziri katika hili. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli kwamba, masomo ya Sayansi ni ghali kuliko masomo ya *Arts*. Tumekuwa tunajadili katika Wizara ni njia gani ambayo tutafanya ili kuwamotisha wanafunzi wengi kuchukua Sayansi na moja ya maeneo ambayo ni lazima tuyaangalie ni hilo ambalo linahusu Wanafunzi wa Sayansi kulipa zaidi na mengine ambayo yapo katika utaratibu huu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wa maandishi nilieleza kwamba, tumekaa kwenye bomu pamoja na

mafanikio ya kuwa na idadi kubwa ya Shule za Kata, pamoja na kuongeza kwa kiwango kikubwa idadi ya wanafunzi, tatizo kubwa ni umbali; watoto wanapaswa kutembea mwendo mrefu sana, jambo ambalo lina athari kwa watoto kwa maana ya kuchoka.

Mbaya zaidi ni tatizo la hawa watoto ambao wanapanga katika kitu kinachoitwa geto, ambapo wanapaswa kupanga kwenye nyumba, wanajihudumia, hawana usalama, madhara yake ni watoto wa kike kupata mamba. Bahati mbaya zinaonekana haraka, lakini watoto wa kiume wanaingia nao kwenye matatizo makubwa yanayoonekana baada ya muda mrefu sana.

Nilitaka kujua bomu hili ambalo pamoja na mafanikio yote, huko tunakokwenda hatujui watoto wetu watakuwa katika hali gani; Serikali inatoa kauli gani ili kwa kila shule, wale watoto wanaotoka mbali wa kiume na wa kike wawe na uhakika wa kukaa mahali ambapo kuna uhakika na malezi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, matatizo haya yapo na yapo katika maeneo mengi. Napenda kuchukua fursa hii, kupitia Bunge lako Tukufu, kuwahimiza wananchi katika Kata zote Tanzania nzima, wajenge hosteli ili kuweza kuboresha elimu na kuwanusuru wanafunzi katika shule zao.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimezungumzia kuhusu tatizo la walimu katika Shule za Sekondari za Serikali, ambao hawana digrii. Naomba Waziri anipe ufafanuzi; shule nyingi zimekuwa na walimu wenye Diploma, yaani Stashahada, kiasi kwamba, inafikia wanafunzi wanahama kutokana na ubora kuwa hafifu na ilifikia hatua nikatoa mfano katika Jimbo langu katika Shule ya Ilembula, wanafunzi wanahama sana kwa sababu yule Mwalimu Mkuu ana uwezo mdogo, ana stashahada; naomba atoe ufafanuzi Sera inasemaje, kwa sababu naelewa kwamba hizi shule ni lazima walau ziwe na mwalimu mwenye shahada katika taaluma ya elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kevela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na utaratibu wa kuwapatia mafunzo walimu hawa wakiwa ndani ya kazi, kwa maana ya mafunzo kazini, ikiwa ni pamoja na kuwapatia Mafunzo ya Uongozi katika Chuo chetu cha Uongozi kilichopo Bagamoyo. Pamoja na juhudi hizo, tumekuwa tukihakikisha kwamba, kila wanapostaafu katika shule hizo tunapeleka, kwa sababu wengi wao unawakuta wamebakisha mwaka mmoja au miwili wanastaafu.

Kwa hiyo, wale ambao wana muda mrefu, wengi wao wapo katika Chuo Kikuu Huria na wale wengine tunawapeleka kwenye mafunzo haya. Suala lake tutalichunguza tena, kama mwalimu angali na muda mrefu, tutafanya utaratibu wa kitaalam.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea matatizo yanayoikumba Shule ya Sekondari ya Iyunga Mbeya. Ningependa kupata ufafanuzi kama hawa waliopo kidato cha nne watapewa mtihani tofauti na wenzao, maana mpaka sasa hawapo shuleni takriban wanafunzi 1400 hawasomi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mpesya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa *O-Level* wa Shule ya Iyunga walifunga shule kwa nusu muhula. Hata hivyo, wanapaswa kurudi shuleni. Kwa Mkoa wa Mbeya hakuna tena tatizo hilo, kwa sababu Wazabuni wao walishalipwa. Kuhusu mtihani wao, muda ule utafidiwa katika mapumziko mafupi yanayoitwa *mid-term* watalipiza zile wiki mbili na watafanya mtihani sawa na wenzao.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, dhima ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi tunasema ni kutoa fursa sawa kwa wote na fursa ya elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeanza kukumbwa na wimbi kubwa la watoto yatima, ambao wanahitaji kusomeshwa. Serikali inajitahidi kutoa fedha kwa idadi ya watoto kadhaa wasomeshwe, lakini wale wanaobaki Waheshimiwa Wabunge ndiyo imekuwa kimbilio. Hata hivyo, Wabunge wanashindwa kuwasaidia watoto hao wote. Mara kadhaa humu ndani, tumeiuliza Serikali inafikiri nini kuhusu watoto hawa ambao aidha wanakosa ile fedha ambayo imetengwa na Serikali, wanakosa wafadhili, wamekuwa wakihangaika na wanafukuzwa wasipolipia fedha za mitihani; hawana mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Serikali itusaidie hii dhima ya fursa sawa na elimu bora kwa wote, kwa hawa watoto ambao hawana mwenyewe wa kuwasomesha; inatoa tamko gani? Kwa nini isifute ada kwa kundi hilo ambalo ama limeshindwa kulipiwa na Serikali au limekosa wafadhili limebaki limezagaa tu hapa katikati? Serikali kwa nini isiwafutie na kuwahurumia hawa watoto waendeane na dhima ya Wizara hiyo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, hilo ndilo lilikuwa tatizo langu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa na mwaka 2007/08, Serikali ilisomesha watoto wa aina hii 21500. Mwaka huu tumelenga kusomesha watoto 51,000 na Serikali Kuu; baada ya Serikali Kuu kusomesha hao Serikali pia inatarajia Halmashauri za Wilaya zitachangia

katika kusomesha watoto hawa na jamii kule walipo pia itasaidia katika kuwahudumia watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Bunge lako Tukufu lielewe hali ilivyo na bajeti yetu ilivyo, eneo hili tutaendelea kuliongeza kwa jinsi ambavyo Bajeti itaongezeka na tunazihimiza Hamashauri zichukue nafasi yake na kuwasaidia pia watoto hawa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kitabu hiki na kwenye mchango wangu niliongelea suala la *text books* na *reading books*. Elimu kama ilivyo, suala la vitabu ni muhimu sana hasa kwa shule za msingi na shule za sekondari. Unaanza kuona sasa *society* yetu tunatumia sana *photocopy,* watu wengi hawasomi vitabu kumbe ni kwa sababu toka mwanzo hakuna msisitizo mkubwa sana wa kusoma vitabu. Nilitaka Mheshimiwa Waziri aniambie, nilikuwa nasoma hapa kwenye changamoto za Wizara na maamuzi muhimu ambayo Wizara itayafanya, huoni hata sehemu moja ambapo *text books* na *reading books* zimepewa kipaumbele cha kutosha. Mimi nadhani suala hili ni la msingi sana kwa elimu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitabu katika shule ni suala kubwa. Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni tatizo ambalo tutakuwa nalo na tutaendelea kulitatua jinsi tunavyokwenda, lakini katika Elimu ya Msingi, MMEM na katika Elimu ya Sekondari na Ualimu, tumetenga fedha nyingi tu, kwa ajili ya ununuzi wa vitabu. Fedha za ununuzi wa vitabu zipo katika Miradi hii mikubwa na hivi tunavyokwenda kwenye Mradi wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MEJU), pia kutakuwa na kasma za kunua vitabu kwa ajili ya maktaba, kwa sababu kuna mwanya hatukuiweka kama ni changamoto kubwa, kwa sababu fedha tunazo na tunatenga mwaka hadi mwaka kwa kila shule kununua vitabu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi, nilimkumbusha Waziri juu ya ahadi iliyotolewa na Serikali ya kujenga hosteli kwa ajili ya Wahadzabe wanaosoma Shule ya Sekondari Mwengeza. Wahadzabe wachache sasa hivi wameamua kusoma na mimi jana nimetoka huko kwao. Serikali ilisema itapeleka hela haraka sana kwa ajili ya kujenga hosteli na hivi sasa wanasikiliza redio, naomba majibu ya Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatekeleza ahadi yake. (*Makofi*)

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilijitahidi sana kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, ahadi yake ya mwaka jana juu ya gari la Ukaguzi Wilaya ya Misungwi. Nilifuatilia kwa karibu sana, nimeenda Wizarani karibu mara tano, *process* ilikuwa inaenda vizuri lakini *finally* ilishindikana; sijui ni kwa nini? Safari hii Waziri anasema nini kuhusu gari la Ukaguzi Misungwi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Serikali haijapeleka magari ya ukaguzi katika Wilaya zote na katika mwaka huu ni magari machache sana ambayo yapo kwenye bajeti, nadhani Waheshimiwa Wabunge wameona. Kutegemeana na ufinyu wa bajeti, tutaangalia kadiri Bajeti ilivyo ili tuweze kumsaidia.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, akubaliane nami kwamba, vigezo vinavyotumika kwa ajili ya *minutes test* vina matatizo. Ningependa kupata ufafanuzi kutokana na wanafunzi wale ambao wamezuiliwa kuona matokeo yao. Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ametuambia kati ya wanafunzi zaidi ya 1000 ni wanafunzi 87 tu ndiyo waliolipa. Kwa kuwa tarehe 25 Agosti kutakuwa na *supplementary,* ina maana 87 wameshajijua kabisa kwamba nani ana *supplementary* na nani hana, lakini ni zaidi ya wanafunzi 800 hawajitambui; na kwa kuwa muda uliobaki ni mfupi; ni nini hatima yake kama wanafunzi watashindwa kulipa ile ada, itakuwa ni kusimamishwa shule au hilo ndiyo lengo la Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kumjibu Mheshimiwa Masolwa, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme vigezo vinavyotumika katika kufanya *minute testing* vinatokana na wanafunzi wenyewe na wanapewa muda wa kutosha kabisa kutoa taarifa hizo. Nitoe taarifa kwamba, vigezo hivi vilifanyiwa utafiti katika shule nyingi kabla hatujaanza kuvitumia. Kwa hiyo, wakituletea ambayo ni sahihi, vigezo vile vinatosheleza na vinatoa taarifa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuhusiana na wale wanafunzi ambao hawajalipa ile pesa, katika utafiti wetu tumegundua kwamba, wanafunzi wengi wanapewa pesa na wazazi; 20 *percent* au 40 *percent* kwenda kulipa shuleni au katika vyuo, lakini wanafunzi wale wanategea wanapofika vyuoni kusubiri migomo kwanza waone kama itatoa matunda watasamehewa. Tumeshagundua hii ndiyo inayofanya wanafunzi wasilipe na wanapoona kwamba, hakuna kusamehewa huwa wanalipa. Kwa hiyo, tunasema wanafunzi ambao hawajalipa hiyo pesa walipe kwa sababu hii ni *cost* sharing na Sera ya Elimu haiwezi kubadilika walipe. Wengine wanafika mpaka hapa Bungeni wanachangiwa. Kwa hiyo, watumie njia na mbinu wanazoweza walipe zile pesa ili warihusiwe kuendelea na masomo na ile pesa tumesema ndiyo inayosaidia kuendesha vyuo.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa mwalimu mzuri, hakuna mtu asiyekuwa na akili wote wana akili. Mimi nilichangia kwa maandishi na hoja yangu ambayo nataka nipewe ufafanuzi ni juu ya upungufu tulionao wa walimu, kwa mfano, Wilaya ya Mpwapwa tuna upungufu wa zaidi ya Walimu 400 na zipo shule kadhaa ambazo zina upungufu wa Walimu 15.

Wanaotusaidia kuziba mapengo haya ni vijana waliomaliza *form four* na ambao hawakupata nafasi za kwenda vyuoni kwa vigezo vilivyowekwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili aliyemaliza *form four* akubaliwe kwenda kwenye Chuo cha Ualimu ni lazima awe amepata *division four* ya *point* 26 na kushuka chini. Mimi nataka ufafanuzi, hawa wanaojitolea na kuonyesha moyo wa kukaa katika mazingira hayo magumu na hawana vigezo hivyo, kwa mfano, ana *division four* ya point 27, 28, 29 lakini pia na kigezo kingine cha umri; Waziri anawafikiriaje hawa kwa sababu ndiyo wanaoendelea kutufanyia kazi ya kutufundishia watoto wetu huko kwa kuziba pengo lililopo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu ambao wanasoma kwenye vyuo wanatakiwa wawe na angalau masomo mawili ya kufundishia. Haya masomo ni lazima wayafaulu ili kweli waweze kuyafundisha. Sasa *point* 28 ni *minimum* kabisa ya mtu kuwa ameweza kumudu masomo mawili katika mtihani ule wa *form four*. Kwa hiyo, kiwango hicho hakiwezi kushuka, kama tunataka kuendeleza elimu, nadhani kule Mpwapwa kuna wanafunzi wengi tu ambao wana-*grade* nzuri zaidi ya hizo na hao ndiyo tutawasomesha ili warudi wakawasaidie wenzao.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Karibu miaka miwili iliyopita, kumekuwa na wimbi la taasisi nyingi sana za kifedha kuwafuata Watumishi kwa ajili ya kutangaza kwamba wanakopesha. Kule kwangu Mbozi nadhani na mahali pengine, kuna kampuni moja inaitwa BayPort Financial Services, inamilikiwa na watu wazito sana katika nchi hii; sasa tukiwataja mara nyingi watu wanasema tunafanya makosa nadhani hatufanyi makosa.

**MBUNGE FULANI:** Mtaje.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Kampuni hii wanasema inaongozwa na aliyekuwa mke wa Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, lakini pia wapo na Wazee wazito wengine katika nchi hii, kwa mfano, Mzee Kaduma ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe. Tatizo ambalo nataka Mheshimiwa Waziri alifafanue ni kwamba, kampuni hii inakopesha watumishi na hususan walimu kwa sababu ndiyo walioleta malalamiko kwangu kule Mbozi. Ukikopa mathalani shilingi milioni moja na ninaomba hapa ndiyo atufafanulie vizuri, Mwalimu akikopa shilingi milioni moja anarudisha milioni tatu, sasa hii ni mikopo ya wapi kama siyo wizi wa waziwazi kwa walimu? Mimi nina mifano, Waziri akitaka naweza nikampa hizi taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu walikuja, nilitaka niongee na Mheshimiwa Waziri, lakini hatukupata muda mzuri. Naomba walimu walionituma wasikie anasema nini, kama hajui awe tayari basi kulifanyia kazi, kwa sababu ni zaidi ya asilimia 67 kama unachukua mkopo wa mwaka mmoja, lakini ukichukulia *accumulatively* nadhani ni zaidi

ya asilimia mia mbili mwalimu anapaswa alipe kwenye mkopo; hii imetokea wapi kama siyo wizi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kukopa shilingi milioni moja na kulipa shilingi milioni tatu inategemea muda, kama umekopa kwa muda wa miaka mitano au sita hiyo inawezekana, lakini kama ni mkopo wa muda mfupi, labda hiyo *interest* ni kubwa mno. Kwa hiyo, suala hili tunalizingatia na tutalifuatilia ili tuone ni kitu gani tunaweza kukifanya. Aidha ni vizuri walimu wawe makini sana na watu hawa ambao wanaleta mikopo rahisi ili wasifike mahali ambapo wanaweza kudanganywa.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Inasikitisha sana hasa tunapotumia muda mwingi ndani ya Bunge hili Tukufu, kuleta maelezo au hoja za wapiga kura wetu, lakini hizi hoja zinachukuliwa hapo hapo tunapojibiwa lakini utekelezaji wake hautekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 niliwahi kuleta hoja juu ya mwalimu ambaye alikuwa ametoweka na fedha za ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari ya Kizaga. Nilieleza juu ya mwalimu yule kwamba, alikuwa amechukua fedha za wahisani lakini pia wananchi walikuwa wamechangia takriban shilingi za kitanzania milioni 75. Inasikitisha mwalimu yule baada ya kueleza hapa, niliambiwa kwamba, hatua zitachukuliwa kama leo alivyojibu Naibu Waziri, sasa wananchi wamevunjika moyo. Wananchi sasa hivi hawawezi kuchangia lile eneo; lile jengo bado lipo vilevile, ninachotaka kusema yule mwalimu amehamishwa amepelekwa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi anashindwa kuchangia shilingi elfu tatu anawekwa ndani, huyu mtu ameondoka na milioni 73 tunamwacha hivi hivi! Naomba ufafanuzi kuhusiana na hili; wanachukua hatua gani kuhusiana na lile jengo ambalo limeachwa pale?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mimi niungane na Mheshimiwa Mbunge, kusikitika juu ya tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itachukua hatua juu ya huyo mtu mwenyewe kwa kumfikisha mbele ya vyombo vya Sheria ili aweze kujibu tuhuma hizo.

La pili, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali itatuma wataalam kule wafanye *assessment,* kazi hiyo ni kubwa kiasi gani na tuone ni jinsi gani tunavyoweza kusaidiana na wananchi wa eneo lile ili kukamilisha hosteli hiyo.

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea na Mheshimiwa Dr. Bilinith Mahenge.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa kuongea na kwa maandishi, niliongea kwa uchungu sana kuhusu tatizo la

janga la *UKIMWI*, ambalo linaikabili Wilaya yangu ya Makete. Janga ambalo limeacha idadi kubwa ya watoto yatima zaidi ya 13,000 na kwamba, janga hilo linajulikana Kitaifa limetangazwa na kila mtu analielewa.

Kwa hiyo, nikamwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, namna pekee ya kuwasaidia watoto wale 13,000 na wengine wanaoishi katika mazingira magumu ni kuwapa elimu ambayo inaweza kuwasaidia, kuwajengea Chuo cha Ufundi *VETA* ambacho kinaweza kuchukua wanafunzi wengi na kupata *skills* za kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake, ameonyesha kukubali na akataja Wilaya tatu; Ludewa, Makete na Geita, kitu ambacho ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipate ufafanuzi kama kukubali kwake kunamaanisha kwamba, Wilaya ya Makete itajengewa Chuo cha Ufundi kati ya vile Vyuo 25 vinavyoanza sasa hivi. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi katika jibu langu kwa Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo Makete, Geita na Ludewa ni Wilaya ambazo wakati wa kufanya *survey* kwanza, Geita ilionekana ina Chuo kidogo sijui cha Sayansikimu ambacho kilihisiwa kwamba ni Chuo cha *VETA* au *FDC*. Waliporudi mara ya pili, wataalam wakakuta kile Chuo kimefungwa. Kwa hiyo, Geita haina chuo kama zile Wilaya nyingine 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makete na Ludewa tunazipa *special preference* kutokana na hali halisi ya *UKIMWI*, kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge na ninaomba niwathibitishie kwamba, zitakuwa *considered* pamoja na hizo Wilaya 25, kwa hiyo, jumla ni Wilaya 28. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, pamoja na hoja nilizokuwa nimezitoa, naomba nipate ufafanuzi mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za sekondari pamoja na za msingi, mbali na kuwa na mahitaji ya walimu, lakini mahitaji ya watumishi wengine nayo ni ya muhimu sana kama walinzi, wapishi kwa shule za *boarding* pamoja na *secretaries.* Cha kusikitisha ni kwamba, kuna baadhi ya shule mfano wapishi wanalipwa chakula kile ambacho ni kwa ajili wanafunzi kwa sababu hawatambuliki au hawalipwi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini halikadhalika baadhi ya walimu wanafika mahali wanakuwa walinzi wa shule *especially* siku za *weekend*. Ningependa kufahamu Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, shule hizo zinapata watumishi badala ya

walimu hao ambao wanafanya kazi ngumu, halafu badala yake wanarudi kuwa walinzi wa shule?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watumishi wasiokuwa walimu kwa shule hizo kwa maana ya wapishi na walinzi, linafanyiwa utaratibu, pale ambapo umuhimu upo Mkuu wa Shule anapaswa kuandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara kumweleza shida yake na Katibu Mkuu anaandika barua Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utumushi wa Umma, kuomba kibali cha kuajiri. Kuajiri watumishi wote lazima tupate kibali. Kwa hiyo, tukipatiwa mgao wetu tunasema tumeruhusiwa kuajiri walinzi 10 au wapishi 10 ndiyo na sisi tunagawa. Vinginevyo, kila Mkuu wa Shule ana utaratibu wake na wanawalipa hao watumishi kwa namna ambavyo wenyewe wanakubaliana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1), zikibakia dakika 10 inabidi tuongeze nusu saa. Kwa hiyo, kwa kutumia kifungu hicho, tunaongeza nusu saa baada ya saa mbili kasorobo. Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nikichangia katika Bajeti ya Serikali, nilizungumzia suala la Sekondari ya Kata ya Ngula na jana nilichangia tena kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 18 wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kuhusu malengo ya mwaka 2008/2009 amesema kwamba, Serikali itatenga ruzuku. Sasa naomba anithibitishie hii Kata ya Ngula, ambayo Wananchi na Diwani aliyepo sasa hivi wanasubiri majibu. Je, watapelekewa vifaa vya maabara katika shule hiyo, tukizingatia kwamba tunataka wanafunzi wa sayansi wapatikane pale?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa kwa ajili ya maabara zitagawanywa sawa kwa kila Mkoa na kule kwenye Mikoa ndiyo wanajua vipaumbele katika Mikoa yao na mahitaji katika Mikoa, wao ndiyo watakaofanya mgawanyo huo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na wenzake kule kwenye Mkoa ili kuhakikisha kwamba shule hiyo inapata mgao.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilijielekeza kwenye matatizo ya walimu nikagundua kwamba, matatizo ya walimu yanasababishwa na walimu kuwa na waajiri wa aina mbalimbali. Waajiri wane, yaani Wizara nne na hivyo matatizo yao yanashindwa kutatuliwa. Kuna maombi ya chombo kimoja cha walimu cha ajira na hilo tumekwisha kulizungumza kwa muda mrefu na Serikali imekwishatuma Tume kufuatilia na kupata majibu. Nadhani limekwishafanyiwa kazi, lakini sikusikia mahali ambapo Serikali imezungumza kwamba, imefikia hatua gani? Naomba kupata majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa ufafanuzi kwamba ni kweli walimu wamekuwa na matatizo mengi na tumekuwa tukijaribu kuyafuatilia na kuona jinsi ya kuyatatua. Kwa kiasi kikubwa, tumeona matatizo ya walimu yametokana na hao walimu kurundikwa kwenye sehemu moja. Sasa hivi walimu wote mafaili yao yapo Tume ya Utumishi wa Umma na kila kitu wanafanyiwa na Tume ya Utumishi wa Umma. Ukilinganisha idadi ya walimu, kwa kweli hawawezi kuhudumiwa na Tume peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi tunachokifanya ni kuangalia kiasi gani tunaweza kufanya *decentralization* ya kuwahudumia walimu badala kuhudumiwa kwa pamoja. Kwa sababu matatizo ya walimu yalikuwa yanafanana na matatizo ya watumishi wa Wizara ya Kilimo.

Kwa kufanya hivyo, sasa hivi kwa kiasi kikubwa sana, matatizo ya Wizara ya Kilimo yameondoka. Kwa hiyo, tunaona hata kwa walimu tukifanya hivyo tutakuwa tumewasaidia badala ya kuwarundika katika kituo kimoja.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, kuna suala la Sekondari ya Geita. Sekondari ya Geita ilikuwa chini ya Bodi ya Wakulima wa Pamba na ikachukuliwa na Serikali mwaka 2006, lakini wazabuni wake ambao wanalisha shuleni hapo hawajalipwa mpaka leo hii. Nataka kuuliza tu kwa sababu wamesema wapo Kanda ya Ziwa, lakini katika Kanda ya Ziwa kuna shule nyingi na kuna mazoea ya kuwalipa wazabuni wa shule zile za zamani na zikaachwa zile mpya na mpaka sasa hivi wale wazabuni hawajalipwa. Nilikuwa nataka nipate ufafanuzi kwamba; je, hao wazabuni wa Sekondari ya Geita watalipwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kuhusu madai ya wazabuni. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, ameeleza utaratibu na kiasi cha fedha tulichopata. Naomba niwasihi wazabuni wote kuvuta subira. Sasa hivi hatupaswi kuwalipa wazabuni bila kufanya uhakiki na yale madeni ambayo yamehakikiwa wanakwenda kuwalipa wazabuni kwa kumtambua kwamba, huyu ndiye Juma aliyelisha shule hapa na wanakwenda shule kwa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo tunaogopa kubatizwa majina, tutawalipa.

**MWENYEKITI:** Majina kama nini? *(Kicheko)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nipate ufafanuzi kuhusu jambo moja. Inaaminika kwamba, Serikali iliwahi kutoa Waraka ambao ulitoa maelekezo kwa Shule za Sekondari za Serikali, kuwasomesha bure watoto wa kike na kiume ambao ni walemavu. Waraka huo umekuwa hautekelezwi, inapokuwa ametokea mlemavu katika shule husika. Mimi ninao mfano wa mtoto wa kike, anayesoma Rugambwa, ambaye anasumbuliwa sana na anao Waraka wa Serikali. Je, Serikali inasema nini kuhusu walemavu wale ambao wapo mashuleni na je,

wataendelea kusumbuliwa ama Serikali itapeleka Waraka mashuleni kusudi wawe wanasoma bila kusumbuliwa kama wanavyosumbuliwa sasa hivi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kulileta suala hilo na Serikali itawakumbusha Wakuu wa Shule kuhusu wajibu wao wa kuangalia hao watoto walemavu katika shule zao.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kupitia mchango wangu wa maandishi niliouwasilisha jana, wenye kurasa nane, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri alinisahau. Kati ya mambo mengi niliyohitaji kupata ufafanuzi, naomba kuuliza jambo moja tu. Katika mchango wangu wa maandishi, niliulizia kuhusu walimu wanaohamishiwa kwenye Shule za Sekondari hasa za Kata kwamba, Serikali inawahamisha bila kufuata taratibu za ajira na stahili zao kiasi kwamba, wanapoteza haki zao kwa mfano, fedha za uhamisho na hawahami na utumishi wao. Sasa tulitegemea kwamba, Serikali ingetamka lolote kuhusu walimu hao ili waweze kujenga imani eneo walilopelekwa kwamba haki zao zitatunzwa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia tarehe 1 Julai, 2008, Shule za Sekondari zitakuwa zimehamishiwa kwenye Halmashauri hatua kwa hatua na wafanyakazi wote hao watakuwa chini ya *umbrella* ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa sababu hiyo, sioni tatizo ambalo linaweza kutokea la utumishi la aina hiyo. Kama kuna walimu ambao wamekuwa na matatizo hayo, waendelee kutuarifu ili matatizo yao yashughulikiwe kwa msingi ule ambao nimesema madeni yote ya walimu yatalipwa.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wakati nachangia kwa maandishi, nilieleza suala la mabadiliko ya mitaala linalotokea na mabadiliko hayo yanapotokea mara nyingi walimu wote katika shule za msingi wanakuwa hawapati semina yoyote ya kuwaeleza mabadiliko hayo ili waweze kuendana na hali halisi. Sasa nilitaka tu kupata ufafanuzi, hao walimu mabadiliko ya mitaala inapotokea nani anawajibika kuwapa semina?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye suala la *BayPort* nitaomba meza yako nikukabidhi au nimkabidhi Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, usianze kuharibu utaratibu, umekwishasema vizuri basi. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi juu ya mafunzo kwa ajili ya mitaala iliyobadilika. Wizara ilikwishatoa mwongozo na mafunzo na kwamba kila Halmashauri ilikwishawezeshwa. Baada ya hapo, ilikuwa ni jukumu la kila Halmashauri kuendelea kutoa mafunzo hayo kwa walimu husika ili waweze kupata uwezo wa kumudu mtaala huo. Kwa maana hiyo basi, kama kule kwenye Wilaya ya Bukombe bado hakujafanyika kitu kama hicho, namwomba Mheshimiwa

Mbunge awasiliane na *DED* wake, pamoja na Afisa Elimu wake, waweze kuona wapi walikwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine tutumie nafasi hii pia kuziagiza Halmashauri zote, kuhakikisha kwamba, wanatoa semina kwa walimu walengwa.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Sina nia ya kutoa shilingi ila nahitaji ufafanuzi katika michango yangu ya muda mrefu; kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nilichangia na jana kwenye maandishi. Ninashindwa kuelewa, miundombinu ya madarasa, maabara, vyoo si muafaka hata kidogo kwa wanafunzi wenye ulemavu na muda wote nimeambiwa kuna ramani maalum zipo. Ninachoshangaa, hivi ramani hizi zimefichwa wapi kwa sababu katika maeneo ambayo nimeyatembelea sijaona mwelekeo wa kurekebisha miundombinu hiyo ili watoto na wanafunzi wenye ulemavu waweze kumudu? Naomba ufafanuzi na ni lini nitakuta mabadiliko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kama Mungu ananijalia hii ni mara ya mwisho kuuliza swali hili, kitakachofuata ni kuondoa shilingi tu kwenye Wizara zinazohusika. Naomba ufafanuzi wa dhati. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo: Mheshimiwa Magreth Mkanga, dada yangu, hoja zake ni za msingi. Kweli tumesambaza ramani nchini kote, zinazoonyesha namna ya kurekebisha miundombinu kuanzia madarasani, kwenye mabweni, kwenye vyoo mpaka kwenye mabwalo ya chakula. Tutumie Bunge lako Tukufu, kuwaomba wahandisi wote wanapojenga shule mpya na zile wanazofanya ukarabati, wafuate utaratibu huo. Kweli ni haki yao tuwasaidie. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba Waziri anieleze kisima ambacho nitaweza kupata walimu wa Shule za Sekondari za Kata, ambazo nimezijenga nyingi kwenye jimbo langu, maana Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naona wamechemsha? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Jamani sasa msimame; nani anataka kuchemsha tena?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kusomesha walimu na kuwasambaza kwenye shule. Kwa hiyo, walimu wataendelea kupatikana hatua kwa hatua na nadhani baadaye Mheshimiwa Dr. Mpanda ataridhika.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nipate ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Wakati nachangia kwa maandishi, nilikuwa nimeulizia utaratibu unaotumika kuwasaidia Shule ya Walemavu Viziwi ya Mkoa wa Tabora, ambayo sasa hivi haina mwenyewe. Ile shule huwa inahudumiwa kwa kuombaomba tu, kwa hiyo, naomba ufafanuzi ipo chini ya nani; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa au chini ya Wizara ya Elimu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi; shule hii awali ilikuwa inamilikiwa na Kanisa Katoliki. Sasa kwa taarifa za hapa ndani ya Bunge, inaelezwa kwamba, imekabidhiwa Serikalini. Kwa kuwa shule ile inahudumia wanafunzi wa shule za msingi, kiutaratibu inapaswa ihudumiwe sasa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ndio maana katika hoja yetu ya msingi tulimwomba tuangalie utaratibu kama wenzetu Kanisa Katoliki walishaiandikia Serikali kutaka kuikabidhi, vinginevyo, tutakuwa tunaingilia majukumu ya watu. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi.

**MHE. JAMES P. MSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi niliomba tujengewe Chuo cha *VETA* Geita, nashukuru Mheshimiwa Waziri amesema watatujengea chuo hicho. Wananchi wa Geita wanashukuru sana. Sasa ufafanuzi katika sehemu ya pili, nilieleza tatizo la maboma ambayo Awamu ya Tatu tuliyajenga zaidi ya 2000; MMEM ya kwanza ikapita, wananchi wamejitahidi kuyapunguza Awamu hii ya Nne, yapo maboma ya madarasa 632 na nyumba za walimu 246. Sasa hivi wananchi wanapaswa kuchangia Shule za Sekondari za Kata michango mingine kama ya *TASAF*, hawana nguvu ya kuendelea kuyajenga haya maboma. Waziri hajasema; kuhusu maboma tukawaambie nini Wananchi wa Geita na wanatusikiliza au tuwaambie wakayabomoe? *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Utaungua vidole ukiwaambia wabomoe.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ni mzoefu na anaelewa mchakato wa bajeti na hela iliyoko, tutaendelea kusaidiana kwa jinsi ambavyo fedha zikavyopatikana. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mheshimiwa Waziri. Katika mchango wangu nilikuwa nimezungumzia suala la mjadala, amelielezea hapa lakini napenda pia alipanue kwamba ni kwa utaratibu gani mjadala huu utafanyika katika kuboresha hiyo Sera ya Elimu?

Napenda pia nipate ufafanuzi juu ya suala la mitihani kupotea katika Chuo Kikuu. Mitihani na *assignment notes* hasa Kitivo cha *Arts and Social Sciences* zimekuwa zikipotea na kuwalazimisha watahiniwa ama kuzirudia kazi zao au mitihani na kuwaongezea gharama nyingine za ziada; una ufafanuzi gani juu ya hilo?

**MWENYEKITI:** Jibu swali la pili, la kwanza usilijibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Arfi kwamba, suala hilo tunaomba utuachie tutalifanyia kazi na tutampa majibu hapa hapa. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea uamuzi kwamba, baadhi ya majukumu ya Wizara yanahamishiwa kwenye Halmashauri zetu. Najua na wewe unajua Halmashauri zetu zimeelemewa na mzigo mkubwa na

mambo mbalimbali ambayo yapo. Je, ni maandalizi gani yamefanywa ambayo yatahakikisha kwamba hayo madaraka yanayokasimiwa kwenye Halmashauri kweli yatatekelezwa na maandalizi gani yamefanywa kuziwezesha Halmashauri zetu ambazo tayari zina *burden* kubwa ya mambo mengi na haya nayo yanakwenda? Tumefanya maandalizi gani kwa sababu tumeambiwa *effective date* ni Julai Mosi mwaka huu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalam wa Wizara yangu na wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wamekuwa wanafanya maandalizi ya utaratibu huu tangu mwezi Machi, 2008. Kufikia sasa, maandalizi haya yamefikia hatua nzuri na hatuna wasiwasi kwamba, yatakwenda vizuri. Usimamizi wa elimu bado unakuwa kwenye Wizara ya Elimu na utaratibu wa utawala utakuwa kwenye Serikali za Mitaa. Tunategemea kabisa kwamba, hakutakuwa na matatizo katika utaratibu huo.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kumwomba Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi wa suala la mitihani ya darasa la nne, pamoja na ile ya darasa la kumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unaweza kubadilisha *topic* maana hili tayari limebishaniwa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Limetolewa majibu lakini majibu yake yapo kwenye utata kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba tuelewane; haturudii wewe tafuta hoja nyingine hiyo ilishazungumzwa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Kambi ya Upinzani, tuliuliza nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi, waendeshaji wa vyuo vya elimu ya juu toka mwaka juzi; Wizara ilisema itatoa nyongeza hiyo, lakini mpaka sasa waliopata nyongeza hiyo ni wahadhili tu. Je, ni lini wafanyakazi hawa watapata nyongeza yao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu suala lililoulizwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu. Kuhusu suala la kuongeza mishahara ya watumishi waendeshaji katika vyuo vikuu vya umma, tulishalifanyia kazi na waliostahili kuongezewa tumeshapeleka barua kwa Msajili wa Hazina ili waweze kurekebishiwa mishahara yao na nakala tumewapelekea chama chao cha watumishi waendeshaji (CHARAHAU). Kwa hiyo, suala hilo tumelimaliza. *(Makofi)*

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Suala la takwimu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na pindi linapopotoshwa linakuwa na matatizo makubwa. Ninadhani ndiyo sababu Mheshimiwa

Waziri, ametuletea hiki kitabu. Kwenye jedwali la kielelezo ukurasa 101, naomba Waziri anipe ufafanuzi kwamba inakuwaje wanafunzi walioandikishwa walio darasa la nne wawe pungufu ya wale walioandikishwa kufanya mtihani wa darasa la nne na vivyo hivyo ni namna gani wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la nne wawe wachache kuliko wale wanaoingia darasa la tano kwa mwaka unaofuata? Naomba ufafanuzi kama hii ndiyo *trend*, tuna uhakika gani kama hizi takwimu zilizoko huku nazo ni sahihi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umeupata ukurasa huo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Hebu atueleze ni ukurasa gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan hebu rudia.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Nadhani Waziri alikuwa hasikilizi, nimesema ukurasa wa 101, jedwali la wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la nne mwaka 2007 kwamba, inawezekanaje wanafunzi walioandikishwa kufanya mtihani wa darasa la nne mwaka huo huo wawe wengi kuliko wale walio darasa la nne. Je, hao wanaofanya mtihani ni wepi; ni wa darasa la tatu au darasa la tano na vile vile ni kwa namna gani wanafunzi hao waliofaulu mwaka huo wawe wachache kuliko wale ambao wameingia darasa la tano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umeliona jedwali hilo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanafunzi wanafanya mtihani kuna wale ambao walirudia mwaka. Kwa hiyo, ukichukua wale ambao waliandikishwa mwanzoni na wale wanaokuja, unaweza kupata majibu kama hayo. Tutaliangalia tena hilo jedwali analolisema na kama kuna kasoro tutazungumza naye zimetokana na kitu gani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Utazungumza na Bunge siyo yeye.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nilitaka kujua kitu kimoja tu; kuna mtoto ambaye anaitwa Kurwa Hussein, ambaye yupo Sekondari ya Mazungwe Kigoma Vijijini, ambaye ni mlemavu hasikii wala hasemi. Nilipeleka taarifa zake Wizarani, wakaamua kumpa barua ya uhamisho kutoka pale Mazungwe kwenda Sekondari ya Tabora ambako wanasomeshwa viziwi na wale wasiosema.

Sasa barua iliyoletwa ni ya kumtaka mzazi wake amsomeshe yeye mwenyewe na wakati yule mzazi hana uwezo. Naomba kuiuliza Serikali; je, motto huyo atasomeshwa na Serikali au itamwacha hivi hivi? Jamani wapeni kipaumbele walemavu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge ametuletea hoja hii, tumeifanyia kazi na huyu mtoto pale alipopelekwa maelekezo yaliyotolewa ni kwamba, atasomeshwa. Sasa huduma nyingine ni mavazi, sabuni na kadhalika. Haya ndiyo nilimwandikia Mbunge nikamwambia itabidi sisi Wabunge wa Viti Maalum tumsaidie huyu binti, ada hatozwi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni wote kwa kutokurudia rudia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 426,341,800
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 1,396,667,800
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 231,784,500
Kif. 1005 – *Procurement Unit* .. ... ... ... ... ... ... ... … Sh. 188, 997,800
Kif. 1006 – *Information, Education and Communication* .... ..... ..... ..... ..... Sh. 53,133,700

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Chief Education Officer*.. ... ... ... ... ... ... ... Sh.4,117,302,700

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi. *Vote 46,* Programu ya 20 *Sub-Vote 1001 – Secondary Education.*

**MWENYEKITI:** Tumeshavuka, tuko 2001.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Inspectorate* ... .. ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 5,650,506,300
Kif. 2003 – *UNESCO Commission* ... ... .. ... ... ... ... … Sh. 381,043,90
Kif. 3001 – *Basic Education* ... ... ... ... ... ... ... … … … Sh.6,929,209,600
Kif. 4001 – *Secondary Education* ... ... ... . ... ... … Sh.108,842,776,300
Kif. 5001 – *Teacher Education* ... ... ... ... ... ... ... … Sh. 24,716,545,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7001 – *Higher Education* ... ... ... ... ... ... … Sh. 227, 537,849,200

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 280500 - *Transfer and Subsidy Institution at the same level of Government,* ambayo ina shilingi bilioni 220. Naamini hii ni fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati na katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri tuliambiwa kwamba, kwa mwaka huu Bodi ya Mikopo imepewa kama shilingi bilioni 119, lakini hapa zinaonekana ni bilioni 220. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri; je, hizi fedha nyingine ni zile *administrative costs* za Bodi au hizi zote ni kwa ajili ya mikopo peke yake?

**MWENYEKITI:** Umekiona hicho anachokisema? Naomba majibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni ndiyo kwamba, fedha hizi zinajumuisha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya *administrative costs* za Bodi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7002 – *Technical Education* ... ..... ... ... ... ... … Sh. 8,684,742,600

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi nipo kwenye *Vote 46, Sub-vote 7002 – Technical Education.* Nahitaji ufafanuzi kidogo tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** *Sub-item?*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ndiyo nataka niangalie hapa. Ni suala la ujenzi wa …

**MWENYEKITI:** Tukija hapa tunaingia kwenye *Sub-item.*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** 270200. Nilichokuwa nataka ufafanuzi kidogo tu; Mheshimiwa Waziri wakati anatoa hotuba yake, alieleza juu ya Wilaya ambazo zitajengewa hizi Shule za *VETA.* Sasa nataka nijue kwa kule kwetu Iramba, tayari tuna majengo tumeyapata kupitia Kampuni ya Ujenzi ya Chiko, iliyokuwa inajenga barabara. Tumepata majengo mazuri sana.

Tulikuwa tumeshakubaliana ili yapitishwe yawe Kituo cha *VETA* cha Wilaya. Sasa nataka nijue kama watakuwa tayari ili waweze kufanya hiyo kazi na ili sisi tuingie kwenye programu ya mwaka huu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mkishaondoka kwenye mshahara wa Waziri, kunakobaki lazima pawe ndio penyewe. Hapa ni *technical equipment, fumigation and cleaning.* Siyo penyewe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... ... ... ... ... Sh. 14,033,332,000
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ... ... ... .. ... ... Sh. 11,515,148,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Chief Education Officer* ... ... ... ... ... Sh. 1,585,319,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margreth Mkanga, tuambie ni wapi unapotaka kuuliza. *(Kicheko)*

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** *Sub-Vote 200, item 4382 – Support to Special Education.* Naomba ufafanuzi; pesa hizi zilizotengwa na tutakazozipitisha; *support* yake ni katika kitu gani *materials* au nini hapa? Naomba tu kufahamu.

**MWENYEKITI:** Umeiona?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na *support* kwa ajili ya watoto wenye ulemavu na mahitaji maalum.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Inspectorate* ... ... ... .. ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 250,000,000
Kif. 3001 - *Basic Education* ... ... ..... ... ... ... ... ... ... ... Sh.8,224,868,000
Kif. 4001 – *Secondary Education* ... ... .... ... ... ... ... Sh. 24,215,614,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – *Teacher Education* ... . ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 533,368,000

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. *Sub-Vote 5001- Teacher Education.* Katika kitabu kuna orodha ya Vyuo vya Ualimu

ambavyo vimeelezwa kwamba, vitafanyiwa ukarabati, lakini nikiangalia fedha iliyotolewa hapa, najaribu kutafuta ni kiasi gani kitakachofanya kazi hiyo sikioni.

Naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze hizo fedha itatoka wapi, kwa sababu kwenye kitabu nimejaribu kutafuta sizioni labda kuna mahali pengine zilipo? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Atafute wapi?

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwenye vitabu vya fedha maana naona hapa kuna milioni 500 ambazo sidhani kama zitakidhi kufanya kazi ya vyuo vilivyoorodheshwa.

**MWENYEKITI:** *Sub-item* ni 4370 - *ICT in Education*.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kitabu cha *development*, nadhani huo ukarabati utakuwa kwenye *development* ndiyo maana nilikuwa natafuta.

**MWENYEKITI:** Kama haupo, Kanuni inasema hatuongezi wala hatupunguzi. Wewe ungeulizia kule kwenye Mshahara wa Waziri ingekuwa sahihi. *ICT* ni mambo mengine kabisa. Ulitaka kueleza habari ya *ICT*?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 6001 – *Culture and National Languages* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 0

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7001 – *Higher Education* ... . ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 63,096,906,500

**MWENYEKITI:** Ndiyo ngoja niwaorodheshe wale wote.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliuliza swali na amenijibu vizuri Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nilikuwa nazungumzia zaidi ujenzi wa hosteli; *Sub-Vote 4391-* Chuo Kikuu cha Muhimbili. Sasa nikiangalia hakijatengewa pesa za ndani, lakini kina shilingi 625,300,000.

Malengo yaliyowekwa kwenye hotuba yake ni mengi sana, pamoja na upanuzi wa Chuo Kikuu, ujenzi wa hosteli na yeye ameniambia kwamba pesa za kukamilisha ujenzi wa hosteli zipo kwenye kitabu hiki upande wa maendeleo. Sasa nilitaka nipate ufafanuzi

hizi milioni 625 zitatosha kukamilisha malengo ambayo yapo kwenye hotuba humu kwa ajili ya Muhimbili? Kwa nini pesa za ndani hazijatengwa kwa ajili ya Chuo Kikuu hiki na kimeanza kujitegemea mwaka mmoja tu uliopita?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *book* hili la fedha za maendeleo, kuna *typing error* kifungu cha 6364, ile iliyoandikwa *Tanzania Cultural Fund, actually* ni *Muhimbili University for Health Sciences.* Fedha zile zilizotengwa pale ni shilingi 3,212,000,000.

**MWENYEKITI:** Wabunge wengine itakuwa kazi hapa, maana muda wa nusu saa umeshakwisha.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 2225 - *Institute of Marine Science Project.* Kule Zanzibar nataka kujua pesa hizi …

**MWENYEKITI:** kifungu chake kipo wapi?
**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Ukurasa wa 71.

**MWENYEKITI:** *Item?*

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** *Item 2225.*

**MWENYEKITI:** Inaitwa *Institute of Marine Science.*

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu pesa za kuendeleza ujenzi wa taasisi hiyo, zimetengewa shilingi bilioni 1.2 sawa na mwaka jana. Je, Serikali itapata wapi pesa nyingine ambapo sasa hivi ni zaidi ya shilingi bilioni sita?

**MWENYEKITI:** Unauliza hizi ndiyo zinatosha?

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Hizi zinatosha, nyingine zitapatikana wapi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao kuhusu Chuo cha *Marine Science* kilichopo Buyuni. Ni kweli kwamba, hizi pesa hazitoshi, lakini tunaendelea kuwasiliana na Hazina ili itoe *guarantee* kwa ajili ya kukopa fedha nyingine *CRDB* ili tuweze kumalizia pamoja hizi fedha zilizotengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, dakika moja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. *Sub-Vote 6336* ni ya *Rehabilitation and Expansion Project Dar es Salaam,* ina-*assume* ni *University of Dar es Salaam* ambapo wametenga shilingi bilioni 2.3. Mheshimiwa Waziri, anafahamu

matatizo makubwa sana ya miundombinu ya madarasa na kadhalika ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika hotuba yake ametuambia kwamba, kuna shilingi bilioni 20 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya ukarabati wa Majengo ya Vyuo Vikuu, lakini siioni katika eneo hili. Pesa hii iko wapi katika eneo hili la fedha ya maendeleo? Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Dunia imetupa dola za Marekani milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa Vyuo vya Elimu vya Teknolojia na sehemu ya fedha hizo itatumika kwa ajili ya ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Fedha hizi zimepitishwa na Bodi ya Benki ya Dunia katika kikao chake cha Mei, 15 na kwa hiyo hazikuwahi kwenye hivi vitabu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7002 – *Technical Education* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 6,111,463,700

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu lilikaa kama Kamati, limepokea na kuipitia Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2008/2009, kifungu kwa kifungu bila kufanya mabadiliko yoyote. Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liikubali Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na tupo nje ya muda.

Nina tangazo; kesho tarehe 16 mmekaribishwa na *NSSF* kwenda kuangalia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Kamati zitakazohusika ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati ya Mambo

ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma na Kamati ya Nishati na Madini. Itabandikwa pale ili kila mtu ajue kama Kamati yake inakwenda kesho saa saba mchana, mabasi yatakuwepo pale na chakula mtapewa kule kule.

Kamati zilizobaki watakwenda tarehe 17. Kwa hiyo, mtaangalia kwenye *Notice Board.* Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 02.27 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 16 Julai, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*